

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MKUTANO WA NNE

MAJADILIANO YA BUNGE

Kikao cha Arobaini – Tarehe 10 Agosti, 2006

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel John Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Taasis ya Utafiti wa Magonjwa Tanzania kwa Mwaka 2004/2005, *(The Annual Report and Accounts of the National Institute of Medical Research Tanzania for the year 2004/2005)*.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI: Maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI: Maoni ya Kambi ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

MASWALI NA MAJIBU

Usafi wa Mazingira katika Fukwe za Bahari

MHE. LUCY F. OWENYA (K. n. y. MHE. MHONGA SAID RUHWANYA)
aliuliza:

Kwa kuwa, Serikali imelivalia njuga suala la usafi wa mazingira kwa ujumla kwa kuangalia zaidi maeneo ambayo yamekwishaharika na uchafuzi wa vyanzo maji, pamoja na hifadhi za miti na misitu ili kuyarudisha mazingira hayo katika hali yake ya kawaida ya kuharibiwa.

(a) Je, isingekuwa wakati muafaka kwa Serikali kulivalia njuga suala la uchafuzi wa fukwe za bahari na mazingira hasa fukwe za Bahari ya Hindi?

(b) Kwa kuwa, fukwe hizi ni urithi wa asili ambapo kila mtu ana haki ya kuzitumia lakini nyingi kama sio zote zimemilikishwa kwa watu binafsi na kwamba watu hawawezi tena kwenda Baharini kujiburudisha, Je, Serikali iko tayari kuzifuta hati miliki hizo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya kwamba kuna haja ya kulivalia njuga suala la usafi wa mazingira ya fukwe za bahari na maziwa. Kutokana na umuhimu huo Serikali inaandaa mkakati wa Hifadhi ya Bahari, Maziwa Makuu na Maeneo yanayozunguka Bahari na Maziwa hayo. Mkakati huo utaaanisha changamoto zilizopo, hatua za kuchukuliwa, muda wa utekelezaji, wahusika na gharama za utekelezaji. Miradi inayotekelezwa sasa katika maeneo hayo itakuwa sehemu ya Mkakati huo. Miradi hiyo ni pamoja na:-

Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Pwani na Bahari (*Tanzania Coastal Management Partnership (TCMP)*); Mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Maeneo ya Pwani (*Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP)*); Mradi wa kuhifadhi mazingira katika Ziwa Victoria; na mradi wa kuhifadhi mazingira katika Ziwa Tanganyika. Tunaandaa Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Nyasa.

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 inaelekeza kutunza na kuhifadhi ukanda wa fukwe za Bahari. Kifungu cha 7(1) (d) cha Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 kinaelekeza kwamba ukanda wa fukwe za bahari ni eneo ambalo ni hatari (*Hazardous*) na kwamba uendelezaji wake unaweza ukaleta madhara kwa uhai ama kusababisha mmomonyoko ama uharibifu wa mazingira kwa eneo lenyewe ama lililoko jirani yaani *contiguous Land*. Ukanda wa Fukwe za Bahari umeainishwa katika Tangazo

la Serikali GN Namba 76 mwaka 1992 kwamba ni upande wa mita 60 baada ya mpaka wa juu wa maji ya Bahari yaani *High Water Mark*. Aidha, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 vilevile inalinda fukwe za bahari, maziwa na mito. Kifungu cha 57(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kinakataza shughuli za binadamu za kudumu zenye madhara kwa mazingira kufanyika katika ukanda wa mita 60 za fukwe za bahari, maziwa na mito. Lengo jingine la Sheria hizi ni kuepusha ubinafsishaji wa fukwe na kuruhusu jamii kufikia na kufurahia eneo la fukwe ambalo ni sehemu ya urithi wa jamii ya Watanzania, bila kizuizi au masharti magumu. Kwa sasa Serikali haina utaratibu wa kufuta hati miliki zilizotolewa kisheria kabla ya Sheria nilizozitaja kuanza kutumika.

Hata hivyo wahasika watakapotaka kuendeleza upya maeneo hayo au wakati muda wa Hati Miliki zao utakapokwisha itabidi Sheria na Kanuni zufuatwe kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya sehemu ya pili ya swali la Mheshimiwa Mhonga yanafanana sana na swali Namba 369 alilouliza jana Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, Mbunge wa Kigamboni ambalo pamoja na maswali yake mawili ya nyongeza na lile la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, yalijibiwa kwa ufasaha na Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa uchafuzi wa Fukwe za Bahari athari yake imeonekana kuwa kubwa sana. Je Serikali inatoa tamko gani kuhusu wananchi wanaochafua fukwe hizo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS alijibu:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud , kama ifuatavyo:-

Wananchi wasichafue Fukwe za Bahari. (*Kicheko*)

Na. 377

Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar.

Swali Lililotajwa hapo Juu Lilifutwa na Muuliza Swali.

Na. 378

Ajira kwa Wananchi

MHE. KABUZI FAUSTIN RWILOMBA (k.n.y MHE. MBARUK KASSIM MWANDORO) aliuliza:-

Kwa kuwa, suala la ajira kwa vijana na wananchi kwa ujumla limepewa kipaumbele na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005; na kwa kuwa, Kanuni za mfumo wa uchumi wa soko na utandawazi inatoa upenyo kwa wawekezaji kutoka nje kutoa nafasi nyingi na kazi kuliko inavyostahili kwa wageni wa nje kutoa nafasi nyingi na kazi kuliko inavyostahili kwa wageni wa nje na kwa kuzingatia kuwa suala la ajira ni mtambuka.

(a) Je, Serikali inaweza kulithibitishia Bunge kuwa mpango thabiti umeandaliwa kuhakikisha kwamba, ajira kwa wananchi itakuwa kama ilivyowekwa bila kuathiriwa na utashi wa wawekezaji?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba, hakuna Wizara au Taasis nyingine ambazo zinakwamisha sera, mikakati na mipango ya kuongeza ajira kwa wananchi?

(c) Je, Serikali ina mpango gani thabiti wa utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji kwa wananchi kiuchumi chini ya mipango, miradi na *program* za MKUKUTA, MKURABITA, *TASAF*, *SELF*, *SIDO VETA* na kadhalika kwa shabaha ya kuongeza ajira?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, napenda kutoa ufafanuzi ufuatao;

Serikali imeweka mazingira ya kuvutia wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuwapa nafasi ya kuajiri wataalam watano wa kigeni ambao mwekezaji anawahitaji ili kusimamia maslahi yake kwenye sehemu kama Uongozi, Uhasibu, Uhandisi na Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa, na kadhalika. Wafanyakazi zaidi ya hao wanaoruhusiwa kisheria wanakubalika tu pale ambapo ujuzi huo ni utalaam muhimu usipoatikana hapa nchini. Hivyo uchumi wa soko na utandawazi hautatufanya tuache kuzingatia taratibu zetu kwani kuna Sera na Sheria zinazotuongoza.

Baada ya kutoa ufafanuzi huo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, lenye sehemu a, b, na c kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo yaliyopo kwenye ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Wizara yangu imechukua hatua ya kushirikisha wadau wote na kuandaa Mkakati wa Kitaifa na Kukuza Ajira yaani *The national Employment Creation Strategy*. Tayari rasimu ya mkakati huu imekamiliwa na kuwasilishwa Serikalini ili kupitishwa rasmi kabla ya utekelezaji kuanza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sekta na Wadau wa Ajira wanahusishwa kikamilifu katika kuandaa mkakati huu, jukumu la kuutekeleza na kuhakikisha unafanikiwa litakuwa la wadau wote. Aidha, Wizara yangu itaendelea na jukumu la kuratibu na kuhakikisha wadau wote pamoja na waajiri wanashiriki kuutekeleza mkakati wa kukuza ajira katika sekta zao. Kwa kiwango hiki cha ushiriki, suala la kuathiriwa na utashi wa wawekezaji halitakuwepo. Aidha, katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu, itafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika makampuni mbalimbali na sehemu za kazi ili kubaini na kuwachukulia hatua wageni wanaofanya kazi kinyume na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne imejizatiti sawasawa kuhakikisha kuwa inaelekeza nguvu zake katika kuwapatia wananchi wake fursa zaidi za kujiendeleza kiuchumi kwa kujenga mazingira mazuri, ikiwa ni pamoja na kusimamia vizuri *program* za kuwawezesha wananchi, MKUKUTA, MKUTABITA, *TASAF*, *SELF*, *SME*, *Guarantee Schemes*, *SIDO* na kadhalika, kama alivyoelezea Mheshimiwa Mbunge. Tunaamini kuwa mafanikio ya mipango hii itawezesha wananchi kuongeza vipato vyao na kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Spika, ili kunufaika na mipango mbalimbali inayotoa fursa za mitaji, wananchi wamehimizwa kujiunga kwenye vikundi vya uzalishaji mali na utoaji huduma na Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo yaani *SACCOS* umedhihirika kuwa na mafaniko makubwa katika kuwajengea wananchi mitaji endelevu kwa shughuli za kiuchumi na ajira.

MHE. KABUZI FAUSTIN RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali inaangalia kwamba wawekezaji wawe na watumishi angalau watano, napenda kufahamu. Je, suala hili halihusu watu wa Migodi hasa ya Dhahabu kwa sababu watumishi wengi sana kiasi ambacho nadhani wanahitaji na wenyewe kuangaliwa.

Na kwa kuwa wanatakiwa watumishi watano je kwa Mgodini wa Nyamungo ambao umeajiri hata walinzi kutoka Nepal. Je, inaweza ikachukuliwa hatua hasa sasa waambiwe waondoke ili waachie Wakurya waweze kufanya kazi hiyo?

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikianza kujibu swali la pili tumelipokea suala hilo na kama tulivyojibu katika swali la msingi kwamba tunakagua makampuni mbalimbali kuangalia kama watu walioajiriwa katika makampuni hayo wamefuata utaratibu na Sheria zilizopo, tumelipokea suala lake tutakagua kampuni hiyo kuona kama ni hatua gani inapaswa kuchukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *TIC* kuanzisha kituo cha Uwekezaji Nchini inawaruhusu wawekezaji wote kuajiri watu watano ambao watawasaidia kuendesha mitaji yao na kusimamia maslahi yao. Pale ambapo wanahitaji wafanyakazi wa ziada wanaomba kwa taratibu ambazo zimewekwa. Aidha, katika eneo la uchimbaji wa mafuta ndiyo tu ambao Sheria ile haiwafungi kuwaajiri watu watano peke yake.

Hata hivyo, kama nilivyosema awali tutapeleka timu za wakaguzi na kuangalia kama hao walioajiriwa wengi kweli wameajiriwa kwa utaratibu uliopo.

Mheshimiwa Spika, Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hili suala la kupeleka timu na kufanya ukaguzi limepitwa na wakati. Tatizo Watanzania wanauliza kwamba ni nafasi zipi ambazo hao wenye makampuni wanapaswa kuziacha kwa ajili ya Watanzania na si suala la kufanya ukaguzi?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali dogo la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, kama ifuatavyo:-

Suala la kupeleka wakaguzi msingi wake ni kwamba masuala ya ajira yanakuwa ni mtambuka siku zote, unapokuwa una – *address* masuala kwa mfano ya migodini lazima uwe na timu ya wataalam wa Wizara ya Kazi na Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Madini. Kwa hiyo, fasheni ya kuwa na timu ndiyo fasheni ya sasa zaidi kuliko kudai kwamba ni fasheni ambayo imepitwa na wakati. Hilo ni la kwanza.

Sasa ni aina gani ya wafanyakazi ambao tunafikiri sasa hawa waajiriwe au ni kada za ajira ziajiriwe kwa misingi lakini hoja inakuwa ni kwamba mwekezaji huyu anakuja na fedha zake kumbe ile Sheria inampa nafasi ya kuwa na wafanyakazi watano ambao anafikiri ni muhimu. Sasa wale wanaozidi kama Waziri Mwenye Dhamana na Waziri wa Kazi kwa maana hiyo tuna timu yetu maalumu ya kuhakiki wataalam wa kigeni na Waziri Mwenye Dhamana anaporidhika kwamba hawa wataalam wanahitajika basi wanaajiriwa.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba suala hili ni gumu kweli na tunalifanyia kazi kwelikweli kwa sababu ni suala ambalo halikuanza leo wala jana. Kwa hiyo, tupeni muda wa kulifanyia kazi tena kwa kasi inayostahili kwelikweli.

MHE. ESTHER KABADI NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, wawekezaji hawa tuliwakubalia waje kwetu ili walinde ajira za Watanzania, lakini wawekezaji hawa wamekuwa na tabia ya kuwaweka wataalam wetu wa Tanzania vibarua kila siku. Je Serikali inawasimamiaje Watanzania hawa ili waepukane na hiyo athari ya kuwekwa vibarua kila siku wasiajiriwe kama wao wanavyokuja na watu wao kutoka nje?

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyawazwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nilikuwa napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, tumeleza katika jibu la msingi kwamba ni wataalam wacheche tu ambao wanaruhusiwa kisheria kuajiriwa moja kwa moja na Mwekezaji. Kumekuwa na tatizo katika utekelezaji wa Sheria na Utaratibu wa kuajiri wageni huko nyuma na kama tulivyoeleza kwenye hotuba yetu ya Bajeti hapa tumeiunda upya Kamati ile ya kuhakiki utoaji wa vibali vya nje na tumewaagiza Maafisa wa *Labour* katika kila mkoa kutuletea *report* ya robo mwaka juu ya wageni ambao wanafanya kazi katika mikoa yao na kwamba vibali vyao viko katika hali gani.

Kwa hiyo, suala hili kwa kweli tunalishughulikia kwa undani na tunatoa vivutio kwa wageni kuja kuwekeza nchini nchini moja ya sababu ikiwa ni kwamba wataongeza ajira kwa wataalamu wetu na, tunalichukulia hilo kwa uzito wake na tunazungumza na wawekezaji kwa karibu kabisa kuhakikisha kwamba hili linatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, tuliomba Bunge lako Tukufu litupe nafasi tukamilishe taratibu hizi ili mambo haya yaende sawasawa. (*Makofi*)

Na. 379

Matatizo ya Watumishi wa Hospitali ya Mirembe

MHE. WILLIAA H. SHELLUKINDO (K.n.y. MHE. BETRICE M. SHELLUKINDO) aliuliza:-

Serikali imeazimia kuboresha huduma za afya kwa wananchi kwa kuhakikisha kuwa huduma bora inatolewa pamoja na madawa ya kutosha na kwa vile Hospitali ya wagonjwa wa kichaa Mirembe inatoa huduma hiyo maalum:-

(a) Je, Serikali inasemaje kuhusu mazingira ya watumishi wa hospitali hiyo ambao wanafanyakazi katika mazingira ya hatari na hawana bima ya maisha yao?

(b) Je, Wizara ya Afya inasemaje kuhusu huduma ya wagonjwa wanaolazwa katika hospitali hiyo hasa kwa upande wa chakula ambapo wagonjwa wanashindwa kupata chakula cha kutosha na kwa viwango vinavyotakiwa kwa kuzingatia aina ya dawa wanayotumia kwa matibabu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa faida ya Bunge lako Tukufu naomba kwanza kwa ruksa yako nitoe ufafanuzi ufuatao kwa neno Kichaa kama utaniruhusu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu Ukurasa wa 157 neno Kichaa maana yake ni upungufu wa akili, wazimu, aliyepungukiwa na akili au mwendawazimu.

Mheshimiwa Spika, kwa maadili ya kitabibu wagonjwa hawa ambao wanajulikana na ni wagonjwa wa kichaa sisi huwa tunasema kwamba ni wagonjwa wenye matatizo ya akili kwa ujumla wao kwani watakapokuwa wanafika hospitalini ni vigumu kujua kwamba huyu ana upungufu wa akili au ni mwendawazimu.

Mheshimiwa Spika, hivyo ningepomba hawa wagonjwa ambao wanasemekana kama ni wagonjwa vichaa basi kama kuwaheshimu binadamu wenzetu tuwaite Wagonjwa wenye Matatizo ya Akili kama ambavyo Vipofu tunawaita ni Walemavu wa Macho, Vilema tunasema ni wenye Ulemavu wa Viungo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo Mbunge wa Kilindi naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wagonjwa wa akili ambao wana uwezekano mkubwa wa kufanya matukio ya hatari wana dalili ambazo zinatambulika kwa watalaam. Aidha zipo taratibu za kuwahudumia wagonjwa kama hao bila kuhatarisha usalama kwa watoa huduma. Mara nyingi madhara ya Wagonjwa hawa yanaweza kutokea iwapo tu watoa huduma watazembea taratibu za usalama.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Beatrice Shellukindo lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Motisha kwa wafanyakazi wa Hospitali ya Mirembe na wafanyakazi wengine wa Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii ni suala ambalo Serikali imelipa kipaumbele. Pamoja na ongezeko la mishahara la mwezi Januari 2006, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma bado inaendelea kuangalia namna

mbalimbali za kuboresha maslahi ya watumishi kwa kuzingatia mazingira ya kazi katika Sekta ya Afya. (*Makofi*)

Aidha, ipo tume ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoangalia namna ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi Serikalini kwa ujumla. Ni matarajio yetu kwamba suala la kuboresha maslahi ya watumishi kwa kuzingatia mazingira ya kazi katika Sekta ya Afya na ustawi wa jamii na Serikali kwa ujumla ikiwa ni pamoja na suala la Bima ya Maisha linafanyiwa kazi na kutolewa mapendekezo.

(b) Wizara yangu inatoa chakula cha kutosha na chenye lishe bora kwa Wagonjwa wa Akili katika Hospitali ya Mirembe. Aidha wagonjwa ambao hufikishwa hospitali wakiwa dhaifu sana, hupewa uji wa maziwa na yai moja kila siku ikiwa ni nyongeza ya mlo wa kawaida.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo katika Mkutano wa Tatu wa Bunge uliopita alitembelea mgonjwa kutoka kwenye Jimbo lake la Kilindi katika Hospitali hiyo ya Mirembe na alikwenda wakati wa saa za chakula na akashuhudia uduni wa chakula hicho.

Aidha, aliona vile mfanyakazi ambaye alivunjwa mkono na mgonjwa. Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba inaweza kuwa fedha nyingi zinatolewa lakini utekelezaji ukawa mbovu je atakubali kwamba ni vizuri kufanya ukaguzi wa ghafla yaani *Surprise* ili kuona kama kweli sera zinatekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo la nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa nakubaliana na Mheshimiwa Shellukindo kwamba pesa inaweza ikawa inatolewa nyingi lakini utekelezaji ukaleta matatizo na ninapenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba nakubaliana naye kwamba ninaweza nikaenda nikafanye ukaguzi wa papo kwa papo ili kuweza kuona hali halisi. (*Makofi*)

MHE. MWAKA ABDULRAHAMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa vitanda na mablanketi ya hospitali ya Mirembe ambayo wanalalia hao Wagonjwa vimejaa chawa kiasi ambacho kinawaathiri wagonjwa hao.

Je, Wizara itawasaidiaje wagonjwa hao?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhan, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba inawezekana mablanketi na mashuka yakawa na chawa kama alivyosema na kama alivyoona alipokwenda kutembelea Hospitali ya Mirembe. Ninachotaka kusema ni kwamba kawaida na inavyotakiwa ni kwamba usafi wa mazingira ya hospitali ni kuanzia usafi wa mgonjwa pamoja na sehemu wanayolala. Sasa kama hayo mablanketi yana chawa basi inabidi hospitali na utawala husika uweze kufanya usafi. *(Makofi)*

Hivyo basi nataka kusema kwamba wale viongozi wa Hospitali ya Mirembe waangalie kwamba kama mablanketi na mashuka yana chawa ni wajibu wao kutafuta njia za kuua wadudu hao na si chawa tu bali pia na uchafu wote ambao uko katika hospitali ile unatakiwa kuwa katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Na. 380

Ujenzi wa Vyuo Kishapu

MHE. JAMES D. LEMBELI (K.n.y. MHE. FRED M. TUNGU) aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Kishapu ni moja ya Wilaya mpya na pia ni moja ya Wilaya zilizo nyuma kielimu. Haina shule za kutosha kulingana na watoto wanaomaliza darasa la saba na kwa kuwa wakati wa kampeni za uchaguzi wa 2005 Mheshimiwa Makamu wa Rais alitembelea Jimbo la Kishapu aliwaahidi wananchi wa Jimbo hilo kwamba, Serikali itajenga Chuo cha *VETA* Wilayani humo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kidharura wa kujenga Chuo cha *VETA* Wilaya ya Kishapu ili watoto wengi wanaomaliza darasa la saba waweze kuandaliwa kujiajiri au kupata ajira?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga Chuo cha Ualimu Mkoa wa Shinyanga ili kusaidia upatikanaji wa Walimu wa kutosha kwa ajili ya Mkoa huu unaokabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA): alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu, Mbunge wa Kishapu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali kwa sasa ni kuhakikisha kuwa kila Mkoa unakuwa na angalau Chuo Kimoja cha Ufundi Stadi kinachomilikiwa na *VETA*. Kwa hivi sasa kuna Vyuo vya Ufundi Stadi 21 katika Mikoa 18 nchini ukiwemo Mkoa wa Shinyanga. Mikoa ambayo haina Vyuo vya *VETA* ni Lindi, Pwani na Manyara.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuwa na Vyuo vya Ufundi Stadi katika kila Wilaya ifikapo mwaka 2010 kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Wizara yangu inaandaa mkakati wa utekelezaji wa mpango huo. Mkakati huo utakuwa ni pamoja na kushirikisha sekta zisizo za Serikali kuhakikisha kila Wilaya inakuwa na Chuo cha Ufundi Stadi ikiwemo Wilaya ya Kishapu.

(b) Mheshimiwa Spika, nchini kuna Vyuo vya Ualimu 52 vilivyosajiliwa na Vyuo 32 ni vya Serikali na 20 visivyo vya Serikali. Vyuo vya Ualimu vilivyopo ni vya kitaifa, ambavyo hupokea wanachuo kutoka Mikoa na Wilaya zote. Wahitimu kutoka Vyuo hivyo pia hupangwa katika Mikoa na Wilaya zote nchini. Kutokuwepo Chuo cha Ualimu Mkoa wa Shinyanga hokusababishi wanaohitimu elimu ya sekondari kutoka Mkoa huo kukosa nafasi ya mafunzo ya ualimu katika vyuo vilivyopo nchini na walimu wanaohitimu kutopangwa katika Mkoa huo wa Shinyanga. Serikali itakapokuwa na mpango wa kuongeza Chuo kingine cha Ualimu kipaumbele kitakuwa katika Mikoa ambayo haina Chuo cha Ualimu ukiwemo Mkoa wa Shinyanga.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa vile Wilaya ya Kahama yenye watu wasiopungua 650,000 pia haina Chuo cha *VETA*. Je, Serikali itawahakikishia wananchi wa Wilaya Kahama kama ambavyo amesema Naibu Waziri kwamba ifikapo mwaka 2010 nao watapatiwa Chuo cha *VETA*?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA): Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi Vyuo vya *VETA* ni vichache sana tunavyo 21 tu nchi nzima. Kuna Wilaya nyingi hazina, lakini kwa sababu Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaelekeza mwaka 2010 kila Wilaya angalau iwe na Chuo kimoja cha *VETA*. Sasa ni wajibu wa wananchi na Halmashauri zao waanze kupanga mipango ile watakayoona inafaa ili kila Wilaya iwe na Chuo chake cha *VETA*. Ni ushirikiano kati ya wananchi, Halmashauri pamoja na Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, hivyo tunamwomba Mheshimiwa Mbunge yeye mwenyewe aishirikishe Halmashauri yake na Waheshimiwa Madiwani wakae wapange waone ni jinsi gani watakavyopanga kuanzisha Chuo cha Ufundi cha *VETA* katika Wilaya yao ya Kahama.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la Vyuu vya *VETA* ni kubwa sana nchini, na Wilayani Bukombe tunao majengo yaliyokuwa yanatumiwa na Cogfa wakati wanajenga barabara ya kwenda Rwanda. Yale majengo mpaka sasa hivi yapo yamekuwa yakipokea watu hata Wilaya wakati inakuja kuanza yalitunza viongozi pale na sasa yako wazi. Je, Serikali iko tayari kuwasiliana na Wizara ya Miundombinu ili majengo yale yatumike kama Chuo cha *VETA* na hatimaye kujenga tu madarasa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA): Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anazungumza kwamba yapo majengo, lakini ni mali ya Wizara ya Miundombinu. Mimi ninadhani ni wakati muafaka Mheshimiwa Mbunge pamoja na Halmashauri waone jinsi ya kuweza kuwasilisha maombi katika Wizara ya Miundombinu, wakague majengo hayo, ili waweze kuthibitisha kama yanafaa. Halafu Halmashauri ionyeshe mfano na nia ya kutaka kuanzisha chuo hicho. Halafu Wizara nayo itaona ni jinsi gani ya kuweza kusaidia katika wazo hili la kuanzisha Chuo cha katika Wilaya hii ya Bukombe.

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, ningependa kuongezea jibu katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, limekuwa ni jambo la kawaida katika Wizara yangu pale tunapojenga makambi na baadaye tukamaliza kujenga barabara na kuondoka kwamba mara nyingine makambi hayo huachwa kwa wenyeji ili wayatumie kwa namna inayofaa. Sasa kwa kuwa hayo ya Bukombe yalikuwa makambi. Ningeomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iyatathmini makambi hayo kuona kama yanafaa kufundishia ufundi na kama wakielewana na Halmashauri wote ni wadau, sisi tutafikiria kuyatumia majengo hayo kwa kazi za namna hiyo. (*Makofi*)

SPIKA: Ningependa tu kusema kwamba hii ni moja ya Wizara ambayo ina Manaibu Waziri wawili. Aliyejibu swali lililopita anaitwa Mheshimiwa Ludovick Mwananzila. Hii taarifa zaidi ni kwa ajili ya wageni sio kwa Waheshimiwa Wabunge. Sasa anayejibu ni Mheshimiwa Naibu Waziri mwingine ambaye ni Mwantumu Mahiza.

Na.381

Adhabu za Viboko Shuleni

MHE. DAMAS P. NAKAI aliuliza:-

Je, Serikali inasemaje kuhusu adhabu ya viboko mashuleni, hasa katika shule za msingi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 iliyotungwa na Bunge lako Tukufu kifungu cha 60(o) na kanuni inayohusu adhabu ya viboko ya mwaka 1979, adhabu ya viboko shuleni inaruhusiwa kwa makosa maalum.

Adhabu ya viboko hutolewa na Mwalimu Mkuu au Mkuu wa Shule au Mwalimu mwingine aliyeruhusiwa na Mwalimu Mkuu. Aidha, Waraka wa Elimu Na.24 wa mwaka 2002 unaohusu adhabu ya viboko unasisitiza kuwa mwanafunzi atachapwa si zaidi ya viboko vinne kwa wakati mmoja. Kumbukumbu kuhusu aina ya kosa, mtoa adhabu na aina ya viboko hutunzwa katika kitabu cha kumbukumbu cha shule.

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini ningependa niulize swali moja dogo la nyongeza. Kama alivyosema sheria hii ipo na inahitaji kwa kweli utekelezaji kwa umakini kabisa. Ningependa kuiuliza Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha au wa kufuatilia utekelezaji wa sheria hii kama ambavyo yeye mwenyewe amejaribu kuifafanua. Maana kwa kwa kweli inaelekea sheria hii haitekelezwi ipasavyo mara nyingine watoto hao wanaadhibiwa na walimu kwa kuchapwa viboko zaidi ya vinne hivyo vilivyosemwa.

Ni vipi Serikali sasa inadhibiti suala hili na sheria hii ikatekelezwa ipasavyo? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA): Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi viboko haviruhusiwi shuleni.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu kurudia tena ni pale tu itakapobidi ndipo taratibu zote zinapaswa zifuatwe.

Mheshimiwa Spika, yapo makosa ambayo mwanafunzi anaweza akaadhibiwa, lakini ni kwa utaratibu ulioelezwa. Nawasihi walimu pote nchini wasiwaadhibu wanafunzi bila kufuata utaratibu. Ni marufuku kutembea na kiboko, ni marufuku kumwadhibu mwanafunzi pasipo na sababu. Naomba pia ili kuepusha adhabu ya kiboko isitumie, wazazi wawe karibu na watoto wao kuwaelekeza maadili mema na kuwapa ushauri nasaha kuepuka wasiadhibiwe ovyo. *(Makofi)*

MHE. HAFIDHI ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ningemwomba Mheshimiwa Naibu alijulishe Bunge lako Tukufu kwa vile kuna utaratibu wa kuchagua walimu katika kuwachapa viboko wanafunzi. Hivi kuna vigezo gani vya walimu hawa kupewa nafasi kama hiyo na wengine kuachwa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA): Mheshimiwa Spika, katika sheria ya mwaka 1978 imeeleza wazi kwamba mwanafunzi msichana ataadhibiwa na mwalimu wa kike, endapo shuleni hapo hakuna mwalimu wa kike, Mkuu wa shule ataelekeza ni nani wa kuadhibu ama yeye mwenyewe au atayekuwa ameidhinishwa na Mkuu wa Shule.

Na. 382

Barabara ya Zamahelo – Kinyamshindo

MHE. PASCHAL C. DEGERA aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Zamahelo –Farkwa- Kwamtoro – Kinyamshindo ni sehemu ya barabara ya Zamahelo – Singida na kwa kuwa, sehemu ya barabara kati ya Zamahelo na Kinyamshindo ni mbaya sana na inapitika kwa shida sana:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia matengenezo makubwa sehemu ya barabara hiyo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, Mbunge wa Kondoia Kusini, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Barabara za Zamahelo – Farkwa – Kwamtoro – Kinyamshindo yenye jumla ya urefu wa kilometa 125.1 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara ya Miundombinu kupitia Wakala wa Barabara Mkoani Dodoma. Barabara hii inaishia mpakani mwa Mkoa wa Dodoma na Singida ambapo inaungana na barabara ya Mkoa wa Kinyamshindo kwenda Kititimo Mkoani Singida yenye jumla ya urefu wa kilometa 47.31.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa barabara hii, Serikali imekuwa ikiipa kipaumbele cha matengenezo mwaka hadi mwaka kama ifuatavyo:-

Sehemu kati ya Zamahelo na Kwamtoro yenye jumla ya urefu wa kilometa 84 ilifanyiwa matengenezo makubwa (*rehabilitation*) kwa gharama ya shilingi bilioni 1.3 ambayo yalikamilika mwaka 1996. Matengenezo hayo yamefuatiwa na matengenezo ya Muda Maalum (*Periodic Maintenance*) ambayo yalifanyika katika sehemu hii katika mwaka 2001/2002 katika jumla ya urefu wa kilometa 36 kwa gharama ya shilingi milioni 151.7.

Sehemu iliyobaki kati ya Kwamtoro na Kinyamshindo imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya Maeneo korofi (*Spot Improvement*) na matengenezo ya muda Maalum (*Periodic Maintenance*) ambapo hadi kufikia mwaka wa fedha wa 2005/2006 jumla ya urefu wa kilometa 20.43 zimetengenezwa kwa gharama ya shilingi milioni 249.761.

Aidha, pamoja na matengenezo ya kiwango kikubwa yanayozingatiwa kama nilivyoainisha, sehemu ya barabara hiyo yenye hali nzuri na wastani yenye jumla ya urefu wa kilometa 95 imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya kawaida (*Routine and Recurrent Maintenance*) na Matengenezo ya Dharura (*Emergency Repairs*) kila inapohitajika ili kuhakikisha kuwa barabara hiyo inapitika katika kipindi chote cha mwaka.

Aidha, kutokana na umuhimu wa barabara hii, Serikali itaendelea kuipa kipaumbele cha kuifanyia matengenezo makubwa, matengenezo ya maeneo korofi na ya muda maalum kulingana na upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, mpango wa kuifanyia matengenezo barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwa sasa hivi haupo kwa sababu Serikali imetoa kipaumbele matengenezo ya aina hiyo kwa barabara Kuu (*Trunk Roads*) zinazounganisha Mikoa na nchi jirani kwanza, kutokana na ufinyu wa Bajeti.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Naibu Waziri mwenyewe amekiri kwamba hii barabara ama sehemu ya barabara hii ilitengenezwa kwa kiwango cha changarawe miaka 10 iliyopita na sehemu iliyobaki haijafanyiwa matengenezo makubwa; na kwa kuwa hivi sasa barabara hii imeharibika sana. Je, Naibu Waziri aone kwamba kuna haja sasa ya kuanzisha mradi mpya ili barabara yote itengenezwe kutoka Zamahelo mpaka Singida ili iweze kupitika kwa urahisi?

La pili, kwa kuwa Wizara ya Miundombinu inashughulika na mawasiliano; na kwa kuwa hivi karibuni Kampuni ya *Celtel* imeanza kujenga mnara pale Farkwa. Je, Wizara itakubaliana na ombi la wananchi kwamba isaidie kuhimiza Kampuni hiyo iweze kujenga minara ya kutosha ili kuweza kuwa na mawasiliano ya simu za mikononi katika Vijiji vyote vya Babayu, Makorongo, Ubunko, Donsee, Farkwa, Mombose, Ubutole, Polo, Pangumu, Kwamtoro, Msera, Ilasee, Magambua, Ovada, Mengu, Kinyamshindo na Makiungu? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema na kama nilivyosema kwenye jibu la msingi barabara hiyo ilifanyiwa matengenezo makubwa miaka kumi iliyopita.

Mheshimiwa Spika, lakini nimesema tumekuwa tukifanya matengenezo katika barabara hiyo kwa vipande vipande kutokana na ufinyu wa Bajeti, na kwa kweli barabara hiyo inapitika. Mimi mwenyewe wiki moja na nusu iliyopita nilipokuwa natoka Singida nilipita kuikagua barabara hiyo na inapitika. Kuna maeneo korofi ambayo na mimi nimeendelea kumwagiza Meneja aendelee kuangalia utaratibu wa kuyafanya matengenezo. Ni kweli kwamba kama kungekuwepo na fedha tungeweza kufanya matengenezo makubwa kama yale ya mwaka 1996. Lakini kwa muda huu kabla ya fedha hizi hazijapatikana Mbunge atuvumilie tuendelee kufanya haya matengenezo madogo madogo hasa katika sehemu korofi.

Kuhusu swali la pili, kwamba *Celtel* wameanza kuweka mnara. Kwanza namshukuru kwamba amekubali kwamba *Celtel* wamefika huko na sisi tutafikisha ujumbe huu kwa *Celtel* ili mnara walioanza kuweka, basi waendelee kuweka minara mingine katika maeneo hayo aliyoyataja kutegemea jinsi wao watakavyoona inafaa kibiashara.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa katika Wilaya ya jirani ya Manyoni, kuna barabara mbaya sana na hii ni barabara inayotoka Nkonko- Njeje na Njeje mpaka Manyoni kiasi cha kwamba magari mara nyingine hulazimika kuikwepa barabara na kupitia katika mapitio ya ng'ombe; na kwa kuwa Barabara hii inategemewa sana na wafugaji na wakulima wa maeneo hayo kupeleka mazao yao katika masoko ya Mji wa Manyoni. Je, Wizara ina mpango gani wa kuweza kutengeneza hii barabara ambayo inategemewa sana na wananchi wengi?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA): Barabara aliyoitaja kwa sababu ameitaja hapa ndani ya Bunge, basi nitalichukua suala hilo kwanza nimwelekeze Meneja wa Mkoa wa Singida akague barabara hiyo aone maeneo korofi ambayo kwa kweli yanazuia usafiri wa watu pamoja na mifugo, ili tuone tunaweza tukafanya nini kurekebisha hali hiyo kwa muda mfupi na vilevile baadaye tuangalie kwa muda mrefu tunaweza tukafanya nini.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa matatizo na ukorofi wa barabara ya Jimbo la Kondo Kusini ni sawa na kule Kusini hasa

kwenyewe katika barabara ya Kibiti- Lindi ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri anaifahamu sana. Kipande korofi katika Daraja la Mkapa mpaka Somanga ambapo Wizara inasema kwamba *contractor* amepatikana, lakini kwa sasa hivi ni mahali pabaya sana sana. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana mipango gani kuhakikisha mpaka Mwezi Novemba, mwaka huu tuwe tunaweza kupitia na kukwepa yale mabwawa yaliyopo katika barabara hii?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA): Mheshimiwa Spika, ni kweli siku za karibuni Waheshimiwa Wabunge wa kutoka Kusini akiwemo Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir na wengine wameniletea malalamiko ya barabara hiyo hasa sehemu hiyo baada ya daraja la Mkapa. Kama tulivyokwisha jibu katika Bunge hili barabara hiyo iko katika matarajio ya kujengwa kwa kiwango cha lami. Lakini kwa sababu utaratibu huu utachelewa kidogo kwa miezi kadhaa kutokana na *process* tu ya ile *procurement*. Nimeahidi kwamba nitamwelekeza Meneja wa Mkoa wa Pwani aitembelee barabara hiyo haraka sana na nitafanya kazi hiyo leo, ili akague maeneo korofi sana yaweze kushughulikiwa wakati huu wa kiangazi ili barabara hiyo iweze kupitika.

Na. 383

Mizani ya Kupima Magari

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwapo na Vituo vya Mizani kwa ajili ya kupima magari na ukusanyaji wa ushuru wa barabara:-

- (a) Je, Serikali inaweza kuonyesha ni asilimia ngapi ya mabasi makubwa yanayolipa ushuru huo kwa kila mwezi?
- (b) Je, ni vigezo gani vinavyotumika kutoza ushuru wa barabara?
- (c) Je, ni kiasi gani cha fedha kinachopatikana kutokana na ushuru wa barabara kwa mabasi makubwa?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kwanza kutoa maelezo ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna vituo vya mizani ya kudumu na ya kuhamishika vipatavyo 23 katika Mkoa wa Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Mbeya, Shinyanga, Mara, Kagera, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mwanza, Ruvuma, Lindi na Pwani.

Kusudi la vituo hivyo vya mizani ni kusimamia na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara zetu. Lengo ikiwa ni kuzilinda barabara ili zisiharibike haraka kutokana na magari mazito yanayozidi kiwango kilichowekwa kwa mujibu wa sheria.

Magari ambayo ni lazima kupima ni yenye uzito wa jumla (*Gross Vehicle Mass*) kuanzia tani 3.5 na kuendelea yakiwa ni magari ya mizigo pamoja na mabasi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haitozi ushuru kwenye vituo vya mizani bali hutoza tozo ambayo kusudi lake ni kusaidia kufidia uharibifu wa barabara ambayo itakuwa imeharibiwa kutokana na uzito wa magari na mizigo.

Wizara yangu imekuwa ikipima uzito bila kutenganisha aina ya magari. Magari makubwa ya mizigo na mabasi yote hupimwa na kati ya hayo, asilimia 7.65 hutozwa tozo kwa kuzidisha uzito.

(b) Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumiwa kutoza tozo za barabara ni kama vinavyoelezwa kwenye kanuni 114(i) p (*maximum weight of vehicle Regulation 114(i) p of 2001*, Sheria ya Usalama Barabarani Na.30 ya mwaka 1973 *The Road Traffic (Maximum Weight of Vehicles)* ya mwaka 2001 ambayo imeweka viwango vya uzito wa kila aina ya gari vinavyoruhusiwa kwa kila *axle* na uzito wa gari lote pamoja na mizigo (*gross vehicle mass*).

(c) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa katika kipengele (a), Wizara hutoza tozo kwa uharibifu wa barabara kwa magari yote bila kutenganisha magari makubwa ya mizigo na mabasi. Kiasi cha fedha zinazopatikana kutokana na tozo kwa mwezi ni wastani wa shilingi milioni 259.

Kiasi hiki cha fedha hukusanywa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) na fedha hizo hupelekwa moja kwa moja kwenye Mfuko wa Barabara (*Road Fund Board*) na baadaye hugawiwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Namshukuru pia Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa kumekuwepo na mtindo wa baadhi ya mabasi kujaza mizigo au abiria au yote mawili kwa pamoja kupitia kiasi na wanapofika karibu na vituo vya mizani, mabasi hayo huwashusha abiria na kuwavusha kwa kutumia daladala.

Je, Serikali inasema nini kuhusu hilo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA): Mheshimiwa Spika, hilo alilolisema ni kweli linatokea na tumekuwa tukilikemea sana.

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue fursa hii niweze kulijulisha Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba kitendo cha wenye mabasi kuzidisha mizigo na abiria na kisha kabla ya kufika kwenye mizani kuwashusha baadhi ya abiria na kupanda kwenye basi baada ya kupitia kwenye mizani ni kitendo ambacho kinavunja sheria. Tunawaomba wananchi waweze kushirikiana na Wizara yetu kwa kutoa ripoti ya vitendo kama hivi ili wenye mabasi husika tuweze kuwachukulia hatua za kisheria.

Suala hili limekuwa likizungumzwa sana na nadhani sasa imefika muda jamii ishirikiane na Wizara katika kutokomeza tabia hii. Kwa sababu barabara hizi tusipozitunza kwa kweli tutakaoumia ni sisi kama nchi.

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza.

Je, Serikali inaweza kuweka *check up* baada vya vituo vya mizani ili kuhakikisha kwamba wale abiria wanaoongezeka baada ya gari kupitia kwenye mizani wanakamatwa na hivyo kusaidia kuzuia vifo vingi vinavyotokea wakati wa ajali?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA): Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwa kweli Wizara imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kujaribu kuzuia hali hiyo.

Lakini ningeshauri vilevile kwa kweli wananchi tushirikiane. Mimi nadhani kama wananchi wakishirikiana na kutoa taarifa, hata hiyo ya kuweka kituo kingine cha pili baada ya kupitia kwenye mizani kuangalia nani tena wamepanda gari kisingeweza kuwepo.

Lakini Wizara itachukua hatua zote ambazo zinahitaji ili kuweza kuwakamata hao wanaohusika. Tukichukua hatua wengine watajaribu kujirekebisha. (*Makofi*)

Na. 384

Kilimo cha Umwagiliaji

MHE. LAUS O. MHINA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Nne, inazungumzia suala la Kilimo hususan cha Umwagiliaji; na kwa kuwa, katika Jimbo la Korogwe Vijijini yapo mabonde mengi yanayofaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji na yanafaa yaingizwe kwenye *National Irrigation Master Plan* yakiwemo Bonde la Mkomazi na Bonde la Magoma:-

Je, Serikali haioni kuwa, sasa umefika wakati muafaka wa kuboresha mabonde hayo ili yaweze kutumika kwa Kilimo cha Umwagiliaji hususan Kilimo cha Mpunga kwa kipindi chote cha mwaka?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Laus Omari Mhina, Mbunge wa Korogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yote yanayofaa kuendelezwa katika Bonde la Mkomazi yameainishwa katika Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji wa 2003 (*National Irrigation Master Plan (NIMP)*). Kinachofanyika sasa ni kuendeleza maeneo hayo kwa awamu kufuatana na upatikanaji wa fedha. Skim zilizokwishaendelezwa na Serikali ni pamoja na Mombo (220ha), Magoma (350ha), Makorora (250ha) na Kwemazandu (180ha).

Aidha, katika Mwaka wa 2004/2005 Wizara yangu ilikamilisha usanifu wa bwawa la Mkomazi linalotarajiwa kujengwa katika *Chamamba Gorge* kwa gharama ya shilingi bilioni 11.6. Fedha hiyo ikipatikana itatumika kujenga miundombinu ya umwagiliaji, kujenga uwezo wa wakulima na kuhifadhi mazingira. Bwawa hilo likikamilika litakuwa na uwezo wa kumwagilia hekta 16000. Maombi ya fedha yamewasilishwa kwa mhisani, *Millenium Challenge Corporation (MCC)* ambaye tayari ameonyesha nia ya kusaidiana na Wizara yangu inaendelea kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maeneo yote katika Bonde la Mto Mkomazi yamekwisha ainishwa katika *National Irrigation Master Plan (NIM)*, hatua inayofuata sasa ni kuibua miradi na kuiingiza katika Mipango ya Maendeleo ya Wilaya ya Korogwe (*DADPs*) ili iweze kuombewa fedha za utekelezaji kutoka katika Kapu la Mfuko wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*ASDP- Basket Fund*).

Kama nilivyokwisha sema huko nyuma katika *ASPD*, sekta ndogo ya umwagiliaji imetengewa takriban shilingi trilioni 1.4. Nimekwishaijeleza Ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda ya Kaskazini iliyoko Mjini Moshi, kuisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe katika mchakato wa kuibua miradi ya umwagiliaji inayofaa kuingizwa katika *DADPs*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa Halmashauri zote hasa nchini kuibua miradi ya kilimo na kutumia fursa hii ya *ASDP Basket Fund*.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Ninayo matangazo.

Kwenye ukumbi wa wageni Mashuhuri wa Mwenyekiti (*Speaker's Gallery*) tunafurahi kumtambua Mama Janet Magufuli, mkewe Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi amekuja na watoto wao wawili Jurgen na Jesca.

Karibuni sana tunafurahi sana kuwaona hapo na nadhani ndio mwendelezo wa kumsaidia Mzee katika harakati hizi ngumu. (*Makofi*)

Pia katika *gallery* kuna mumewe Mheshimiwa Joyce Masunga, anaitwa Meja Mstaafu Mohamed Ndaro, yule pale amevaa suti. Taarifa nilizonazo ni kwamba alikuwa muhimu sana kwa kumwezesha Mheshimiwa Masunga kuweza kufika humu Bungeni kwa sababu ni mahiri sana kwa kampeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Faida Bakar, anaye mgeni wake ambaye ni Mheshimiwa Abdul Khamis Feruzi. Karibu sana Mheshimiwa Feruzi. Naona anashangiliwa sana kwa sababu yeye alikuwa Mbunge katika Bunge lililopita na hivi sasa ni Mjumbe wa *NEC*. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge wa Manyoni yaani Manyoni Magharibi Mheshimiwa Lwanji na Manyoni Mashariki Mheshimiwa Capt. John Chilligati, ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Diwani Charles Mongo. Naomba wasimame tafadhali. Wale pale upande wa kushoto. Ahsante sana. (*Makofi*)

Ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Pia upande wa kulia wapo Madiwani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa ni wageni wa Mheshimiwa Mbunge wa jimbo hilo ambaye ni Waziri wetu wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Msolla. Madiwani naomba msimame, wale pale Madiwani wa Kilolo. (*Makofi*)

Karibuni sana tunashukuru sana ujio wenu hapa. (*Makofi*)

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Fatma Mikidadi yeye anaitwa Omar Salum Chitanda wa Lindi ni kiongozi wa siku nyingi amekaa katika vyama mbalimbali CCM, *NCCR-MAGEUZI*, CHADEMA. Loo!!! Yuko wapi sijui?

Yule pale. Alianzia CCM akaenda *NCCR-MAGEUZI* halafu CHADEMA, sasa amerudi tena CCM. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Masha ni Mheshimiwa Elirehema Kaaya, ni kiongozi kutoka Nyamagana, Mwanza na ndiye aliyekuwa *Campaign Manager* wa kampeni za Mheshimiwa Mbunge wa Nyamagana, ambaye sasa ni Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Yule pale. (*Makofi*)

Karibu sana na natumaini uliyemfanyia kampeni hakukusahau.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama Mheshimiwa George Mkuchika, Kapteni Mstaafu, anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwamba leo saa 5.00 asubuhi katika ukumbi Namba 219 watakuwa na kikao kifupi.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mwenyekiti Kamati ya Miundombinu, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu wakutane leo saa 7.00 mchana chumba Namba 428.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 7.00 mchana chumba kimegongana basi Katibu atawasaidia sidhani kama itakuwa 428 kwa sababu muda ni ule ule wa Kamati ya Miundombinu labda ikiwa wanakutana kwa pamoja, lakini kama ni Kikao tofauti basi saa 7.00 mchana jengo la Utawala wataelekezwa chumba cha kufanyia mkutano.

Mheshimiwa Dr. Zainab Amir Gama, Mwenyekiti wa *APNAC*. Kutakuwa na kikao cha *APNAC* kuendelea kujadili maandalizi ya Mkutano Mkuu wa *GOPAC* utakaofanyika Arusha tarehe 18 – 24 Septemba, 2006. Kikao hicho kitafanyika saa 7.00 katika Ukumbi wa zamani za Bunge. Mnaombwa Wajumbe wote wa *APNAC* tafadhali mhudhurie kikao hiki muhimu.

Mheshimiwa Athumani Janguo, Mwenyekiti wa Wabunge wote wa Mkoa wa Pwani, anaomba Wabunge wa Mkoa wa Pwani wakutane leo baada ya Kikao cha Bunge cha asubuhi kule kwenye jengo la Utawala.

Mwisho, Mheshimiwa William Shellukindo Mratibu wa zoezi la kulenga shabaha anatangaza kwamba tarehe 12 Agosti, 2006 kutakuwa na zoezi la kulenga shabaha huko Makutopora. Usafiri utakuwapo Ofisi ya Bunge saa 7.00 mchana. Wale wanaopenda kushiriki wajiorodheshe kwenye meza ya *Order Paper* ukumbi mpya wa Bunge.

Hayo ndiyo matangazo yetu ya leo na sasa nitamwita Katibu kwa shughuli inayofuata. (*Makofi*)

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Kuhusu utaratibu.

Kanuni ya 38 ibara ndogo ya kwanza. Naomba kusoma Mheshimiwa Mwenyekiti.

SPIKA: Endelea Mheshimiwa Mbunge !!!!

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Kanuni yenyewe inasema, na ninanukuu: “Baada ya muda wa Maswali kwisha Mbunge yeyote aweza kutoa Hoja kuwa Bunge liahirishe shughuli zake kama zilivyoonyeshwa katika Orodha ya Shughuli ili lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa Umma”.

Mheshimiwa Spika, jambo halisi na la dharura kwa Umma wa Watanzania linahusu filamu ya *Darwins Nightmare*. Kwa hivyo ningepomba Mheshimiwa Spika, kupitia kifungu hicho tuweze kulijadili jambo hili. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, haina haja ya kuungwa mkono kwa Kanuni hiyo. Ila tu nataka niombe muda kidogo wa kutafakari kulingana na mpangilio wa shughuli za leo hapa Bungeni na ninadhani ninaweza kulipatia nafasi wakati fulani.

Lakini ningepomba kwanza tuendeleo na shughuli zingine zilizopangwa kwenye *Order Paper* kwanza.

MISWADA WA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria Kwa ajili ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa 2006
(The Local Authorities Pensions Fund Bill, 2006)

Muswada wa Sheria ya Udhhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu wa Mwaka 2006
(The Anti-Money Laundering Bill, 2006)

Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho kwenye Sheria Mbalimbali wa mwaka 2006
(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2006)

Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2006
(The Local Government Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2006)

(Miswada iliyotajwa hapojuu ilisomwa Bungeni kwa mara ya Kwanza)

HOJA ZA SERIKALI

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naomba usubiri Mheshimiwa Waziri.

Kwanza Mheshimiwa Kagasheki anaomba Wabunge wote wa CCM kutoka Mkoa wa Kagera, wakutane hivi sasa pale Kantini. Pili, kutokana na shughuli ambazo zinanikabili inanibidi nibadilishane Kiti na Mheshimiwa Ndugai, ili asimamie shughuli zitakazoendelea. Kwa hiyo, nitamwomba sasa asogee ili aweze kuchukua Kiti hadi hapo baadaye.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuchaguliwa kuwa Wabunge na kukutana hapa leo hii katika Bunge lako Tukufu la Awamu ya Nne. Ninazidi kuwapongeza Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Aman Abeid Karume kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nakupongeza wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika, Samwel Sitta na Naibu Mwenyekiti Mheshimiwa Anna Makinda, na Manaibu wote na Wenyeviti wote kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge hili kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje kwa ushauri maoni na maelekezo ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa katika maandalizi ya hotuba hii na kuiwekea vipaumbele vya kiutendaji kwa kipindi cha bajeti hii. Kama ilivyo ada, Bunge lako Tukufu limekwishapokea na kuzingatia misingi ya Jumla ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2006/2007, kupitia Hotuba za Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezesaji. Nawapongeza na kuwashukuru wote kwa Hotuba zao nzuri. Kufuatia misingi hiyo ya jumla, Hoja yangu itajielekeza katika kuainisha malengo na mikakati ya utekelezaji katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, naomba kutoa Hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2006/2007. Wizara yangu inaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ambayo ni kusimamia Sera na Sheria za Ardhi katika utoaji, uhifadhi na utumiaji endelevu wa ardhi nchini, upimaji ardhi na uhifadhi wa alama za mipaka kati ya nchi yetu na nchi jirani, kutafsiri mipaka ya maeneo mbalimbali ya kiutawala (ya mikoa, wilaya, kata na vijiji) nchini mwetu, uendelezaji makazi endelevu mijini na vijijini na kuwaendeleza kitaaluma na kiutumishi wafanyakazi wa Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya Shilingi 9,043,330,000 kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Juni 2006, Wizara imekusanya jumla ya Shilingi 9,482,723,630 ambazo ni sawa na asilimia 105 ya lengo. Kati ya makusanyo hayo, Shilingi 8,494,039,762 ambazo ni sawa na asilimia 90 ya makusanyo, ni kodi ya pango la Ardhi itokanayo na viwanja pamoja na mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati mbalimbali imekuwa ikitumiwa na Wizara kwa lengo la kuboresha makusanyo. Mikakati hiyo ni pamoja na: Kuendelea kuboresha hazina ya kumbukumbu za ardhi. Kuongeza idadi ya mashamba na viwanja vilivyopimwa nchini. Kuhamasisha ukusanyaji zaidi wa kodi ya pango la ardhi katika Halmashauri za Miji na Wilaya nchini kote. Kujenga uwezo na kuboresha vituo vya makusanyo kwa kuvipatia vifaa mbalimbali zikiwemo kompyuta na programu ya kukadiria kodi, kutunza kumbukumbu na kujibu hoja mbalimbali. Kutambua miliki za ardhi katika maeneo yaliyojengwa kiholela mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mikakati mbalimbali ambayo imekuwa ikitumika kwa lengo la kuongeza makusanyo, sasa hivi Wizara imejizatiti katika kuboresha kumbukumbu za umiliki wa ardhi. Katika kufuatilia walipa kodi, imebainika kuwa kumbukumbu za walipa kodi kwenye Halmashauri nyingi zina upungufu. Kwa vile kumbukumbu sahihi za umiliki wa ardhi ndiyo msingi wa ukusanyaji kodi, Wizara imeagiza Halmashauri zote ziwasilishe orodha ya viwanja vilivyopimwa, wamiliki wake, ukubwa wa viwanja husika, matumizi yake na viwango vya kodi kwa kila mita mraba. Hadi Juni 2006, Wizara imepokea taarifa kutoka Halmashauri 115. Pamoja na mambo mengine, kumbukumbu hizi zitasaidia kukadiria makusanyo halisi yanayotarajiwa kupatikana katika miaka ijayo. Naziagiza tena Halmashauri zote ambazo hazijawasilisha taarifa kufanya hivyo kabla ya tarehe 31 Agosti, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 11,722,395,044 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 2,100,000,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika tengeo la fedha za Bajeti ya Kawaida, Shilingi 2,380,235,044 zilitengwa kwa ajili ya Mishahara na Shilingi 9,342,160,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Fedha hizi zilikuwa kwa ajili ya kutekeleza malengo mbalimbali ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2005/2006 yalikuwa yafuatayo: Kuongeza ufanisi na kiwango cha makusanyo ya maduhuli yatokanayo na huduma za ardhi. Kutoa Elimu kwa Umma juu ya Sera, Sheria na Kanuni za Ardhi. Kutayarisha, kusajili na kutoa Hatimiliki za Ardhi, Vyeti vya Ardhi ya Vijiji, na Nyaraka nyingine za Kisheria. Kujenga mfumo wa mawasiliano wa Wizara ili kuunganisha mifumo iliyopo ya kila idara kwa lengo la kurahisisha mawasiliano (*Ministry of Lands Information System (MOLIS)*).

Kuimarisha mipaka ya kimataifa, upimaji mipaka ya vijiji, viwanja mijini, utayarishaji ramani pamoja na kujenga uwezo wa matumizi ya teknolojia ya kisasa katika upimaji kwenye ardhi na majini na utayarishaji wa ramani. Kuandaa mipango ya muda mfupi na mrefu ya uendelezaji wa miji, kuhuisha Sheria ya Mipango Miji na Vijiji (Sura ya 378) ya Mwaka 1956 na Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Na.3 ya Mwaka 1984 kwa lengo la kuandaa Sheria ya Mipango ya Miji na Vijiji, na Sheria ya Kusimamia Taaluma ya Mipangomiji. Kutambua na kurasimisha maeneo yaliyojengwa kiholela na kuyatolea Leseni za Makazi. Kufanya utafiti kuhusu vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu, teknolojia rahisi za ujenzi na kusambaza matokeo

yake kwa kuendesha semina na mafunzo kwa vitendo. Kukusanya kodi ya pango la nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*), kujenga nyumba mpya za kuuza au kupangisha kwa kushirikiana na sekta binafsi na kuzifanyia matengenezo nyumba zilizopo. Kuboresha mazingira ya kazi na kuendeleza taaluma za watumishi wa Sekta ya Ardhi; na, Kuimarisha ofisi za Sekta ya Ardhi nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza malengo yaliyotajwa, hadi kufikia mwezi Juni 2006, Wizara ilikuwa imepokea kutoka Wizara ya Fedha Shilingi 11,722,395,044 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 500,000,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kazi zilizotekelezwa katika mwaka wa fedha 2005/2006 ni pamoja na: Kutoa miongozo mbalimbali inayolenga kuboresha ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na huduma ya ardhi, na kukagua vituo 31 vya makusanyo ambavyo ni Tanga, Pangani, Muheza, Lushoto, Handeni, Korogwe, Baraza la Ardhi na Nyumba Moshi, Hai, Moshi Mjini, Moshi Vijijini, Same, Mwanga, Arusha, Baraza la Ardhi na Nyumba Arusha, Arumeru, Kiteto, Loliondo, Monduli, Morogoro, Mvomero, Ifakara, Ulanga, Kilosa, Kilombero, Mahenge, Mkuranga, Kisarawe, Mbeya, Mbeya Vijijini na Dar es Salaam. Wizara imetoa msukumo wa pekee katika kuimarisha vituo vya makusanyo katika Manispaa za Morogoro na Moshi, Jiji la Arusha, Mwanza na Mbeya kwa kuwapatia mafunzo, vitendea kazi, programu ya kukadiria kodi pamoja na kuwaunganisha kwenye mtandao wa mawasiliano ya kompyuta (*Wide Area Network (WAN)*).

Elimu juu ya Sera, Sheria na Kanuni za Ardhi ilitolewa kwa wadau mbalimbali wakiwemo baadhi ya Wabunge, viongozi wa baadhi ya Mikoa, Wilaya na Halmashauri, na kwa njia ya uchapishaji, na usambazaji wa Sheria za Ardhi, Kanuni zake na kushiriki katika maonyesho mbalimbali. Jumla ya Hati miliki 5,488 za Ardhi pamoja na Hakimiliki 1,088 za Kimila na nyaraka mbalimbali 9,354 zilisajiliwa. Jumla ya miliki 347 za viwanja na mashamba zilibatilishwa na kumilikishwa kwa waombaji wengine. Uthamini wa nyumba na mali 4,941 ulifanyika na kuiingizia Serikali Shilingi 202,155,088. Wizara imeteua Makandarasi watatu wa kujenga mfumo wa mawasiliano ya nje ya Wizara (*WAN*), kuunganisha mifumo ya habari ya Idara zote. (*Ministry of Lands Information System - MOLIS*) na mfumo wa masijala ya ardhi inayotumia teknolojia ya kompyuta (*Computerised Movable Shelves*).

Jumla ya ramani za msingi kwa miji 38 katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na Kagera zimekamilika. Upimaji picha (*Ground Photo Control*) ulifanyika katika Mikoa ya Iringa (miji 6) Mbeya (miji 11), Kagera (miji 3), Kigoma (miji 10), Tabora (miji 9) na Rukwa (miji 4). Vijiji 119 vilipimwa Mkoani Iringa katika Wilaya za Njombe (43), Mufindi (13), Iringa Vijijini (55) na Kilolo (8). Viwanja 30,633 vilipimwa Jijini Dar es salaam. Aidha, kazi za Upimaji zenye viwanja 21,710 mashamba 1,631 na vijiji 232 zilipokelewa toka Halmashauri mbalimbali na kazi zilizoidhinishwa ni viwanja 17,262, mashamba 660 na Vijiji 311. Rasimu ya Programu ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Songwe imekamilika na imebainisha miradi mitano ambayo utekelezaji wake utasaidia kuimarisha mpaka kati ya Tanzania na Malawi. Mawasiliano yanaendelea kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji. Mipango ya Muda Mfupi ya Matumizi ya Ardhi Mijini (*Interim Urban Land Use Plans*) kwa miji ya Babati, Mererani, Ushirombo, Misungwi, Tandahimba, Tunduru na Namtumbo imekamilika. Mipango ya kimkakati ya

kuendeleza miji ya Lushoto na Masasi nayo imekamilika. Aidha, zoezi la ukusanyaji takwimu kwa ajili ya mpango wa kimkakati kwa mji wa Bukoba na mpango wa uboreshaji mji wa Chalinze umekamilika.

Uhuishaji wa Sheria ya Mipango Miji na Vijiji (Sura ya 378) ya Mwaka 1956 na Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Na.3 ya Mwaka 1984 umefanyika na miswada itawasilishwa Bungeni hivi karibuni. Michoro 102 ya mipangomiji yenye viwanja 45,411 vilivyobuniwa iliidhinishwa kutoka katika Halmashauri za miji mbalimbali. Sampuli 40 za michoro ya nyumba ziliandaliwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba katika miji. Sampuli hizi zitapunguza gharama za kutengeneza ramani na zitauzwa kwa wananchi kwa bei nafuu. Aidha, mpango wa uendelezaji upya maeneo ya katikati ya Jiji la Tanga na mji wa Singida umeandaliwa.

Wizara imefanya uhakiki wa miliki na kufanya usaili wa wamiliki 27,000 katika maeneo yaliyojengwa kiholela ambao taarifa zao zilikuwa hazijapatikana. Aidha, wakazi 30,212 wamepatiwa leseni za makazi Jijini Dar es Salaam. Jumla ya shilingi 338,826,618 zimekusanywa kutokana na kodi ya pango la ardhi na ada ya leseni. Semina za uhamasishaji na mafunzo ya vitendo kuhusu ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu zilifanyika katika Wilaya za Mvomero, Babati, Handeni, Kilindi, Namtumbo, Kasulu, Kinondoni, Ilala, Temeke, Singida Mjini, Singida Vijijini na Ileje. Pia, utafiti wa mashine za kufyatua matofali yanayofungamana (*Hydraulic type*) umekamilika.

Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) limefanyia matengenezo jumla ya majengo 1,481, kukamilisha ujenzi wa nyumba 148 za makazi za kuuza, majengo 8 makubwa ya biashara na kukusanya kodi ya pango Shilingi 18 bilioni hadi Juni, 2006. Watumishi 260 wa Serikali wamepatiwa mikopo yenye jumla ya Sh. 1,187,715,960 ya kujenga nyumba kutoka kwenye Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali (*Revolving Housing Loan Fund*). Mazingira ya kazi yaliboreshwa na watumishi 135 waliwezesha kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi. Aidha, Watumishi wapya 84 wameajiriwa na watumishi 43 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo katika kipindi husika. Mashauri 4,105 yalifunguliwa katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Kati ya hayo, mashauri 2,073 yalisikilizwa na kutolewa maamuzi. Pia, mashauri 131 kati ya 211 yaliyokuwepo katika Baraza la Usuluhishi wa Ardhi yalisikilizwa na kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2006/2007 unalenga katika kutekeleza MKUKUTA na ibara ya 42 na 68 za Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 ikiwa ni pamoja na kurasimisha ardhi na nyumba, kupima mipaka ya vijiji na kuwapatia wananchi hati za kimila za kumiliki ardhi na kuwawezesha wananchi kuwa na makazi bora. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha utawala bora katika Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa rasilimali ardhi katika kuwapunguzia wananchi umasikini, Wizara yangu itaendelea na utoaji na uhakiki wa hatimiliki, utwaaji ardhi kwa manufaa ya umma, ukaguzi na uhakiki miliki kwa ajili ya utatuzi wa migogoro kiutawala, usajili wa hatimiliki pamoja na nyaraka mbalimbali,

utoaji vibali vya uwekaji rehani hakimiliki za ardhi na uhamisho wa miliki, uthamini wa mali na utoaji elimu kwa umma kuhusu Sheria za Ardhi. Aidha, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Halmashauri katika umilikishaji ardhi na ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na huduma za ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea na jukumu la kusimamia utoaji miliki kupitia Halmashauri za Miji na Wilaya. Katika kutekeleza majukumu hayo, imebainika kuwa katika Halmashauri nyingi, sekta ya ardhi haitengewi fedha, kuna uhaba mkubwa wa watumishi wenye sifa, ofisi na vitendea kazi. Hali hii inasababisha utunzaji hafifu wa kumbukumbu, ukusanyaji mdogo wa mapato, utoaji huduma hafifu ikiwemo miliki pandikizi (*double allocation*), ucheleweshaji wa kutoa hati za kumiliki ardhi na usumbufu wa mara kwa mara kwa wananchi. Wizara yangu itaendelea kushauriana na TAMISEMI kuhusu namna bora ya kuziwezesha Halmashauri ili ziweze kutekeleza majukumu yaliyokasimiwa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia inao wajibu kisheria wa kutoa miliki za ardhi yenye ukubwa wa kuanzia hekta tano na kuendelea, ukanda wa pwani (fukwe), visiwa vidogo, ardhi ya uwekezaji chini ya Kituo cha Uwekezaji (*Tanzania Investment Centre (TIC)*), Taasisi za Serikali, viwanja kwa ajili ya Balozi mbalimbali na maeneo ambayo matumizi yake ni ya manufaa kwa Taifa kama vile viwanja vya ndege na migodi. Aidha, Wizara inapokea hati kutoka katika Halmashauri zote nchini kwa ajili ya kuzihakiki, kuzisaini na kuzisajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2006/2007, hatimiliki za ardhi 6,000 na nyaraka mbalimbali za kisheria zinatarajiwa kusainiwa. Aidha, hati za mashamba yaliyotolewa kwenye ardhi ya vijiji katika kipindi cha kuanzia tarehe 01/05/1999 na baadaye Halmashauri kuandaa hati, zinahitaji kufanyiwa utaratibu wa ziada ili ziweze kukamilishwa kwa mujibu wa Sheria. Kimsingi, hati hizi zilitakiwa ziandaliwe kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 5 ya Mwaka 1999 ambayo inataka milki za ardhi ya vijiji zitolewe, zisainiwe na kusajiliwa katika ngazi ya vijiji na wilaya. Kutokana na uwezo mdogo wa Serikali wa kuweka miundombinu ya kutosha kutekeleza kazi hiyo katika ngazi hizo, Wizara imekuwa ikihawilisha ardhi husika kutoka ardhi ya kijiji kuwa ardhi ya kawaida (*general land*) ili kuwezesha hati hizo kukamilishwa chini ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara yangu imeendelea kushughulikia utatuzi wa migogoro mbalimbali ya ardhi nje ya taratibu za Mahakama na Mabaraza ya Ardhi. Katika mkoa wa Dar es Salaam, ukaguzi wa viwanja, uhakiki wa milki na utatuzi wa migogoro ya viwanja uliendelea katika maeneo ya Tegeta, Mbezi na Tabata. Mkoa mingine iliyotembelewa ni Pwani, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Mara na Mtwara. Malengo ya kazi hizi ni kuendelea kujenga hazina ya kumbukumbu sahihi za miliki za Ardhi, kuhakikisha usalama wa miliki na uendelezaji ardhi kwa amani na usalama, kutekeleza taratibu za kisheria zilizowekwa za kufuta miliki za viwanja ambavyo havijaendelezwa kwa muda mrefu kwa kusudio la kuvitoea kwa wananchi wengine wenye nia na uwezo wa kuviendeleza kwa wakati kulingana na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kupambana na wimbi la migogoro, kamati za kusikiliza na kutatua migogoro kiutawala zimeundwa nchi nzima chini ya ofisi za Wakuu wa Wilaya. Hivyo natoa wito kwa wananchi wenye malalamiko halali kuzingatia utaratibu huu kwa kuwasilisha malalamiko yao kwenye kamati hizo. Kamati hizo zitashughulikia migogoro ambayo haijafikishwa kwenye vyombo vya kisheria. Vilevile, natoa wito kwa wananchi wanaomiliki ardhi kuzingatia masharti ya uendelezaji, ili kuepuka migogoro na uvamizi wa ardhi iliyomilikishwa. Serikali haitasita kufuta miliki za viwanja vilivyoachwa muda mrefu bila kuendelezwa. Kwa kuzingatia tamko la Serikali lililotolewa hivi karibuni, Katika Mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu itaendelea kufuta miliki za viwanja ambavyo havijaendelezwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara yangu imebatilisha miliki 347 za viwanja na mashamba katika mkoa mbalimbali na imeidhinisha vibali vya uhamisho wa miliki 648 na vibali vya rehani 307 nchini. Pia, katika kipindi hicho, mashauri 73 yanayohusu Wizara yangu yalishughulikiwa na Mahakama Kuu – Kitengo cha Ardhi. Lengo ni kuhakikisha kuwa ardhi inaendelezwa kwa wakati kulingana na masharti ya uendelezaji. Aidha, Wizara yangu imeendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu Sera na Sheria za Ardhi kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara imeweza kusajili hatimiliki na nyaraka mbalimbali 14,842 za kisheria. Kati ya hizo, zimesajiliwa hatimiliki 5,488 za ardhi na nyaraka nyinginezo 9,354. Chini ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 Wizara yangu inawajibika kusimamia Masjala za Ardhi za Vijiji kupitia Masjala za Wilaya. Kwa lengo hilo, Wizara imekuwa ikisimamia uzinduzi wa utoaji na usajili wa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji na Hatimiliki za Kimila katika ngazi za Wilaya na Vijiji. Utoaji wa vyeti vya ardhi ya Vijiji na ujenzi wa masjala za mfano ngazi ya Wilaya na kijiji umeendelea katika Wilaya mbalimbali nchini. Tangu zoezi lianze, jumla ya Masjala za Wilaya nne na Masjala za Vijiji 17 za mfano zimezinduliwa. Jumla ya Vyeti vya Ardhi ya Vijiji 202 vimetolewa na Hatimiliki za Kimila 1,262 zimesajiliwa. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Masjala za Ardhi za Wilaya 2 na Masjala za Ardhi ya Vijiji 10 zilizinduliwa katika Wilaya za Handeni na Babati. Aidha, Vyeti vya Ardhi ya Vijiji 189 vilitolewa na Hatimiliki za Kimila 1,126 zilitolewa kwa Wanavijiji. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu inatarajia kuzindua Masjala za Ardhi za Wilaya 10 na za Vijiji 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia ina jukumu la kuthamini nyumba na mali nyinginezo kwa madhumuni mbali mbali yakiwemo ya; kulipa fidia, kutoza kodi ya ardhi, mauzo (*transfer*), meзания (*balance sheet*), kuweka rehani au kuombea mkopo na mirathi. Hadi kufikia mwezi Juni, 2006 Wizara imethamini nyumba na mali nyingine 609 ambazo zimeingizia Serikali ada ya uthamini ya Shilingi 35,889,630. Pia, Wizara katika kipindi hicho ilipokea na kupitisha jumla ya taarifa za uthamini 4,332 kutoka makampuni binafsi ya Uthamini na Halmashauri za Miji na Wilaya na kukusanya ada ya uhakiki (*approval fees*) ya Shilingi 166,265,458. Vile vile, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara imeweza kuthamini nyumba na mali nyingine za Balozi za Tanzania kwa madhumuni ya kuziua au kuzinunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ikiwa ni msimamizi wa taaluma ya uthamini, imeendelea na jukumu la kujenga hazina ya kumbukumbu za uthamini (*Valuation Data Bank*) kwa lengo la kuwezesha uthamini wa mali kufanyika kulingana na viwango vya bei ya soko. Hadi Juni, 2006, utayarishaji wa programu ya kutunzia takwimu umekamilika na zoezi la kuingiza takwimu za viwango vya thamani ya mali katika kompyuta litafanyika katika mwaka wa fedha 2006/2007. Zoezi la kuhuisha viwango vya thamani ni la kudumu na litaendelea kila mwaka kwa vile thamani ya ardhi na majengo katika soko hubadilika kadri miaka inavyopita. Kwa mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara imejiwekea lengo la kuthamini nyumba na kuhakiki taarifa za uthamini kutoka kwa makampuni binafsi pamoja na Halmashauri za Miji na Wilaya kadri maombi yatakavyowasilishwa Wizarani. Utunzaji na Upatikanaji wa Kumbukumbu za Ardhi na Upanuzi wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imetoa kipaumbele katika kuboresha mifumo ya habari na mawasiliano kwa lengo la kuboresha huduma kwa wananchi. Mikakati inayotekelezwa ni kuweka mtandao wa mawasiliano ya mbali (*WAN*) utakaounganisha Wizara na Ofisi za Usajili wa Hati za Kanda, kuboresha tovuti ya Wizara (www.ardhi.go.tz) ili kuunganisha Wizara na Ofisi za Ardhi katika Halmashauri, kujenga Mfumo wa habari na kumbukumbu za ardhi wa Wizara (*MOLIS*) na kujenga mfumo wa kisasa wa masjala ya ardhi (*Computerised Movable Shelves*). Sambamba na juhudi hizo, Wizara imeendelea kuboresha mifumo ya kufuatilia barua za wananchi, mienendo ya majalada ya viwanja na mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za michoro ya upimaji (*Survey Registration System*). Juhudi zote hizi zinalenga kuboresha huduma zitolewazo na Wizara kwa wananchi na kupunguza kero katika mfumo mzima wa uandaaji na umilikishaji wa ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za kuimarisha matumizi ya kompyuta makao makuu, Wizara yangu imeazimia kusambaza taaluma na matumizi ya kompyuta katika Ofisi za Ardhi za Halmashauri. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara iliendesha mafunzo kwa watumishi 10 na kupeleka vifaa vya kompyuta pamoja na mfumo wa ukadiriaji na utunzaji wa kumbukumbu za kodi ya pango la ardhi vyenye thamani ya jumla ya shilingi milioni 250 kwa Halmashauri za Mbeya, Mwanza, Arusha, Morogoro na Moshi. Hadi kufikia Juni 2006, taarifa za viwanja (*plot details*) 200,000 na ramani 20,000 zimeingizwa katika kompyuta; walipa kodi 78,000 katika mkoa wa Dar es Salaam, 24,500 Jiji la Mwanza, 15,400 Manispaa ya Arusha, 7,500 Manispaa ya Moshi, 14,500 Jiji la Mbeya na 13,000 Manispaa ya Morogoro wametambuliwa na taarifa zao zimehifadhiwa kwenye kompyuta. Katika Ofisi za Usajili wa Hati, jumla ya taarifa za hati 38,340 zimeingizwa kwenye kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu inategemea kukamilisha ujenzi wa mtandao wa mawasiliano, uboreshaji wa tovuti ya Wizara, mfumo wa hazina ya kumbukumbu za ardhi pamoja na mfumo wa masijala ya ardhi unaotumia kompyuta. Pia, Wizara itaendelea kuboresha kumbukumbu za ardhi pamoja na mkakati wa kuziwezesha ofisi za Ardhi za Halmashauri zetu kuongeza

matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa lengo la kuboresha huduma na kupanua wigo wa makusanyo ya maduhuli yatokanayo na huduma za ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inasimamia utekelezaji wa Sheria ya Mahakama za Ardhi Na 2 ya Mwaka 2002 (*The Land Disputes Courts Act, 2002*) ambayo imeanza kutumika tarehe mosi Oktoba, 2003. Sheria hii inaeleza mamlaka na majukumu ya vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba vilivyotajwa katika Sheria za Ardhi za Mwaka 1999. Vyombo hivyo ni Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Mabaraza ya Kata yanayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yanayosimamiwa na Wizara yangu na Mahakama Kuu - Kitengo cha Ardhi na Mahakama ya Rufaa chini ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Mfumo huu mpya wa utatuzi wa migogoro unaoanzia ngazi ya kijiji, una lengo la kutatua migogoro haraka na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara yangu imeendelea kuimarisha Mabaraza 23 ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yaliyoundwa katika mwaka wa fedha 2004/2005. Kwa kuwa vyombo hivi ni vipya na uwezo wa Serikali ni mdogo, Mabaraza haya yamepatiwa ofisi za kufanyia kazi ndani ya majengo ama ya ofisi za Wakuu wa Mikoa au Wilaya. Hata hivyo, Wizara imelazimika kukarabati ofisi hizo ili ziweze kukidhi mahitaji ya Baraza. Aidha, Wizara imeweza kuyapatia samani na vitendea kazi muhimu ikiwa ni pamoja na kompyuta kwa kila Baraza na magari kwa Mabaraza ya mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Mbeya. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu inatarajia kuunda Mabaraza 7 ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika Wilaya zenye migogoro mingi ili kuwapunguzia Wananchi gharama za kusafiri umbali mrefu hadi Makao Makuu ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imechapisha na kusambaza nchi nzima nakala 13,200 za Sheria Na. 2 ya Mwaka 2002. Vilevile, imeandaa Mwongozo wa Sheria hiyo kwa madhumuni ya kutoa elimu kuhusu mfumo mpya wa utatuzi wa migogoro ya ardhi. Jumla ya nakala 10,000 za Mwongozo zimechapishwa na tayari zimesambazwa katika Mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Rufaa la Ardhi limeongezewa muda wa mwaka mmoja kuanzia Januari hadi Desemba, 2006 kusikiliza rufaa ambazo hazikumalizika katika kipindi cha mpito cha miaka miwili, yaani Oktoba 2003 – Septemba 2005. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yalipokea jumla ya mashauri 4,105 na kati ya hayo mashauri 2,073 yamesikilizwa na kutolewa uamuzi. Mashauri 3,510 yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi nchini yana migogoro ya ardhi, ambayo inaweza kupatiwa ufumbuzi katika ngazi ya Vijiji na Kata. Hata hivyo, imebainika kuwa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Mabaraza ya Kata ama hayajaundwa au yameundwa bila kuzingatia Sheria Na. 2 ya Mwaka 2002. Kutokana na upungufu huo, wananchi wanalazimika kusafiri hadi kwenye ngazi ya Mkoa ambako kuna Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Huu ni usumbufu na kero kwa wananchi na ni kinyume na matakwa ya Sera ya Taifa ya Ardhi. Natoa rai kwa Halmashauri zote ziunde Mabaraza ya Ardhi ya

Vijiji, kufufua na kuimarisha Mabaraza ya Kata kwa madhumuni ya kuwaondolea wananchi usumbufu na kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inaendelea na jitihada za kwenda pamoja na teknolojia ya kisasa katika masuala ya upimaji ardhi, utayarishaji wa ramani za nchi na utunzaji wa kumbukumbu zitokanazo na kazi hizi. Hatua hii imeiwezesha Wizara kuongeza tija katika upatikanaji viwanja nchini, utayarishaji ramani, utoaji plani za hati, kutatua migogoro ya mipaka ya viwanja na mashamba na kutoa ramani kwa ajili ya upangaji wa Matumizi Bora ya Ardhi na Hifadhi ya Mazingira. Teknolojia ya kisasa inasaidia kuhuisha ramani haraka kwa kuonyesha mabadiliko juu ya ardhi, raslimali na miundombinu iliyopo tayari na hivyo kuwezesha kubuni, kuamua, kupanga, kutekeleza na kuratibu mipango mipya ya maendeleo ya Taifa katika sekta zote kwa ufanisi. Katika kujijengea uwezo wa utayarishaji wa ramani kwa teknolojia ya kompyuta, Wizara yangu imenunua vifaa maalum (*Scanner* na *Digital Photogrammetric Workstation*), ili kuweza kutumia picha za anga na za satellite katika mifumo ya kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ramani za msingi za nchi huonyesha umbile la uso wa nchi na uoto asilia, miundombinu na maendeleo yaliyofanyika kwenye ardhi. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu ililiahidi Bunge lako tukufu kuwa itakamilisha uchoraji wa ramani za msingi za miji 38 katika kanda ya Ziwa Victoria. Aidha, itawianisha picha na ardhi (*ground photo control*) katika miji 35 kanda ya Magharibi iliyopigwa picha za anga mwaka 2004/2005 na kuingiza ramani zipatazo 1,263 za uwiano wa 1:50,000 kwenye kompyuta ili ziweze kutumiwa kwa ufasaha zaidi katika mifumo ya mipango ya maendeleo na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa uchoraji wa ramani za miji 38 katika kanda ya Ziwa Victoria na uwianishaji picha na ardhi katika miji 35 kanda ya Magharibi uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, miji 4 zaidi katika Mkoa wa Mbeya na miji 3 katika Mkoa wa Kagera ilifanyiwa uwianishaji wa ardhi na picha kwa kutumia picha za anga za mwaka 1999 za mradi wa Usangu *Wetlands Catchment Area* za mwaka 2006. Kwa sasa kazi ya miji 43 imefikia hatua ya uchoraji wa ramani. Wizara yangu ilitoa zabuni kwa Kampuni ya Kimataifa kupiga picha za anga na kutayarisha *digital orthophotos* kwa eneo lote la Jiji la Dar es Salaam. Kutokana na kuwepo kwa ukungu angani katika msimu wa upigaji picha Julai – Oktoba 2005, mkandarasi alifanikiwa kupiga picha nusu tu ya eneo la mkataba. Kazi hii ilisitishwa kusubiri msimu mwingine wa kupiga picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utayarishaji wa ramani mpya na uhuishaji wa zile za zamani ni kazi ya kudumu kwa sababu sura ya nchi na uoto juu yake hubadilika mara kwa mara kutokana na maendeleo ya binadamu. Mwaka huu wa fedha Wizara yangu inatarajia kupiga picha za anga na kutayarisha *digital orthophotos* za Jiji la Mbeya na Manispaa ya Morogoro kwa ajili ya kuendeleza mradi wa kupima viwanja. Picha hizo pia zitafaa kwa ajili ya kudhibiti ujenzi holela. Baada ya kukamilika upigaji picha katika kanda ya Kusini, kanda ya Magharibi, kanda ya Ziwa na kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2006/2007 itapiga picha za anga katika kanda ya

Mashariki inayojumuisha miji 128 iliyopo katika mikoa ya Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Manyara, Arusha, Singida, Dodoma na sehemu ya Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inalo jukumu kubwa la kupima na kutayarisha ramani za maeneo ya Ardhi chini ya Bahari ya Hindi na Maziwa makuu. Kikwazo kinachoikabili Wizara yangu ni ukosefu wa uwezo katika vifaa vya msingi na wataalam wa kufanya kazi hiyo. Gharama ya mahitaji haya ni kubwa na msaada wa kiufundi na fedha kutoka ndani na nje ya nchi unahitajika. Kwa kutambua hilo, Wizara iliwasilisha pendekezo la mradi kwa Shirika la *International Hydrographic Organisation (IHO)* kwa ajili ya kuomba fedha. Wizara inaendelea kufuatilia maombi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wengi wanajitokeza kugharamia upimaji ardhi mijini na vijijini kutokana na kutambua manufaa ya kuwa na hati za kumiliki ardhi. Haya ni matunda ya juhudi za makusudi za Serikali kuelimisha na kutekeleza sera na mipango iliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2005 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA). Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara yangu ilipokea kazi za upimaji kutoka Halmashauri za Miji, Wilaya na Makampuni ya Wapima binafsi zinazojumuisha viwanja 21,710, mashamba 1,631 na vijiji 232. Kazi zilizoidhinishwa zinajumuisha viwanja 17,262, mashamba 660 na vijiji 311 Wataalam wa upimaji katika Halmashauri hawatoshi na vifaa vya upimaji vilivyopo ni duni. Hivyo, bado huduma za upimaji ardhi katika Halmashauri zetu ni duni pia. Natoa wito kwa Halmashauri zote kujenga uwezo wa upimaji ardhi ili kukidhi mahitaji ya upimaji viwanja na mashamba nchini. Pia, wananchi watumie wapima ardhi wa sekta binafsi kupima maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakadiriwa kuwa mahitaji ya viwanja mijini hivi sasa ni 500,000 kwa nchi nzima. Kero ya ukosefu wa viwanja mijini imeendelea kupungua kutokana na mafanikio ya Mradi wa Kupima Viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam ulioanza mwaka wa fedha 2002/2003 ukiwa na dhana ya uchangiaji wa gharama iliyoufanya mradi kuwa endelevu. Mpaka sasa viwanja 30,655 vimekamilika kupimwa Jijini Dar es Salaam kwa gharama ya Shilingi bilioni 29.7 ikiwa ni pamoja na gharama za fidia, upimaji, umilikishaji na barabara. Jumla ya viwanja 23,765 vimemilikishwa kwa wananchi na kuiingizia Serikali kiasi cha Shilingi 26,094,879,000 na uuzaji wa viwanja hivyo unaendelea. Mradi huu umefanikiwa kutokana na kutumia mbinu shirikishi katika mchakato mzima wa utekelezaji. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara imewezesha kupima viwanja 9,500 katika Jiji la Mwanza, viwanja 4,000 katika Manispaa ya Morogoro na viwanja 5,000 katika Jiji la Mbeya. Katika Jiji la Dar es Salaam Wizara, kwa kushirikiana na Manispaa ya Temeke, imelipa fidia ya jumla ya Shilingi 1.7bilioni kwa ajili ya kupima viwanja 5,000 katika eneo la Kibada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia upimaji wa viwanja katika miji iliyopatiwa fedha ili kuhakikisha kuwa upimaji wa viwanja vilivyokusudiwa unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utandawazi na maendeleo ya teknolojia Duniani yanalazimu kubadilisha mbinu na mikakati ya utoaji huduma za upimaji. Wizara yangu

imekwishaanza kuandaa mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu za upimaji wa ardhi kwa kutumia mfumo ya kompyuta (*Survey Registration System (SRS)*) ili kurahisisha rejea na matumizi mengine. Kwa Jiji la Dar es Salaam, asilimia 80 ya kumbukumbu za upimaji ardhi zilizopo zimeingizwa kwenye kompyuta. Wizara itaendelea kujenga hazina ya kumbukumbu za ardhi hadi kila kipande cha ardhi nchini kimebainishwa matumizi na umiliki wake. Aidha, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara itanza kutayarisha Sera na Sheria za Upimaji Ardhi kuendana na Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 na mabadiliko ya teknolojia Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianzisha Mfuko Maalum wa Kupima Viwanja (*Plot Development Revolving Fund (PDRF)*) mwaka 1993 kwa nia ya kuwezesha Halmashauri za Miji kukopa fedha hizo na kupima viwanja kwa mfumo wa wananchi kuchangia gharama na hivyo kuufanya Mfuko kuwa endelevu. Hadi sasa Wizara yangu imetoa mikopo kwa Halmashauri 31 yenye jumla ya Shilingi 385,889,813 lakini ni Halmashauri 10 tu ndizo zimekamilisha marejesho ya Shilingi 136,599,080.50 ya mikopo hiyo. Katika mazingira haya, Halmashauri zingine zinakosa fursa ya kutumia fedha ya mfuko huo kutokana na kuchelewa kwa marejesho. Wizara yangu imetembelea Halmashauri zote nchini zilizokopeshwa ili kutathmini utekelezaji wa miradi iliyoombewa mikopo na matatizo yanayosababisha kuchelewa kwa urejeshaji. Taarifa iliyopatikana inachambuliwa ili kupata mwelekeo wa kuboresha usimamizi na uendeshaji wa mfuko huu. Natoa wito kwa Halmashauri zote zinazodaiwa kuhakikisha kuwa zinarejesha fedha iliyokopwa ili mfuko uweze kuwa endelevu. Wizara inaendelea na zoezi la upimaji vijiji. Hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2004/2005 jumla ya vijiji 6,100 kati ya vijiji 14,000 nchini vilipimwa. Katika mwaka wa fedha 2005/06 kazi ya upimaji vijiji ilifanyika katika Mkoa wa Iringa ambapo jumla ya vijiji 119 vimepimwa. Vijiji hivyo vimepimwa katika wilaya za Njombe (43), Mufindi (13), Iringa Vijijini (55) na Kilolo (8). Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu imeweka lengo la kupima vijiji 3,000 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utawala bora linajumuisha uimarishaji wa usalama na amani kati ya nchi yetu na nchi jirani. Ili kutekeleza hili Wizara yangu, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, imeendelea kuhakiki mipaka ya nchi yetu ili kudumisha ujirani mwema. Kutokana na Serikali ya Comoro kuonyesha dalili za kurejea mazungumzo ya mpaka baharini kati yetu na wao, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2006/2007 itafanya mashauriano na Serikali za Comoro na Msumbiji kwa pamoja ili kuweka mpaka katika Bahari ya Hindi. Hilo likikamilika, Wizara yangu itawasiliana na Serikali husika ili kukamilisha protokali ya sehemu ya mpaka inayohusisha Tanzania, Comoro, Msumbiji na Shelisheli. Aidha, Wizara yangu itaendelea na majadiliano ya kuhuisha mipaka kati ya Tanzania na Malawi, Zambia, Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya matatizo ambayo hufikishwa mara nyingi Bungeni ni migogoro ya mipaka ya maeneo ya utawala hasa kati ya wilaya na wilaya. Baadhi ya migogoro ni ya muda mrefu na kila ikifanyiwa kazi na Wizara yangu bado inajirudia. Kutokana na uzoefu wa muda mrefu, wa kushughulikia migogoro ya mipaka hii imebainika kuwa chanzo kikubwa cha migogoro ya mipaka ni Mamlaka za Utawala

za Wilaya kutokufahamu wala kujishughulisha na mipaka rasmi ya maeneo yao hadi pale mgogoro unapozuka. Uongozi wa Wilaya kwa kutofahamu mipaka yake hupelekea utoaji huduma mbalimbali nje ya mipaka na hatimaye kusababisha migogoro ya kiutawala. Pia, Wananchi wasipofahamu mipaka rasmi, hutumia mipaka yao ya mazoea ambayo mara nyingi inatofautiana na mipaka rasmi iliyo katika matangazo ya Serikali (*Government Notices*). Aidha, Kamati za Ulinzi na Usalama za kila Wilaya zimekuwa hazitekelezi wajibu wake wa kufahamu mipaka rasmi ya wilaya zao. Hali hii inaonyesha kukosekana kwa usimamizi madhubuti na hivyo kufanya mipaka ya wilaya kukosa mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inachukua hatua za makusudi za kukusanya GN za Wilaya zote nchini na kuzisambaza ili kila Mkuu wa Wilaya awe na nyaraka hizo wakati wote. Kupitia Bunge lako Tukufu, ninaomba GN za mipaka ya utawala zihesabiwe kuwa ni mojawapo ya nyaraka za lazima katika makabidhiano kati ya Wakuu wa Wilaya wanapobadilishana madaraka. Iwapo kila Wilaya itatumia GN yake kutambua, kukagua, kufyeka, kuelimisha na kuonyesha Wananchi wanaoishi mpakani alama za mipaka, migogoro ya mipaka itapungua sana. Hata migogoro ikitokea inaweza kutatuliwa kiurahisi na wilaya zinazopakana na hivyo kuimarisha utawala na uongozi bora nchini. Natoa rai kwa Wakuu wa Wilaya nchini kuwa, mara wakipata nakala ya GN ya mipaka ya wilaya zao, wafanye mikutano ya ujirani mwema ili kujifahamisha na kutambua mipaka rasmi ya wilaya zao na kujiridhisha na tafsiri zake. Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo miji yake inakua kwa kasi. Katika kipindi cha miaka 26 iliyopita, idadi ya watu waishio mijini imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 8 kwa mwaka. Takwimu zinaonyesha kwamba mwaka 1967 nchi yetu ilikuwa na jumla ya watu 11,959,000 na kati ya hao asilimia 5.7 walikuwa wakiishi mijini. Kutokana na Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2002, Tanzania ilikuwa na watu 34, 443,603 ambapo asilimia 23 yao walikuwa wakiishi mijini. Kwa mwenendo huo ni dhahiri kuwa idadi na asilimia hiyo inazidi kuongezeka. Kwa sasa hivi asiimia 25 ya Watanzania wanaishi mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa inakadiriwa kuwa wastani wa asilimia 75 ya wakazi wa mijini huishi katika maeneo ambayo hayajapangwa na hayana huduma muhimu za makazi. Ili kukabiliana na ukuaji huu inabidi kuwepo na rasilimali za kutosha kutoa huduma bora kwa watu wanaoongezeka mijini. Inabidi Halmashauri za miji ziwezeshe ili ziweze kuboresha huduma muhimu kwa wakazi wa mijini. Pamoja na ukuaji wa miji pamekuwepo na mahitaji makubwa ya nyumba za kuishi ili kukabiliana na ongezeko la watu. Mpaka sasa mahitaji ya nyumba katika miji yetu yanakadiriwa kuwa ni nyumba 2,000,000 lakini nyumba zilizopo ni 1,448,000 tu. Kwa upande wa vijijini upungufu wa nyumba siyo mkubwa bali tatizo ni hali ya nyumba hizo kuwa duni. Kutokana na utafiti uliofanyika karibuni kuhusu hali ya nyumba za vijijini ni kuwa asilimia 52 ya nyumba zimejengwa kwa miti na tope, asilimia 41.2 zimezekwa kwa nyasi au makuti, asilimia 67 hazina msingi wakati asilimia 24 ni za sakafu ya udongo. Nyumba hizo hudumu kwa wastani wa miaka 5-7. Hali hii duni ya makazi nchini, imefanya Serikali kuchukua hatua mbali mbali kwa lengo la kuyaboresha. Katika uendelezaji wa miji Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya huandaa mipango ifuatayo ya kusimamia ukuaji na uendelezaji miji:-Mipango ya Muda Mfupi ya miaka 5 – 10 (*Interim Urban Land Use Plans*). Mipango Kabambe ya Muda

Mrefu ya miaka 10-20 (*Master Plans*). Mipango ya Kimkakati ya Kuendeleza Miji (*Strategic Urban Development Plans*). Mipango ya Uendelezaji Upya Maeneo ya Katikati ya Miji ya miaka 5 – 15 (*Redevelopment Plans*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia miaka ya 1960 hadi 1990 usimamiaji na ukuaji wa miji ulikuwa unaongozwa na Mipango Kabambe. Kuanzia Mwaka 1992 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za miji zilianza kuandaa Mipango ya Kimkakati ya Kusimamia Ukuaji na Uendelezaji Miji. Licha ya kuwa mipango hii ya kimkakati inaandaliwa kwa kushirikisha wadau wote, imeonekana kutokidhi mahitaji yaliyopo ya kusimamia ukuaji na uendelezaji miji. Mipango hiyo huchukua muda mrefu na gharama kubwa katika utayarishaji wake ukilinganisha na uwezo wa Serikali na hivyo kushindwa kutoa mpango unaotarajiwa kwa wakati. Kwa mfano, maandalizi ya mpango wa kimkakati wa jiji la Dar es Salaam umechukua muda wa zaidi ya miaka 10 na bado haujakamilika.

Kutokana na sababu nilizotaja, kuanzia mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu itaendelea kuandaa Mipango Kabambe (*Master Plans*) na Mipango ya Muda Mfupi (*Interim Land Use Plans*) ambayo itazingatia dhana shirikishi badala ya Mipango ya Kimkakati. Jukumu la kuandaa Mipango ya kuendeleza miji ni la Halmashauri lakini Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri hizo katika maandalizi haya mpaka zitakapokuwa na uwezo. Vijiji vingi hapa nchini vinakua na kuwa miji midogo. Kutokana na Tangazo la Serikali Na. 353 la Mwaka 2004 miji midogo 91 ilitangazwa. Miji midogo hii inatakiwa iandaliwe mipango ya kuongoza uendelezaji wake ili isikue kiholela. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara iliandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya muda (*Interim Urban Land Use Plans*) kwa miji ya Tandahimba, Tunduma, Namtumbo, Ushiroombo, Misungwi, Babati, Mererani na Masasi. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara itaandaa mipango ya namna hiyo kwa miji mingine nchini.

Aidha, Wizara itaanza kuandaa Mipango Kabambe (*Master Plans*) kwa Jiji la Dar es Salaam, Mwanza, na Miji ya Mtwara na Bukoba. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini ambazo zina vijiji vilivyotangazwa kuwa miji midogo kuandaa mipango ya kuendeleza miji hiyo ili isikue kiholela. Wizara yangu imekuwa ikiandaa Mipango ya Kimkakati ya Kuendeleza Miji (*Strategic Urban Development Plans*). Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Halmashauri za miji ya Lushoto na Masasi imetayarisha mipango ya namna hiyo kwa ajili ya kusimamia ukuaji na uendelezaji wa miji hiyo. Pamoja na utekelezaji wa kazi hizo Wizara yangu imekamilisha maandalizi ya mpango wa kuboresha miji wa Chalinze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya katikati ya miji huwa ni vitovu vya maendeleo ya miji hiyo. Katika maeneo hayo huwepo shughuli muhimu za biashara, makazi na ofisi. Maeneo hayo mara nyingi huwa na huduma muhimu na thamani ya ardhi huwa ni kubwa, hivyo kuna umuhimu wa kuyaendeleza upya wakati yanapochakaa ili yaweze kutekeleza majukumu yake. Kutokana na umuhimu huo Wizara imekuwa ikiandaa mipango ya kuendeleza upya maeneo yaliyochakaa ya katikati ya miji. Maandalizi ya mipango hii pia yanazingatia Sheria ya Mambo ya Kale Na. 22 ya Mwaka 1979 kwa kuzingatia maeneo na majengo yote yaliyopendekezwa kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara yangu ilishirikiana na Halmashauri za miji ya Singida na Tanga kuandaa mipango ya kuendeleza upya maeneo ya katikati ya miji hiyo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mpaka sasa maandalizi ya ramani za msingi za miji hiyo zimekamilika. Hatua zinazofuata ni kuandaa mipango yenyewe. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri husika kuandaa mipango ya kuendeleza upya baadhi ya maeneo kongwe katika Jiji la Dar es Salaam ambayo ni Upanga, Magomeni na Temeke pamoja na eneo la katikati la Mji wa Lindi. Aidha, katika kipindi hiki Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam itanza kutekeleza mpango wa kuendeleza upya eneo la Kurasini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekuwa ikipokea na kuidhinisha michoro mbalimbali ya mipangomiji kutoka kwenye Halmashauri. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara ilipokea michoro 113 na kuidhinisha michoro 102 yenye viwanja 45,411. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Wizara yangu ilikuwa na jukumu la kuhuisha Sheria ya Mipangomiji na Vijiji (Sura 378) ya Mwaka 1956 pamoja na Sheria ya Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Na.3) ya Mwaka 1984. Aidha, Wizara ilitakiwa kuandaa Sheria ya kusimamia taaluma ya Mipangomiji. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Waraka wa Baraza la Mawaziri umeandaliwa na inatarajiwa Miswada husika itawasilishwa Bungeni hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo ya Nyumba, mwaka jana Wizara yangu ililieleza Bunge lako Tukufu juu ya umuhimu wa kuwa na Sheria ya Nyumba (*Housing Act*) ili kuwezesha utekelezaji wa maamuzi mengi yaliyoko kwenye Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi. Kazi hiyo inatarajiwa kuanza katika mwaka huu wa fedha. Aidha, Wizara itashirikiana na Halmashauri za miji kuandaa michoro mbalimbali ya mifano ya nyumba ambayo ikitumika inaweza kupunguza gharama za ujenzi. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara, kwa kushirikiana na Halmashauri husika iliandaa michoro ya namna hiyo kwa miji ya Mwanza, Tabora, Dodoma, Mbeya na Dar es Salaam. Katika mwaka wa fedha 2006/2007, michoro ya namna hiyo itaandaliwa kwa miji ya Arusha, Moshi, Bukoba, Iringa, Mtwara na Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uhaba wa nyumba za kuishi kwa watumishi wa Serikali hasa walioko mijini, Serikali ilianzisha Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali chini ya Waraka wa Utumishi Na. 8 wa Mwaka 1992. Mikopo inayotolewa na Mfuko huu ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mpya, ununuzi wa nyumba, ukamilishaji wa ujenzi au ukarabati wa nyumba. Mfuko huu unasimamiwa na Wizara yangu na unaendeshwa chini ya Bodi ya Ushauri. Watumishi wa Serikali walioajiriwa kwa masharti ya kudumu na kuthibitishwa kazini wanastahili kuomba na kufikiriwa kupewa mikopo ya nyumba kutoka mfuko huu. Mikopo hii huchukuliwa kwa kuweka rehani hati miliki ya kiwanja au shamba. Muda wa marejesho ya mkopo ni miaka 5 hadi 30 na hutozwa riba ya asilimia 3 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali umeendelea kutoa mikopo kwa watumishi wa serikali kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba ili kuwawezesha kuwa na makazi bora na ya uhakika. Tangu mfuko uanzishwe mwaka 1992, hadi kufikia mwezi Juni, 2005 yamepokelewa jumla ya maombi 1,676 yenye thamani ya shilingi 9,532,893,371. Kati ya maombi hayo watumishi waliopewa mikopo ni 779 ambao ni sawa na asilimia 46 ya waombaji wote. Fedha zilizokopeshwa zilifikia shilingi 2,838,179,536. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara yangu ilipewa Shilingi Bilioni 2 kwa ajili ya kuongezea mtaji wa mfuko huu. Hadi kufikia mwezi Juni, 2006 Wizara ilikuwa imeidhinisha mikopo yenye thamani ya Shilingi 1,187,715,360 kwa watumishi 260. Kati ya watumishi waliopewa mikopo, wanawake ni asilimia 36 (Jedwali Na. 11). Marejesho katika mwaka wa fedha 2005/2006 yalikuwa ni Shilingi 140,172,057.96 sawa na asilimia 129.4 ya marejesho yaliyotarajiwa katika kipindi hicho. Kiasi hiki kimeweza kukusanywa kutokana na juhudi za Wizara katika kufuatilia mikopo na baadhi ya wakopaji kuamua kurejesha mikopo yao kwa mkupuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kutambua Miliki Kwenye Maeneo Yaliyojengwa Kiholela. Wizara yangu kwa kushirikiana na Manispaa za Jiji la Dar es Salaam inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kutambua Miliki Kwenye Makazi Yaliyojengwa Kiholela katika Jiji la Dar es Salaam ulioanza mwaka wa fedha 2004/2005.

Mradi huu ni jitihada za Serikali za kurasimisha rasilimali hizo na kuziingiza katika mfumo rasmi wa uchumi ili kuwawezesha wamiliki kupunguza umaskini. Utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huu ulikamilika Juni, 2005 na miliki 220,131 zilitambuliwa. Kati ya miliki hizo taarifa za wamiliki 194,251 zilihakikiwa na kumbukumbu zao kuingizwa kwenye kompyuta kwa Mitaa yote 180 iliyofikiwa katika zoezi hili. Takwimu hizi zimekabidhiwa kwa Manispaa zote tatu za Ilala, Kinondoni na Temeke kwa ajili ya kuwapatia wananchi Leseni za Makazi kwa mujibu wa Kifungu cha 23 cha Sheria ya Ardhi Na.4 ya Mwaka 1999. Hadi kufikia Juni, 2006 wamiliki 39,428 walikuwa wametayarishiwa leseni, kati yao 30,212 wamechukua leseni zao (Jedwali Na. 12a). Ntoa wito kwa wananchi ambao hawajachukua leseni wafanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wameshaanza kunufaika kwa kuzitumia leseni hizi kama dhamana Mahakamani, na kupata mikopo ya mafunzo kwa Wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu, biashara, n.k. Serikali pia inanufaika kwa kukusanya mapato kutokana na wamiliki kulipa pango la ardhi ambalo walikuwa hawalipi kabla ya utekelezaji wa Mradi huu. Hadi Juni, 2006 kiasi cha Shilingi 143,878,996 zilikusanywa kati ya Shilingi 792,471,600 zilizotarajiwa kukusanywa kama kodi ya pango la ardhi na ushuru. Vilevile, kiasi cha Shilingi 194,947,622 zilikusanywa kama ada ya leseni na fomu kati ya Shilingi 1,100,655,000 zinazotarajiwa (Jedwali Na. 12b). Ningependa kuziagiza Manispaa zote tatu kuongeza kasi katika kukusanya maduhuli husika. Ni kwa kufanya hivyo tu zitaweza kunufaika na mgao wa fedha wa asilimia 20 ya kodi ya pango la ardhi zitakazokusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huu katika Jiji la Dar es Salaam ambao utaendelea katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 unahusu

utambuzi wa miliki katika maeneo ya pembezoni mwa Jiji. Maandalizi ya kazi hii tayari yamefanyika ikiwa ni pamoja na kupiga picha za anga. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itaendelea kutekeleza mradi kama huu wa kutambua miliki katika miji mingine hatua kwa hatua kulingana na uwezo wa fedha. Urasimishaji wa maeneo haya utafanyika kwa kuyawekea huduma za kiuchumi na kijamii kupitia mpango shirikishi kama unaoendelea katika baadhi ya maeneo ya Jiji la Dar es Salaam, Manispaa ya Dodoma na katika Jiji la Mwanza ili kuboresha maeneo haya. Urasimishaji wa maeneo haya, utaongeza usalama wa miliki na kuboresha maeneo hayo, utazuia ujenzi holela na kupunguza umaskini hivyo kutekeleza mikakati ya kitaifa ya MKUKUTA na MKURABITA. Vilevile, utekelezaji huu ni njia mojawapo ya kufikia lengo la Kimataifa la Milenia la kuboresha hali ya wakazi milioni 100 wanaoishi katika maeneo yaliyojengwa kiholela mijini ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi. Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilianzishwa kwa Sheria Na. 3 ya mwaka 1984, ikiwa ni mshauri mkuu wa Serikali katika masuala ya matumizi ya ardhi. Nia ya Serikali ni kuwezesha kuwepo kwa mipango ya matumizi ya ardhi yenye uwiano na inayoshirikisha walengwa wote. Wadau wakuu wa Tume ni Wizara zile zinazohusika na usimamizi wa rasilimaliardhi, zikiwemo Wizara za Maliasili na Utalii, Kilimo na Chakula, Maendeleo ya Mifugo, Maji, Nishati na Madini. Wengine ni Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za msingi za Tume ni kuandaa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi, unaotoa dira ya Kitaifa ya mgawanyo wa matumizi makuu ya ardhi na Kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kanda inayoelekeza maeneo ya hifadhi, vijiji, kilimo, ufugaji, miundombinu na mengineyo ili kuondoa uhamiaji holela. Vilevile, Tume inaratibu na kuziwezesha Halmashauri za Wilaya na za Vijiji kutayarisha Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya na Mipango Shirikishi ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji inayoandaliwa na wanavijiji wenyewe. Mipango ya Wilaya inazisaidia Halmashauri za Wilaya kusimamia ardhi ngazi ya Wilaya na kufanya maamuzi yenye busara juu ya matumizi ya ardhi, kama vile kutenga maeneo ya ufugaji, uwekezaji, hifadhi za misitu, wanyamapori, n.k. Mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji ni nyenzo kuu ya usimamizi wa ardhi ya kijiji kwa Halmashauri za Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya ushirikishwaji jamii na kuandaa mipango ya uwiano (*Integrated Land Use Plans*) ndiyo inayoongoza mchakato wa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi hivi sasa. Kila Wilaya inatakiwa kuunda timu ya wataalam kutoka sekta mbalimbali, kwa ajili ya kuandaa mipango hii na kusimamia utekelezaji wake. Kazi ya Tume ni kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya na za Vijiji kwa kutoa miongozo, ushauri na mafunzo juu ya upangaji shirikishi wa matumizi bora ya ardhi. Chini ya utaratibu huu, wilaya 34 zimewezesha kuunda timu za wilaya na vijiji 38 vimewezeshwa kuandaa mipango shirikishi. Mwongozo wa Mipango Shirikishi ya Upangaji na Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi Vijijini na Mwongozo wa Utaarishaji wa Mipango ya Wilaya imeandaliwa na kusambazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2005/06 Wizara imeendelea kujenga uwezo kwa Halmashauri za Wilaya na za Vijiji wa kuaandaa na kusimamia utekelezaji wa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji. Timu za upangaji zimeundwa na kupatiwa mafunzo katika Wilaya za Kilwa, Same, Iramba na Kilolo, ambako mchakato wa upangaji umeanzishwa katika vijiji 7. Aidha, vijiji 11 vya mfano vimewezeshwa kukamilisha mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji katika Wilaya za Iringa, Mbozi na Masasi. Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Wilaya imekamilika kwa Wilaya za Handeni na Kilindi. Mipango hii iliyoandaliwa kwa kutumia mbinu shirikishi, itatumika kama mfano wa uandaaji wa mipango ya aina hiyo kwa Wilaya zingine nchini. Katika mwaka huo huo wa fedha Tume ilianza mchakato wa kutayarisha Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi. Mapendekezo ya awali juu ya Mpango huo yamewasilishwa na kujadiliwa na wadau mbali mbali. Mpango utakamilishwa katika mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imejiandaa kutekeleza Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji unaoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Lengo la mkakati ni kudhibiti uharibifu wa mazingira unaotokana na ufugaji kwenye vyanzo vya maji; kilimo kwenye miteremko ya milima, mabonde na vyanzo vya maji. Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inalo jukumu la kuratibu utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ambayo ni nyenzo muhimu katika kutimiza azma hii. Kazi muhimu zitakazofanywa na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ni pamoja na kufanya utafiti na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo ambayo kwa asili ni maeneo ya ufugaji, lakini wafugaji wanayahama na kuingia kwenye vyanzo vya maji. Lengo la mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo haya ni kuwezesha kuwepo kwa matumizi endelevu. Wilaya zitakazohusika ni pamoja na Manyoni, Dodoma Vijijini, Singida, Shinyanga, Ilemela na Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume itaratibu utayarishaji na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Wilaya na Vijiji katika Wilaya za Mbarali, Mbeya Vijijini, Chunya, Makete, Njombe, Iringa, Kilombero, Mvomero, Ulanga na Morogoro Vijijini. Aidha Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi itafanya utafiti ili kubaini na kushauri kuhusu maeneo mbadala yanayofaa kwa kupeleka wafugaji na wakulima watakaolazimika kuhama kutoka maeneo yaliyoharibika na ambayo yamehifadhiwa. Maeneo yatakayokubalika yataandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kuepusha kuhamisha tatizo la uharibifu kutoka eneo moja kwenda lingine. Maeneo hayo yatahusisha Wilaya za Lindi, Kilwa, na Nachingwea mkoani Lindi. Sanjari na shughuli hizo, Tume itafanya kazi ya kufuatilia mabadiliko ya matumizi ya ardhi nchini (*Monitoring of land use change*) ili kubainisha sababu na athari za mabadiliko hayo kwa matumizi endelevu ya rasilimali ardhi na hifadhi ya mazingira na kupendekeza hatua stahili za kukabiliana na athari za mabadiliko hayo. Shughuli hizi ni kubwa hivyo natoa wito kwa Wizara, Taasisi mbalimbali, Halmashauri za Wilaya na Vijiji kutoa ushirikiano kwa Tume, na kuipa kipaumbele mipango hii.

‘Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (*NHBRA*). Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi ulianzishwa tarehe 1 Septemba, 2001, kwa Sheria ya Wakala wa Serikali Na.30 wa Mwaka 1997. Jukumu kuu la Wakala ni kutafiti, kukuza, kushauri, kuhamasisha na kusambaza matokeo ya tafiti na utaalamu wa ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu ili kuboresha hali ya nyumba za kuishi na kuinua maisha ya wananchi mijini na vijijini. Katika mwaka wa fedha 2005/06 Wizara kupitia Wakala ilipanga kufanya kazi zifuatazo: Kuendesha semina za uhamasishaji wa ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu na kutoa mafunzo kwa vitendo katika wilaya tatu, kutangaza na kusambaza teknolojia za ujenzi kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushiriki maonyesho ya Kitaifa na Kimataifa, kufanya utafiti, ukandarasi, kupima udongo kwenye maabara na kutoa ushauri kuhusu ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza kazi zilizotajwa, Wakala uliendesha semina za uhamasishaji kwa Wananchi, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Madiwani, Wahandisi na Maafisa wengine. Aidha, mafunzo kwa vitendo (*practical training and demonstrations*) yaliendesha kwa wanavikundi vya ujenzi, wanaushirika wa akiba na mikopo, wananchi binafsi na wataalam mbalimbali. Kazi zilizotekelezwa ni kupima udongo na uimara wa vifaa mbalimbali vya ujenzi. Vilevile, utafiti wa mashine za kufyatua matofali yanayofungamana umefanyika ili kuziboresha kutoka aina ya manual kwenda aina ya hydraulic. Ili kuhakikisha kuwa teknolojia ya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu inafika kwa wananchi wote, Wakala ulitangaza huduma zake katika vyombo mbalimbali vya habari na kushiriki katika maonyesho ya Kitaifa na Kimataifa (Jedwali Na. 13).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wakala utaendesha semina za uhamasishaji wa ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, mafunzo kwa vitendo na maonyesho yatatolewa katika Halmashauri zilizohamasishwa. Vilevile, uhamasishaji na usambazaji wa teknolojia za ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu kwa njia za Redio, Magazeti na Televisheni utafanyika pamoja na kushiriki katika maonyesho ya Kitaifa na Kimataifa. Wakala utaimarisha miundombinu pamoja na maabara yake ya utafiti kwa kununua vifaa vipya. Napenda kutoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuwasiliana na Wakala kutumia teknolojia zake ili kuboresha makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma ya Shirika la Nyumba la Taifa. Shirika la Nyumba la Taifa limeendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Sheria Na. 2 ya Mwaka 1990. Majukumu hayo ni ya kujenga nyumba kwa ajili ya kupangisha au kuuza kwa wananchi; kusimamia nyumba au majengo yaliyopo na kuendesha shughuli za ujenzi kama Mkandarasi. Ili Shirika liweze kufanikisha hayo, sheria imetamka bayana kuwa ni lazima lijiendeshe kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya Shirika yanatokana na upangishaji, uuzaji wa nyumba na ukandarasi. Shughuli ya upangishaji ndiyo chanzo kikuu cha mapato ya Shirika ambacho kinachangia asilimia 88 ya mapato yake. Mapato hayo yametokana na

nyumba zake 16,021 za makazi na biashara zilizopo kwenye miji mbalimbali. Pamoja na ukweli kuwa kodi za nyumba za Shirika ziko chini ya kiwango cha soko, bado kuna tatizo la ulipaji kodi hizo. Baadhi ya wapangaji wamekuwa wakikaidi kulipa kodi za nyumba wanazopanga. Serikali imeliona tatizo hilo na hivyo mwezi Juni, 2005 Bunge lako Tukufu lilirekebisha na kufuta Sheria zilizokuwa zinawalinda wasiolipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho hayo yaliwezesha Shirika kukusanya kiasi cha Shilingi 19,260,840,032 sawa na asilimia 123 ya lengo la mwaka 2005/2006 katika kipindi cha Julai 2005 hadi Aprili 2006. Makusanyo haya yamepanda ukilinganisha na wastani wa asilimia 75 kwa kila mwaka katika miaka ya nyuma. Kutokana na mapato hayo Shirika limelipa Shilingi 1,528,777,788 ikiwa ni kodi mbalimbali za Serikali. Hivyo, kwa wapangaji wa Shirika kutokulipa kodi kwa wakati au kupinga kodi zinazopangwa na Shirika, ni sawa na kuzuia maendeleo ya wananchi wote. Shirika linatarajia kurekebisha viwango vya kodi za nyumba zake katika mwaka wa fedha 2006/2007 ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Ninatoa wito kwa wapangaji wote wa Shirika la Nyumba la Taifa kutekeleza matakwa ya sheria inayomtaka kila mpangaji alipe kodi ya pango kulingana na mkataba wake wa upangaji. Serikali imetoa tamko lake juu ya kutowavumilia wapangaji wasiolipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Shirika liliendelea kuwekeza kwenye matengenezo makubwa ya nyumba na majengo yake. Hadi kufikia Juni, 2006, Shirika limetumia Shilingi 3,733,095,968 kugharamia matengenezo ya nyumba zipatazo 1,481 (Jedwali Na. 14). Katika mwaka wa fedha 2006/07 Shirika litaendelea na matengenezo yaliyoainishwa kwenye mpango na mkakati wa Shirika wa miaka mitano (2006/2007 – 2010/2011).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika limeendelea na zoezi la uuzaji wa nyumba ndogo na za gharama ya kati kwa wapangaji. Hadi kufikia mwezi Aprili 2006, nyumba 4,666 zilizoidhinishwa kuuzwa tangu mwaka 1993, zimelipiwa kikamilifu na kulipatia Shirika mapato ya Shs. 6,377,583,299.30. Shirika limewatambulisha kwa barua wanunuzi wote wa nyumba waliokamilisha malipo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Miji na Wilaya husika ili wapewe barua za toleo (*Letter of Offer*) na hatimaye hati miliki. Wanunuzi waliobakia ni wale walio kwenye maeneo ambayo yana matatizo ya kiutaalam. Wengine waliochelewa kupata barua za toleo ni wale wenye nyumba kwenye maeneo yenye Hatimiliki 47 zilizowekwa rehani kwa iliyokuwa Benki ya Nyumba (*THB*). Hati hizo zilirejeshwa na Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) ambayo ilikabidhiwa jukumu la kusimamia ufilisi wa *THB*. Kati ya hati hizo 2 zilikuwa za Dodoma zenye viwanja 86 za nyumba ndogo. Hati hizo zimekabidhiwa kwa Halmashauri ya Dodoma ili kila mnunuzi atayarishiwe Hatimiliki yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ujenzi wa nyumba, Shirika limekamilisha ujenzi wa nyumba 148 za kuuza katika Mikoa ya Dar es Salaam (Boko, na *Mbezi Beach*) na Arusha (Kijenge). Aidha, Shirika limekamilisha majengo mawili (2) ya ofisi katika Mikoa ya Mwanza na Mtwara. Vilevile, kwa kushirikiana na Wabia, Shirika limekamilisha ujenzi wa majengo sita (6) ya vitega uchumi na kuendelea na ujenzi wa majengo mengine 14. Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Shirika limepanga kujenga

nyumba 239 kwa ajili ya kuuza na kupangisha katika Mikoa ya Dar es Salaam (Boko, Mbweni JKT, *Mbezi Beach*, Msasani na Mwongozo), Arusha (Kijenge na Mwandamo), Dodoma (*Mpwapwa Flats*). Aidha, Shirika kwa kutumia mtaji wake na kushirikiana na Wabia litajenga majengo makubwa 28 ya makazi na biashara katika majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na miji ya Kigoma na Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, shughuli kuu za Shirika ni pamoja na ujenzi wa nyumba kwa ajili ya makazi na biashara. Hata hivyo, shughuli hii bado haijapata kasi kubwa kutokana na sababu mbalimbali. Sababu ya msingi ni kutokuwepo na mfumo rasmi na mpana wa utoaji wa mikopo ya ujenzi na ununuzi wa nyumba hapa nchini. Tatizo hili limelilazimisha Shirika kujenga nyumba za kuuza sehemu zenye soko la uhakika tu na hivyo kulifanya lisiwe na sura ya Kitaifa. Serikali katika mwaka 2006/2007 inakusudia kulipatia ufumbuzi tatizo hili kwa kuanzisha tena mfumo utakaowezesha kukopa kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba. Kuwepo kwa mfumo huu utaliwezesha Shirika kujenga nyumba sehemu kubwa ya nchi yetu na hivyo kuwapatia Wananchi makazi bora na kukuza sekta ya nyumba ambayo ni kioo cha maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii kokote duniani. Aidha, kutapanua sekta ya ujenzi, kuongeza ajira, kuboresha makazi pamoja na mazingira ya miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Utawala na Utumishi. Maendeleo yoyote yanategemea sana rasilimali watu ambao ndio mhimili wa rasilimali zote, hivyo ili kufanikisha hilo ni lazima nyenzo zote zitakazowawezesha kutekeleza majukumu yao zitumike ili kuleta ufanisi wa kazi. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara yangu iliendelea kutoa mafunzo, kuboresha mazingira ya ofisi, kuwapatia watumishi stahili zinazoendana na ajira zao pamoja na kudumisha Utawala Bora. Aidha, msisitizo ulilenga katika kudhibiti nidhamu, kupiga vita rushwa, kutoa huduma bora na kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara imeboresha utendaji kazi kwa kununua vitendea kazi, ikiwa ni pamoja na kompyuta, samani za ofisi, magari na jenereta kwa ajili ya kutoa huduma kwa ufanisi. Watumishi wapya 32 wameajiriwa na katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara inatarajia kuajiri watumishi wengine 166 wa fani mbalimbali. Kwa kuzingatia kuwa uboreshaji wa huduma ni pamoja na kuwapatia Watumishi maslahi yao, Wizara yangu imewapandisha vyeo watumishi 43 (Jedwali Na. 15). Vilevile, ukarabati wa jengo la Ardhi unaendelea na unatazamiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2007/08. Ukarabati huu licha ya kuleta mandhari nzuri ya jengo, utaboresha mpangilio wa ukaaji wa wazi unaosaidia kuleta ufanisi zaidi katika utendaji. Pia, ujenzi wa jengo la Upimaji na Ramani unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya Utumishi wa Umma yanayoendelea Serikalini yanalenga katika kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii. Kwa kutambua hilo, Wizara yangu imeendelea kutekeleza maboresho kwa kuzingatia dhana ya uwajibikaji.

Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Watumishi wa ngazi ya juu na ya kati waliingia mkataba na viongozi wao katika sehemu zao za kazi, kwa kutumia mfumo wa wazi wa upimaji kazi (*OPRAS*). Mfumo huu unasaidia katika kuwawezesha Watumishi kujituma katika kutekeleza majukumu yao kwa viwango vilivyowekwa na hivyo kuiwezesha Wizara kufikia malengo yake. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu imekusudia kuendeleza mfumo huu ili uwafikie Watumishi wa ngazi ya chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa michezo, Wizara yangu imekuwa kati ya Wizara zinazoshiriki ipasavyo katika michezo mbalimbali kama vile SHIMIWI, Bonanza na Mei Mosi. Michezo hii inawafanya Watumishi kujenga miili yao kwa kuwa wakakamavu na hivyo kutoa nafasi ya wao kuwa wepesi katika kufikiri na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha na kudumisha utendaji kazi, Wizara yangu ilitoa mafunzo juu ya utoaji wa huduma bora kwa mteja (*customer care service*) kwa Watumishi wote 663 wa Makao Makuu. Watumishi wengine wa Sekta ya Ardhi wapatao 650 kutoka ofisi za Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri za Miji na Wilaya nao walipata mafunzo hayo mwezi Februari, 2006. Mafunzo haya yamesaidia kuwafanya watumishi kuelewa mahitaji na matarajio ya wateja wao. Katika kusimamia utekelezaji wa mafunzo hayo, Wizara imeunda kamati yenye jukumu la kufuatilia kero na matatizo yanayoweza kuzuia utoaji wa huduma bora kwa umma, kwa lengo la kuyatafutia ufumbuzi. Vilevile, katika kujenga uwezo wa Watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, Wizara yangu imeendelea kuwawezesha Watumishi kuhudhuria mafunzo ya aina mbalimbali. Jumla ya Watumishi 135 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi, kati yao 13 ni kutoka Halmashauri za Miji na Wilaya (Jedwali Na.16).

Mheshimiwa Mwenyekiti, UKIMWI ni janga ambalo limeendelea kuiathiri jamii kwa kupoteza nguvu kazi pamoja na kutumia fedha na muda mwingi kwa matibabu na matunzo kwa waathirika. Katika mwaka wa fedha 2005/06, waelimisha rika 26 wamepatiwa mafunzo na kupewa jukumu la kutoa elimu kwa Wafanyakazi wenzao juu ya kupambana na janga la UKIMWI. Pamoja na hilo, Watumishi katika idara zao walihamasishwa kupima UKIMWI kwa hiari. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara inatarajia kuongeza idadi ya waelimisha rika kufikia 80 ikiwa ni wastani wa Watumishi 10 kwa mwelimisha rika mmoja. Aidha, ili kufahamu hali halisi ya maambukizi, Wizara ipo katika maandalizi ya kumteua mtaalam mwelekezi atakayeandaa taarifa ya hali ya maambukizi Wizarani na mikakati inayohitajika kukabiliana na janga hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Ardhi Wizara inavyo vyuo viwili vya Ardhi vya Tabora na Morogoro ambavyo vinatoa mafunzo ya Diploma katika fani za Urasimu Ramani na Upimaji Ardhi. Pia, vyuo vinatoa Cheti katika fani za Umiliki Ardhi na Uthamini, Uchapaji Ramani na Upimaji Ardhi. Fani hizi ni muhimu kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la mafundi sanifu wa ardhi. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 idadi ya wahitimu ilikuwa 128 kati yao 55 walitoka Chuo cha Ardhi Morogoro na 73 walitoka Chuo cha Ardhi Tabora (Jedwali Na. 17).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho kwa muhtasari, kazi zinazotarajiwa kutekelezwa na Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2006/2007 zina malengo makuu matatu; Kwanza, kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato ya Serikali katika Sekta ya Ardhi na Makazi ili kuwa na uwezo kifedha; Pili, kuwezesha wananchi kutumia rasilimali ardhi kuwa nyenzo muhimu ya kuwaletea maendeleo na kuondoa umaskini na Tatu, kuimarisha utawala bora katika Sekta ya Ardhi na Makazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili kudumisha haki na amani miongoni mwa watumiaji ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na malengo hayo matatu zipo changamoto nyingi zilizoko mbele yetu katika Sekta ya Ardhi na Makazi hapa nchini. Nitaje chache tu, Kwanza, ni kukosekana kwa chombo cha kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba. Tukiwa na Chombo hiki tutaweza kuwapatia wananchi wetu makazi bora, tutapanua shughuli za Sekta ya Ujenzi na hivyo kuongeza ajira na kupunguza umaskini wa wananchi wetu. Pia, tutaboresha mazingira ya miji yetu. Pili, kutokuwa na uwezo mkubwa kifedha kuendelea na zoezi la kutambua maeneo yote yaliyojengwa kiholela nchini ili tuweze kutimiza malengo ya milenia. Tatu, kasi ndogo ya kupima viwanja isiyoendana na mahitaji ya wananchi wetu waishio mijini na vijijini. Nne, kuendelea na mtazamo wa kuendeleza miji yetu kwa kujenga majengo/nyumba tandavu (*horizontal*) badala ya shadidi (*vertical*), Tano kuendelea kupima vijiji nchini kwa kasi ndogo, Sita kutokuwa na mipango ya kupima na kutoa hati miliki kwa maeneo ya hifadhi ya mbuga za wanyama za Taifa na Mwisho, kupima maeneo yenye madini ili wamiliki wa machimbo wasiendelee kuvamia maeneo ya wananchi yaliyo jirani

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizo na nyingine nyingi zinatekelezeka. Suala ni mipango madhubuti. Ndiyo maana siku zote tumekuwa tukitumia kauli mbiu kuwa ili tuendeleo tunahitaji vitu vinne, Watu, Ardhi, Siasa Safi na Uongozi Bora. Hivi sasa watu wapo na wamefikia 35 milioni, Ardhi pia ipo ambayo inafikia mita za mraba 945,000 tena iliyo na eneo la kutosha la tambalale na mabonde yenye rutuba. Siasa Safi na Uongozi Bora tayari vimo ndani ya CCM. Kwa hiyo kinachohitajika baada ya kuwa na vitu hivyo muhimu ni kuelekeza fedha, akili na nguvu zetu katika vipaumbele vinavyotoa matokeo yanayogusa wananchi wetu moja kwa moja katika maendeleo yao na Taifa kwa ujumla. Katika vitu hivyo vinne hapa nasisitiza suala la ardhi, ardhi ni mtaji na ardhi ni mali kwa hiyo tuitumie ipasavyo tuondokane na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shukrani napenda kutumia fursa hii kumshukuru, Mheshimiwa Rita Mlaki, Naibu Waziri, Bibi Salome Sijaona, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara/Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu. Pia nakushukuru wewe Mheshimiwa Mwenyekiti. Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakitoa kwa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Aidha, napenda kutoa shukrani kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote nikielekeza shukrani maalum kwa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, kwa kukamilisha kazi ya kupitia, kujadili na kutoa ushauri kuhusu bajeti ya Wizara yangu na hatimaye kuidhinisha Bajeti

ya mwaka 2006/2007. Wizara yangu itaendelea kuzingatia ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati katika Bajeti hii. Wizara pia, itaendelea kuyafanyia kazi maelekezo yote yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili Bajeti hii. Vilevile, shukrani zangu za dhati ziende kwa vikundi vyote vinavyotoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makazi. Mwisho, napenda kuwashukuru Wananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi la Biharamulo Mashariki kwa kunichagua bila kupingwa kuwa Mbunge wao kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Ninawashukuru sana, pia kwa kukipatia kura nyingi Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005, ninawashukuru sana

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara yangu iweze kutekeleza malengo iliyojipangia, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2006/2007 kama ifuatavyo:-

- (i) Shilingi 10,747,833,000 kama Makusanyo ya Mapato ya Serikali.
- (ii) Shilingi 3,666,109,000 kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.
- (iii) Shilingi 12,542,580,000 kwa ajili ya Matumizi mengineyo.
- (iv) Shilingi 2,065,994,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Jumla ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni Sh. 18,274,683,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Tunakushukuru sana, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi. Kabla sijamwita Msemaji wa Kamati niwaandae tu wachangiaji watakaofuatia katika hoja hii ambayo imeshatolewa na kuungwa mkono. Tuna maombi ya wachangiaji 23, kwa vyovyote vile haiwezekani wote wakapata nafasi. Sasa niwaandae wale wa mwanzo mwanzo ambao wamechangia mara moja watakuwa ni hawa wafuatao:

Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Nakei, Mheshimiwa Nyami, Manyanya, Mheshimiwa Zainab Gama, Mheshimiwa Galinoma na Mheshimiwa Suleiman Saddiq na kama muda utaruhusu basi Mheshimiwa Mohamed Abdallah na Mheshimiwa Savelina Mwijage wajiandae

MHE. KIDAWA HAMID SALEHE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI): Naomba sasa nitoe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi kuhusu Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo na Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006, Pamoja na Ushauri wa Kamati Kuhusu Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007. Kwa mujibu wa Kifungu Na. 81(1) cha Kanuni za Bunge (Toleo la 2004), napenda kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kuhusu utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2005/2006, pamoja na kutoa ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha taarifa hii naomba nichukue fursa hii adhimu Kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwake na Mkutano Mkuu wa CCM ulifanyika mwezi Julai mwaka hu kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa. Uchaguzi huo ulikuwa wa aina yake kwani wajumbe wote walimpa kura za ndiyo isipokuwa mmoja na kufanya asilimia ya ushindi kuwa 99.999. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM Taifa kwa kupendekeza jina langu kwa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama chetu kuwa kati ya majina ya wajumbe wa Sekretarieti ya CCM Taifa kwa nafasi ya Katibu wa Idara ya Oganaisesheni, na Halmashauri Kuu kupitisha jina hilo. Nami ninaahidi kufanyakazi kwa nguvu na uwezo wangu wote. Aidha ninawapongeza wajumbe wenzangu wote wa Sekretarieti walichaguliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa kwa nyadhifa tofauti kama ifuatavyo; Mheshimiwa Luteni Yusuf Makamba Katibu Mkuu, Mheshimiwa Jaka Mwambi Naibu Katibu Mkuu Bara, Mheshimiwa Sarehe Feruz Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Mheshimiwa Aggrey J. Mwanri Katibu wa Idara ya Itikadi na Uenezi, Mheshimiwa Rostam Aziz Katibu wa Idara ya Uchumi na Fedha, Mheshimiwa Asha-rose Migiro Katibu wa Idara ya Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Viongozi na wanachama wa CCM kwa pongezi walizonimiminia kwa kuteuliwa kwangu kuwa Katibu wa Idara ya Oganaisesheni. Lakini lililonipa faraja zaidi ni kule kunihakikishia kuwa watanipa ushirikiano wa hali ya juu na msaada wa hali na mali katika kukiendeleza mbele chama chetu cha Mapinduzi na kukipatia ushindi wa kishindo katika chaguzi zote zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa mara nyingine tena kwa akinamama wa Kaskazini Unguja kwa kunichagua na kunirejesha tena Bungeni. Ninaamini hivi sasa wanaisikiliza naomba wapokee shukrani zangu za dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru familia yangu na wale wote waliokaribu nami kwa kunipa moyo na kwa msaada wanaoendelea kunipa wakati wate. Ninaamini kuwa Mwenyezi Mungu yupo pamoja nasi sote kwa maendeleo ya nchi yetu na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo napenda sana kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi Kamati kwa ushirikiano na umakini wao wakati Kamati inachambua bajeti ya Fungu 48 – Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Naomba kuwatambua wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Maida H. Abdallah, Mjumbe, Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mjumbe, Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mjumbe, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mjumbe, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mjumbe, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mjumbe, Mheshimiwa Manju S. Msambya, Mjumbe, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mjumbe, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mjumbe, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mjumbe, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mjumbe, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mjumbe, Mheshimiwa Fred T. Mpendazoe, Mjumbe, Mheshimiwa Mwadini A. Jecha, Mjumbe, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mjumbe na Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi ilikutana Dar es Salaam tarehe 2 Juni, 2006 ili kupitia utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2005/2006, pamoja na kupitia na kutoa maoni na ushauri juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2006/2007. Ili kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilizingatia utaratibu ufuatao: -

(i) Kupitia utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati wakati wa uchambuzi wa bajeti ya mwaka uliopita.

(ii) Kuchambua utekelezaji wa malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

(iii) Kuchambua na kupitia kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2006/2007 na maombi ya fedha kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliridhika na hatua zilizochukuliwa na Wizara katika utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati iliyoutoa wakati wa kuchambua bajeti ya mwaka wa fedha 2005/2006. Hata hivyo, Kamati ilitoa maoni na ushauri kadhaa katika maeneo ambayo yalionekana yanahitaji ufanisi na kuboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2005/2006. Mafanikio hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Utoaji wa vyeti 202 vya ardhi ya vijiji na hati 1,262 za kimila katika wilaya za Mbozi, Handeni, Kilindi na Babati.

(ii) Utoaji wa elimu ya sheria za ardhi na kanuni zake kupitia semina na vyombo vya habari.

(iii) Kuzifanyia marekebisho sheria za ardhi zinazokwamisha ustawi wa sekta binafsi hasa ya biashara nchini ambazo ni *Land Registration of Documents Act, Chattels Transfer Act na Valuers Act*

(iv) Kuongezeka kwa shughuli za uthamini ambapo katika mwaka wa fedha 2005/06 mali 2,003 zilifanyiwa uthamini na kuipatia Serikali jumla ya shilingi 202,215,758 na hivyo kuvuka lengo kwa asilimia 52.

Mafanikio mengine ni, Vijiji 119 vilipimwa mkoani Iringa katika wilaya za Njombe (43), Mufindi (13), Iringa Vijijini (55) na Kilolo (8). Aidha, viwanja 4,000 vilipimwa Jijini Dar es Salaam. Jumla ya ramani za msingi kwa miji 38 katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na Kagera zimekamilika.

Upimaji picha (Ground Photo Control) ulifanyika katika mikoa ya Iringa (Miji 6), Mbeya (Miji 11), Kagera (Miji 3), Kigoma (Miji 10), Tabora (Miji 90) na Rukwa (Miji 4).

Plani za upimaji zenye viwanja 17,262, mashamba 660 na vijiji 311 ziliidhinishwa.

Kutoa leseni 30,212 katika zoezi la kurasimisha rasilimali kwenye maeneo yaliyojengwa kiholela katika jiji la Dar es Salaam. Leseni hizi zinawasaidia wananchi kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara. Changamoto hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Ukosefu wa ramani za msingi (*base maps*) kwa nchi nzima ili kuwezesha uandaaji mipango ya matumizi bora ya ardhi na upimaji wa viwanja na mashamba.

(ii) Gharama za fidia ni kubwa sana kiasi cha kuzuia utwaaji wa maeneo kwa ajili ya kupima viwanja vya kutosheleza mahitaji ya wananchi mijini.

(iii) Uhaba wa vitendea kazi na nafasi za ofisi kwa baadhi ya watendaji.

(iv) Ukosefu wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na ununuzi wa nyumba zinazojengwa na Mashirika kama Shirika la Nyumba (*NHC*), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) na kadhalika.

(v) Uelewa mdogo wa Sheria ya Ardhi Na.4 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya vijiji Na.5 ya mwaka 1999

(vi) Halmashauri nyingi hazijaajiri wataalam wenye sifa za kusimamia na kutoa huduma za ardhi. Aidha, ofisi za ardhi kwenye Halmashauri hizo hazipewi kipaumbele katika kugawiwa rasilimali na Hazina (ruzuku) pamoja na Halmashauri zenyewe kutotenga fedha kwa ajili ya sekta ya ardhi

(v) Ukosefu wa fedha za kutosha kutekeleza utambuzi wa makazi yaliyojengwa kiholela katika jiji la Dar es Salaam na miji mingine.

(vi) Ukosefu wa fedha za kutekeleza Mpango wa Urekebishaji Upya wa eneo la Kurasini ili kuwezesha upanuzi wa shughuli za bandari kwenye eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Kamati ilipitia utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha uliopita na kutoa ushauri mbalimbali kwa Wizara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya mipaka ya ardhi ya Kitaifa na Vijiji, tatizo la mipaka ya ardhi kati ya nchi yetu na baadhi ya nchi jirani halijapatiwa suluhu ya kudumu. Aidha, migogoro ya mipaka ya ardhi kati ya wilaya na wilaya katika baadhi ya mikoa bado inaendelea. Tatizo hili lisipotafutiwa ufumbuzi wa kudumu linaweza kusababisha migogoro mikubwa zaidi na hivyo kutishia usalama wa wananchi wetu na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanza zoezi la kutambua na kuhakiki mipaka baina ya nchi yetu na nchi jirani mfano mpaka kati ya mkoa wa Kagera na nchi ya Uganda pamoja na kudhibiti mipaka kati ya wilaya na wilaya ndani ya nchi yetu. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa zoezi hili liendeleo kwa kasi zaidi ili kupunguza migogoro mbalimbali na kuwa na uhakika wa mipaka yetu na nchi jirani. Wizara ishirikiane na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI katika kuhakiki mipaka kati ya wilaya na wilaya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti,aidha, kwa kuwa zoezi hili ni la gharama kubwa, Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha Wizara kwa kuiongezea fedha kwa ajili ya zoezi hili muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kugawa ardhi ya vijiji/wilaya, migogoro mingi ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima hutokana na utaratibu usiozingatia maslahi ya pande zote mbili. Mfugaji asipopatiwa ardhi nzuri kwa ajili ya malisho ya mifugo yake, matokeo yake huwa ni kuhamahama kwa ajili ya kutafuta maeneo ili kuongeza tija ya mifugo yake. Huu ndio mwanzo wa migogoro kati yake na mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ili kutatua tatizo hili, Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kuweka utaratibu muafaka wa kuwagawia wafugaji ardhi nzuri ili nao waongeze tija ya mifugo yao. Maeneo yapimwe, yatengwe na kumilikishwa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutenga maeneo kwa ajili ya Uchimbaji Madini hivi karibuni tumeshuhudia mgogoro mkubwa unaowahusisha wachimba kokoto katika eneo la Kunduchi jijini Dar es Salaam. Ili kuepuka matatizo hayo, kuna umuhimu wa kuweka utaratibu endelevu ambao utatatua tatizo badala ya kulitafutia ufumbuzi wa muda mfupi na kisha tatizo kujitokeza tena baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuwa makini inapotenga maeneo kwa ajili ya shughuli za uchimbaji madini na kokoto ili kuepuka athari zitokanazo na utaratibu usio endelevu wa kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli hizo. Aidha, Wizara za Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Nishati na Madini pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI zishirikiane kushughulikia suala la uchimbaji wa kokoto; maeneo yatengwe na yaeleweke kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hati miliki za ardhi na mashamba vijijini. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuchukua hatua madhubuti kwa kuwapimia wananchi ardhi na mashamba vijijini na kutoa hati miliki kwa kutumia kompyuta. Mpaka hivi sasa Wizara imeshapima vijiji kati ya 6000 na 7000. Hatua hii sio tu itawawezesha wananchi walio wengi vijijini kuwa na dhamanakwa ajili ya kukopa kwenye taasisi za fedha, bali pia inaenda sanjari na sera ya uwezeshaji wananchi chini ya mpango wa MKURABITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri zoezi hilo liendelee na kuharakishwa ili kuliongezea ufanisi. Kadhalika, Serikali inashauriwa kutenga fedha za kutosha ili kuharakisha zoezi hili muhimu. Aidha, Kamati inashauri, maeneo yenye migogoro na matatizo mengi ya ardhi yapewe kipaumbele wakati wa utekelezaji wa zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Udhhibiti wa Watendaji wa Halmashauri, matatizo mengi ya ardhi tunayoyashuhudia hivi sasa kwa kiasi kikubwa yanatokana na utendaji kazi usio makini na kutokuwepo udhibiti wa karibu wa watendaji wa Halmashauri. Utaratibu ulivyo hivi sasa ni kuwa watendaji wa ardhi wako chini ya Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri husika na hivyo wanawajibika kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote ni mashahidi wa jinsi watendaji wengi wa Sekta ya Ardhi katika Halmashauri wanavyokiuka taratibu za utoaji wa hati za viwanja, ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za Mipango Miji na kadhalika

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuleta uwajibikaji na kurejesha maadili miongoni mwa watumishi hao, Kamati inaishauri Serikali iendeleze mfumo wa uboreshaji wa utekelezaji wa shughuli zake katika ngazi ya Halmashauri kwa kuongeza usimamizi na uwajibikaji. Ingawa watendaji wa Ardhi wanawajibika kwa Wakurugenzi wa Halmashauri, kuwepo na utaratibu mzuri wa kudhibiti utendaji kazi wao kwa ushirikiano kati ya Wizara za Utumishi, TAMISEMI na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi holela wa nyumba mijini. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha Mpango wa Utambuzi wa Makazi yaliyojengwa kiholela katika Jiji la Dar es Salaam. Hata hivyo, Kamati inaamini kuwa mpango huo ambao utekelezaji wake unahitaji fedha nyingi, ni matokeo ya kutokuwa na utaratibu muafaka wa kudhibiti ujenzi holela mijini pamoja na kutopima viwanja kwa ajili ya makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahenga walisema “kuzuia ni bora kuliko kuponya”. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Serikali ifanye maandalizi ya kudhibiti na kuboresha ramani za miji na miji midogo ili kuepusha matatizo ambayo tunayashuhudia hivi sasa Jijini Dar es Salaam pamoja na miji mingine nchini. Aidha, watendaji wa Sekta ya Ardhi na wadau wengine wazingatie taratibu na kuheshimu Sheria na Kanuni za mipango miji.

Wizara iendeleo kutathmini na kushirikiana na mamlaka za miji katika kusimamia na kudhibiti ujenzi na uendelezaji wa miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu kuhusu Sheria na Sera ya Ardhi. Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Ardhi No. 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji No.5 za mwaka 1999. Aidha, Wizara imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi kwa njia mbalimbali ili waweze kuzifahamu na kuzitekeleza. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara imepanga kutoa elimu kwa viongozi wa vijiji na kata juu ya Sera na Sheria hizi katika kata kumi na tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia ukubwa wa nchi yetu, itatuchukua muda mrefu kueneza elimu kuhusu sera na sheria hizi. Hivyo, ili kuleta ufanisi katika zoezi hili Kamati inaishauri Wizara kuongeza kasi zaidi. Aidha, Wizara itumie utaratibu wa *Training of Trainers (TOT)* ili kuharakisha azma hiyo. Katika kutekeleza zoezi hili, Kamati inaishauri Wizara izingatie Mkakati wa Utekelezaji wa Sheria za Ardhi (*Strategic Plan for Implementation of Land Laws (SPILL)*) na iwashirikishe wadau wote wanaohusika, ikiwa ni pamoja na wahisani inapobidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukusanyaji wa Madeni na Kodi za Viwanja. Kamati inaipongeza Wizara kwa kutumia njia mbalimbali kama vyombo vya habari, kufuatilia wadaiwa, kutoa elimu na kulipa asilimia 20 kwa vituo vya makusanyo ili kukusanya Kodi ya pango la ardhi. Kamati inaishauri Serikali kuweka nguvu zaidi katika utoaji elimu kwa walipa Kodi.

Aidha, Wizara iendeleo kutumia utaratibu wa kuwafikia walipa kodi kwa muda maalum kama wanavyofanya *TANESCO* na Mamlaka za maji ili kujihakikishia mapato yake. Vilevile, Wizara iweke utaratibu utakaowawezesha wananchi kulipa ada za viwanja bila kupoteza muda mrefu kwenye vituo vya kulipia kodi au ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendelezaji wa Eneo la Kurasini. Mojawapo ya matatizo yaliyoikabili Wizara katika utekelezaji wa malengo yake kwa mwaka uliopita ni ukosefu wa fedha za kutekeleza mpango wa urekebishaji upya wa eneo la Kurasini.

Eneo la Kurasini ni nyeti na linaweza kuleta mafanikio kiuchumi iwapo litarekebisha upya ili kuwezesha upanuzi wa shughuli za bandari katika eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu huo, Kamati inaishauri Serikali kuipatia Wizara hii fedha ili itekeleze mpango wa urekebishaji wa eneo hili na hivyo kufanikisha mipango ya upanuzi wa shughuli za Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uharibifu wa Ramani za Nyumba zilizouzwa. Miaka michache iliyopita Serikali kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilibuni utaratibu wa kuwauzia wapangaji wake kote nchini nyumba ndogo na za kati ili wazimiliki.

Pamoja na nia nzuri ya mpango huo, baadhi ya wamiliki wapya wa nyumba hizo wamekiuka ramani za nyumba hizo kwa kujenga mabanda, kujenga maduka madogo na kuzipanua. Hali hii imeharibu mandhari ya maeneo hayo na kuyafanya yaonekane kama ni maeneo ya ujenzi holela *Squartars*. Kamati inaishauri Wizara itathmini tatizo hili na kuchukua hatua zinazostahili ili kurejesha sura nzuri ya nyumba hizo. Aidha, zoezi la kutoa hatimiliki kwa waliouziwa nyumba hizo likamilishwe mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) ni chombo muhimu cha kuwahakikishia wananchi makazi bora Mijini na Vijijini. Hivi sasa Shirika linamiliki nyumba 16,021. Ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwake, Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Shirika, kuendelea na ujenzi wa nyumba za makazi ili kukidhi mahitaji ya wananchi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alipokuwa akizindua ujenzi wa nyumba za makazi Mjini Dodoma tarehe 13 Julai, 2006, pamoja na mambo mengine, alieleza umuhimu wa kuwa na chombo cha kutoa mikopo ya ujenzi wa nyumba. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha uanzishaji wa chombo hicho ambayo ni njia endelevu ya kuwawezesha wananchi kukopa fedha kwa ajili ya ujenzi au ununuzi wa nyumba bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha miezi 36 kilichotengwa kwa wamiliki wa viwanja kuviendeleza ni kidogo sana hasa ukizingatia kwa sasa Serikali haina chombo cha utoaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuongeza muda zaidi ili wananchi wanaopatiwa viwanja wawe na muda wa kutosha kuviendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi ni pamoja na kufanya utafiti, kutoa elimu, taarifa na kushauri vyombo mbalimbali kuhusu matumizi bora ya ardhi Mijini na Vijijini. Ili kutekeleza majukumu hayo ipasavyo, Kamati inaishauri Wizara kuiwezesha Tume ili iendeleo kufanya tathmini ya matumizi bora ya ardhi Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei kubwa za vifaa vya ujenzi ni kikwazo cha ujenzi wa makazi bora miongoni mwa wananchi walio wengi. Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi ilianzishwa ili kusaidia upatikanaji wa malighafi za

ujenzi hapahapa nchini na hivyo kupunguza gharama za vifaa vya ujenzi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuiwezesha Wakala hii, hususan kifedha na kazi za Wakala zitangazwe kwa wadau mbalimbali ili waweze kuifahamu na kunufaika na huduma zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa UKIMWI unaendelea kuwa tishio kubwa kwa rasilimali watu mahali pa kazi. Hali hii inatoa changamoto kubwa kwa Wizara kubuni njia za kuwasaidia waathirika ili waendeleo kuwa na afya na kutoa mchango wao katika maendeleo ya nchi. Kamati inaipongeza Wizara hii kwa kutenga kiasi cha Shilingi milioni 169 kwa ajili ya kuhudumia watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI na familia zao.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara iendeleo na utaratibu wa kuwashirikisha watumishi kwenye michezo kama njia mojawapo ya kuimarisha afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipitia vifungu mbalimbali vya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2006/2007. Kamati imebaini kuwa kiasi cha fedha kilichotengewa Wizara hii ni kidogo sana ukilinganisha na majukumu iliyonayo.

Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara imetengewa kiasi cha Shilingi bilioni mbili tu kwa ajili ya kupima ardhi na mashamba Vijijini nchi nzima. Kutokana na uchache wa fedha, ni Vijiji 1,800 tu ndivyo vitakavyonufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa zoezi hili katika kuwawezesha wananchi kiuchumi na majukumu ya Wizara kwa ujumla, Kamati inaishauri Serikali kuipatia Wizara fedha za kutosha ili kufikia azma yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa John P. Magufuli, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Ritta L. Mlaki, kwa kushirikiana nasi wakati Kamati inachambua Bajeti ya Wizara hii. Nawapongeza Watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Bi. Salome Sijaona kwa maandalizi mazuri ya Bajeti na mpango wa maendeleo kwa mwaka 2006/2007.

Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Wajumbe wa Kamati hii, kwa ushirikiano na umakini wao wakati wakichambua Bajeti ya Wizara hii. Namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S. L. Foka na Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Daniel Eliufoo, Ndugu Frank Mbumi wakisaidiwa na Bi. Maria Mwakasege kwa kuratibu kazi za Kamati hadi Taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inaliomba Bunge lipitisha Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi fungu 48 ambayo ni Sh. 18,274,683,000/= . Kati ya fedha hizo, Sh. 16,208,689,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 2,065,994,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Kidawa H. Salehe. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii, Mheshimiwa John M. Cheyo. Hii Wizara, Waziri na Waziri Kivuli, wote Wasukuma. *(Kicheko)*

MHE. JOHN M. CHEYO - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Ahsante sana Mtani wangu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2006/2007 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 45(3)(b)(c) na 81(1) toleo la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwako wewe kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wetu wa Bunge pamoja na Mwenyekiti mwenzi, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, pamoja na pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Spika na Naibu wake kwa pamoja, wanaliendesha kweli Bunge hili kwa viwango ambavyo vinastahili kuigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutoa shukrani kwa Wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu za Serikali ambao wamenichagua kuwa Mwenyekiti. Nawashukuru sana. Aidha, natoa pongezi zangu za dhata kabisa kwa viongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa kwa kazi kubwa wanayoifanya ili kuiongoza Kambi yetu ambayo sasa iko pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutoa shukrani zangu za dhata kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la langu la Bariadi Mashariki kwa kura nyingi sana walizonipa dhidi ya Chama Cha Mapinduzi na kunifanya mimi niwe Mbunge wao. Nashukuru sana na nawaahidi kwamba nitawatumikia kwa moyo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa pia nataka kutumia nafasi hii kuishukuru familia yangu sana kwa kunipa ushirikiano katika kazi hizi za Siasa.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mnajua Siasa ni sawa sawa na bangi. Unaweza ukaacha shughuli za familia kwa kupenda bangi, kwa kupenda Ubunge. Kwa hiyo, unahitaji familia kuwa nyuma yako. Kwa hiyo, namshukuru kwa dhata mke wangu mpenzi, Elizabeth Cheyo na familia yote kwa ujumla. Pia, nawashukuru wale wote walioshirikiana na mimi katika kuhakikisha kwamba tunapata Ubunge kwa kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajikita katika Bajeti hii, pia napenda kuwapongeza watu wa Bariadi. Juzi ilikuwa Nane Nane na kweli wamepata matunda ya kuwa na Chama cha Upinzani katika Wilaya kwa kuwa wamepokea ng'ombe 20 *Wagalo* na *Wagika* ambao ni sawasawa na milioni 20. Hela kibao hiyo! Wamepokea pesa taslim karibu Shilingi milioni 1.2 kutoka kwa Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Pesa kibao hizo! Pia, wamepokea kama Sh. 800,000/= kutoka kwa Mbunge wa Bariadi Mashariki. Jumla inakuwa kama Shilingi milioni 22.06. Haya ndio matunda ya kuwa na Wilaya ambayo ina upinzani ulio madhubuti. Kwa hiyo, natoa wito kwa wengine pia kama wanataka hayo mamilioni na wenyewe waimarishe Kambi ya Upinzani. Nina hakika Serikali itakayoingia kule itakwenda kuhakikisha kwamba wanawapa pesa kibao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nijadili Bajeti ya Wizara hii. Kwanza, kabla sijaendelea na hotuba hii, napenda kusema kuwa shabaha ya hotuba hii ni kutoa mtazamo mbadala wa majukumu ya Wizara hii ambayo kwa maoni yetu ni kama ifuatayo:-

- (i) Wizara iwe chanzo cha ufahamu wa hazina ya ardhi yetu na mpango endelevu. Iwe kama *Land Bank* ili mtu kama leo anataka hekta 20,000, anaweza akazipata kwa sababu Wizara hii inazo na inaweza ikatoa uhakika wa ardhi hiyo;
- (ii) Wizara ipate nafasi ya kujikita katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini (*MKUKUTA*) na kuwa na Mpango wa Kurasimisha Biashara Tanzania (*MKURABITA*); na
- (iii) Kupanga matumizi bora ya ardhi yetu, ndilo liwe jukumu kubwa la Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa, kama Serikali itaweza kujikita katika kufuata mambo niliyoyataja hapo juu, itaonyesha wazi kabisa migogoro ya ardhi ambayo imetamkwa na Waziri na ipo katika Taifa letu, itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kabisa takwimu zinatonyesha kuwa nchi yetu haina uhaba wa ardhi. Kwa mfano tu, jumla ya ardhi katika Taifa letu ni hekta milioni 94.4. Inayolimika sasa hivi (*arable land*) ni hekta milioni 44. Iliyolimwa (*cultivated*) mpaka hivi sasa ni hekta milioni 10. Inayofaa kumwagiliwa ni kama hekta milioni 29. Mashamba makubwa ni kama hekta milioni 1.5. *Range lands* ambayo ni miti na inafaa kwa ufugaji, ni kama hekta milioni 50. Ardhi ambayo inaweza ikachungika kwa kuchunga tu (*Land under livestock*) ni kama hekta milioni 26. Kwa hiyo, kwa hali kama hii, hatuna *really* uhaba wa ardhi katika Taifa letu. Lakini watu kwa kukosa mipango, wengi tu umiliki wao ni ule ambao hauna utaratibu ulio kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umiliki wa ardhi (*Land ownership*) kwa sasa hivi ni kama ifuatavyo:-

- Umiliki wa kimila ni 58% ya ardhi yote inayotumika;
- Ardhi waliyonunua toka kwa wamiliki wa asili ni 16%;
- Ardhi iliyokodishwa ni 8%;
- Ardhi iliyokopeshwa (*borrowed land*) ni 8%;
- Ardhi inayomilikiwa kwa hati miliki ambayo imepimwa (*Land Ownership Certificate*) ni 5% tu ya ardhi inayotumika. Kwa hiyo, kazi ya kupima haijafanyika vya kutosha tangu miaka 40 tujitawale; na
- Umiliki wa aina nyinginezo mbali mbali ni 4%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kosa kubwa ambalo tunalionga la Serikali ni kwamba Serikali inasubiri pale wananchi wanapotengeneza makazi yao, ndio Serikali inaingia pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaliona hili kuwa ni udhaifu wa Serikali yetu, kwani inaonyesha wananchi wako mbele ya Serikali yao na kwamba Serikali inakuwa imelala na baada ya wananchi kuweza kufungua makazi, mashamba, ndipo inaamka na ndio inawafuata kwenda aidha kuwaondoa na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la Serikali ni kuanzisha maeneo mapya kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na vile vile shughuli za makazi. Kinyume na hapo, wananchi wenyewe wataanzisha maeneo yao kiholela, kitu ambacho kinasababisha maeneo kujengwa bila ya kutokuwa na mipango endelevu kama vile kutokuwa na barabara, sehemu za wazi, Shule za Watoto, Zahanati na kadhalika. Hii inatokana na sababu kuwa Serikali bado imelala usingizi wa pono. Ikishazinduka, ndipo tunaona wananchi wanaanza kubomolewa nyumba zao kwa kisingizio kuwa haziko kwenye ramani ya mipango Miji au zimo ndani ya Hifadhi za Barabara na kadhalika. Aidha, hakuna utaratibu wa ardhi ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iache kutumia dhana ya kuwa ardhi ni mali ya umma na hivyo inaweza kubomoa makazi ya watu bila kuwafidia kwa bei ya ardhi ya soko, kuhamisha watu na mifugo yao bila fidia na upotevu wa malisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ardhi ipo, Serikali iweke utaratibu wa kuanzisha maeneo mapya kabisa ambayo yatakuwa yamepangwa kama itakavyokuwa imeridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi katika nchi yetu ni mali ya Serikali na katika mikakati yote inayofanywa na Serikali, inalenga katika kuiendeleza ardhi. Dhana ya kuiendeleza Ardhi inamfanya yule mwenye nayo kupata vishawishi vingine vya kupata fedha za haraka haraka kwa minajili ya kuiendeleza ardhi hiyo. Hapa ndipo chimbuko la rushwa, wizi na uchafu mwingine utakaomwezesha kupata fedha ili aweze kuiendeleza hiyo ardhi kabla hajanyang'anywa na Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, dhana hii inaondoa ile dhana ya umiliki ambayo inalenga kwa mwananchi kuwa na umiliki wa raslimali hiyo. Kambi ya upinzani

inaamini ardhi ni mali kama ilivyo nyumba na mali nyingine ambazo zinamilikiwa na wananchi au Serikali. Mazingira mazuri katika kuhakikisha mwananchi anakuwa na umiliki wa ardhi yake ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya kuiendeleza ardhi inamnyima mwananchi asiyekuwa na uwezo kuendelea kuimiliki ardhi hiyo, kwani kwa mujibu wa dhana hii, Serikali inaweza kuichukua ardhi hiyo kwa kuwa mwenyewe ameshindwa kuiendeleza. Leo Waziri ametuambia ana azma ya kuchukua ardhi nchi nzima kwa viwanja ambavyo bado havijaendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaliona hili kuwa kwa upande mmoja linapingana na maana halisi ya *MKURABITA* ambayo lengo lake hasa ni kwa wananchi kile wanachokimiliki kuthamanishwa bila ya upendeleo wa kuwa kumeendelezwa au la.

Aidha, hivi karibuni katika vyombo vya habari tumesikia kuwa Waziri wa Ardhi ana mpango wa kuvitwaa viwanja vyote nchi nzima ambavyo bado havijaendelezwa na wamiliki. Katika Mkoa wa Dar es Salaam peke yake, maeneo ya Mbezi imetangazwa kuwa Waziri wamenyang'anya viwanja wamiliki zaidi ya 300 kwa sababu ya kushindwa kviendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alihakikishie Bunge hili ukweli wa jambo hili na kama sheria Na. 4 ya Ardhi, Sehemu ya Nne (*sub-part 4 - Breach of conditions of right of occupancy, sect 44-50*), hizi sections zimefuatwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vifungu hivyo vya sheria vinatoa haki kwa mmiliki kujitetea, Kamishna kutoa adhabu, Kamishna kumwongezea muda, Kamishna kutoa *notice* ya pili. Aidha, vifungu hivi havimtaji Waziri kama mwenye mamlaka ya kutamka kwenye vyombo vya habari kuwa amewanyang'anya watu ardhi bila ya kufuata hatua zilizopangwa na sheria. Kambi ya Upinzani pia inamtaka Waziri awataje kwa majina watumishi wote ambao wana viwanja vya kugushi na amechukua hatua gani juu yao? Tunaomba hili ili kuondoa dhana ya kutumia kisingizio cha watumishi wa ardhi wachache katika kuhalalisha azma ya Waziri kuwapora watu walio wengi ardhi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mazingira ya Sera mbalimbali zinazohusu ardhi na kuwa na mali au kutajirika yamekuwa kikwazo kikubwa kwa mmiliki kuendeleza ardhi. Kwa mfano, wale ambao wanajua historia ya nchi hii, Sera ya *Block Farms* na Azimo la Arusha, enzi za J. K. *No. 1*, mtu huwezi ukaringa kuwa una nyumba tano. Kila mmoja ana nyumba moja. Hali ya Sera hii ilizuia watu wasiweze kuendeleza makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Vijiji ya mwaka 1973 iliwafanya watu waondolewe katika makazi yao na kwa hiyo, kuacha sehemu zao ziweze kukatwa miti hovyoy. Zamani watu walikuwa na *ngitili* zao, lakini pakaja na sera hii ya Vijiji, *Operation Vijiji*, watu wakaondolewa katika makazi yao. Pia, enzi hizi hazikuwa enzi ambazo mtu unaweza kujivuna kutumia rasilimali yoyote ile kuweza kujenga nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya uhujumu uchumi mwaka 1980 -1985 ina julikana jinsi watu walivyonyang'anywa nyumba zao na mali zao na pia ilikuwa sio wakati ambapo mtu unaweza ukajivuna kuwa umejenga nyumba *A, B, C, D*, bila kuingia katika matatizo. Ilikuwa enzi pia ya mashamba makubwa ya Serikali ya kulima chakula kama Mabarali, kufuga *ranches* za Serikali. Mengi ya mashamba haya yalipatikana kwa kumfukuza mkulima mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Ruksa 1985 -1995, hii iliweza kuiondoa Serikali kama mhodhi wa uchumi. Katika enzi hii, watu binafsi wamechukua, wamenunua mashamba ya Serikali na wengine wamejenga na wamepewa kwa njia ya kupimiwa na Serikali na hata wale waliohamishwa wakati wa *operation* Vijiji, wengi wao walirudi kwenye mahame yao na kumiliki kimila mashamba yao. Wengine waliwafukuza waliowakuta pale kwa kupewa na *operation* Kijiji, wengine walishitakiana kwenye Mabaraza ya Ukoo, Kijiji, Mahakamani, kwa Viongozi wa Kiasia na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka hii, wengine walihamia katika Mikoa mbalimbali kama vile ya ufugaji na pia waliingia katika *Game Reserves* kama *Maswa Extended Game Reserve*. Wafugaji pia wengine walikwenda Nyanda za Juu Kusini kama Iringa, Mbeya, Rukwa, Songea na mengineyo.

Kwa hiyo, hii ilikuwa ni wakati wa kuchukua kinachowezekana. Wazawa wengi walionekana ni wanyonge na hawakuwa na fedha za kuweza kuendeleza makazi yao. Pia, watu wengi kwa sababu ilikuwa ni hali ya ruksa ruksa, waliingia katika Miji na kutengeneza *squatters cities, Municipalities* na sehemu kama Manzese, Kipawa, Mwanza na sehemu nyingine ambazo sasa hivi hazina mpangilio wowote. Hizi zilikuwa zama za ruksa na mambo yake yalikuwa ya ruksa ruksa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera za ubinfisaji na ugenisishaji yanwaja 1995-2005 ya Awamu ya Tatu, hii ilikuwa ni sera ambayo iliwaruhusu wageni zaidi kuweza kuingia katika Taifa letu kuchukua ardhi, aidha kama wachimbaji wa madini. Wakati huo pia ndio wakati ambao *South Africa* imekuwa huru na Mandela amechukua hatamu na *Wa-South Africa* wamefunguliwa kuweza kwenda mahali popote pale Duniani na ndio walijaa hapa na hapakuwa na upendeleo wa wazawa. Ardhi kubwa iligeuzwa matumizi na kuweza kuchukuliwa na wageni kwa mfano kama kwa uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Nne ambayo ni Awamu ya sasa na yenyewe imekuja na lake. Awamu hii ni Awamu ya Sera ya Kasi Mpya na mashamba makubwa na kunyang'anya viwanja vya wale ambao hawajaviendeleza na mazingira na imeanza kwa kishindo kwa hatua za kupunguza ng'ombe kama njia ya kuhifadhi mazingira. Wenye ruksa ya kuharibu mazingira ni wanyamapori tu. Lakini sio ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali kama hiyo nilioieleza, mtu anawezaje kuiendeleza ardhi au kwa kujenga nyumba au kuendeleza mashamba? Hivyo, Kambi ya Upinzani haikubaliani na dhana ya uendelezaji kama msingi wa kumiliki ardhi. Tunaiunga mkono Ibara ya 24 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inayosema kuwa:

“Kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria.” Ardhi ni mali ya msingi (*basic property*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ardhi ni ya umma kama nilivyosema mapema na ipo mikononi mwa Rais. Rais amepewa mamlaka na sheria ya ardhi kutoa ardhi kwa kuzingatia haki kwa kipindi cha mpaka miaka 99.

Kiutendaji, kamishna wa Ardhi ndiye amepewa mamlaka ya utawala. Pia, Sheria Na. 5 imetoa jukumu hili kwa Halmashauri ya Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika zama hizi za mtu binafsi ndiyo injini ya uchumi, wakati umefika kufikiria ardhi kama mali (*property*) na ina mwenyewe na kama mali inaweza kuuzika, kuwekwa rehani kwa ajili ya mikopo nakadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza pawepo na Mamlaka ya Ardhi (*Tanzania Land Authority*) itakayojitegemea kiutendaji na kujiendesha kibiashara, ambayo itaundwa rasmi kwa sheria ya Bunge na sio vinginevyo. Kazi zake zitakuwa kama zifuatazo:

(i) Kupima maeneo mapya kwa matumizi mbali mbali, mfano, mashamba makubwa ya kibiashara (*Commercial Farms*), Vijiji vipya vya kisasa, mashamba madogo madogo ya wanavijiji na mashamba ya wafugaji (*ranchies*);

(ii) Kuuza mashamba makubwa na madogo kwa wale wanaohitaji;

(iii) Kutengeneza miundombinu kama vile barabara, maji, shule, umeme, hospitali inayotakiwa katika maeneo mapya yatakayopimwa;

(iv) Kukusanya fedha kutokana na mauzo ya mashamba makubwa na madogo. Dhana hii ya kuuza mashamba tayari inafanywa na kukubalika katika Serikali, kwani mashamba yote yaliyokuwa chini ya *NAFCO* sasa yameuzwa. Sasa kama Serikali inaweza kuuza, sioni kwa nini mtu mwingine binafsi aweze kuruhusiwa kuuza kama mali yake.

Mfano mashamba ya mpunga ya Kapunga na Mbarali yenye jumla ya hekta 13,400, Mashamba ya ngano ya *West Kilimanjaro*. Mashamba ya Mifugo ya Mkata, Dakawa na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafikiri kwamba kuanzisha Mamlaka ya Ardhi ni utaratibu mbadala na endelevu utakaokidhi mahitaji ya Watanzania na uwiano sasa na ya upeo na Dira ya Taifa ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miji yetu inakua kwa kasi ya ajabu sana na hili halina mjadala, kwani linatokana na jinsi watu wanavyohamia maeneo hayo kutoka Vijijini. Hivyo basi, Serikali inatakiwa iwe mbele zaidi kimipango kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilivyo sasa inaonesha wananchi wako mbele zaidi ya Serikali na ndiyo maana kila mara Serikali inakuwa nyuma, inaweka mipango katika maeneo ambayo tayari wananchi wamekwishahamia na kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kurekebisha maeneo ambayo tayari yana watu ni kubwa mno, kwani ni lazima ihusishe fidia kwa watu mbalimbali na hizo zote ni uzembe mkubwa kiutendaji kwa upande wa Serikali. Jambo la msingi ni Serikali kuibua Miji mipya na kuipanga kutokana na mahitaji muhimu ya Miji (*satellite towns to be developed*). Ardhi ya kutosha tunayo na kwa sasa kutokana na dunia kuwa kama Kijiji, umbali sio kosa, maana mtu unaweza kufanya kazi hata ndani ya Ofisi yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa ni chombo ambacho tayari kimeshajidhatiti sana katika kufanya kazi ya kujenga nyumba na kwa dhana ya kupunguza matumizi ya Serikali. Ni muhimu Serikali ikarekebisha shughuli za chombo cha *Tanzania Bureau Agency* ili chombo hiki kijikite kutawala nyumba za Serikali tu na sio biashara ya majumba (*real estate business*) na kuliimarisha zaidi Shirika la Nyumba la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa njia hii Shirika litawezeshwa na kujenga nyumba na kuziua kwa Serikali au kwa watu binafsi wenye uwezo wa kuzinunua na zoezi hilo litaendeshwa kibiashara zaidi na bila kukiuka Sheria ya Manunuzi ya Serikali (*Procurement Act*). Tofauti na sasa ambapo Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi mno kwa kukarabati nyumba zake kwa gharama kubwa na kuziua kwa bei karibu na bure. Kwa mfano mpaka Juni, 2006, Serikali imeuza nyumba 8,320 kwa Sh.60,054,556,439/= ambayo ni wastani wa Sh.7,218,095/= kwa kila nyumba. Umeona wapi? Haijawahi kutokea katika Taifa hili! Unapata kiwanja hata kwa milioni zaidi ya 100, leo unauza nyumba *Oysterbay* kwa wastani wa milioni saba! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili vizazi viweze kuangalia jinsi Serikali yao inavyotumia mali ya mtu mnyonge, mali ya mtu maskini, natoa hapa muhtasari wa jinsi Serikali ilivyouza nyumba hizo.

Awamu ya Kwanza, Serikali imeuza nyumba 2,961 kwa thamani ya Sh.22,822,521,569/= kwa wastani wa bei ya Sh.7,707,707/=. Awamu ya pili, nyumba zilizokuwa za Serikali 1,267 zimeuzwa kwa Sh.10,034,870,553/= kwa bei ya wastani wa Sh.7,920,158/=. Nyumba zilizotokana na Mamlaka ya Bandari 1,092 ziliuzwa kwa Sh.9,045,259,000/= kwa wastani wa Sh.8,283,204/=. Awamu ya tatu Serikali na Mashirika ya Umma iliua nyumba zilizokuwa za Serikali 511 kwa Sh.4,570,351,736/= kwa wastani wa Sh.8,926,468/=. Nyumba za *TAC* 19 zimeuzwa kwa bei ya Sh.312,900,000/= kwa wastani wa Shilingi milioni 16.4. Nyumba za *STAMICO* 29 ziliuzwa kwa Sh.352,063,000/ = kwa wastani wa Shilingi milioni 12.1. Nyumba za Mamlaka ya Bandari 111 ziliuzwa kwa Sh.1,180,879,000/= kwa wastani wa Shilingi milioni 10.6. Nyumba zilizotoka Shirika la Reli 2,000 ziliuzwa kwa Shilingi bilioni 8.7 kwa wastani wa Shilingi milioni 4.3 kwa kila nyumba. Awamu ya nne, Serikali iliua nyumba 329 kwa Sh.3,021,331,921/= kwa wastani wa Shilingi milioni 9.2. Nyumba hizi pia ziliuzwa kwa mkopo wa miaka 10. Tunataka hili jambo Watanzania walisikie ili

waone jinsi Serikali inavyoweza kutumia raslimali ya watu wanyonge kwa kutoa bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasisitiza, kuondokana na yote hii kuwa *National Housing Corporation* (Shirika la Nyumba la Taifa) lipewe umuhimu wa kipekee ili lichukue majukumu yote ya ujenzi yanayofanywa na *TBA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Mheshimiwa John Cheyo kwa mawasilisho hayo. Sasa tunaingia kwenye kipindi cha uchangiaji wa jumla toka kwa Waheshimiwa Wabunge na kama nilivyosema, tunaanza na Mheshimiwa Aziza Ally, atafuatiwa na Mheshimiwa Ponsiano Nyami na Mheshimiwa Ligallama ajiandae.

MHE. AZIZA S. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuongea asubuhi hii. Namwomba Mwenyezi Mungu akujalie sana. *(Makofi)*

Awali ya yote, naomba kwanza nipongeze Vyombo vya Habari hususan *TVT*. Nasema *TVT* kwa sababu wanaweka kipindi chao siku zote asubuhi ambacho kinamnukuu Mheshimiwa Rais wakati alipotembelea Wizara zote na kuwakumbusha Viongozi wa Umma wajibu wao. Kwa kauli mbiu hiyo ya Mheshimiwa Rais kupitia *TVT*, kwa kweli nawashukuru kwa kuwa wanafanya kama ni ibada, kwa sababu mtu yeyote anapotoka nyumbani kwenda kazini, kile kipindi anakiona.

Kwa hiyo, ni mojawapo ya kuwakumbusha ni kitu gani wanatakiwa kufanya wakiwa ni Viongozi au Watumishi wa Umma. Tuzingatie kuwakumbusha Watumishi wa Umma kuwa Mtumishi wa Umma anatakiwa awe mnyenyekevu, asiwe mjeuri, aheshimu watu, asitoe wala kupokea rushwa na kubwa zaidi kuheshimu taaluma walizonazo. Kwa kweli kwa hili nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Pili, nampongeza kwa kutembelea katika Wizara zote na nina imani matamshi haya ameyatoa kwa sababu anaelewa kuna matatizo. Kama hakuna matatizo, asingeweza kuyatoa haya na *TVT* wasingeweza kuweka kipengele hiki cha kuwa wanawakumbusha Watumishi wa Umma kila siku kwa sababu na wao wanajua kuwa matatizo yapo, hususan katika Wizara hii ambayo pia ametoa mwongozo wake wa kusema kuwa kwenye Halmashauri zote kuwepo na Kamati ambazo zitasimamia kero za wananchi kuhusu masuala ya ardhi. Kwa kweli ninampongeza na ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa siku ya leo, kutokana na niliyonayo, napata wasiwasi sana kuunga mkono, ila nitaunga mkono kama kaka yangu Magufuli atayajibu ya kwangu kiufasaha. Hili naomba niwe wazi kwa sababu sitaitendea haki nafsi yangu, ni lazima na nafsi yangu nitendee haki kwa kuipa uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu la kwanza liko Tabora ambako ninaishi, kwa wapigakura wetu. Mwaka 1993 Shirika la Nyumba liliidhinisha nyumba zote wanazoishi wananchi za *National Housing* waweze kuuziwa na wakatangaziwa, wenye kuwa nacho wakatoa. Ilipofika mwaka 2000 wakapelekewa tamko tena la kuambiwa kwamba, yule ambaye bado mpaka sasa hajalipia nyumba zile atanyang'anywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu walikopa, walitumia njia mbalimbali ili waweze kupata pesa za kulipa nyumba hizo na wakalipia. Mpaka sasa nashangaa wananchi hawa bado hawajapata hati zao! Yaani hapa ndiyo nashindwa kuelewa! Mpaka sasa hawajapata hati za kumiliki zile nyumba ambazo tayari wameshazilipia na nina imani sio Tabora peke yake. Ni hizo nyumba za *National Housing* katika maeneo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka nimesimama hapa, nimelifuatilia suala hili kwa undani zaidi. Tatizo ni ramani. Ramani wamekwenda kupima, wametafuta kampuni ya nje, wameikubalia imekwenda pale imepima, baada ya kupima imepeleka Wizara ya Ardhi, lakini mpaka sasa Wizara ya Ardhi bado haijapitisha ile ramani na kutokupitisha kwao ramani ndiyo kumechangia wale watu wasiweze kupimiwa maeneo yao. Tunasema kuhusu *MKURABITA*, kuhusu *MKUKUTA*, kuhusu kuwawezesha wananchi kwenda kukopa, watakopaje wakati bado hawajapewa hati za kumiliki nyumba zao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena nashangaa zaidi! Miaka miwili au mitatu nyuma zimeuzwa nyumba zile ambazo wamenunua Mawaziri, Makatibu Wakuu. Taarifa niliyonayo, wale wote wanazo hati za nyumba zao. Kwa hiyo, hapa tuna mipaka ya wananchi na tuna mipaka ya viongozi. Nina imani hili ni suala zuri, wale wananchi kwa kuwa suala lao ni la muda mrefu, basi wangeweza kusikilizwa na kupewa hati zao. Wale pia ni walipakodi na sisi tunakaa humu ndani kutokana na hao wananchi wenyewe. Ni kwa nini hatuwatendei haki wananchi? Ndiyo maana nasema, najisikia uchungu sana kusema ninaunga mkono hoja kwa sababu ni lazima wananchi wetu tuwe na imani nao na uchungu nao, hata kwa zile pesa zao wanazozitoa katika Serikali yetu. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kulifuatilia hili na kunijibu vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa *National Housing* nimewaambia: “Naomba msifanye lolote, sisi ni viongozi wenu, mmetupa majukumu haya tutayafikisha na kuweza kuyasimamia na Serikali itatoa tamko.” Lakini bado na wao wanadai: “Kama sisi tumetoa pesa zetu na zimekaa huko muda wote na tumecheleweshewa hati zetu na sisi tuna haki pia ya kudai fidia kwa muda wote huu ambao tumechelewa kupewa hati.” Kwa hiyo, ni lazima tuelewe kuwa na wananchi wetu wana haki ya kulipwa fidia ya kucheleweshewa kwa sababu ni usumbufu mkubwa ambao wamewapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni la *National Housing*. Suala hili nikilisema, watu wanaweza wasinielewe vizuri. Lakini kwa wale wenye kulielewa, wanaelewa vizuri zaidi na wako Wabunge ambao wanalielewa kwa ufasaha na linawahusu, linawagusa. *National Housing* ni zile nyumba ambazo Mheshimiwa Mwalimu Nyerere alizitaifisha. Mheshimiwa Naibu Waziri siku ambayo alikuwa anajibu

hapa, alijibu kuwa wako ambao walirudishiwa na kuna utaratibu mwingine ambao utaendelea au hawataweza kurudishiwa tena. Lakini bado nasema, miaka 10 ya mwanzo walitangaziwa kuwa nyumba zile, yeyote anayedai aweze kurudishiwa, wakaenda wakaandika wakarudishiwa.

Lakini napenda kusema kwamba, nyumba hizi zina matatizo. Wapo Watendaji wetu ambao wameweza kutumia upenyo wa ule muda wa miaka 10 kuweza kupotosha nyumba hizi kwa utaratibu uliopo au kuziua au kupitia sehemu nyingine yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiongea, sisemi kama yanatoka kichwani tu, ni kwa uthibitisho nilionao na nitakukabidhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza ninukuu kidogo barua hii ya Shirika la Nyumba. Kuna Mzee alikuwa akiitwa Mzee Ngalambele. Huyu Mzee alikuwa ni DC mwaka 1960 mpaka 1980 wa Wilaya ya Mbarali, ni kiongozi wetu. Ilipofika mwaka 1990 watoto wake wakaandika barua kwa Rais, baadaye wakapewa maelekezo mengine wakaenda *National Housing* kuuliza hii nyumba: Je, iko kwao na inamilikiwa na nani? Naomba kunukuu *National Housing* walivyowajibu: “Nyumba tajwa hapo juu inamilikiwa na mtu/kampuni binafsi na sio miongoni mwa nyumba zinazomilikiwa na Serikali. Kwa niaba ya Serikali, tafadhali wasiliana na mkazi wa nyumba hiyo ndiyo mwenye nafasi nzuri ya kujua ni nani mmiliki wa nyumba hiyo. Wako, Shirika la Nyumba la Taifa, kwa niaba ya Mkurugenzi.” Aliyeandika ni Nsanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi nyumba zimetaifishwa, yeye ameirudisha Serikalini, Shirika la Nyumba wanasema hawaifahamu na wala hawajui yule anayeiliki. Sasa nahitaji kujua, hii nyumba ni ya nani? Lakini watoto wake waliondoka kufuata ile nyumba na kuangalia ni maeneo gani, wakakuta nyumba ile imefungwa, hakuna mtu anayekaa, ila kuna mlinzi. Ndiyo maana nasema nyumba hizi zina matatizo. Naomba majibu ya kina sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakukabidhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nyumba nyingine ya Mzee Maswanya. Mzee Maswanya alikuwa ni kiongozi wetu, pia alikuwa ni Waziri Wizara ya Mambo ya Ndani, ameshakuwa ni Marehemu. Lakini pia alikuwa na nyumba yake. Mke wake baada ya kufuatilia kwa Mheshimiwa Rais Mwinyi, Rais aliandika barua na kuhakikisha kuwa wampe *flat* moja yenye vyumba vitatu, lakini mpaka sasa hakuna ambacho alikipata na ile nyumba kuna mtu anakaa. Baada ya kufuatilia, wanaambiwa, nyumba hii kuna Mhindi ndiye aliyejenga na wala siyo tena Mzee Maswanya. Kwa hiyo, hapa napata wasiwasi sana. Hizi ndiyo ambazo tunazifahamu: Je, zile ambazo watu wameshasahau, wenyewe wamekufa na watoto wao hawafahamu zimekwenda wapi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kuwepo utaratibu wa kufuatilia hizi nyumba ambazo zilitaifishwa na Mwalimu Nyerere ni ngapi na ziko wapi na wanalipa kodi akina nani na wanaolipwa ni akina nani. Zipo nyumba ambazo zimeandikwa “Msajili wa Majumba”, lakini kodi hailipwi Serikalini, wanalipwa watu binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni kuhusu viwanja ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema atavichukua au ameshavichukua, siwezi kufahamu. Naomba niseme kwamba, muda ambao umeandaliwa katika sheria ile ambao ni miezi 36 ni muda ambao kulikuwa na *THB*, lakini sasa *THB* ile haipo. Hata hizo nyumba ambazo nilisema Mwalimu Nyerere alizichukua, wale waliojenga zile nyumba walikwenda kukopa *THB*. Ushahidi wa gazeti hili la Rai la Juni 9 – 15 ninao. Humu wametoa matangazo wale wote waliokwenda kukopa *THB* waende kuchukua hati zao za nyumba.

Sasa hawa wote walikwenda kukopa ndiyo maana nyumba zilionekana nzuri na zikataifishwa. Hata tukizingatia kwenye gazeti hili, ile *Bugando Hospital* na yenyewe walienda kukopa *THB* ndiyo wakajenga hospitali ile, *CDA Dodoma* walikwenda kukopa *THB* wakajenga nyumba hizi za Dodoma. Sasa mwananchi wa kawaida hata awe Katibu Mkuu wa Wizara, mshahara anaopata awe anasomesha mtoto, anakula nyumbani kwake, ina maana ni kwa muda gani ataweza kujenga nyumba na kuweza kuikamilisha kama siyo wizi au hajatumia njia nyingine yoyote ambayo itakuwa ni kinyume cha utaratibu! (*Makofi*)

Pili, tusikae tunawalinganisha wananchi wetu na sisi baadhi yetu. Nyumba zile wameuziana au wameuziwa na Serikali ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwamba muda wa
Mzungumzaji kumalizika)*

MHE. AZIZA S. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono kama Mheshimiwa Waziri atanjibu.

MWENYEKITI: Tunakushukuru Mheshimiwa na tunaomba hizo karatasi ulizosema utawasilisha Mezani.

MHE. PONSANO D. NYAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami nakupongeza kwa kazi yako nzuri na ninakuombea kila aina ya baraka Kiti hicho uendelee kudumu nacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati dada yangu mdogo Mheshimiwa Aziza anasema anaona mashaka kuunga mkono Bajeti ya kaka yangu, mimi nategemea kuiunga mkono, lakini nitasemea machache mawili/matatu. Nasema hivyo kwa sababu kwanza Mheshimiwa Aziza ameongea vizuri sana na naomba niwapeni ujumbe. Nilipokuwa ninatembea katika baadhi ya Mikoa wakati Bunge linaendelea, akina mama wengi na hata wanaume wengi wameridhishwa sana na michango inayotolewa na akina mama kwa kipindi hiki. Wanasema wamekuwa jasiri, wanasema mambo mengi ya msingi na waliyofuatilia na wana uhakika na yale wanayoyasema. Kwa hiyo, naomba kumpongeza Mheshimiwa Aziza, amesema vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kama ifuatavyo: Tunaposemea ardhi ina matumizi mengi, tunatazama kilimo, hapo hapo ni kwenye ardhi, maji ni kwenye ardhi, madini ni kwenye ardhi, chakula tunachopata ni kutokana na ardhi, pamoja

na uhai wa viumbe vyote vinavyoishi ni ardhi. Kwa hiyo, ardhi ni roho na kwa kweli ni matumaini ya maisha ya viumbe vyote vinavyoishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuja kwenye suala la ugawaji wa ardhi hasa katika suala zima la kumilikisha, ardhi kwa umuhimu wa kwanza amilikishwe mwananchi wa eneo linalohusika. Mwenyezi Mungu alipotumba ametumia udongo (ardhi), ili atupatie uwezo, katumia pumzi yake.

Kwa hiyo, umuhimu wa ardhi ni kwa kila binadamu mahali alipo na Mwenyezi Mungu katupatia ardhi kwa kutuweka kila watu sehemu zao. Kama ni Wachaga watakaa eneo lao, kama ni Wafipa watakaa eneo lao, Wazungu eneo lao na wengine maeneo yao. Iweje basi kama mimi nimepewa eneo langu la Tanzania tena la Nkasi au eneo lolote lile la Dar es Salaam, la Unguja, la Pemba la Chato, anakuja mwananchi wa kutoka eneo lingine anachukua eneo alilonipa Mwenyezi Mungu, mimi ninapewa *second hand* au kutopewa kabisa. Yule aliyekuja mgeni ndiyo anakuwa wa kwanza kupewa. Iweje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Magufuli ninaamini kwa umahiri ulionao na jinsi ambavyo amekuwa akifanya kazi vizuri, ingawa wengi wanamwonea wivu, unapokuwa katika Wizara hii iliyokuwa imeoza, ninajua atairekebisha. Nasema aendeleo na uzi huo huo, wengi tunamuunga mkono na wananchi wengi wanamuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotazama suala la upimaji wa ardhi, kama kawaida, tumekuwa na baadhi ya viongozi wanaojipendelea. Nani ambaye atakataa kwamba walio wasomi wengi ni wale wanaotoka maeneo ya Kaskazini? Kwa hiyo, tunaposema maendeleo, tunatazama eneo la Kaskazini. Kama ni Vijiji, utakuta maeneo ya Kaskazini yamepimwa, lakini maeneo ya Kusini mengi hayajapimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juzi tu ndiyo Iringa imepimwapimwa, mengine yamesahaulika. Kwa nini? Tunajaribu kutazama Sheria ya Ardhi ya Umma pamoja na ile Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999, Sheria Na. 4 pamoja na ile Na. 5 zikienda pamoja. Pale tunaona kwamba, umuhimu wa kwanza Vijiji ndiyo vinapewa ardhi. Lakini Vijiji hivyo hivyo havina ardhi iliyopimwa, ndiyo maana migogoro inakuwa mingi. Wanavijiji wanagombana: “Mpaka wangu huu, mpaka wangu huu.” Vijiji hivyo havijapimwa. Ninaomba Wizara hii ishughulikie sana suala la upimaji wa ardhi za Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri pale aliposema kwamba ataweza kutoa michoro ya ramani ya kila Wilaya kwa mipaka yao na kusisitiza viongozi wa Wilaya hizo wakae vikao vya ujirani mwema kutambua mipaka yao. Hilo nalipongeza sana, tena naomba ikiwezekana lifanyike mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama Sheria Na. 2 ya mwaka 2002 ni sheria ile inayotoa mamlaka kwa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, Kata, Wilaya na kuendelea. Ninachoomba hapa, kwanza Wizara ijitahidi kutoa ile Sheria ya Ardhi ambayo imetafsiriwa kwa Kiswahili ili kusudi Mabaraza haya, pamoja na wanavijiji wenyewe

waweze kuelewa sheria yenyewe, maana tumeyapa Mabaraza mamlaka, lakini hawana mafunzo na wengi hawajui nini la kufanya. Kwa hiyo, wapewe mafunzo ili wasiendelee kuingiliwa na Mahakama za Mwanzo ambazo zinavunja sheria. *(Makofi)*

Nilipokuwa katika ziara ya Vijiji vyangu, kitu cha kwanza ilikuwa ni kujua: Je, katika kila Kijiji ile Kamati ya Ardhi ya watu saba ipo na imezingatia sheria kwamba kama wapo wanaume, wapo wanne? Wanawake watatu ni lazima wawepo pia! Maeneo mengine nilikokuta sheria imekiukwa, nilisema kwa kweli Kamati hii ni batili. Fanyeni tena uchaguzi mwingine, wamefanya hivyo. Vijiji vyangu vyote vya Nkasi 102 vimeshafanya uchaguzi huo, bahati mbaya hawana vitabu vya sheria. Nilikuwa naomba vitabu vya sheria pamoja na mafunzo maalum. *(Makofi)*

Mahali nilipokuta Mahakama za Mwanzo, labda unakuta kesi yao ni ya mwaka 2003/2004 Mahakama za Mwanzo, zimeamua migogoro ya ardhi, nimekuwa nikiwaelekeza wananchi kwamba kwanza hiyo ni batili. Mahakama hizo tena hazina mamlaka. Wanachoweza kushughulikia ni kama endapo katika kugombania ardhi, vitendo vya jinai vilifanyika kama vile kupigana na kuumizana. Hivyo ndivyo vinavyoweza kwenda Mahakama ya Mwanzo na kadhalika. *(Makofi)*

Lakini sio pale ambapo mgogoro ni wa ardhi tu, Mabaraza yale ndiyo yanayohusika. Pale ambapo tayari Mahakama zilikuwa zimekwishaamua, nimewaelekeza wananchi kisheria na nadhani ndiyo hivyo na nimelifuatilia, bahati nzuri Jaji anayehusika akasema ndiyo hivyo. Kwa hiyo, pale Mahakama zilipoamua hivyo ni kinyume cha sheria wananchi wanaohusika walirudisha suala hilo Mahakama ya Wilaya itatengua. Kwa hiyo, mahali popote Tanzania ambapo pana tatizo hilo waweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba utoaji wa hatimiliki katika Vijiji na wale wanaomiliki hasa wazalendo upewe umuhimu wa kwanza. Lakini andaeni mafunzo maalum ya matumizi ya ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Mazingira, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara nyingine zinazohusika na masuala ya ardhi ili kusudi wananchi waweze kujua matumizi sahihi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mambo ya ujenzi wa nyumba pamoja na makazi, ninachoshangaa ni kuona viongozi au watumishi wa Idara zinazohusika na ardhi ndiyo wanakuwa wa kwanza kujipatia viwanja vingi, kutoa *double allocation* ya viwanja na kusababisha migogoro mingi. Hili Mheshimiwa Waziri ameshaanza kulishughulikia. Mimi nafurahi na nampongeza sana. Aanzie huko huko. Huwezi ukampiga nyoka kwa kuanzia mkiani, unanza kumpita nyoka ukianza kichwani. Nyoka mwenye sumu kichwa chake kiko pale kwake kwenye Wizara hiyo. Aanze kwanza kupiga kile kichwa, halafu aje analizie kwenye mkia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati kengele inagonga. Upimaji wa viwanja katika Miji, kuna Miji mipya midogo na kadhalika inapima viwanja. Lakini hamfuatili ujenzi yake, nyumba inajengwa inakwisha ndipo mnakuja mnasema hapa ulijenga haitakiwi, bomoa. Je, wale Maafisa Ardhi wanakuwa wako wapi? *(Makofi)*

Jiji la Dar es Salaam, ukipita angani kwenye ndege ni kama vile mabati machafu yaliyozolewa yakatupwa jalalani. Ni maeneo machache tu kama vile Msasani, Osterbay na *Mbezi Beach* ndiyo yanaonekana kama kule kuna Mji.

Huo wote ni upimaji mbovu wa kutokuwa na Mitaa na pale inapopimwa hamzingatii nyumba zinapojengwa zijengwe za aina gani kwa sababu hamtoi ramani kwa wananchi. Kwa hiyo, mwananchi anajiundia tu ramani kichwani, wanajenga nyumba wanayotaka. Naomba kitengo cha ramani kianzishwe, ziwepo nzuri ili wananchi waweze kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba katika suala zima la *planning*, makazi haya kwenye Wilaya mpya na Miji midogo na kadhalika, iwepo kama vile Dodoma ambayo ina *plan* kama hiyo. Nilipotembelea Kijiji fulani cha Mpitimbi, Songea kwenye Jimbo la Peramiho, nilikuta hakuna mipango yoyote. Kwanza Maafisa Ardhi hawana. Kuna migogoro mikubwa na mimi nampongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kushughulikia sana suala lile, naomba uzidi kutuelimisha wengine ili tunapopata matatizo kama hayo tuweze kuyatatua. Kwa hiyo, naomba Maafisa Ardhi wapewe pia vifaa vya kupimia viwanja ili kusudi waweze kuifanya kazi hiyo kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Manispaa ya Dodoma na hasa *CDA* kwa kujali na kuzingatia ujenzi mzuri wa nyumba hapa Dodoma, upimaji wa viwanja na hata utoaji wa viwanja kwa haraka. Ninaomba waendeleo na hilo na maeneo mengine waige mfano huo. (*Makofi*)

Mwisho kabisa, ni katika ule mfuko wa kukopesha Halmshauri ili kusudi zipime viwanja. Nkasi ilikuwa ni ya kwanza kukopa mwaka 1999 na tukarudisha mwaka 2000 kwa faida na ni Halmshauri 10 ndio zimerudisha tena nyingi za Kusini, za Kaskazini takribani zote hakuna iliyorudisha hata moja na wamekopa mamilioni mengi ya fedha, hawarudishi. Tunaomba mfuatilie: Je, wamezifanyia kazi au wamekula? Kwetu, tumefanyia kazi na tumerudisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, aone umuhimu katika hizi Halmshauri 10 ambazo zilikopa na zikarudisha *surplus*, saba zimerudisha *surplus*, tatu zimerudisha ile ile iliyokopwa uweze kuzishawishi au zishawishike kwenda kukopa zaidi ili kusudi wapima viwanja zaidi Miji yao iendelee kupendekeza. (*Makofi*)

Mwisho kabisa, naomba wananchi wengi mtembelee Miji kama vile ya Sumbawanga, Nkasi na Mpanda, hatujengi kiholela, tunajenga vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nikushukuru wewe. Napenda nimshukuru Waziri na Naibu wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa hotuba ambayo inajieleza vizuri. Bahati nzuri mimi niko kwenye Kamati ya Ardhi na Kilimo. Napenda pia nimshukuru

aliyekuwa Waziri wa Awamu iliyopita, Mheshimiwa Gideon Cheyo kwa mchango wake mkubwa. *(Makofi)*

Katika Azimio la Arusha, tulisema, ili tuendelee, tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Nafikiri hiyo inabaki mpaka leo. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri amebainisha katika malengo yake ya mwaka 2006/2007, kwamba lengo mojawapo ni kuwawezesha wananchi kutumia rasilimali ardhi kama nyenzo muhimu ya kuwaletea maendeleo na kuondoa umaskini. Kwa maana hiyo, inasisitiza umuhimu wa ardhi. Pia, akasema kuongeza idadi ya mashamba na viwanja vitakavyopima kwa kipindi hiki. Mimi naungana naye na ndiyo tutakuwa na maendeleo katika Sekta hii muhimu ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwarudishe nyuma kidogo. Wakati nachangia kwenye Bajeti ya Kilimo, nilisema kwamba Mheshimiwa Rais, wakati anawapongeza wananchi wa Morogoro, alisema angependa Mkoa wa Morogoro tuingia kwenye Mikoa inayozalisha chakula. Sasa Rais akishasema hivyo, ni agizo. Kinachobaki ni utekelezaji. Tutakeleza vipi? Kwa sababu lengo ni kutumia rasilimali ardhi ambayo amesema ni nyenzo muhimu kwa kuwapa wananchi wetu uwezo wa kuzalisha chakula. *(Makofi)*

Sasa mimi naomba niongelee zaidi mchango wa ardhi ambayo tunaiweka kwa wenzetu wawekezaji. Bahati nzuri mimi katika Wilaya yangu na Wilaya ya jirani ya Ulanga, sisi tuna ardhi ya kutosha ya kuweza kuwaita wenzetu waje wawekeze. Kwa maana hiyo, natekeleza hilo alilosema Rais kwamba anataka Mkoa tuzalishe chakula kwa niaba yenu nyinyi wenzetu wa Tanzania. Tunapiga kelele ili yatekelezeke haya tunayoyaongea. Bahati nzuri yale yaliyotokea Mbarali kwa upande wangu mimi naona ni changamoto kwamba sasa hivi watu wanaelewa umuhimu wa ardhi pamoja na migongano hiyo, lakini *at least* mwananchi wa kawaida anajua ardhi maana yake nini.

Sasa sisi katika Mkoa wa Morogoro, tunaishukuru Serikali, tumepata *scheme* 63 za umwagiliaji maji kwa kipindi hiki, mpaka mwaka 2010. Kwa hiyo, ni mojawapo tutapiga hatua kwa matumizi ya ardhi. Lakini nataka niongelee ardhi ambayo ina mashamba makubwa. Mimi katika Wilaya yangu, nina mashamba matano makubwa. Manne ndiyo nataka niyaongelelee zaidi.

Baadhi ya Wabunge wamefika Chita *JKT* pale, tuna shamba la hekta kama 7,000 halina mwekezaji. Wenyewe Jeshi wanajaribu kutafuta sasa mwekezaji, lakini kuna vitu ambavyo mwekezaji anataka akija aone. Katika mradi wa viwanja 20,000 pale Dar es Salaam ukienda Mbweni, Ukienda Boko, Mbweni Mpiji, Mbweni *JKT* kuna miundombinu inatangulia halafu sisi tunaonunua viwanja ndiyo tunakuja kufanya kazi ya mwisho;; barabara za Mitaa, umeme, maji kwa hiyo wewe unakuja unaweka nyumba yako pale. *(Makofi)*

Hali kadhalika, kwenye uwekezaji wa mashamba makubwa viti hivi ni muhimu. Sasa mwekezaji unamwonyesha pori hili hapa amepitia Wizara ya Ardhi amepewa ardhi, amepitia *TIC* amepewa kibali, anakuja anaonyeshwa pori, hakuna umeme, hakuna maji, hakuna miundombinu kama barabara na hakuna hata simu. Sasa mimi mwezi uliopita

nilipata wageni kutoka Roseanna Marekani wao kule wanalima mpunga wakaja wakaliangalia shamba letu la Mgeta, wakalipenda.

Lakini wakinieleza kitu kimoja, tulivyoongea Dar es Salaam kwamba Mheshimiwa *MP* katika maisha yetu sisi hatujawahi kukaa siku tano bila kuongea na wake zetu. Japo kwako tumekaa siku tano bila kuongea, hakuna mawasiliano ya simu. Likaja la barabara, wanasema *We think when we come back next time the road will be better*. Sasa mimi kama Mbunge nitasemaje? Sasa ndiyo itakuwa *better*. Nataka waje, lakini *how better*, mimi nitawezeshaje kuifanya ile barabara iwe nzuri? Wale watu shamba lile wamelipenda na sisi kwa *production* yetu tunasema hekta moja ingetupa gunia 50, lakini wao walisema tunaweza kupata tani 20 kwa hekta, yaani kilo 20,000 ambayo ni tani 20 na wanasema tunaweza kulima mara mbili kama tutamaliza miundombinu ya bwawa la kumwagilia ndiyo vitu tunavyotaka sasa hivi. (*Makofi*)

Sasa na shamba hilo la *JKT* - Chita bahati nzuri Wanajeshi wenyewe wanatafuta wawekezaji na shamba hilo ambalo wa Roseanna wamekuja. Nina shamba la Lwipa ambapo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alisema tutatafuta wawekezaji.

Sasa hapa naomba niongelee kitu kimoja, yupo mwekezaji mmoja ambaye anaitwa *Lwipa Sugar Company Limited Al-Hashu Investment Tanzania Limited*. Hawa wameanzia Kijijini, wameomba ardhi Kijijini wamekwenda mpaka Wilayani, Wilaya wakasema ardhi mnayoomba ni kubwa, tutaipeleka kwa Kamishna wa *lands*, imekuja kwa Mheshimiwa Waziri.

Halafu yupo mwekezaji ambaye yuko *Kilombero Sugar Company Ilovo*, Wizara inampa Ilovo. Mheshimiwa Waziri katika Bajeti yake alisema Ilovo anapendekeza iendele na *capacity expansion* yao. Ilovo inashindwa kumaliza miwa ya Kilombero mpaka Kiberege, leo unampa tena ardhi nyingine, si atahodhi tu! Sisi wenyeji wa kule tulipenda uwepo ushindani kwa kuwapa kampuni nyingine ambayo ndiyo hiyo *Al - Hashu*. Kile nasikia *Al - Hashu* wamenyimwa ardhi, Ilovo wamepewa ile ardhi. Vitu hivi vya kutoa ardhi ni vizuri Kamishna afike *physically* aende pale, wale wameongea na wana kijiji, ile kampuni nyingine, huyu mwingine amepewa tu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ligallama iweke *microphone* yako vizuri kidogo usikike vizuri.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Huyu mwingine anapewa tu; huyu mwingine amefuata taratibu Kijijini wamemkubalia Wilayani, wamesema ardhi ni kubwa unayoomba tupeleke Wizarani. Sasa Wizara nasikia inampa Ilovo. Ilovo miwa nasikia kule hamalizi, anakuja anapewa tena sehemu mpya, anakuja kuhodhi ardhi na sisi tunataka uzalishaji sasa hivi. Kwa nini tumsilete huyu akaleta ushindani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Waziri hapa katika majumuisho atueleza ni kigezo gani walichotumia kumnyima huyu *Al-Hashu Investment Tanzania Limited* ardhi hiyo wakampa Ilovo? Ilovo wakasema anafidia ardhi ambayo tumewapa Kijiji sisi kule. Wakati wa ujamaa tuliweka baadhi ya Vijiji vyetu ndani ya shamba la Kilombero. Sasa

kwa sababu tumeliuliza, wale wanadai fidia eneo lile tuliwapa Vijiji. Lakini eneo lile halifikii kiasi walichotoa wao. Lile eneo linafika kama hekta 4,900 tu, kwa hiyo, tunaomba hapa Waziri atueleze kwa nini hii Kampuni nyingine ambayo iko tayari kujenga kiwanda isifanye kazi hiyo?

Suala lingine ni kuhusu ndugu zetu wa Taasisi za Mambo ya Ndani, Magereza. Nafikiri siyo kwetu tu, ni sehemu nyingi wana tabia ya kuhodhi maeneo makubwa, hawawezi kuyalima na hawataweza kuyalima hata siku moja wakayamaliza. Sasa kuna wananchi wanazunguka maeneo haya kuwepo na sheria, mbona sisi ukichukua kiwanja cha kujenga nyumba unapewa miezi 36? Hao Magereza kwa nini nao wasipewe muda? Kama hawawezi tupunguze, watu walime. Tunataka *production* ya chakula, kusiwe na njaa tena hapa. (*Makofi*)

Sehemu ya Gereza la Kiberege kuna Kijiji cha Sululu pale Ziginali wao wanalamika kwangu kwamba mashamba ya Magereza ndiyo yamekuwa ni maficho ya wanyama waharibifu wa mazao. Basi wawaachie hawa wananchi walime hata *lease* walipe hata magunia mawili mawili ili mradi tuwalishe wafungwa wetu, Gereza lijitegemee kuliko kuhodhi ardhi miaka nenda miaka rudi na haitawezekana siku moja Gereza lolote lile lenye ardhi hiyo wamalize kulima, haitawezekana. Kwa hiyo, tupitisha sheria, labda Waziri utaona jinsi utakavyofanya ili kama hawawezi kabisa imegwe, sisi tumeongezeka!

Kama Wilaya yangu, watu wengi wamehamia na hatuwezi kuwafukuza. Ni watu wana uhuru wa kuhamia mahali popote wanapotaka. Lakini ardhi kama hawana, imegwe hiyo ardhi inayokaa miaka nenda miaka rudi. Kuna Gereza la Kiberege na Gereza la Idete nalo lina tatizo hilo. Aidha, vifanyike vitu viwili wa-*lease* kwa gunia mbili mbili kama ni ekari 200 si unapata gunia 400 bwana! Si hujalisha Askari, si linakuwa Gereza limejitegemea kwa chakula! Au wawaruhusu tu walime, si wananchi wanasafisha shamba! Kwa hiyo, hayo mawili naomba yatekelezwe na Waziri ataona jinsi anavyofanya mwenyewe. (*Makofi*)

Baada ya kuongea hayo, naomba sana, hasa wenzetu wanaokuja kuwekeza kwenye mashamba yetu tuwape umuhimu wa pekee wakute kila kitu kipo. Najua sio jukumu la Mheshimiwa Waziri kuweka umeme, lakini aongee na Waziri wa Nishati na Madini kwamba pale tuna shamba tume- *remark* na watu wanataka kuja peleka *IRT*. Hii *energizing rural transformation* kuwe na vipaumbele, tusipeleke tu umeme ilimradi tu kuwasha nyumbani; sasa sisi tunataka kuzalisha chakula kwa ajira ya Tanzania. *IRT project* isiende tu hovyoyovyoyo. Siku zote nasema mimi nazalisha umeme, inaniuma sana, umeme unatoka Kihansi unapita tu na mashamba yote haya yanapita tu hayo niliyoyataja manne yanapitwa tu na umeme hakuna. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba sana bahati mbaya siwaoni wahusika, lakini *Hansard* ipo, watasoma kwamba tunaomba mashamba haya yapewe umeme, yapewe miundombinu, maji, sisi tunayo maji msitupe, tutatafuta wenyewe tutaweka, lakini umeme uwepo. Hawa wawekezaji hawaelewi, wakija hapa wanaona hakuna umeme, hakuna hata simu, hata barabara, barabara hiyo hiyo yule Mzungu anasema nimeumia kiuno na kilometa

sijui 70 tu, Mzungu ameshika kiuno chake, anasema bwana nikija tena itakuwaje barabara hii? Sasa tunapoteza wawekezaji kwa sababu ya barabara. Tunaomba barabara itengenezwa ili tuweke *conducive environment for investment* kwamba tunataka kuongelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii. (Makofi)

MWENYEKITI: Nina tangazo dogo kabla hatujaendelea na Mheshimiwa Abbas Mtemvu, linawahusu Wabunge walioteuliwa na Spika, kuhudhuria *workshop* itakayofanyika *Kilimanjaro Kempiskei Hotel* na wamepata bahasha kubwa za kaki kwenye meza zao leo hii wanaombwa kuhudhuria kikao sasa hivi kinachoendelea katika Ukumbi wa zamani wa Bunge.

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ya Bajeti na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara. Lakini pia niungane na mwenzangu nimpongeze sana Waziri aliyetangulia katika Wizara hiyo ambaye ni jirani yetu, Mheshimiwa Cheyo kwa kazi nzuri aliyofanya na yeye ya kubadilisha Wizara hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara yangu ya pili kuchangia. Mara ya kwanza nilichangia Hotuba ya Waziri Mkuu, lakini nirudie kusema tena, nawashukuru sana wananchi wa Temeke kwa kunichagua kwa kura nyingi sana za kishindo kuwa Mbunge wao wa kishindo na mimi nawaahidi sitawaangusha, nitawatumikia kwa kadri ya uwezo wangu ambao Mwenyezi Mungu atanijalia kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kidogo katika Wizara hii muhimu sana. Nirudie tena kumpongeza Waziri wetu na nimkumbushe kwamba, wananchi wa Temeke wanamkumbuka wakati wa kampeni alitutelemba pale Mbonde, Yangu Macho na Tandika na ulizungumza sana. Aliwapa ahadi nzuri sana, wananisumbua sana, lakini nimewaambia, ninavyomjua Mheshimiwa Waziri, atatekeleza tu. Kwa hiyo, nikimfuata ajue nafuatilia ile ahadi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie Shirika la Nyumba. Kwanza nirejee kumpongeza Mheshimiwa Waziri. Waziri aliyetoka alifanyakazi nzuri sana ya kuhakikisha wafanyakazi wanaweza kupata nyumba na kumiliki wenyewe. Temeke wananchi wengi tu wamepata nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa, tatizo ni kama lile la dada yangu Aziza kwamba wengi hawajapata hati. Naamini kwamba utakaposhughulikia la Tabora na la Dar es Salaam Temeke utalishughulikia.

Lakini nirejee hapo hapo, faida gani tunaona sasa baada ya wananchi wale kuuziwa nyumba zile? Nyumba zimekuwa safi, nyumba zile zinapendekeza. Sasa ombi langu, mmeleta mgawanyiko mkubwa sana kwa sababu sijui ni Kiswahili kizuri, nikisema mliwauzia wale ambao wana nyumba za chini na nyumba za maghorofani

hawakupata haki hiyo. Sasa maeneo ya pale Chang'ombe *Flat*, Keko, Tandika Maghorofani, nikiondoa Temeke *Quarter* pale ambapo wana mgogoro wa Mahakamani, lakini nikienda na Ilala na Dar es Salaam kwa ujumla wananchi wengi wamekuwa na huzuni juu ya suala hilo.

Kwa hiyo, ningeshukuru sana Mheshimiwa Waziri, leo angezungumza kidogo, sijui Wizara yake inasemaje kuhusu wananchi wale wa maghorofani ambao na wao wanastahili kuuziwa nyumba zile kama *apartment!* Mandhari tulitenda kwa wakubwa, basi na wadogo tutende ili na wao wale matunda ya nchi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie tena katika suala la viwanja. Tunapozungumza viwanja kunyang'anywa na kuuzwa, kwa kweli waathirika wakubwa tutakuwa Dar es Salaam. Ndugu zangu, mimi nataka kuwaambia Dar es Salaam huwa tunapata shida kweli wakati wa kampeni. Sasa mengine tunaomba mtusaidie mtuonee huruma. Kule Temeke tulipata shida kweli! Kuhusu *Kilwa Road*, ilivunjwa kabla ya wakati, kulikuwa hakuna maelezo, hakuna fidia, basi ilikuwa hekaheka, kura tulizitafuta kwa kupiga magoti. Sasa ombi langu nimwombe Mheshimiwa Waziri hebu alifikirie hili, maana yake toka waingie Wizara ile ndio kwanza wana miezi saba au nane. Hebu akae kwanza atulie japo miaka miwili ndiyo afikirie kunyang'anya viwanja hivyo. (*Makofi*)

Sheria zipo, hatukatai, lakini ubinadamu na hii Serikali ya Awamu ya Nne inasifiwa sana kwa ubinadamu na uungwana, lakini viko vigezo vya msingi vinavyofanywa watu wale washindwe kujenga. Hatuna Benki ya Nyumba. Nchi zote duniani zina mabengi ya nyumba ndizo ambazo zinasaidia wananchi wao wanyonge wanapewa viwanja, wanapewa hati wanakwenda kwenye mabengi ya nyumba wanakopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo unamnyang'anya maskini huyu ambaye alikuwa pale kwenye bonde la Jangwani amenunua kiwanja *Mbezi Beach* au Tegeta kwa bei kubwa unamnyang'anya, unakwenda kukiiza kwa tenda, tena sisi watu wa Dar es Salaam tulishangaa kweli kusikia Mheshimiwa Waziri anataka kuuza viwanja kwa tenda. Unatarajia kiwanja kile atapata mnyonge? Hawezi kupata mnyonge, unataka kumnyang'anya mnyonge umpelekee tajiri ambaye tayari anacho, unataka kumwongezea! (*Makofi*)

Lakini Mheshimiwa Waziri, kuna moja mimi sijui maana yake. Mimi ni Mwenyekiti wa Wabunge wote wa Dar es Salaam, ndiyo maana nikisema naisemea Dar es Salaam yote, kunyang'anya viwanja vya Mbezi na Tegeta pia unamuumiza Naibu Waziri. Sijui kama unalijua, maana ndiyo Mbunge wa kule. Kama hasemi, lakini kwenye vikao vyetu vya Mkoa ananung'unika chini chini.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri hili alitazame kwa makini, tulipe muda. Kama iko haraka ya kunyang'anya viwanja, viko viwanja sisi Dar es Salaam tutawaambieni. (*Makofi*)

Pale kwangu Yombo Makangarawe kuna kiwanja ekari karibu 4,000 wamemilikishwa watu toka mwaka 1939 mpaka leo hakijaendelezwa. Tunaweza kuanzia hapo. Tuna Mzungu mwingine Mbagala, kaanza Mbagala mpaka Mkuranga wote tunamjua. Nilikuwa Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, pale tunayo maeneo mengi ya kunyang'anya na kugawa. Mheshimiwa Waziri chonde chonde, hebu hili kwanza lipe muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kulipa muda, basi tutafakari kweli tuna lengo la kuwasaidia wananchi wetu tutafakari namna ya kuanzisha Benki ya Nyumba, tutafakari kweli kama tuna lengo la kuwasaidia wananchi wetu tutafakari namna ya kuanzisha nyumba kwa haraka. Ule mpango alioanzisha Mzee Cheyo, ndiyo maana nampongeza sana wa kwamba unapata kiwanja unapata na hati. Tukiwa na Benki, mtu anapata hati yake anakwenda kwenye Benki anapata fedha, anajenga nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoanzisha mpango huu wa kupima viwanja Dar es Salaam, lengo letu kubwa lilikuwa kuondoa watu wa mabondeni ambao walikuwa karibu na kaya 5,500 aliniambia Katibu Mkuu akiwa Mbunge kabla hajawa Katibu Mkuu.

Lakini toka tumeanza mpango huu, hata kwenye hotuba yake hawataji kabisa wale watu wa mabondeni. Juzi *RC* wangu ametamka watu wale wa mabondeni wanatakiwa kuondoka na sisi Wabunge kwa kweli tunaunga mkono hilo, hatupingi. Lakini hawa tuliwalenga sana kwenye viwanja vile. Sasa sijui tunawapeleka wapi! Sijui katika huu mpango wa upimaji viwanja nao tumewapa! Lakini sio hivyo, viwanja vyenyewe navyo bei yake ni kubwa. Kiwanja milioni moja, milioni mbili, milioni tatu. Hebu nalo hilo tulitazame. *(Makofi)*

Lakini sio hivyo tu, kama Mheshimiwa Waziri atashikilia kuchukua viwanja hivyo, basi afikirie masuala ya viwanja hivyo tuvitoe sasa, kwa sababu Dar es Salaam tuna uhaba mkubwa wa viwanja vya shule kuliko kuuza kwa tenda. Tuvitoe, tujenge mashule, hatuna masoko, hatuna viwanja vya kuchezea watoto, hatuna viwanja vya mpira, itakuwa siyo wazo baya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunateleza teleza, wengine ni mara ya kwanza tunaingia Bungeni, ndio tunajifunza. Mara nyingi ndio maana tunakuwa kimya hatutaki kuwa na haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya ardhi, juzi tu tuliangalia kwenye *TV*, tukaona kuna Mkorea mmoja ameingia kule Vijibweni amejichukulia eneo anavyojua mwenyewe, wananchi wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namwomba sana Mheshimiwa Waziri, katika suala ambalo napenda alipe kipaumbele katika Wizara ile ni kuondoa migogoro. Migogoro ile inaletwa na watu ambao wako pale pale kwenye Wizara.

Leo pale Dar es Salaam kuna magorofa tunaambiwa baada ya Wakaguzi kupita, magorofa karibu 50 yameonekana yana matatizo. Lakini unakaa unajiuliza, vibali vya kujenga walipata wapi hawa? Walijiandikia wenyewe? Basi sasa tuwe na maamuzi.

Tunapoamua kuvunja magorofa kama hayo na wahusika wote waliokuwa kipindi kile kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wawajibike. *(Makofi)*

Maana yake, unakaaje kwenye Wizara, Watendaji wako wanatoa vibali vya kujenga majengo ambayo yana mushkeli, halafu baadaye wenye majengo wanavunjiwa nyumba lakini wao wanabaki. Mimi nafikiri hivi sasa tuwe na utaratibu wa kueleweka namna hiyo. Lakini bado liko tatizo kwenye Wizara, bado kuna Watendaji, kwa kweli wana matatizo.

Mimi na Mheshimiwa Zungu tuliwahi kufika pale, tukiwa tunafuatilia wananchi wetu. Wako Wazee kama Mzee Kimicho, Jaji yuko Saba Saba Mbagala kule, ameomba kiwanja chake kibadilishwe matumizi yatumike ya aina nyingine. Lakini imefika Halmashauri ikapitishiwa Temeke, imefika Wizarani leo karibu mwaka wa tatu. Huyu ni Jaji Mstaafu, anafanyiwa hivi. Je, mwananchi wa kawaida unatarajia nini?

Yuko Kamishna Mstaafu Pundugu, yuko pale Kigamboni, naye ameomba kubadilishiwa matumizi.

MWENYEKITI: Kengele ya pili, Mheshimiwa Mbunge!!

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ni kaka yangu, namheshimu, naunga mkono. Lakini kwenye mafungu tutaonana. Naona Mheshimiwa Waziri anacheka. *(Makofi)*

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia hoja ya hotuba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa John Magufuli, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Rita Mlaki, kwa hotuba nzuri na nawapongeza sana kwa kazi hiyo ya kuandaa hotuba nzuri waliyoileta mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maeneo machache ya kuboresha kwa ajili ya faida ya wananchi na nchi kwa jumla. Kama tunavyofahamu, ardhi ni moja ya misingi ya kujiletea maendeleo, kwamba kuna watu, ardhi, siasa safi, uongozi na siku hizi wanasema na mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua, ardhi haiongezeki. Lakini tunaokaa kwenye hii ardhi tunaongezeka. Kwa maana hiyo basi, ardhi inahitaji menejimenti kubwa sana, menejimenti makini ili kila mmoja anayeishi katika ardhi hii aweze kupata huduma muhimu na kuitumia ardhi hii ipasavyo kujiletea maendeleo yake. Kinyume chake ni kwamba kutakuwa na migogoro ya hapa na pale.

Ni dhahiri hapa kwetu nchini Tanzania kuna migogoro mingi ya ardhi. Ndiyo maana hata Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete amefikia hatua ya kutoa agizo kwa Halmashauri zetu kuondoa kero zilizokithiri.

Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba kuna matatizo makubwa ya ardhi katika nchi yetu, lakini sina hakika kama kweli agizo hili la Mheshimiwa Rais tumelipokea na kulifanyia kazi ipasavyo.

Nionavyo mimi, katika Jimbo langu, agizo hili bado halijafanyiwa kazi ipasavyo. Mheshimiwa Rais amelirudia agizo hilo akiwa nchini Nigeria, hii inaonyesha *seriousness* ya matatizo na migogoro ya ardhi tuliyonayo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, aya ya 29 niseme tu kwanza, katika Jimbo langu la Babati Vijijini, bado hatuna Mabaraza ya Ardhi yanayofanya kazi. Kinachofanyika pale ni Baraza la Ardhi na Nyumba Wilayani ndiyo inapokea matatizo ya wananchi. Kwa sababu siku hizi kule Vijijini, kwenye Kata, kwenye Vijiji, hakuna anayesikiliza matatizo ya wananchi. Kwa mujibu wa taratibu zilizoko sasa ni kwamba, Mabaraza hayo yangukuwa yanafanya kazi, lakini sasa hayafanyi kazi, yapo tu, yameanzishwa mahali hapa na pale.

Sasa sijui inakuwaje, lakini matokeo yake ni kwamba, wananchi wanalazimika kwa mfano kule kwangu wanasafiri kilomita 70 kutoka kona moja ya Wilaya kwenda Mkoani au Wilayani pale kufuata haki yao hiyo. Lakini wengi wanakata tamaa kwa sababu kwenda kilomita 70 ni gharama kubwa. Niseme tu kwamba, Baraza la Ardhi halina tofauti sana na Mahakama. Kwa hili, unakuta wanyonge wanakata tamaa. Tatizo kubwa zaidi ni kwamba Watendaji wa Vijiji na Kata hawafanyi kazi zao kabisa za utawala na matatizo mengi yanasababishwa na utawala.

Niseme tu kwamba, kwa mfano katika Kijiji kimoja, kinaitwa Endanachani, Kata ya Ayasanda Jimboni kwangu, mwananchi anayelitwa Abeid Ali alinyang'anywa shamba lake na Serikali ya Kijiji pamoja na kufika mpaka Makao Makuu hapa Dodoma kumwona Waziri Mkuu. Lakini pamoja na maagizo aliyopewa mwananchi huyo, bado kanyang'anywa shamba. Agizo la Waziri Mkuu halikutekelezwa. Sasa hatujui nani atalisikiliza tatizo la mwananchi huyu.

Mfano mwingine kwenye Jimbo langu, kuna wananchi ambao nitawataja mmoja mmoja angalau wananchi kama nane hivi wenye matatizo mbalimbali ili kuonyesha hali ya matatizo haya. Kuna mmoja anaitwa Amedeusu Yohani, huyu anahangaika na anahangaishwa na kesi ya Mahakamani kwa miaka mitano. Lakini *purely* suala la *administration* katika eneo husika wanaliacha hawaliangalii. Kuna mwingine anaitwa Mathayo Duwanghe. Sijui kama *Hansard* inaweza kunasa majina haya. Huyu, Baraza la Ardhi halikumsikiliza. Mwingine anaitwa Samuel Marko, Tsere Harry, Happe Slaa, Mama Amsi Lagwen. Hawa wamekata tamaa kabisa, wameachia kabisa mashamba yao kwa sababu hakuna anayewasilikiza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya kufuata kilomita 70 haki yao inakuwa ni taabu kweli kweli. Mwingine anaitwa Gabriel Malange, anahangaika sana Mahakamani kwa miaka mitano sasa na kesi ya ardhi sasa imegeuzwa kuwa kesi ya jinai. John Clement, shamba lake amenyang'anywa baada ya Baraza la Ardhi kutozingatia ushahidi uliotolewa kwenye Baraza. Kwa hiyo, mambo haya yanachanganyikana na yote kwa pamoja yanamzonga huyu mtu ambaye kwa kweli ni mnyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kijiji kingine cha Guse, mwanakijiji kashinda katika Baraza la Ardhi hilo la Wilaya. Pamoja na gharama kubwa aliyogharamikia, lakini maagizo yaliyotolewa na Baraza hilo la Ardhi hayakutekelezwa. Mtendaji wa Kata, Mtendaji wa Kijiji anatakiwa atekeleze, lakini hakutekeleza hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wote hao niliowataja wamepitia ngazi mbalimbali, hatua zote za kiutawala. Mtendaji wa Kijiji, Mtendaji wa Kata, Katibu Tarafa, DC hata Ofisi ya Mkoa, kote huko wamepita, lakini bado matatizo yao yapo pale pale. Sasa kama hatua zote hizi hazifanyi kazi, sijui mwananchi huyu aende wapi! Naomba Serikali isaidie ili, hatimaye wajue kwamba wako katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine kubwa katika Jimbo langu ni migogoro kati ya wakulima wakubwa na wananchi. Wakulima wakubwa na wanavijiji kwa mfano, mashamba ya Kiru yana migogoro mikubwa, mipaka yao wananchi wanasukumana na hao wakulima wakubwa. Naomba Serikali ilianganalie jambo hilo. *(Makofi)*

Mashamba ya *Rift Wall Estate* ya Magara. Wananchi wa jirani na mashamba hayo wanafikia hatua ya kuambiwa sasa waondoke, lakini wasijue waondoke waende wapi. Hayo mashamba waligawiwa na Serikali husika kama ni ya Kijiji na kadhalika. *(Makofi)*

Wananchi wapatao 44 wamelazimika kufuata ngazi mbalimbali wamefika kwa DC wamefika kwa RC, lakini bado hatima yao haijulikani. Wanachotakiwa ni kwamba waondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya tatu, kumekuwa na migogoro ya mipaka, kati ya *Tarangire National Park* na wananchi wa Vijiji vya Gijedebung, Ayamango na Gedamar katika Kata za Mamire na Galapo. *(Makofi)*

Hao wameagizwa wahame ifikapo tarehe 30 mwezi huu. Kwa hiyo, tuna siku chache tu karibu 20 wawe wameondoka. Hawajui waende wapi, lakini agizo hilo bado linasimama pale kwamba waondoke. Nasi tunauliza, wahame waende wapi? Walipo kuna matatizo gani? Ni ajabu kwa kweli.

Lakini tunapozungumza sasa hivi, wananchi hao katika maeneo hayo hayo wamejenga Shule za Msingi. Wamejenga Shule ya Msingi ya Manyara. Wamejenga Shule ya Msingi Morongi, wamejenga Shule ya Msingi Gijedabung. Pia, wananchi hao wamejenga mabwawa ya kuvunia maji ya mvua kwa ajili yao, kwa ajili ya mifugo yao na wote hao wamefanya kazi hiyo kwa kuhamasishwa kwa njia ya miradi shirikishi kwa mfano, wamejenga mabwawa kwa njia ya mradi shirikishi wa PADEP uliogharimu Shilingi milioni 30. Miradi ya uchimbaji visima vifupi, Shilingi milioni tatu. Haya maendeleo yamezingatia mpaka unaofahamika wa barabara ya *National Park* ambayo iko wazi tangu mwaka wa 70 *Tarangire National Park* ilipoanzishwa.

Sasa Halmashauri ya Wilaya ya Babati inafahamu na ndiyo maana imehamasisha wananchi wake kwamba wafanye kazi hiyo ya kujenga ya kujiletea maendeleo kwa

kujenga shule na kuchimba hayo mabwawa katika maeneo hayo ambayo yanafahamika kwa njia kama nilivyosema ni mpaka unaofahamika, ambao ni barabara ya *National Park*. Sasa leo wanaambiwa wahame na kwa vipi wahame? Wamekosa nini? Hili ni tatizo ambalo tunajiuliza na Serikali ilikuwa wapi wakati wanafanya shughuli za maendeleo? (*Makofi*)

Halmashauri ya Babati nayo ni Serikali. Sasa kama walihamasisha hawa watu, je, ni kosa la nani? Nani waadhibiwe? Kwa hiyo, mimi nafikiri tufahamishwe Serikali ina mpango gani kuhusiana na wananchi hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro mwingine, leo nazungumzia habari ya migogoro tu, kwa sababu kwa kweli tatizo kubwa ni migogoro na migogoro hii inawafanya wananchi wapoteze muda katika kuhangaikia utatuzi wake badala ya kufanya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni mpaka wa *Lake Manyara National Park*. Hawa wanazozana na Kijiji cha Mayoka iliyoko katika Kata ya Magara. Mara ya mwisho *TANAPA* na Kijiji cha Mayoka walizungumza kwa pamoja pale *AICC* Arusha na kuwekeana maazimio, lakini mpaka sasa maazimio hayo hayajatekelezwa, lakini bado mzozo huo upo na kwa kweli wanachoomba wananchi leo ni kwamba kuwe na Mkutano wa pamoja kati ya wadau ili waweze kufikia muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine katika Jimbo langu ni mgogoro wa kiwanda cha Mbolea cha Minjingu. Tatizo la kiwanda cha Mbolea cha Minjingu limekuwa ni tatizo la muda mrefu. Wananchi kwa kweli pale hawana maelewano. Lakini namshukuru Mkuu wa Mkoa, ameweza kukaa nao na matokeo bado yanasubiriwa. Lakini wananchi wana wasiwasi kwamba ushiriki wao haukuwa wa kutosha katika kujadili tatizo hilo kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ya kwangu ya msingi yalikuwa ni hayo na kabla labda sijagongewa kengele nyingine, niseme tu kwamba, naiomba Serikali Kuu au Serikali inayohusika sijui ya Mitaa au Serikali Kuu kwa njia ya Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ije Babati kufanya uchunguzi juu ya migogoro niliyoitaja, kwa sababu ni sugu na ni ya muda mrefu. Kwani *administration* ya Babati sasa haiwezi kufanya kazi hiyo kabisa, kutatua matatizo hayo ya wananchi yaliyokithiri kwa muda mrefu. Naomba Wizara ije Babati kutatua matatizo haya, wananchi wa Babati waweze kutulia, wananchi wa Babati waachane na migogoro na *TANAPA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kwa niaba ya Wahandisi wenzangu wote Tanzania, napenda kutoa pongezi kwa hawa Waheshimiwa Wahandisi Mawaziri wawili katika Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. (*Makofi*)

Vile vile, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Kampuni ya *Land Care* ambayo inaongozwa na mama kwa kutuongezea thamani katika eneo letu hili la hapa Bungeni kwa bustani nzuri zilizotengenezwa. (*Makofi*)

Naomba nichangie katika maeneo makuu mawili na kama nitakuwa na muda, nitaongezea maeneo mengine. Kwanza kuhusiana na *TIRDO*, Kiwanja cha *TIRDO* kilichopo Msasani, mimi ni Mjumbe wa Bodi. Kulikuwa na Hati ya *TIRDO* ambayo ilikuwa kiwanja chake kimemegwa kwa ajili ya kuipatia hospitali ya *CCBRT*. Uamuzi huo wa Serikali, nasema ulikuwa ni mzuri kwa sababu hospitali ile imekuwa na matumizi mazuri kwa walemavu na wagonjwa wengine.

Kwa hiyo, nasema ilikuwa ni maamuzi mazuri katika kutumia kiwanja hicho. Lakini sasa, kitu kinachonisikitisha ni kimoja, baada ya kugawa ardhi ile ni kwamba *CCBRT* yenyewe ilifanikiwa kupata hati zake. Lakini *TIRDO* ambayo ni Taasisi tunayoitegemea, haijaweza kupata hati mpaka leo. Hata ile hospitali ilipoongezewa kiwanja, wale ambao walipewa kwenda kuongeza kile kiwanja hawakujali kwamba pale pana *investment* nyingine zimeshafanyika kwa upande wa *TIRDO*.

Kwa mfano, *Cesspit tanks* pamoja na vibanda vya kutunzia uyoga. Kwa hiyo, mimi naona ilikuwa imefanyika kazi ambayo kiuhandisi haikufuata taratibu zinazostahili. Naomba Mheshimiwa Waziri afuatilie mgogoro huo ili uweze kukamilika na *TIRDO* kama Taasisi ya Serikali inayoaminika iweze kuwa na hati zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba nihamie kwenye mradi wa viwanja 20,000 ambao hasa nitazungumzia kwa upande wa Mbweni na Bunju. Pamoja na juhudi kubwa ambazo zimeshafanyika, ambazo nazipongeza sana kwa kuwa zimetatua hili tatizo la viwanja, mimi mtazamo wangu upo hasa katika miundombinu hususan ya umeme kwa wakazi ambao wanakuwa wamepangiwa viwanja vile. Mheshimiwa Waziri, inasikitisha sana kuona *TANESCO* jinsi inavyohangaika kwa ajili ya kuweza kuwahudumia wateja ambao wamekuwa wanapewa vile viwanja bila kufikiriwa kwamba katika gharama ambazo wamelipia zinahusika pia na mtandao wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba ujenzi wa *line* unatumia gharama kubwa na Mheshimiwa Waziri anafahamu. Imekuwa ni mara nyingi sana viwanja vinatolewa katika maeneo bila kuangalia kwamba hawa watu wanapata vipi umeme. Ujenzi wa kilomita moja ya umeme wa *vote* 11,000 unagharimu mpaka milioni 15 mpaka 20. Inategemeana na eneo. Vile vile, unapokuwa na viwanja 2,000 au 3,000, lazima kuwe na *sub-station* kubwa ya kuwawezesha hawa wateja kuwa na matumizi mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, panapokuwa hakuna mipango thabiti kama hiyo, matokeo yake kunakuwa na malalamiko makubwa ya watu kushindwa kupewa huduma hiyo na vile vile katika yale maeneo mengine ambayo viwanja vyake vimechanganywa kwa matumizi husababisha kuwa na matumizi ambayo yanasababisha athari kwenye vifaa vya watumiaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia pia eneo la Kinondoni. Eneo la Kinondoni limeshajaa. Linahitajika sasa hivi liongezwe *sub-station*, lakini hakuna kiwanja ambacho unaweza ukaweka *sub-station*. Upimaji hauzingatii huduma nyingine. Mara nyingi imekuwa upimaji, nasema kwangu ni kama vile mtu anakuwa anachora tu kwamba pawe na kiwanja. Hapajali kwamba watoaji huduma wengine wataweka wapi huduma zao. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba, kwa kuwa sasa Wizara hii wameichukua Wahandisi ambao wanafahamu matatizo ya kutokuwa na ushirikishwaji, tunaomba mlizingatie hilo. Ili huduma zote ziweze kutolewa inavyostahili.

Mfano mkubwa mwingine ambao naweza kuutoa ni ubadilishwaji wa majengo ya pale Kariakoo ambao ulisababisha *transforma* ya pale Ilala kuungua na hivyo kuwafanya watu kukosa umeme kwa kipindi cha wiki mbili, tatu. Hiyo yote ilikuwa ni malalamiko kwamba, nenda *TANESCO* au Wizara ya Nishati. Lakini ukiangalia ni nani ameanzisha tatizo ni Wizara ya Ardhi. Kwa hiyo, ninaomba kwamba mipango yote ni mizuri na tunahitaji. Lakini kimsingi basi mikakati hiyo iwe inaandaliwa mapema. Ikiwezekana, uchangiaji wa gharama uwepo. Kwa sababu kama tunavyojua Shirika hili limekuwa likifanya kazi zake hasa kwa kuzingatia mipango ya Kiserikali na ndiyo maana tunasema *TANESCO* haitengenezi faida. Haitengenezi faida kwa sababu kuna wakati *TANESCO* inalazimika kupeleka umeme zaidi ya kilomita tano mpaka ishirini kwenye Kijiji, ili mradi wananchi waweze kupata umeme na kuweza kuamsha maendeleo ya pale, hata kama mradi ule haulipi kwa wakati ule.

Kwa hiyo, kwa misingi hiyo, mimi naomba Wabunge wote tunapoiangalia *TANESCO* tujiangalie kama Shirika nyeti linalotuwezesha. Tuliombe misaada inayostahili na siyo tu kulilaumu kila wakati ili tuweze kufanikiwa maombi yetu tunapohitaji umeme katika maeneo yetu. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri, kwa mfano sasa hivi katika eneo la *Oysterbay* pale tayari Kituo kimeshajaa, kina Megawati 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kunusuru maeneo yale yaweze kuwa na umeme mzuri, inatakiwa lazima ijengwe *line* ya kilovolt 132 kutokea Ubungo kufika pale. Lakini *line* ile haina hata sehemu ya kuipitisha, *live way* hakuna kwa sababu maeneo yote yalishagawiwa viwanja. Huwezi kujenga juu ya nyumba za watu. Kwa hiyo, inabidi ma-*tower* Shirika litafute pesa za kuweza kutoa malipo ya fidia kwa ajili ya wale ambao wamejenga katika maeneo hayo.

Kwa hiyo, haya yote yanakuwa ni matatizo yanayoingiliana na matokeo yake mwishoni anayelaumiwa ni yule wa mwisho. Lakini tatizo linakuwa limesababishwa na wale ambao walikuwa wameanzia katika mipango mibaya ya mwanzo. (*Makofi*)

Kwa misingi hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu una nia ya kuendeleza makazi katika viwanja vingine, basi wakati ule mnapokuwa mmechukua mikopo hiyo kwa ajili ya kubuni viwanja hivyo, tuweze kuweka na hiyo miundombinu, kwa mfano maji, umeme na simu, ziwe zimetangulia kule. Hizo zitawawezesha wananchi kuwa na hamu ya kuendeleza maeneo yale badala ya kusubiri mpaka mwingine atakapoanza.

Sio hivyo tu, kuweza kumfikishia umeme mtu ambaye yuko kiwanja chake labda kule mwisho kabisa, inabidi umpelekee yeye peke yake kilomita moja. Lakini kama ingekuwa hizo taratibu zimewekwa vizuri, ina maana tayari yeye anachukua umbali ambao ni mfupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona wananchi jinsi ambavyo wanalalamikia kukosekana kwa hiyo huduma ya umeme na unakosa jibu. Siku ya kwanza unamwambia njoo baada ya wiki mbili labda tutapata pesa. Unakaa tena, hujapata pesa. Kwa hiyo, inaleta malalamiko makubwa sana. Naomba tuangalie hili eneo ili tuweze kuboresha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa sikutaji sana kwa sababu ulikuwa umesema utanipa muda kidogo. Nilikuwa nakwenda moja kwa moja kwenye mada. *(Kicheko)*

Lakini vile vile nilikuwa naomba niongelee kuhusu kuongeza kwa ajira katika maeneo ya Miji. Katika kufuatilia mradi wa *Public Private Sector Partnership* kuna maeneo mengi ambayo ni ya wazi ambayo yangeweza kuwa bustani za kupumzikia na zikaleta sura nzuri katika Miji yetu.

Maeneo yale mimi nayafikiria kwamba yangeweza kupewa hao vijana wakaweza kuyaboresha na kwa hizi pesa kidogo ambazo zitakuwa kwa ajili ya kuwaendeleza vijana kama watawezesha tutakuwa tumefanikisha mambo mawili. Kwanza bustani zetu zitakuwa nzuri na wao watapata ajira.

Vile vile watoto wetu watapata sehemu za kwenda kucheza na hata sisi pamoja na wapenzi wetu tutakwenda kupumzika wakati tunapojisikia. *(Makofi)*

Kwa misingi hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nikiwa kama mmojawapo wa wapenzi wa utunzaji wa mazingira, tutumie nafasi hiyo katika kuongeza ajira kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi uliniomba nitumie dakika 10, nimetumia chini ya dakika 10. Nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mhandisi Stella Manyanya. Kwa hatua tuliyofikia, ningepomba kutangaza Taarifa ya Kikao cha Kamati ya Fedha na Uchumi, tangazo linalotoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Adamu Malima, kwamba wakutane leo saa 7.00 Chumba Na. 133 ghorofa ya kwanza.

Pia, Mwenyekiti, Mheshimiwa John Cheyo wa Kamati ya Hesabu za Serikali na Mheshimiwa Mgana Msindai wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa wanawaomba Wajumbe wa Kamati hizo mbili *PAC* na *LAAC* kwamba watakuwa na Kikao cha pamoja kesho, muhimu sana saa 5.00 asubuhi katika Ukumbi No. 432.

Vile vile, ningependa kutangaza hapa kwamba Kamati ya Maliasili na Mazingira nayo ikutane kesho saa 5.00 asubuhi kwa ajili ya kile Kikao muhimu pamoja na Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Aziza Ally alileta vielelezo vyake ambavyo vimefika Mezani. Sasa naomba nivipeleke moja kwa moja kwa Mheshimiwa Waziri John Magufuli ili iweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Vielelezo hivyo ni kuhusu nyumba Na. 405, Mtaa wa Longido, Upanga ya Mzee Salum Ngalambela na nyumba Kiwanja Na.446 Mtaa wa *Oysterbay* ya Mzee Said Ali Maswanya.

Jioni ya leo endapo tutaendelea na hoja iliyo mbele yetu, kama mnavyojua, kulitokea suala la dharura ambalo Mheshimiwa Spika hajalifanyia uamzi, natumaini kikao kitaporejea saa 11.00 jioni kutakuwa na uamuzi wa kipi kifuatwe.

Lakini endapo tutaendelea na hoja iliyo mbele yetu hivi sasa ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, basi wazungumzaji watakaofuata ni Mheshimiwa Dr. Zainab Gama na Mheshimiwa Suleiman Saddiq waendeleo kujiandaa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kufikia hapo, naomba sasa nisishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni.

(Saa 06.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawaita wachangiaji wetu wa mwisho jioni ya leo, niwape tu utaratibu kwamba, ataanza Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, atafuatia Mheshimiwa Suleiman A. Sadiq, halafu atafuatia Mheshimiwa Naibu Waziri.

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi naanza kusema kabisa naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Kwanza, naomba niishukuru Serikali, iliamua kuifanya Mamlaka ya Mji wa Kibaha kuwa mji kamili na kutokana na hiyo likaundwa jimbo na mimi nikawa Mbunge wa Jimbo hilo. Kukosa maamuzi hayo, nafikiri aidha mimi au Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, mmojawapo angeondoka. Kwa hiyo, naomba niishukuru Serikali kwa maamuzi haya, imetufanya mimi nimerudi na kaka yangu, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha amerudi, ahsante sana. *(Makofi)*

Naomba niishukuru Wizara kwa kusaidia kabisa kulifanya lile eneo la Kibaha lilikuwa la viwanda na sasa hivi lile eneo kati ya watu ambao tunawafikiria kuwapa eneo ni watu wa *SIDO*, ili kauli na ahadi ya Rais, pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ajira kwa vijana na wananchi itakuwepo. Baada ya kusema hivyo, labda mimi

ningemwomba Waziri, Mawaziri wote wawili ningeomba, Halmashauri na Serikali kwa ujumla, tusaidiane kuhakikisha ahadi ya Rais inatekelezeka. Rais ameahidi kwamba, atahakikisha Mji wa Kibaha Mjini unakuwa ni wa kufanana kama Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani. Kwa sasa hivi mji ule ni pori tu, bado ni kijiji ameahidi kuleta viwanda, ameahidi barabara na ameahidi mji huu uwe na sura.

Sasa sisi watu wa Kibaha, tunaomba Waziri atusaidie, tumeanza tumeshaandaa mradi wetu ambao tunataka kuuweka Mji wa Kibaha uwe ni mfano, usiwe mfano wa miji mingi inayoanza kwenye *shanty town*. Kwa hiyo, tumeandika mradi, tutaomba msaada wataalam wao watusaidie, *UN Habitat* watusaidie ili mji ule tuupange, kama kutakuwa na soko hapa lijulikane, mahali pa kuishi wananchi ijulikane, stendi ijulikane, ili tukiwa na mpango huu na mchoro huu tayari maafisa ardhi ambao sasa wamekuwa ni matatizo, kwa kugawa viwanja ovyo ovyo watasutwa, watasema ramani yetu na *site plan* yetu hii, mpango wetu ni huu, wewe ilikuwaje uligawa viwanja, mimi naomba hii tusaidiane.

Lakini ninaomba pia mtusaidie tushirikiane na Chuo Kikuu cha Ardhi na watu wa *CDA*, ambao wao wanajua kupanga mipango yao na sisi tunataka ule mji tusaidiane. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri nisaidie, kwa sababu TAMISEMI wanatusaidia na wametuma mtu wao, tumekaa nao kwa bahati mbaya mtu wa Wizara, wakati huo mlikuwa mnapanga bajeti, mkashindwa kumleta lakini naamini utatusaidia kaka yetu.

Lakini la pili nataka unisaidie sheria za ugawaji wa ardhi hasa katika miji, hivi sasa Mji wa Kibaha tuna matatizo, watu wa Dar es Salaam, baada ya maeneo mengi kuchukuliwa sijui mashamba tena yamekuwa viwanja, hivi sasa kinachotendeka, wanakuja wanakimbilia Kibaha na wakija wanachukua maeneo kuanzia eka 50 mpaka 100 ndani ya Mji wa Kibaha. Matokeo wanawayake Wenyeviti wanagawa haya maeneo, *despite* wameitwa na Mkuu wa Wilaya kukatazwa hawakubali, *despite* Mkurugenzi na Madiwani bado wanaendelea kugawa. Sasa naomba tuambiwe sheria inatuambiaje, maana yake tumesikia sheria kama kugawa *maximum* eka tatu na ikiwezekana ipitie Halmashauri. Lakini sasa hivi kwa rushwa hizi na vihelahela vinavyotolewa na wenzetu wa Dar es Salaam wenye uwezo, wanaokimbia sasa wanakuja Kibaha, wametufikisha hatua sasa tusipokuwa tumefanya shughuli hizi haraka, tumeandaa mipango hii haraka, sasa hivi Mji wa Kibaha utajengwa kwa mfumo wa sharti tano.

Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri, atuambie sheria inasemaje ili tuweze kutumia sheria hiyo, tufanye nini ili mji huu tuandae. Lakini naomba unisaidie kitu kimoja, mimi kama Mbunge au mtu binafsi, hebu niambie suala la *EPZ* na eneo la tamko, kuna *confusion*. Eneo ambalo lilikuwa la *EPZ*, Halmashauri imeona ndio kitovu cha mji lakini bado eneo la tamko kiwanda kiko pale, tayari kunakuwa kuna mvutano kati ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Sasa tunaomba Waziri atuambie ili tuweze kujua sasa katika ile mipango yetu pale tunapafanya, tunarudisha *EPZ* au inakuwa kitovu cha mji au kiwanda kile kinafanywa nini? Hilo nilikuwa nataka unisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatwa na wazee wa Maili Moja, wananiambia hivi kwa nini Serikali inanyanyasa wakazi wa Maili Moja? Wanasema sheria ya *road reserve*, ambayo Waziri alisema ilikuwa katika miaka ya 1930, ilionesha Kibaha pale itakuwa eneo kubwa chini ya *road reserve*, wanasema miaka hiyo barabara ile ilikuwa haipo. Sasa hiyo *road reserve*, sheria ya miaka 30 ilikuwaje? Naomba msaada wako. (Makofi)

La pili, wanasema sheria ilikuwa mwaka 1930 na kitu, lakini sheria ya *operation* vijiji ilikuwa 1974 na wao walitolewa walikokuwa wakaletwa pale, sasa wanaomba msaada, hawajui la kufanya, ni *contradiction*. Naomba leo Mheshimiwa Waziri, utusaidie ili hawa wananchi wetu na bahati mbaya kama nilivyokuambia, Kibaha angalau ni mji, basi pale Maili Moja ndio mjini sasa hivi.

Nakuomba pia Mheshimiwa Waziri, kama ulivyosema mwenyewe na wengine walivyosema, hizi Kamati hizi za usuluhishi wa migogoro ya ardhi, naomba uziendeleze. Acha hizo Kamati ambazo Rais alitamka, lakini tungependekeza basi tuwe na Kamati za kudumu, kwa sababu maafisa ardhi, bado hawajaingia katika mfumo wa Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya. Bado wana mtindo ule wa zamani, sasa ni bora tuwe na hizi Kamati za Kudumu.

La mwisho, ambalo nilitaka nikutaarifu, Mheshimiwa Waziri usipoangalia, eneo linaloitwa Kurasini, Shimo la Udongo, linaweza kusababisha *scandal*, nyumba nyingi zilizokuwepo pale, ambazo Serikali pia imechukua, kuna watu wamepanga, kuna baadhi ya viongozi hata ndani ya Bunge hili na wao wananunua, lile eneo liko chini ya Mahakama na Kabidhi Wasii Mkuu ndio ameshikilia eneo lile, ndugu bado hawajaelewana. Siku ndugu wakielewana kwenye familia, wale wote walionunua maeneo ya Kurasini Shimo la Udongo na waliopewa nyumba kule na Serikali, itakuwa *scandal*. Hivi sasa wanamtumia ndugu mmoja wa hiyo familia, ndio wanamdanganya, anakwenda anachukua nyumba hii anauza, anachukua nyumba hii anauza, lile eneo liko chini ya Kabidhi Wasii, urithi wao unachelewa zaidi ya miaka 30. Nataka nikuambie tu Waziri, hili ulijue, eneo la Kurasini Shimo la Udogo na ukitaka *information*, nina *documents* na wahusika wa familia ile ninawafahamu na wamenionba nije nikuambie Waziri wananyanyaswa, eneo lao hawapewi, kesi haiishi, matokeo nyumba zinachukuliwa na hata watu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, mimi sikuwa na mengi, naomba tu Waziri chonde, dada yako nisaidie, nionekane Mbunge wa kweli kweli. Ule mji ukiwa ndio mfano wa mji Tanzania, nitasifiwa na mimi nitakuwa kila siku nakusifia wewe. Nikikaa nitamshukuru Mungu, matokeo na wewe utafanikiwa kaka yangu, naomba msaada wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MHE. SULEIMAN A. SADIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii nyeti ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuzungumzia suala la ardhi katika Wilaya ya Mvomero. Wilaya ya Mvomero ni mpya, kila mmoja anafahamu, ni wilaya ambayo wananchi na Serikali kwa pamoja, wametoa uamuzi wa kujenga katika eneo la Wami Sokoine. Tumepewa eneo kubwa, tunaishukuru Serikali. Mipango ya ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya ilianza mapema mwaka 2003. Tunaishukuru sana Serikali, imetupatia hekta 3,000 kwa ajili ya kujenga mji wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo moja zito, ambalo linatia hofu miongoni mwa wananchi wa Wilaya ya Mvomero na Mkoa wa Morogoro, ni jinsi gani utendaji wa Wizara ya Ardhi unavyofanya kazi. Viwanja vimepimwa leo zaidi ya miaka miwili, *approval* hazitolewi, sisi wa Wilaya tumepeleka kwenye mkoa, mkoa unasema *approval* kutoka kwa Mkurugenzi wa Ardhi Makao Makuu bado, kila unapokwenda bado. Viwanja vilivyopimwa ni zaidi ya 1,500, leo tunaambiwa viwanja ambavyo vimepata *approval* ni 187, lakini hivyo 187, hakuna hata mwananchi mmoja, ambaye amepata *offer*, tatizo lililopo ni taifa na mkoa, wilaya tunakwenda, tunarudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Kasi Mpya na Nguvu Mpya, naona Wizara ya Ardhi haipo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suleiman A. Sadiq, ungeweka vizuri hicho chombo, ili usikike vizuri zaidi.

MHE. SULEIMAN A. SADIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, huku nyuma viti vina matatizo kidogo, lakini natumia chombo hiki cha pili, ahsante sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sasa hapa nafikiri mambo yatakwenda vizuri. Wizara ya Ardhi, naona viongozi wa juu, kazi yao ni kutema cheche, lakini utekelezaji ni sifuri. Watu wanakaa maofisini, wanatema cheche, ukienda kwenye utekelezaji mambo hayafanyiki, sasa nataka kuuliza, hivi kutoka Dar es Salaam, Makao Makuu ya Wizara ya Ardhi, kwenda Wilayani na Mkoani, kuna haja ya kufanya *booking* ya ndege? Ni kiasi cha Waziri na Naibu wake na Katibu Mkuu, kuchukua magari kwenda kwa wananchi kufanya kazi na kujua matatizo yako wapi. Leo wilayani tuna matatizo, Wilaya ya Mvomero Wabunge wanapita pale maeneo ya Dakawa, wanakuta kuna bango limeandikwa Makao Makuu ya Wilaya, hawaoni majengo, hawaoni kinachoundelea, matokeo yake ni lawama kwa Mbunge na kwa Serikali. Sasa tutajenga vipi viwanja hatupewi? Wilaya imepima, *approval* haitolewi, wananchi wameomba zaidi ya 2,000, hakuna hata mwananchi mmoja aliyepewa *offer* katika Wilaya ya Mvomero, kwa ajili ya makazi mapya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili nitahitaji maelezo ya kina ya Mheshimiwa Waziri, katika vifungu, kwa kweli leo sina mjadala wowote, maana sasa wananchi wamechoka na mimi nimevuta subira, nimesubiri Wizara hii tokea nilipomaliza

kuchangia Wizara ya Fedha kwa maana ya bajeti kuu, nikawa navuta subira hadi leo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili Mheshimiwa Waziri, anijibu kwa kina, kuna matatizo gani Wilaya ya Mvomero, viwanja vipya havitolewi na vimeshapimwa na Makao Makuu, kuna tatizo gani? Naomba Mkurugenzi wa Ardhi, kwa kushirikiana na Waziri, wanipe majibu leo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo nalo ni tatizo, Wilaya ya Mvomero ni mpya, Idara ya Ardhi tuna watumishi watatu, kuna bwana ardhi wa wilaya mmoja, tuna *planner* mmoja na *surveyor* mmoja. Lakini ukiangalia Wilaya nyingine, utakuta wako watatu, wanne, wawili, sasa wale wenzetu walioko pale ni wachache na ni wilaya kubwa, ina migogoro ya wakulima na wafugaji. Kila kukicha watumishi wale wako barabarani wanakwenda kutatua migogoro, kazi nyingine hazifanyiki. Naiomba Wizara, ituondolee tatizo hili kwa kutongezea watumishi katika Wilaya ya Mvomero, katika idara nyeti ya ardhi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna migogoro ya ardhi, ambayo Wilaya tumeshindwa, tumeipeleka mkoani, mkoa nao unasuasua kutoa maamuzi, naomba Wizara sasa iingilie kati. Tuna migogoro katika Vijiji vya Mlumbilo, Kidundwe, Lungo na Mela. Hivi karibuni vyombo vya habari viliripoti kuna mapigano pale Mela, Wilaya tumekwenda tumerekebisha mambo kidogo shwari. Lakini tunachotaka ni amani na utulivu wa kudumu, ili mambo yaende, tujue mipaka nayo ikoje na Wizara itusaidie, Wilaya kama Wilaya tumefikia mahali tumekwama, kwa hiyo, naomba itusaidie katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo masuala ya *National Housing*. *National Housing* sasa hivi wana sera ya ubia, sera hii imechukua kasi kubwa sana katika Mkoa wa Dar es Salaam na imeonekana inakwenda kwa *speed* kubwa, lakini sera hii ya ubia ni ya nchi nzima. Mimi naona sera hii kwa mikoani ina upungufu, ndio maana wawekezaji wengi wa mikoani, bado hawajachangamkia ubia kupitia Shirika la Nyumba la Taifa. Shirika la Nyumba la Taifa lina wajibu wa kuiangalia sera hii, kwa mkoa ambayo uchumi wake bado uko chini. Uchumi wa Dar es Salaam kila mmoja anaelewa, watu wanajenga maghorofa lakini kwa mikoani kwa maana ya asilimia 25 kwa 75, bado ni tatizo. Mikoani hakuna mtu anayejenga nyumba ya ghorofa kumi wala ghorofa nane, wala ghorofa sita, mtu kaenda mbali ghorofa nne. Kwa hiyo, sera hii inawaumiza wawekezaji wa mikoani, wengi hawajitokezi kwa sababu gharama za ujenzi kwanza mikoani ni kubwa kuliko Dar es Salaam, lakini ukiangalia sana wanaofaidika ni watu wa Dar es Salaam na hii ni Sera ya Taifa. Ili *National Housing* iende iwe Shirika la Nyumba la Taifa, sera hii kwa mkoa iangaliwe upya, ili na sisi wa mikoani, tupate nafasi ya kushiriki katika *joint venture* na Shirika la Nyumba la Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kulishauri Shirika la Nyumba la Taifa, liwekeze katika wilaya, mfano wilaya mpya ya Mvomero, ndio hayo masuala ya viwanja leo tunazungumzia viwanja vimepimwa zaidi ya 1,500, tunasubiri *offer* zitolewe, wananchi waanze kujenga. *National Housing* na wao waje, jengo la ofisi ya Mkuu wa Wilaya, karibu linakamilika, lakini watumishi watakuwa hawana nyumba. Tunaomba

Shirika la Nyumba la Taifa, liangalie kuwekeza katika wilaya mpya ambazo zinahitaji nyumba kwa watumishi na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni Sheria ya Ardhi, ambayo wananchi wa vijijini, pamoja na elimu kutolewa, bado haijawasaidia sawasawa, ndio maana migogoro inaibuka kila kukicha. Ningeomba kiundwe chombo maalum cha kwenda kutoa elimu ya Sheria ya Ardhi na pale kwenye migogoro tuweze kusaidiana kwa pamoja. Lakini bado nchi yetu inatakiwa iwe na sheria inayotamka wazi kwamba, ardhi ni mali, leo huwezi kukopa benki bila ya kuwa na ardhi au kuwa na nyumba au kuwa na *property* yoyote. Sasa tukiwa na sheria ambayo inatamka wazi kwamba ardhi ni mali, hiyo itakuwa imetusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza mengi, lakini liko swali au liko suala la tamko la Waziri kuhusu ujenzi ndani ya miezi 36. Ni tamko lenye nia njema, ambalo linataka watu wajenge, lakini hivi tujiulize mtumishi wa kawaida, mwananchi wa kawaida, kweli ana uwezo wa kujenga nyumba kwa miezi 36, kwa kipato chake cha mshahara tunaoujua sisi au kipato ambacho Wabunge tunafahamu wananchi ambao tunaishi nao? Leo unapotoa miezi 36, hivi wananchi wetu watamudu?

Mshahara ule ule ajenge, mshahara ule ule asomeshe watoto, mshahara ule ule amalize matatizo yake na familia yake. Kwa hiyo, hili suala la miezi 36 tuliangalie, watakaojenga ni matajiri, watakaojenga na kuwekeza ni wale wafanyabiashara wakubwa. Huyu Mtanzania mwenye kipato cha chini, kwa hii miezi 36 hatamudu hata siku moja, kama nia na lengo ni kumsaidia, basi lazima tuhakikishe tunamwezesha kwa kumpatia mkopo, ili aweze kujenga ndani ya hiyo miezi 36, la sivyo tutawanyang'anya viwanja wanyonge, tutawapa matajiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara injibu hayo, lakini lipo jambo moja ambalo napenda kulizungumza, asubuhi ya leo kuna kiongozi mmoja wa Upinzani alizungumza neno moja, ambalo kwa kweli mimi naomba nilizungumzie kidogo. Wenzetu wa Bariadi wanadumisha utamaduni wao wa sherehe za nane nane, wanaita *Mbina*, nampongeza sana Mheshimiwa Andrew J. Chenge, ameweza kutoa ombi kwa Serikali sikivu ya CCM, hatimaye Waziri Mkuu na Rais wamepeleka salamu kwa wananchi wa Bariadi na wamefanikisha zile sherehe.

Lakini sherehe zile zimefanikiwa kwa sababu Mbunge wa CCM, ameomba Viongozi Wakuu, sasa leo anakuja Kiongozi wa Upinzani anasema sherehe zimefanikiwa kwa sababu kule kuna Upinzani. Hizi ni kauli potofu, kule kwa sababu kuna Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, Mbunge anayesema anasikilizwa, ameweza kumvuta Waziri Mkuu na kumpeleka. Mheshimiwa Andrew J. Chenge, nakupongeza sana kwa kufanikisha sherehe za *Mbina*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi sisemi naunga mkono au siungi mkono, kilio changu ni Mvomero, kilio changu ni watendaji wa ardhi kuanzia ngazi ya mkoa na taifa, wabadilike na hii ari mpya wanayozungumza, wazungumze kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasubiri majibu ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, huyo ndio alikuwa msemaji wetu wa mwisho, kwa hoja ya Wizara hii. Kabla sijamwita Mheshimiwa Naibu Waziri, nawatambulisha wageni 30 kutoka Matawi ya Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Kati wa NBC, ambao wako kwenye *public gallery*, karibuni sana. *(Makofi)*

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DR. LAWRENCE K. MASHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupewa nafasi hii kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Awali ya yote, naomba kusema kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ningependa pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hati zetu za ardhi zinazotolewa na Wizara, zinatoa muda maalum wa kujenga, muda huo ikiwa kati ya miaka mitatu hadi mitano. Ukishindwa kujenga katika kipindi kilichowekwa, unaweza kunyang'anywa hati yako kama inavyofanyika katika zoezi linalofanyika katika baadhi ya sehemu za nchi yetu hivi sasa. Je, Serikali haioni kwamba, huu ni uonevu hasa ukichukulia kwamba, ni Taasisi moja tu ya kifedha, *Azania Bancorp*, inaotoa mikopo ya kujenga nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuuliza kama Serikali haioni kwamba, ni busara kuandaa mikakati ya kuhakikisha kwamba, taasisi za kifedha zinaandaa mipango ya mikopo ya kujenga nyumba kabla ya kunyang'anya watu hati zao?

MHE. ANIA S. CHAUREMBO: Napenda kuchangia kwa maandishi hoja ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na timu ya wataalamu, kwa matayarisho ya hotuba ya Wizara ambayo ina matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni muhimu sana katika jamii ya Watanzania. Kumekuwa na tatizo la kudumu la ujenzi holela wa nyumba mijini na hasa katika Jiji la Dar es Salaam (*squatters*). Pamoja na mipango ya Wizara ya Ardhi, kuanza kutambua ujenzi huo na kuanza kuweka utaratibu wa kuziweka nyumba hizo katika kumbukumbu za Serikali, bado Wizara iangalie njia ya maeneo hayo kujenga ujenzi wa kisasa ili kuweka mandhari nzuri ya mijini. Pamoja na kuwapa leseni ili zivasaidie mikopo ya kujengea lakini wasijenge tena katika ramani hizo, wapimiwe upya na kuwekewa barabara na miundombinu mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara inipe ufafanuzi juu ya utaratibu huu ambao unatumiwa na baadhi ya Ofisi za Ardhi, Nyumba na Makazi katika Halmashauri za Wilaya, mfano, Bagamoyo. Wananchi ambao wameomba viwanja Ofisi ya Ardhi

imewataka kulipia Sh.300,000/= kwa kila kiwanja kikubwa, malipo ya awali na kuwapa akaunti namba ili wakalipie fedha hizo ni kwa ajili ya gharama ya kupimia viwanja na kuwaeleza baadaye ndio watalipia gharama za viwanja. Sasa ni muda mrefu zaidi ya mwaka mmoja na miezi sita, hakuna taarifa yoyote na wakiuliza jibu ni kwamba, zoezi bado linaendelea. Wizara haioni hii ardhi watakapokuwa tayari, wanaweza kuwapa wananchi wengine na kusababisha usumbufu usio wa lazima?

Napenda kuikumbusha Wizara ya Ardhi, kwa muda mrefu sasa viwanja vya burudani kwa watoto na hata watu wazima, havipo vya kutosha, Wizara iangalie jamii inakosa sehemu hii muhimu.

Siku za karibuni kumekuwa na tatizo la ukiukwaji wa taratibu za ujenzi wa nyumba za ghorofa katika Jiji la Dar es Salaam, hii inatokana na wahusika na wasimamizi wa Serikali kutofuata sheria zilizopo. Naomba Waziri alifahamishe Bunge suala hili limefikia hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, ilitangaza wananchi waliomiliki viwanja vya eneo la Boko na *Mbezi beach* kwa muda mrefu bila kujenga, vinarudishwa Wizarani ili wapewe wananchi wengine. Ningependa kujua viwanja hivi vyote vimerudishwa Wizarani na pia ningependa kujua baada ya zoezi hili, zoezi litaendelea maeneo mengine nchi nzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Napenda kukupongeza kwa hotuba yako nzuri, ambayo imepoza mengi ambayo nilitaka kuchangia. Hotuba imefafanua mengi. Kwa kuwa Wizara yako inatarajia kupima vijiji ambavyo havijapimwa, naomba muda wa kupima mpaka vijiji wapate cheti ni mkubwa sana utaratibu uharakishwe wananchi wapate vyeti haraka kuokoa migogoro inayotokea.

Bunge lililopita limepitisha Sheria ya kuthaminisha ardhi kuwa na thamani lakini ardhi haitopata thamani bila kupimwa, wananchi wapimiwe viwanja vyao ili waweze kupata mikopo kwenye vyombo vya fedha. Migogoro ya wakulima na wafugaji inatokea kwa ajili ya maeneo ya wafugaji kutopimwa. Wakulima nao wanapoanzisha mashamba kwenye maeneo ya wafugaji, husababisha eneo la wafugaji kupungua na kuanza migogoro hasa wakulima wanapofunga maeneo ya njia za mifugo.

Serikali inaweza kutenga maeneo ya wafugaji na wakulima na kuwawekea *Beacon* ili kila upande waheshimu mipaka yake. Mheshimiwa Waziri, ardhi ndiyo chanzo cha uchumi, maendeleo na makazi, kwa hiyo, ni muhimu kwa kila jambo. Sasa tatizo la migogoro ni maingiliano. Napenda kuzungumzia ardhi ambayo wanapewa wachimbaji migodi. Wachimbaji migodi wanapopewa eneo la mgodi bila wenye kijiji kuelezwa ni mgogoro mkubwa, uharibifu wa mazingira unapotokea wanaoathirika ni wanakijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi kuhusu mashamba ya wanavijiji ambao wanahitaji kupimiwa, tatizo hakuna wataalam wa kupima. Pili,

gharama ni kubwa sana, wananchi wasio na kipato hushindwa kulipia upimaji huo. Katika jimbo langu la Longido, wananchi wameshindwa kupima mashamba na viwanja vyao, kutokana na gharama kubwa za upimaji. Kwa kuwa mahitaji ya wananchi ni makubwa, naomba Wizara yako itusaidie wapimiwe mashamba waweze kupata mapato.

Kuna migogoro ya wananchi na watu wenye maeneo ya kuwafugia wanyamapori, jambo ambalo linaleta mgogoro kwa wananchi wa vijiji wanaozunguka eneo hilo, wamekuja hapa Dodoma kulalamika kwamba, eneo lao limeporwa na Mzungu huyo. Shamba hilo ni la *West Kilimanjaro*, ambalo ni eneo lililoachwa bila kutumika.

Naomba msaada wa Mheshimiwa Waziri, hasa kutokana na Wilaya yangu kuwa bado ni mpya kama Wilaya yako, kila mara eneo jipya linahitaji mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Kata yakiimarishwa, yatapunguza migogoro. Kwa kuwa Mabaraza haya yako karibu na wananchi zaidi na gharama ya kufuatilia migogoro ni ndogo. Mabaraza haya yaimarishwe, watu wenye uwezo ndio tu wanaoweza kwenda Mahakamani. Kwa kuwa tatizo la Mabaraza haya ni elimu yao ndogo, elimu itolewe kwa wale ambao wanaongoza Mabaraza hayo. Bila elimu Wajumbe wa Mabaraza, hawatatoa haki, kwani Sheria ni ngumu, inahitaji mafunzo. Kwa kuwa chombo hiki ni muhimu, basi Wizara waimarishwe kwa maeneo ya vijijini ambako wako mbali na Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurudia kuunga mkono hoja. Mungu awabariki wote walioko kwenye Wizara.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Naipongeza Wizara kwa hotuba yake nzuri. Awali ya yote, ninaiomba Wizara inisaidie kupata maelezo juu ya kunyang'anya viwanja vya Mbezi/Tegeta inalenga nini, inakusudia jamii iendelee kujenga kwenye maeneo yasiyo rasmi au inalenga kukiuka Sheria ya Ardhi inavyotaka kutenguliwa?

(a) Iwapo Serikali iliweza kugawa viwanja toka miaka ya mwanzoni mwa 1980 katika maeneo ya *Mbezi Beach* hadi leo hii haijaweza kukamilisha miundombinu (barabara, maji, umeme na simu); iweje mwananchi wa kawaida ambaye hajaweza kujenga leo hii anyang'anywe kiwanja chake?

(b) Sheria ipi ambayo imempa uwezo Mheshimiwa Waziri, afute umiliki wa ardhi wa mwananchi?

Naomba Wizara iondoe kero ya ulipaji wa ada za viwanja, ambapo ofisi ya malipo inafunguliwa saa 1.30 asubuhi, lakini ulipaji unianza saa 3.00 asubuhi hadi saa 7.00 mchana, ambapo walipaji huwa wengi na wanaotoa huduma huwa wachache na hatimaye huleta kero ya kujazana kila wanapokwenda kulipa. Kwa nini Serikali/Wizara, isitafute ufumbuzi wa kuondoa kero hii ya miaka nenda miaka rudi? Nahitaji majibu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Awali; Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Waziri na Naibu wake, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, kwa kuanza kutekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2005 kwa kasi inayokidhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi, kuna mambo kadhaa yanayofaa kuzingatiwa katika mipango ya Wizara kama ifuatavyo:-

Kwanza, kutenga maeneo ya wafugaji. Wilaya ya Kahama ni Wilaya ya jamii ya wakulima na wafugaji. Pia Wilaya ina rasilimali nyingi hasa madini. Mchanganyiko wa wakazi na ushindani katika matumizi ya ardhi umekua sana katika miaka ya karibuni. Kutokana na kuwepo madini, Serikali imekuwa ikitoa vibali vya kutafuta/kutafiti madini kwenye maeneo makubwa sana na hili limewanyima fursa wananchi kutumia ardhi yao kwa shughuli zao. Waathirika wakuu ni wafugaji. Naomba Wizara, kwa kutumia Sheria ya Ardhi Na. 4 na 5 ya 1999, ipime mashamba na kuyamilikisha kwa wananchi.

Pili, gharama kubwa za upimaji viwanja. Juzi juzi katika kikao cha Baraza la Madiwani Kahama, tulipewa taarifa ya gharama za upimaji viwanja. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, gharama ya kupima hekta moja inanzia zaidi ya Sh.80,000/= na inaongezeka hadi kufikia zaidi ya Sh.300,000/= kutegemea na eneo. Kwa gharama za namna hii, naona Wizara itakuwa kikwazo cha utekelezaji wa MKURABITA, kama haitazingatia gharama hizi. Taarifa ilionesha kuwa, gharama za upimaji wa viwanja, inajumuisha posho za safari, nauli na hata gharama za malazi za viongozi, eti wakiwa safarini kupeleka michoro Mwanza. Naomba gharama hizo, zisizo na maana, zisibebeshwe wananchi kama ilivyofanywa Wizara ya Kilimo, kufuta ushuru na ada mbalimbali kwenye bei ya mazao ili kuongeza bei ya mazao kwa mkulima. Naomba pia Wizara iondoe gharama zisizostahili kwa mwananchi.

Tatu, kumekuwepo na matatizo na urasimu sana katika upatikanaji wa hati. Pamoja na sababu nyingine, sababu kubwa ya tatizo hili ni uhaba wa Ofisi/Idara za Ardhi Mikoani. Naomba Wizara iongeze mamlaka na vitendea kazi kwenye Idara za Ardhi Mikoani ili ziweze kutoa hati za muda mrefu za kumiliki ardhi (*decentralize the powers and authority of the registrar of titles*). Tumieni kompyuta (mfumo) ku-control title numbers badala ya kusafirisha mafaili hadi Ofisi za Kanda au Makao Makuu, eti kwenda kutafuta *registration* ya hati.

Nne, utambuzi wa makazi holela, zoezi hili hasa Dar es Salaam linaenda vizuri, lakini hati au leseni za makazi zinazotolewa ni za muda mfupi mno (miaka miwili). Muda huu ni mfupi sana kiasi cha kufanya leseni hizo zisikubaliwe na mabenki kama dhamana. Wakati mwingine mabenki yanapokubali leseni hizi kutumika kama dhamana, lakini mikopo inayotolewa inabidi ilipwe kwa muda mfupi sana unaoendana na uhai wa leseni husika. Naomba Wizara, irekebishe kipindi cha uhai wa leseni walau iwe miaka kumi ili leseni hizi ziaminike na kutumiwa kama dhamana ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kumpongeza kaka yangu, Mheshimiwa John P. Magufuli na dada yangu, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, kwa bajeti nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na kuwatakia kila la kheri katika utekelezaji wa mipango yake. Ahsante.

MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI: Naunga mkono hoja ya Waziri asilimia mia kwa mia.

Mipaka ya Tanzania na nchi jirani (Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Kongo, Zambia, Malawi na Msumbiji). Mipaka iliyopo iliwekwa na wakoloni (Wabelgiji, Wareno na kadhalika). Pamoja na kwamba nchi wanachama wa iliyokuwa *OAU* na sasa *AU*, wamekubaliana kuwa mipaka iliyorithiwa kutoka kwa wakoloni, itatambulika na kuheshimiwa kama ilivyokuwa wakati wa nchi kupata uhuru, bado ipo haja ya kuchukua hatua za ziada ili kuondoa uwezekano wa siku zijazo kuwepo kiongozi wa nchi, miongoni mwa majirani, ambaye hataheshimu Mikataba ya Kimataifa kama huo wa *OAU/AU* kwa kutaka kubadili mipaka ya nchi kwa maslahi yake. Aliyekuwa Rais wa Malawi, Dr. Banda alifanya hivyo kwa kudai eneo la Mikoa ya Mbeya, Iringa na Ruvuma katika miaka ya 1960. Aidha, Iddi Amin wa Uganda, alizua balaa la vita vya Kagera mwaka 1978, kwa kudai na kuliteka eneo la Kaskazini la Mto Kagera hadi aliposhindwa kivita na eneo hilo kukombolewa na Watanzania wenyewe.

Hatua au mkakati ninaoupendekeza ni kwa Tanzania na kila nchi jirani, moja baada ya nyingine, kuingia Mkataba utakaotambua mipaka kama ulivyokuwa wakati wa Uhuru kwa kutaja kila *beacon* ilipokuwa *latitude* na *longitude*. Baada ya Mkataba huo kuwekewa sahihi ni budi uridhiwe na kila Bunge. Kwa mfano, Tanzania - Kenya, Tanzania - Uganda na kadhalika. Baada ya Mikataba hiyo kuridhiwa, nakala zitakabidhiwa kwa Umoja wa Mataifa. Zoezi hili sio geni, Canada na Marekani (*USA*), zilifanya hivyo baada ya vita yao kuhusu mpaka ya mwaka 1812.

Naipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, viongozi na watumishi wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuleta maendeleo na kusimamia maslahi ya Tanzania. Kasoro zinazojitokeza miongoni mwa watumishi wachache, zisiwavunje moyo. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika Wizara hii. Nitaanza kwa kusema, katika Mkoa wa Kigoma viwanja vya ujenzi au vya kujenga, vinagawiwa mara mbili mbili kwa watu tofauti. Je, hii ni halali kwa watu hao; kama siyo halali, Serikali inasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga nyumba hizo, unakuta jirani aliyejenga karibu yako, anachukua na sehemu yako, anapitiliza kabisa. Unapokwenda Ofisi ya Ardhi wawapimie upya, wanakuta kabisa yule mtu aliyejenga nyumba hiyo amejenga na sehemu yako na ofisini hawana uamuzi wowote kwa vile alishajenga. Akiambiwa abomoe sehemu hiyo iliyozidi, habomoi. Serikali inasemaje kwa hilo na inawasaidiaje wale ambao ni wanyonge?

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri, yenye ufafanuzi mzuri kuhusu Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayofanya, pamoja na mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa zipo Sheria za Ardhi ambazo zinakwamisha utekelezaji wa Sekta ya Ardhi na hazijaeleweka vizuri kwa wananchi na hasa umiliki wa ardhi katika vijiji.

Je, ni lini marekebisho ya Sheria hizo yatafanyika na kutoa elimu kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vijiji vingi vimepimwa katika Mkoa wa Dodoma ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa; je, ni vijiji vingapi vimepimwa na kupewa hati za kumiliki ardhi katika Wilaya ya Mpwapwa na kama hati miliki hazijatolewa, je, ni lini upimaji wa vijiji utakamilika katika Wilaya ya Mpwapwa kwa kuwa bado kuna vijiji ambavyo havijapimwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa miji mingi imejengwa kiholela kwa kukosa *Master Plan*, je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha hali hiyo ili miji yetu ijengwe kufuatana na *Master Plan* ya miji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa fedha zinazotengwa katika Halmashauri za Wilaya, hazitoshelezi kutekeleza majukumu ya Sekta ya Ardhi, je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha katika Halmashauri za Wilaya kuliko hali ilivyo sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Watendaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na hasa waliopo katika Halmashauri za Wilaya, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, kwa kukosa vitendea kazi, usafiri na vifaa vya kisasa vya upimaji wa ardhi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha hali hiyo, kwa kuwa Halmashauri za Wilaya uwezo wao ni mdogo kimapato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali itakubaliana nami kwamba, hati za nyumba vijijini ni muhimu sana kwa wananchi kupata mikopo kutoka vyombo vya fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali imeweka mikakati gani ya kutatua migogoro ya mipaka na ugawaji mbaya wa viwanja katika miji yetu (*Double Registration*) na hatua gani zimechukuliwa kwa wote waliohusika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja hii. Naipongeza hotuba ya Waziri na pia naipongeza Serikali, kwa zoezi lake la kupima na kuuza viwanja Dar es salaam na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia kitendo cha kuunda Kamati za kutatua kero zinazohusu matatizo ya ardhi kote nchini. Hata hivyo, Wizara inakabiliwa na kero nyingi na ikizingatiwa kwamba, kazi mojawapo kubwa ya Serikali ya Awamu ya Nne nitaje mbili tu ambazo ni ufutaji wa hati miliki na bomoa bomoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio Utawala Bora na pengine uvunjaji wa haki za binadamu, kuamka na kutangaza kuhusu ufutaji wa hati miliki, kwa kutoendelezwa kwa kufuata picha za angani bila kuchambua na kutathmini sababu zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwa vile wengi wa walioshindwa kuendeleza ni maskini, wazee, wajane na kadhalika, Wizara iwape nafasi ya kujitetea. Wale wanaosemekana wanahodhi viwanja na ni watumishi wa Wizara, hawa sheria ichukue mkondo wake papo hapo, izibe mwanya huo. Muda wa miaka mitatu kwa maskini wanaoishi *below poverty line*, ni mfupi. Muda huo uongezwe hadi miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bomoa bomoa inayosababishwa na maendeleo ya kweli, lakini zipo kero zinazotokana na bomoa bomoa ambayo haina mantiki. Mifano michache ifuatayo inathibitisha hayo:-

(i) Kijiji cha Mseke Kata ya Mlolo, Jimbo la Kalenga, barabara ndiyo iliyosogezwa karibu na wananchi na sio wananchi kujenga karibu ya barabara. Wanatakiwa kuhama kwa miaka kumi sasa.

(ii) Barabara ya Iringa hadi Mzumbe Jimboni Kalenga, nyumba nyingi zimetiwa X.

(iii) Mbezi Luis karibu ya Dar es salaam kuna zaidi ya watu 300 waliohamishiwa hapo mwaka 1973 toka vijiji vya pembeni. Sasa wanatakiwa na *TANROADS* kuhama na wamekuwa wanapigwa danadana kwa miaka mitatu. Jaji Longway analifahamu sana suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri elimu itolewe kuwaelimisha wazingatie umbali gani na pia ukaguzi ufanyike mara kwa mara kuhakikisha wananchi hawapati nafasi ya kuvunja sheria na taratibu zilizowekwa.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nitoe mchango kuhusu Wizara hii. Kwanza, naomba kumpongeza Waziri, Mheshimiwa John P. Mgufuli, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, kwa hotuba nzuri na mipango yao thabiti katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie katika upimaji wa viwanja hasa katika Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo kuhusu upimaji wa viwanja, kwani wananchi wa Busweru katika Wilaya ya Ilemela, wanalalamika kwamba, wapimaji wa viwanja huenda huko na kupima mashamba yao, hata kama shamba limetoa viwanja vinne au sita, mwenye shamba hupewa kiwanja kimoja tu na hulipwa Sh. 300,000/=, kisha huambiwa kukilipia Sh. 360,000/= kwa kiwanja hicho hicho. Hapo mimi sielewi tunafanya nini? Naomba maelezo juu ya hili na uhalali wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Mtaa wa Lumbumba katika Jiji la Mwanza, kuna matatizo ya viwanja vya nyumba ambazo tayari zilijengwa tangu enzi za Mkoloni, baadae katika viwanja hivyo, watu wengine wamepewa kwa nyuma ya nyumba hizo na ni wageni, yaani wamekuja nyuma. Najua huenda Waziri anafahamu ni kwa nini waambiwe hawa wa zamani waondoke na waliojenga nyuma wabaki. Naomba maelezo ya kina kuhusu hilo, utatuzi wake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia ndogo za majengo, tunaomba Waizara kuwa makini sana katika fidia za majengo. Mtu aliyejenga nyumba mwaka 1970 na ukaja kuithaminisha mwaka 2006, ni wazi mtu huyu atapata uthamini wa chini, ambao kwa sasa hatoweza kupata nyumba kutokana na kupanda bei za vifaa. Hivyo, naomba kujua ni kwa nini wasitumie thamani ya sasa kwa kumlipa mtu ambaye anapaswa kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii iwe na wepesi wa kutoa hati za nyumba kwa wahitaji wa hati hizo, ili watu waweze kumiliki hati za mali zao bila mzunguko usio na sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iende ndani zaidi hasa vijijini kwa kutoa ushauri kwa watu wa vijijini waweze kujenga nyumba zinazokidhi haja na kutimiza hali bora kwa kila Mtanzania. Hatuwezi kuwa na nyumba za tembe halafu tuseme maisha bora kwa kila Mtanzania. Kuna haja ya kufanya sababu za makusudi ili tuweze kujenga maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nyumba za Msajili, kodi hupanda mara dufu bila kujali kipato cha Mtanzania. Katika Jiji la Mwanza, Msajili hupandisha kodi bila kujali kwamba, kuna wananchi wa kawaida ambao wanaishi katika nyumba hizo. Tunaomba angalau marudio ya sensa yafanyike ili kodi iendane na maisha ya Watanzania wengi walio maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie hili kwa umakini sana kwani kama ni biashara, basi tujue nyumba za Msajili zilianza biashara siku nyingi tangu 1967. Hivyo, tunaomba jicho la huruma kwa wananchi wa hali ya chini, wanaoishi katika nyumba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna migogoro mikubwa katika mipaka hasa kati ya Raia na Jeshi la Ulinzi katika Kikosi cha 601 katika Wilaya ya Ilemela, Kata ya Ilemela, eneo la baadhi ya vijiji vya Nyanguku kuhusu mipaka na fidia. Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya anajua, aliyekuwa Mkurugenzi wa Jiji anajua, Mipango Miji wanajua. Naomba Wizara hii iangalie mipaka hiyo na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, iweze kuwafidia wananchi waliochukuliwa ardhi yao na mgogoro uondoke. Naomba tufuatilie mipaka hiyo ili haki itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Waziri, Mheshimiwa John P. Magufuli na Naibu wake, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, pamoja na Katibu Mkuu, kwa jinsi wanavyofanya kazi kuitumikia nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuchangia mambo yafuatayo: Wizara hii hivi sasa ina tatizo kubwa la ucheleweshaji wa kupata hati miliki za viwanja, kutokana na kuwepo kwa mashine moja tu ya kutengeneza hati. Mashine hiyo mara nyingi huharibika hivyo, kusababisha mlundikano wa wateja wanaosubiri kupewa hati mara baada ya kupatiwa *offer*. Naishauri Wizara iliangalie hili kwa namna nyingine ili kero hii iondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tarafa ya Kigamboni, kuna tatizo la mgogoro wa ardhi, juu ya fidia ya ardhi na mimea na ardhi baina ya wananchi na Mkorea, ambaye anataka kuwekeza katika eneo hilo. Tathmini ilifanyika na wote, yaani pande mbili na kila mmoja aliliridhika na tathmini hiyo ya awali ya malipo ya fidia. Mkorea hivi sasa halipi kwa mujibu wa makubaliano hayo, bali anafanya tathmini mpya ya malipo, jambo ambalo limezua kutoelewana na wananchi wenye mashamba yao. Ngazi ya Wilaya limeshughulikiwa tatizo hilo lakini bado linasuasua. Hivyo, naomba rasmi, Mthamini Mkuu wa Serikali, aingile kati tatizo hili lipate suluhu ya haraka. Jambo hilo limeshatoka kwenye vyombo vya habari mara nyingi tu hivyo, ni aibu kwa Serikali. Naomba tuliwahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tuna tatizo la uanzishwaji wa kiwanda cha gesi huko huko Vijibweni. Naomba nalo Mheshimiwa Waziri, atembelee na tayari nimeshamwandikia, najua analishughulikia na wataalam wake. Wananchi wamechanganyikiwa na wana hofu kubwa ya maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali sasa ina mpango gani wa kutoa mikopo kwa wananchi kiasi cha Sh. 500,000,000/= kila Mkoa? Hii huenda ikawasadia baadhi ya wamiliki wa viwanja, ambao viwanja vyao hawajaviendeleza na kuwakwamua kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara, iwaongezee muda wananchi wote ambao hawajaviendeleza viwanja vyao kwa misingi hiyo, badala ya hatua zinazochukuliwa za kufuta umiliki. Aidha, kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 – 2010 ya Chama Tawala, imekusudia kusimamia uanzishwaji wa Taasisi za kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba nchini. Kwa misingi miwili yote hiyo,

naendelea kuishauri Wizara, kusitisha uamuzi wake huo wa kufuta miliki za viwanja visivyoendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la fidia ya mazao, ninaishauri pia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Kilimo, waangalie viwango vya fidia vilivyopo hivi sasa. Viwango hivyo ni vidogo sana, ukilinganisha na mapato ya mimea yenyewe kwa mwaka. Ni muhimu tathmini sasa izingatie mapato ya mimea na uhai wa mimea wenyewe, badala ya kulipa kwa mfano, mwembe Sh. 26,000/=, wakati mapato yake kwa mwaka ni Sh. 200,000/= hadi 300,000/=, mbali ya uhai wake. Huku ni kuwaongezea wananchi umaskini badala ya kuwapunguzia.

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja hii. Natoa pongezi kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa hotuba yake nzuri na fasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ajitahidi kuhakikisha kwamba, *Government Notice No. 121* ya tarehe 13 Juni, 1975, inazingatiwa kuanzia kupima mipaka baina ya Hifadhi ya Wanyama ya Mikumi na vijiji vya Mikumi, Lumango, Ruhembe, Ilundo, Matambiko, Kitete Msindazi na Kidogobasi. Pia Waziri awaagize wapimaji, wawashirikishe wazee waliokuwepo miaka hiyo ya nyuma ili waweze kuwaonesha wapimaji mawe ya mipaka yaliyopandwa miaka hiyo ili kupata *bearings* zilizo sahihi. Kwa kuzingatia mwelekeo huu, kutaepusha mfarakano baina ya wanavijiji na Serikali kupitia Wapimaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanavijiji katika maeneo yaliyotajwa, wanatambua umuhimu wa Hifadhi katika uchumi wetu. Lakini wanavijiji wanatambua pia kuwa, idadi yao imeongezeka sana tangu mwaka 1975, jumla ya miaka 30 hadi sasa. Wanavijiji wameomba kwa zaidi ya miaka kumi, mipaka ya Hifadhi iongezwe kiasi cha kuwapa nafasi ya kupanua kilimo na huduma za jamii na kiuchumi. Ili wanavijini hawa waweze kutimiza azma ya Miradi ya MKUKUTA, MKURABITA na maisha bora ya kila mwanakijiji, ni muhimu Serikali ilimalize tatizo hili ili wanavijiji wajenge imani kwa Serikali na Hifadhi na kuwa walenzi shirikishi wa Hifadhi ambayo ni maliasili adimu ya Taifa letu. Naomba suala hili lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili muhimu ni kuhusu wanavijiji wengi katika Jimbo la Mikumi, ambao wanapakana na waliokuwa waajiriwa wa wawekezaji waliokuwa wamiliki wa mashamba makubwa, kama vile pamba, katani na alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya ushindani mkali wa soko huria katika uzalishaji mazao, wawekezaji wengi wa mashamba makubwa katika Jimbo la Mikumi, wamedhoofu mno, wengine wamechoka kabisa na hawana dalili za kufufua uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kudhoofu kwa wawekezaji hao, wenye kumiliki zaidi ya ekari 7,000, kunawatenga waliokuwa waajiriwa katika mashamba hayo na wanavijiji wengine wanaopakana na mashamba hayo katika kutumia ardhi iliyo karibu nao kwa kilimo. Chakula na mazao ambayo yamezalishwa katika eka 7,000 ni kingi sana. Kwa

hiyo, naomba kuwasilisha kilio cha wanavijiji kuwa Serikali itumie sheria husika haraka iwezekanavyo, kumega au kuwagawia moja kwa moja wanavijiji katika vijiji vifuatavyo: Kijiji cha Mhenda, zipo ekari 1,500, Kijiji cha Ulaya ekari zaidi ya 3,000, Kijiji cha Kilangali ekari 750, Kijiji cha Kisanga ekari 580, Miyombo ekari 300 na Kijiji cha Kivurugu ekari 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ieleweke kwamba, waliokuwa waajriwa katika mashamba haya, sasa hawana namna ya kujiendeleza kimaisha kwa kilimo, pasipo kuwezesha kulima katika maeneo hayo ya mashamba yaliyotelekezwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali, ilianganalie suala hili muhimu katika kuinua uchumi wa wananchi waliomo katika mazingira haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam umezuka mtindo katika mitaa fulani wa wamiliki wa *flats* za chini katika majengo fulani fulani, kujenga au kuongeza majengo ya viduka au vyumba vya ziada na au garaji za magari, ambayo yanasababisha *obstructions* za kupita magari na pia kuzuia nafasi ya wapangaji wengine ku-*park* magari. Si hayo tu, bali wanahatarisha usalama wa majengo ya *flats* hizo. Kwa kuwa suala hili limeachwa bila kukemewa, naiomba Serikali itoe tamko la wazi kupiga marufuku mtindo huu, ambao kwa namna isiyoieleweka, baadhi ya waliojenga vijengo hivyo, wanadai kupewa kibali na Wizara ya Ardhi au Manispaa za maeneo hayo. Maeneo yaliyoathirika kwa ujenzi wa namna hiyo ni pamoja na Upanga – Mitaa ya Mfaume, Mazengo na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia hayo, napenda kumaliza kwa kuiomba Serikali, iharakishe upimaji wa maeneo ya wafugaji na wakulima katika Jimbo la Mikumi, ambako sasa hivi wafugaji wengi wamehamia kufuata malisho ambayo ni mazuri. Ugomvi baina ya wakulima na wafugaji umeongezeka sana. Kata husika ni Mabwerekwere, Tindiga, Ulaya, Zombo na Mikumi na Msolwa Kata ya Kisanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Naibu wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kushughulikia mambo kadhaa, yenye migogoro ndani na nje ya mipaka yetu ili kuisawazisha migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, napenda kutoa mchango wangu husika maeneo yafuatayo:-

Wizara imeanza kulishughulikia suala la mipaka yetu, kutokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kushughulikia mipaka yetu na nchi jirani yenye migogoro. Nashauri kasi iongezwe katika kulishughulikia suala hili na hasa mpaka wetu na Malawi katika Ziwa Nyasa. Ramani zote sasa zinaonesha kwamba, Ziwa hili ni mali ya Malawi peke yake. Mgogoro huu ni wa muda mrefu, hauna budi kutafutiwa ufumbuzi wa haraka kadri itakavyowezekana.

Ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa uamuzi wake wa kuwanyang'anya Maafisa wa Wizara yake, viwanja walivyojilimbikizia kwa nia ya kuvifanyia biashara na kujitarisha kwa kutumia nafasi zao kama watumishi wa umma. Napendekeza kasi iongezwe katika zoezi hilo ili viwanja hivyo viweze kugawiwa kwa wanaotaka kujenga, nikiwemo mimi na sio kuachiwa wanaotaka kujitajirisha. Pamoja na hatua hiyo, hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya wale waliojilimbikizia viwanja hivyo kinyume na utaratibu.

Wapo watu walioishi katika nyumba za *NHC*, hasa zile zilizokuwa za Msajili tangu pango la nyumba likiwa shilingi 300/= hadi sasa zimefikia shilingi 34,000/=. Mfano, nyumba za Upanga na kadhalika. Napendekeza Wizara kufikiria kuwauzia wale wapangaji halali waliokuwemo katika nyumba hizo tangu mwanzo badala ya kuwaongezea kodi mwaka hadi mwaka. Isitohwe kwa kiwango kikubwa, nyumba hizi sasa zinahudumiwa na wapangaji wenyewe kwa matengenezo. Ni vyema basi wakafikiwa kuuziwa kama vile walivyozuiwa watumishi wengine wa Serikali. Kwa kufanya hivyo, Serikali itaipunguzia *NHC*, mzigo wa kuhudumia nyumba hizi ili shirika liweze kujikita zaidi katika ujenzi wa nyumba mpya.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa hotuba nzuri yenye kuleta matumaini. Pia nampongeza Naibu Waziri, kwa kazi nzuri anayoifanya katika kufuatilia majukumu yake ya kila siku, Katibu na watendaji wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, napenda nitoe mchango wangu kama ifuatavyo:-

Imekuwa ni tatizo sugu katika upimaji wa ardhi kwa kisingizio cha Serikali kukosa fedha na vifaa vya upimaji. Lakini baadhi ya watendaji huonekana wakipima viwanja vya watu binafsi, kwa kutumia vifaa vya Serikali tena kwa malipo na pia hutumia muda wa kazi kwa maslahi binafsi. Tatizo hili ndilo linalosababisha watu kujenga nyumba bila utaratibu na mpangilio unaofaa. Rushwa imekuwa ndio sala katika idara hii inayohusu ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ntoa mfano katika maeneo ya Chanika, Msongola, Kinyerezi, Pugu, Kitunda na maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam, ambayo hayajapimwa kutokana na Wizara hii kutoupa kipaumbele upimaji wa viwanja. Tatizo hii linaathiri mpangilio mzima wa ujunzi na kuruhusu ujenzi holela katika Jiji.

Picha za anga imekuwa ni ndoto katika maeneo ya Chanika, Msongola na hata Kisarawe. Serikali ichukue hatua za makusudi, kutatua tatizo hili sugu na wananchi hawana imani na Idara ya Ardhi, hii ni kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Maofisa Ardhi, waheshimu taaluma zao kama alivyosema Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Kusema kweli urithi tutakaowaachia vizazi vyetu ni nyumba za ovyo vichochoroni kama tabia hii haitaachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ni mtu mwenye uwezo mkubwa katika kufuatilia mambo. Hivyo basi, namwomba asiwaonee haya hawa baadhi ya watendaji, wasiowajibika kufanya kazi za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima na afya na kuweza kuchangia hotuba hii. Nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuiweka Wizara hii inayoshughulikia ardhi na makazi pia kwa kumteua Mheshimiwa John P. Magufuli kuwa Waziri na Mheshimiwa Rita L. Mlaki kuwa, Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa John P. Magufuli na Mheshimiwa Rita L. Mlaki, kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii, ambayo ina majukumu makubwa, kwa umahiri wao pamoja na uongozi mzima wa Wizara. Ni mategemeo makubwa migogoro ya ardhi sasa itakwisha pia manung'uniko ya wananchi yanayotokana na rushwa ya utoaji viwanja na upatikanaji wa hati miliki, itapungua au kumalizika kabisa kutokana na juhudi tulizokwisha kuziona kwa viongozi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii ndiyo yenye mamlaka ya utoaji na usuluhishi wa migogoro inayohusu ardhi, naomba Mheshimiwa Waziri, alieleze Bunge lako Tukufu, kuhusu hatima ya kiwanja cha Shirika la Taifa la Tija (*NIP*), ambapo inasemekana kiwanja chake walianza kukiendeleza kwa gharama ya shilingi 213,900,000/=, kimechukuliwa na kupewa mtu mwingine wa nje. Hali ambayo imeleta kero kwa shirika hilo, kwa kukosa kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika limedai kupewa kiwanja kingine, pamoja na kurejeshewa gharama walizotumia, lakini hadi leo hakuna lililofanyika. Mheshimiwa Waziri, angetueleza kuna mipango gani ya kulimaliza tatizo hili ili shirika liweze kujenga ofisi yake na kubaki kuwa tegemezi katika ofisi za idara nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unaishia hapo, nategemea majibu mazuri. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo kuhusu Sheria ya *NHC* ya kuwanyanyasa wapangaji na kuwatoa bila ya wao kusikilizwa. Siwatetei kwa kutolipa kodi, lakini wana haki ya kusikilizwa. Shirika hili halipati hasara kwa kutolipa kodi tu, bali na matumizi mabaya ya pesa kwenye shirika pamoja na ajira zisizokuwa na tija.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, wanaofanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwe muwazi kwa Mheshimiwa Waziri kwamba, nitaunga mkono tu hoja ya Wizara hii, hapo nitakapopatiwa majibu ya kuridhisha kwa niaba ya wananchi wa Iramba Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka zaidi ya mitatu iliyopita, nimekuwa naomba wataalam toka Wizarani, wanaohusika na mipaka kati ya mkoa na mkoa, waje Iramba Mashariki waangalie mpaka ulioko kati ya Mikoa ya Manyara (Mbulu), Arusha (Karatu) na Singida (Iramba Mashariki), unaoanzia Mto Endaguluda kuelekea Ziwa Eyasi, mpaka leo hawajafika kwa kisingizio cha ukosefu wa fedha. Pia wakidai Wilaya husika, zichangie gharama. Mipka ya nchi na mikoa ipo chini ya Wizara, kwa nini ikwepe majukumu yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, wakati wa kuhitimisha hotuba yake, atamke wazi kazi ya kupitia mpaka huo kwa kuzishirikisha Wilaya nilizozitaja hapo juu, itafanyika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kusema ya kwamba, tatizo la kuwaacha watendaji wa ardhi kukaa kituo kimoja kwa mda mrefu, linawafanya wasahau kazi zao na kuanza kufanya mambo yasiyostahili. Maafisa wa Ardhi wa Wilaya ya Iramba, wamehamisha mpaka wa Kijiji cha Kijana, kilichoko Iramba Magharibi na kuingilia kienyeji kuchukua eneo la Kijiji cha Kinankamba kilichoko Iramba Mashariki na bila kutumia vikao halali. Mpaka ulikuwa unatoka *TM 380* mpaka *TM 163*, yaani juu ya mlima, yeye akaushusha hadi ndani ya Kijiji cha Kinankamba *TM 383* hadi *NP* iliyoko chini ya *TM 163*. Kazi hii ameifanya kwa maslahi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi wa tendo hili baya lililofanywa na Afisa Ardhi wa Iramba, ambaye sasa amehamishiwa Wilaya ya Mpwapwa, upo uwezekano wa kufanya maovu hata huko. Kwa upande wa kuwataka Wakuu wa Wilaya wawe wanatembelea maeneo yao na kutatua matatizo ya mpaka. Naunga mkono hata ile kuwa kwenye hati ya makabidhiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema ya kwamba, nitaunga mkono hapo nitakapopata majibu ya kuridhisha.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa hotuba nzuri na yenye mwelekeo.

Napenda kujua hatima ya viwanja vya Ukuni kule Bagamayo. Wananchi wa eneo hili, walitangaziwa kuwa upimaji wa viwanja unafanywa na viwanja hivyo vitagawiwa kwa wananchi. Wananchi walitakiwa walipe gharama za viwanja hivyo, ambapo walilipa kama ifuatavyo: Viwanja vikubwa (*Low Density*), shilingi 300,000/= na viwanja vidogo shilingi 70,000/=. Gharama hizi zilishalipwa tokea mwaka 2005 na viwanja vyote vilivyolipiwa ni kiasi cha 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetokea nini, mbona mpaka leo hawajakabidhiwa? Vipo visingizio mbalimbali, lakini mimi napenda kupata maelezo juu ya ufafanuzi wa kadhia hii. Nawatakia kila la kheri. Ahsante sana.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa John P. Magufuli, Naibu Waziri, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, Katibu Mkuu na watendaji wote, walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri, ambayo imeonesha mafanikio ya hali ya juu na kuwasilishwa kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niendeleo kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa jinsi walivyoipokea Wizara hii na kuanza uwajibikaji kwa kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya, kwani mambo mengi sasa yametatuliwa, hasa migogoro ya ardhi, viwanja na kadhalika. Ninawaomba kwa Mwenyezi Mungu, waendeleo na kauli mbiu hiyo hiyo katika kutekeleza bajeti hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, sasa naanza kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Kwanza, magofu na nyumba chakavu katikati ya Miji, Manispaa na Majiji yetu. Ninaipongeza sana Serikali, kwa jinsi inavyojitahidi kuboresha mazingira ya Miji, Manispaa na Majiji yetu, bali bado yapo magofu na nyumba chakavu sana katikati na miji mingi pamoja na Mji wa Singida. Wakazi wanaoishi kwenye nyumba hizo ni wazee, vikongwe na watu wasio na uwezo. Naishauri Serikali iwajengee wananchi hawa nyumba nje na miji na kujenga majengo mazuri katikati ili kuboresha miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukiri kuwa huduma ya kupata hati miliki ipo ingawa ni mlolongo mrefu sana. Ninaomba sana Serikali sasa ione uwezekano wa kurahisisha huduma hii mfano, Mkoa wa Singida, hati miliki hutolewa ofisi ya kanda iliyoko Dodoma. Endapo hati miliki zitatolewa Mkoani, nina imani wananchi wote watakuwa na *lease* za nyumba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwani iliona umuhimu wa mitaa yetu kuwa na viwanja vya kuchezea watoto. Hata hivyo, napenda kukufahamisha kuwa, viwanja vingi vimevamiwa na kujengwa majengo ya aina mbalimbali.

Je, Serikali inasema nini katika hili na ina mpango gani wa kutoa viwanja vingine mbadala ili watoto waweze kupata maeneo ya kuchezea kwa ajili ya mazoezi ya viungo na kuwaweka maeneo ambayo hawawezi kupotea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza juhudi za Serikali za kujenga barabara nyingi za Kitaifa na Mkoa katika kiwango cha lami. Ikumbukwe kuwa, juhudi hizi zimesababisha nyumba nyingi ambazo barabara zimepita humo, zimebomolewa. Vile vile naishukuru Serikali, kwa kutoa fidia kwa wakazi wengi walioguswa na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwe na utaratibu mzuri wa kutathmini majengo haya ili fidia zinazotolewa ziwe zinalingana na gharama halisi ya nyumba hizo, kuliko ilivyo sasa. Wapo wakazi wengi hawakuridhika kabisa na fidia walizopata na wengi hulipwa fidia kubwa kuliko thamani ya nyumba, banda au shamba. Ninangoja maelezo ya Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali sasa izitazame upya Kamati za Vijiji zinazogawa viwanja, kwani nyingi hazina watu waaminifu ili kutoa huduma vizuri. Vile vile hata miji midogo, ambayo Halmashauri za Wilaya hupima viwanja, nazo zinafanya kazi pole pole sana. Tunaomba tamko litolewe ili wananchi wapewe viwanja na waweze kuanza ujenzi ili kuboresha miji yetu. Suala la vitendea kazi nalo ni kikwazo kwa watendaji wetu katika kuendesha zoezi la kupima viwanja vitakiwavyo mfano, kuweka *beacon* kwa haraka zaidi kuliko ilivyo sasa au vipindi vilivyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mtazamo wa Serikali wa kuuza nyumba zake kwa nia njema, zipo nyumba ambazo zimeuzwa na kuathiri huduma za watendaji wa Serikali mfano, nyumba walizokuwa wanaishi madaktari wa Hospitali ya Mkoa wa Singida. Nyumba hizi zilijengwa na Serikali ili kuwa karibu na eneo la kazi, ili dharura yoyote ikitokea, waweze kuwahi eneo la kazi na kuokoa, hata kama gari litakosekana kwa tatizo lolote. Vile vile walionunua nyumba, wana uhuru wa kutumia nyumba hizo kwa shughuli yoyote kama ilivyotokea hapo Singida, nyingine ni baa, maduka na kadhalika. Hali ambayo inaathiri hata wagonjwa ambao hawahitaji kelele. Nipate maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo hapo juu, nimalizie kwa kuiomba Serikali irudishe huduma ya kukopesha wafanyakazi fedha, ili waweze kujenga nyumba kwa maandalizi ya baadaye. Nyumba ambazo zinazwa sasa, zina gharama kubwa na hakuna mtumishi wa kawaida, anayeweza kununua. Watendaji wanaouza viwanja mara mbili, wachukuliwe hatua, wakazi wanaochelewa kujenga viwanja, vigawiwe upya na wakazi waliojilimbikizia viwanja vingine, wavirudishe vigawiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuunga mkono bajeti hii, kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa John P. Magufuli, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Naibu Waziri, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, kwa kuandaa vizuri hotuba yenye mwelekeo unaotia matumaini kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Namtumbo, kuna vijiji vilivyopakana na hifadhi ya wanyama, ambavyo kwa muda mrefu vimekuwa vikilima kando ya hifadhi hiyo, lakini katika kipindi cha karibuni, kuna baadhi ya makampuni ya uwindaji yamepewa vibali vya vitalu vya kuwinda. Kinachoshangaza wameweka mipaka yao mpaka katika mashamba ya wanavijiji hivyo, yaani kwa mujibu wa wanavijiji hao wenye mashamba hayo.

Ninachoomba kwa Wizara, iwasiliane na Wizara ya Maliasili na Utalii na waende wakaone jinsi gani ya kuweka mipaka hiyo vizuri na kuviachia ardhi ya kutosha kwa kilimo, ambacho ndicho kinachowaletea tija. Ili kukidhi mahitaji ya ardhi ya baadaye, Serikali izingatie kuwa familia za vijiji hivyo zinaongezeka hivyo, mahitaji yao pia yanaongezeka kwa kasi.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha, iko kwenye mchakato wa kuanzisha Benki ya Maendeleo. Benki hii itasaidia sana kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wafanyabiashara, maana sasa hivi mabenki yanatoza riba ambayo ni kubwa mno.

Nashauri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ishirikiane na Wizara ya Fedha ili Benki ya Maendeleo iwe na kitengo cha mikopo ya ujenzi wa nyumba. Naamini huu utakuwa mwanzo wa kufufua benki ya nyumba.

Sasa hivi Halmashauri Mikoani na Wilayani, ndizo zenye dhamana ya kugawa viwanja. Pia Maafisa Ardhi wako chini ya Wakurugenzi. Ugawaji wa viwanja ni wa mashaka sana, maana umejaa upendeleo na pia unaashiria vitendo vya rushwa. Nashauri Wizara ibuni na kuanzisha utaratibu wa kuwasimamia watumishi hao wa ardhi kwenye Halmashauri, ili kuondoa kabisa kero hii kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. ZUBEIR ALI MAULID: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, kwa kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri, kwa hoja hii ya bajeti, ambayo imewasilishwa mbele yetu. Nitakuwa mwizi wa fadhila, nisipompongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii, Mama Salome Sijaona.

Mimi sina mengi ya kuchangia, bali napenda kutoa ushauri kidogo ili baadhi ya maeneo yaweze kurekebishwa. Suala la Nyumba, pamoja na pongezi ninazotoa, naiomba Serikali iliangalie kwa karibu suala hili kwa mintarafu ya umiliki na ukodishaji. Ninachokusudia kukisema ni kwamba, Wizara hii ipewe umiliki wa nyumba zote za Serikali, pamoja na ukodishaji au upangaji usimamiwe na Wizara hii. Baada ya hapo, Serikali iangalie hali halisi ya vipato vya wananchi halafu ilinganishe na uhalisia wa bei inazotoa kama kodi kwenye nyumba inazomiliki.

Kwa mfano, hapa Dodoma, nafahamu kwamba, nyumba zinamilikiwa na Wizara ya Miundombinu, lakini ningependekeza hata hizi ipewe Wizara hii kwa ajili ya uendeshaji wake, kisha bei ziangaliwe upya. Ni nani mbali na Wabunge, atakayeweza kukaa katika nyumba za Kisasa kwa bei ya Sh. 150,000/= kwa mwezi; tena Dodoma? Maghorofa ya *Area D* – Dodoma yamepandishwa bei mpaka Sh. 120,000/= kwa mwezi kutoka Sh. 80,000/=, bila hata usimamizi wa kufanyia matengezo. Hii pengine inatokana na ukweli kwamba, suala la nyumba si suala la kipaumbele kwa Wizara ya Miundombinu, ndio maana nashauri lipelekwe Wizara ya Ardhi na bei ziangaliwe upya.

Wizara hii ni mojawapo inayolalamikiwa sana na wananchi, lakini uteuzi wa Mheshimiwa John P. Magufuli, pamoja na Mheshimiwa Rita L. Mlaki, umerudisha imani ya wananchi kwa namna Wizara hii itakavyotenda kazi zake.

Ninachoshauri ni kwamba, msimwanguzhe Mheshimiwa Rais, lakini pia msiwaangushe wananchi, kwa vile wana matumaini makubwa nanyi. Nakuombeeni kila lenye kheri katika utendaji wenu katika Wizara hii, nami daima nitawaunga mkono kwa vile nami nina imani kubwa nanyi.

Narudia kwa msisitizo, ninaunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia moja na naomba fedha zote zinazoombwa na Wizara hii wapewe.

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara, kwa bajeti nzuri na naunga mkono hoja. Ninaomba ufafanuzi na kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Ukurasa wa 15 ibara ya 17, kwa nini Wizara inachukua muda mrefu mno kuidhinisha vibali vya uhamisho wa miliki? Ukurasa wa 32 ibara ya 43, naipongeza Wizara kwa hatua hii. Nashauri Wabunge tupewe nakala za ramani za Wilaya zetu na GN za mipaka yake. Ukurasa wa 39 Ibara 58, Wilayani Lushoto Nyumba zote za Serikali ziliuzwa isipokuwa makazi ya DC. Wizara itajenga lini nyumba mpya za Wakuu wa Idara? Ukurasa wa 58 ibara ya 87 ni lini Serikali itaanzisha chombo au vyombo vya kutoa mikopo ya nyumba?

Halafu katika ukurasa wa 68(e), Tanga Mji mdogo wa Mlola, uwemo katika mpango.

Mwisho, Wizara ifikirie kuongeza muda wa waendelezaji viwanja kwa wenye vipato vidogo iwe miaka kumi badala ya miaka mitatu ya sasa.

MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa John P. Magufuli, kwa hotuba yake nzuri, yenye mwelekeo sahihi. Ninaunga mkono hoja. Naomba nitoe mchango wangu kidogo kama ifuatavyo:-

Kwanza, ninalo tatizo ambalo linanihusu mimi binafsi. Miaka mitano iliyopita nilinunua nyumba iliyoko Mbezi, *Block J, Medium Density, Plot No 751*. Nimekuwa nikihangaiwa kupata *title deed* mpaka leo. Ninazo hati zote za mtu aliyeniuzia, lakini kila ninapotuma watu wangu wamekuwa wakizungushwa tu. Hati zote za kisheria zipo, ninahitaji msaada wako Mheshimiwa Waziri.

Pili, katika Mkoa wa Kigoma, watumishi wa Wizara hii, wamekaa kwenye kituo kimoja kwa muda mrefu sana. Kwa mfano, Afisa Ardhi Mkoa na pengine na maafisa wengine, wamekaa muda mrefu sana zaidi ya miaka kumi. Tatizo la *double allocations ni order of the day*, kwa mfano, Kigoma. Lakini muda mfupi nilinyang'anywa kiwanja hicho *without notice*, akapewa Mkuu wa Mkoa aliyekuwapo, Bwana Mgumia, ikabidi

nitulie vinginevyo kungetokea mgongano na Mkuu wa Mkoa huyo. Nieleze kwamba, kiwanja hicho kilikuwa kwenye jina la mtoto wangu, Shepherd Kilonsti, aliyekuwa anasoma nje ya nchi wakati huo. Tafadhali naomba ushauri juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri pamoja na Wasaidizi Wakuu wote. Naunga mkono hoja.

MHE. FATMA OTHMANI ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kuchangia kuhusu utoaji viwanja kiholela na hili hasa linawahusu watendaji wa Ardhi, kwani wao ndio wahusika wa kutoa viwanja na huwezi kutoa kiwanja hicho lazima ukakague sehemu kilichopo. Leo la kushangaza baada ya muda, unasikia ndani ya vyombo vya habari wananchi wanasikitika kajenga nyumba tajiri ya ghorofa katikati ya nyumba za chini na kuziba mitaro ya maji; je, hawa wahusika huwa wako wapi? Baada ya hapo utasikia kauli mwananchi huyo asimamishe ujenzi huo haraka. Je, huo sio uonevu, kwani kinachotakiwa wakati wa ujenzi huo, uwe unaangaliwa kabla haujafikiwa mwisho. Lingine kiwanja kimoja inakuwaje kupewa wananchi wawili, kwani kwenye Jiji la Dar es Salaam kila leo hutokea matatizo ya kiwanja kimoja kilichopimwa hujitokeza na mwananchi mwingine naye akidai kwamba na yeye amepimiwa. Je, hapa huwa panatokea nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Idara ya Mipango Miji, katika kila Halmashauri na Mabaraza ya Miji, hali ya makazi ya wananchi inazidi kuwa mbaya siku hadi siku, kutokana na uhaba mkubwa wa viwanja vilivyopimwa na kusababisha wananchi kujenga katika sehemu zenye msongamano mkubwa wa watu na hakuna miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakadiriwa asilimia 70 ya wakazi wote wa Jiji la Dar es Salaam, wanaishi katika maeneo yaliyojengwa kiholela na yenye msongamano mkubwa na baadhi wamejenga sehemu za mabondeni na hivyo, kuhatarisha usalama wa maisha na mali zao wakati wa mvua za masika

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ifanye juhudi za makusudi za kuwahamisha wale wote waliojenga sehemu za mabondeni na ihakikishe wale wote wanaohamishwa, wapatiwe maeneo katika sehemu nyingine, zenye viwanja vinavyofaa wajenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri; je, ipo sheria inayowataka wale wote wenye nyumba chakavu katika baadhi ya Miji, wasizikarabati nyumba zao eti kwa sababu nyumba hizo zinahitaji zijengwe ghorofa kwa maeneo yaliyotengwa kufanywa hivyo? Je, Serikali haioni kuwa, inawapotezea wahusika hali ya kumiliki viwanja husika kwa vile hawana uwezo wa kujenga

maghorofa? Kama kweli sheria hii ipo, haionekani kuwa ni sheria ya ukandamizaji, pia ni yenye kuongeza kiwango cha umaskini miongoni mwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutenga maeneo kwa shughuli maalum kama, vituo vya daladala, kwa kweli vituo vya daladala katika baadhi ya Miji haviridhishi. Mfano hai, Jiji la Tanga, sehemu ya kituo cha daladala ni mahali ambapo ni pafinyu sana. Sehemu hii ipo sokoni, kwenye msongamano wa watu kaisi cha kufanya sehemu hiyo kuwa ni hatari kwa wafanyabiashara, wateja na watu tu watembeao kwa miguu. Naiomba Serikali izihimiza Halmashauri, zitenge sehemu za kutosha na kukidhi vituo vya daladala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo tokea awali yalikuwa yamaechwa wazi (*open spaces*), kwa ajili ya viwanja vya burudani kwa watoto. Matokeo yake viwanja hivyo vimetolewa kwa ajili ya watu kujenga na matokeo yake watoto wanacheza mpira wa miguu katikati ya barabara, jambo ambalo mara nyingi linasababisha ajali na wananchi hawawezi tu kujenga katika *open spaces*, bila ya kupata kibali toka Idara za Mipango Miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wamachinga ni wafanyabiasara walioajajiri wao wenyewe, ambao wanaiongeza Serikali kasi ya upatikanaji ajira. Wananchi hawa wanadhalilishwa kwa kufukuzwa fukuzwa kila wanapoweka bidhaa zao. Naiomba Serikali iwatengee sehemu kwa ajili ya shughuli zao na iwe sehemu ambayo ni rahisi kwa wanunuzi kufika na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wanapenda kuishi mahali pazuri, lakini tatizo ni ukosefu wa nyumba. Naiomba Serikali, ihakikishe kila mwenye uwezo wa kuomba kiwanja, anapewa kiwanja na viwe vinatolewa kwa gharama nafuu. Pia wananchi wapewe elimu juu ya ujenzi wa nyumba bora na zenye gharama nafuu. Wengi wameshindwa kujenga nyumba bora, kutokana na bei ya vifaa vya kujengea kuwa juu sana. Mfano saruji, kiwanda cha Saruji cha Tanga, kipo karibu na Mjini kabisa, cha kushangaza mfuko mmoja wa saruji unauzwa kwa shilingi 9,500/= na wengine shilingi 10,000/=. Kwa mtu ambaye amepata kiwanja na anahitaji kujenga kwa kubana matumizi, atashindwa kujenga nyumba ya kisasa badala yake atajenga nyumba ya matope ilimradi tu aweze kuishi kutokana na ughali wa vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kuna baadhi ya makampuni ambayo yana uwezo wa kujenga nyumba za gharama nafuu, ambazo wangeweza kuzigawa kwa wananchi mbalimbali kwa mikopo ya masharti nafuu. Hii itawasaidia wananchi kujikwamua katika maisha duni na kuweza kuishi maisha bora ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri, Mheshimiwa John P. Magufuli, Naibu Waziri, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, Katibu Mkuu, Ndugu Salome Sijaona, pamoja na watendaji wao, kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango kidogo ili kuboresha shughuli za Wizara, hasa kuleta *impact* kwa wananchi wa Jimbo la Mbinga Mashariki.

Kwanza, kuhusu upimaji wa vijiji na kutambua makazi yasiyo rasmi. Naomba Wizara sasa ifanye bidii ya kuhakikisha vijiji katika Wilaya ya Mbinga vinapimwa na vinapewa hati.

Pili, *NHC* sera ya kujenga na kuuza nyumba, hili ni Shirika la Umma, ni mali ya Serikali. Huduma zake hasa ni sera ya kujenga na kuuza imeelekezwa zaidi Mijini. Naomba kumhakikishia Waziri kwamba, wananchi wa Mbinga wanao uwezo wa kununua nyumba. Naomba sasa shughulihizi za *NHC* zielekezwe Mbinga. Kama Mbunge, ninaahidi kushirikiana nanyi, kuhakikisha mnapata ardhi ya kujenga na wananchi wa kununua nyumba hizo, hata kama tutaanza na nyumba chache kama 50 tu.

Mwisho, nitafurahi kupata taarifa tu mipango ya Wizara juu ya Wilaya ya Mbinga, maana sijaona kitu katika hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitakia Wizara kazi njema na yenye mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii.

MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kuchaguliwa kuwa Wabunge na kutupa uwezo wa kukutana ndani ya Bunge hili Tukufu na kuwatumikia wananchi wa Tanzania kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ili ifanye kazi zake kwa umakini, wafanyakazi na viongozi wote, wapewe elimu na semina, waweze kuwa wakweli, waaminifu na kujali kazi, si yao ni ya Taifa na kujali maendeleo ya Taifa hili. Mheshimiwa Waziri, sina shaka naye. Namwomba azidishe bidii na usimamizi mzuri pia wa kujali maisha bora kwa kila mtu na ari ya Serikali ya Awamu ya Nne. Tunaweza kutumia ardhi vizuri, kwa ajili ya kupata mikopo ya nyumba, viwanja, mashamba na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya ardhi, pamoja na mipango mizuri ya Wizara; hii migogoro itamalizika lini? Naiomba Serikali isimamie vyema na kuwezesha Wizara kutatua migogoro yote inayotokana na ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ramani za Miji ziwe zinazoendana na wakati kwa maslahi ya nchi, zisiwe zile zinazorejesha nyuma maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo ya nyumba, maandalizi yaendeleo na ikitolewa itolewe vizuri, kujali maslahi ya wananchi na iwe mikopo yenye unafuu na sio mikopo yeye riba ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza hotuba nzuri na bajeti iliyoandaliwa vizuri. Nawapongeza kwa kuendeleza shughuli vizuri na kuanza kuipa Wizara mwelekeo.

Pili, nawapongeza kwa upimaji wa viwanja, hili linapunguza uhaba wa viwanja. Nashauri hili liendelee na katika miji mingine pia tofauti na Dar es Salaam.

Tatu, ninazidi kushauri benki ya kutoa mikopo ya ujenzi iwepo ili kusaidia wananchi.

Nne, katika eneo la *Murongo Crossing*, Wilaya ya Karagwe, wananchi hatujui kwa uhakika mpaka wa nchi yetu na Uganda unapitia sehemu gani. Tunadhani suala hili lifuatiliwe.

Hii ni kwa kuwa, hata wafanyakazi wa Serikali ya Uganda, majengo wanayotumia kama ofisi pale mpakani katika sehemu inayochukuliwa kuwa ni Uganda, ni majengo ya Serikali ya Tanzania, zamani yalikuwa ya *PWD* hivyo, eneo hili ni la Tanzania.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaunga mkono hoja. Pamoja na kuunga mkono hoja, ninampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa bajeti nzuri, inayoleta matumaini kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninapenda kuzungumzia hoja moja, ambayo Serikali inatakiwa kuitupia macho. Nayo ni hoja ya tatizo la wawekezaji kununua maeneo na kuanzisha mashamba makubwa bila ya kufuata sheria na taratibu za nchi. Kwa mfano, kule Kahama, mwekezaji wa Kampuni ya Tumbaku *DIMON*, alinunua shamba lenye ukubwa wa hekta zisizopungua 300, mali ya kijiji na ndani ya eneo hilo limo eneo la jadi, yaani Makao ya zamani ya Chifu wa eneo hilo, lenye makaburi na maeneo ya kuabudu.

Matatizo kama hayo yasipodhibitiwa, yanaweza kuleta migogoro mikubwa baina ya wananchi na wawekezaji, jambo ambalo sio zuri.

MHE. MWANAWETU S. ZARAFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilwa ni moja ya Wilaya ambayo inajitahidi kujenga kwa kufuata utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya hii, wanayo malalamiko kuhusu Hati Miliki. Ni kipi kinachosababisha ucheleweshwaji wa kutolewa kwa Hati Miliki, wakati taratibu zote zinapokuwa zimeshakamilishwa na hata majengo yanakuwa yameshajengwa kwa miaka kadhaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inawakosesha mambo mengi ambayo yanatakiwa yadhaminiwe na mtu mwenye Hati Miliki, mfano, mikopo Benki na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara hii ifanye utaratibu wa kufaa zaidi na wa haraka ili wananchi wa Wilaya ya Kilwa wapate Hati Miliki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ombi kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, aweze kuwaruhusu watendaji wake wa Wizara, waende Wilaya ya Kilwa, Kijiji cha Mnazimmoja, eneo la Sanga ili wakatatue mgogoro wa ardhi uliopo kati ya wananchi wa eneo hilo na Maafisa Ardhi wa Wilaya au Mkoa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hilo lilianza kukaliwa kabla ya mwaka 1980, likiwa na ukubwa wa hekari 50. Mwaka 1985 Idara ya Ardhi ilishauri kwamba eneo hili liwe kwa ajili ya makaburi. Waliwataka wananchi wasiendeleo kukaa pale, hivyo basi, watawalipa fidia kwa mali zao. Waliweka Mawe katika eneo hilo bila ya kuwalipa wahusika fidia ya mali zao ili waweze kutoka katika eneo hilo. Hadi leo hii ni miaka 21, Idara hii haikutoa fidia na hata mawasiliano, hivyo basi, wananchi waliendelea kukaa na kuongeza majengo pia kuwapa maeneo wenzao ambao walihitaji kwa shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa 2006 Idara ya Ardhi, ilifika kwa kusudio la awali na kuwataka wananchi wahame na kuwaita wavamizi na fidia hawataki kutoa, kwani wahusika wengine walishafariki. Nasisitiza kusema kwamba, mgogoro ni mkubwa na haujawahi kutokea katika Wilaya ya Kilwa. Namwomba Waziri na Watendaji wake, walishughulikie haraka suala hili, kwani tahadhari zilizotolewa na wananchi hao ni za kutishia amani. Nahofia hali isiyo ya kawaida inaweza ikatoea kati ya wananchi na Maafisa Ardhi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanadamu yeyote akitaka kufanikiwa katika maisha yake, sharti atumie ardhi kama msingi wa maendeleo yake, ardhi ni Mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda anaopewa kuiendeleza ni miezi 36, ni muda mfupi sana. Tanaiomba Serikali, ifikirie muda huu uongezwe angalau kufikia miezi 60. Kipato cha Watanzania wa kawaida ni kidogo mno kuweza kujenga ndani ya miezi 36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wowote ule wa kibiashara unahitaji maandalizi makubwa wakati mwingine unahitaji mikopo. Pia hiyo ardhi inatumika kama dhamana ya kukopea. Ni vyema viwanja hivi visiwekewe muda wa miezi 36, kwani ni muda mrupi mno. Tunaiomba Serikali kufikiria kutokuweka muda wowote ule. Wenye kumiliki mashamba, nadhani hawana muda huu. Ni vyema wawekezaji katika viwanja vya Biashara wapewe fursa hii pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingi za mijini kumejengwa majumba mengi bila kufuata taratibu. Haya ni makosa yaliyotokea, hili ni kosa la Serikali na wajenzi. Ni vyema majumba hayo yakafanyiwa *inspection* na kama ujenzi hauna hatari kwa wakazi,

wapigwe faini wenye hayo majumba na kuyaacha. Yale ambayo yatakutwa na dosari kubwa yabomolewe. Nyumba ni mali ya nchi na sio mali ya wenye hayo majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ardhi inatambulika kuwa na dhamana, ni vyema Serikali ikaangalia upya sera yake na kuacha sera ya kuwanyang'anya ardhi waliopewa kwa kutoziendeleza. Mwananchi awe huru kuendeleza ardhi yake na kama hana uwezo, awe huru kuuza kwa kuwa ni mali yake.

MHE. JUMA A. NYWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kuwasilisha vizuri hotuba ya makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Rita L. Mlaki, Naibu Waziri, Bibi Salome Sijaona, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara, kwa kusimamia Sera na Sheria ya Ardhi vizuri.

Pamoja na hayo, nina mapendekezo yafuatayo: Kule Wilayani mtu akiomba kupatiwa kiwanja, huchukua muda mrefu mtu huyo kupatiwa kwa maelezo kuwa Maafisa Ardhi wenye vibali vya kutoa viwanja hivyo, yaani wenye sifa za kusaini *Documents* wapo mkoani na hivyo wanasubiri waje Wilayani au wapelekewe. Utaratibu huu una usumbufu mkubwa na hasa hushangaza zaidi inapokuwa yule anayetoa maelezo hayo ni *Graduate* katika *Bsc/Urban and Rural Planning*. Ushauri wangu ni kuwa, ni vyema sasa watendaji wenye sifa za *Diploma/Shahada* katika fani za Ardhi walioko Wilayani, wapewe vibali hivyo ili kurahisisha utendaji na kupunguza usumbufu kwa wananchi wenye matatizo ya viwanja.

Upo utaratibu mrefu sana baada ya kupimwa kwa viwanja mawilayani, kwani kanuni huhitaji michoro na mapendekezo kusainiwa na kupata *approval* toka Makao Makuu ya Wizara. Ni vyema sasa utaratibu huo ukaangaliwa upya ili kutoa nafasi na uharaka kwa matumizi ya maeneo yaliyopendekezwa.

Upatikanaji wa Hati Miliki za Ardhi au Nyumba uliopo sasa, una urasimu sana. Wakati umefika kupunguza urasimu uliopo, kwani *collateral* hii husaidia sana kupunguza umaskini kwa Watanzania, kwa kutumika kwenye mikopo (Taasisi za Fedha).

Wizara ya Ardhi, iangalie upya thamani ya vitu vinavyofidiwa kama vile nyumba, miti, mazao na kadhalika. Bei inayorejeshwa kwa wananchi hivi sasa hailingani kabisa na thamani ya vitu hivyo. Zoezi la kuzitambua nyumba zilizojengwa kiholela nchini (*squatters*), kwa kuzipa *Right of Occupation*, lifanyike kwa haraka. Kuna upole kwenye zoezi hili. Ni vyema kipaumbele kikatolewa kwenye zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja hii. Nampongeza Waziri, Mheshimiwa John P. Magufuli, Naibu Waziri,

Mheshimiwa Rita L. Mlaki na Katibu Mkuu wa Wizara hii, pamoja na *Commissioner* Msangi na Watalaalam wake wote.

Wizara hii ilikuwa na kero nyingi nchini hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Sera za Awamu hii ya Nne zimetolewa na viongozi bora wa Wizara, matatizo mengi yanaweza kuchukua sura mpya ya kuleta maendeleo.

Pamoja na Wizara kupima viwanja vingi katika Mkoa wa Dar es Salaam, bado limekuwa na utata mwingi kuhusu viwanja vilivyokuwa ni mashamba ya watu katika maeneo ya mijini, vimechukuliwa viwanja hivyo kupewa kwa watu wengine, kwa wale waliopima wenyewe au waliopimiwa, kupata *Letter of Offer*.

Aidha, imejidhirisha kuwa, kuna baadhi ya watendaji wa Ardhi, waliogawa viwanja hivyo kwa upendeleo au kwa rushwa. Maafisa wa aina hiyo wamepitwa na wakati na bora wasimamishwe kazi kabisa. Viwanja vingine vimetolewa mara mbili zaidi. Viwanja vipya vilivyopimwa katika maeneo mbalimbali katika Wilaya zote za Mkoa wa Dar es Salaam, muda uliotolewa kwa wamiliki wa viwanja hivyo, kuanza kujenga, ni mchache sana. Mfano, katika eneo la Bunju, viwanja vimeuzwa kwa gharama ya juu ya nadhani mara mbili zaidi kufuatilia maeneo tofauti. Wananchi wachache sana wanaweza kupata uwezo wa kununua viwanja hivyo na kuanza kujenga, kwa muda mfupi chini ya miezi sita. Napendekeza Serikali, ifikirie kuongeza muda huo ili mwananchi akusanye nguvu tena aanze kujenga, athari yake ni kupelekea wananchi wenye utajiri tu kumiliki ardhi na nyumba.

Naipongeza Wizara kwa kujenga nyumba na kuuza katika mikoa mbalimbali humu nchini, chini ya Shirika la Nyumba. Aidha, itakuwa kama katika Jiji la Dar es Salaam, nyumba za Shirika la Nyumba (*NHC*), ambazo zimo mijini ni za zamani sana, zijengwe upya hataka au ziuzwe kwa wananchi ambao wana uwezo. Ni bora Wizara ikawahamasisha wananchi waweze kujiunga na kuchukua mikopo ili waweze kukopa na kununua nyumba hizo au katika kuingia ubia na *NHC*, badala ya kuachia matajariri tu.

Hati Miliki za viwanja imekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wengi na kwa muda mrefu sana. Tunaipongeza Wizara kwa hatua walizochukua katika kutoa hati kwa vile viwanja vipya vilivyopimwa hivi karibuni.

Kuhusu viwanja vingi vya zamani, bado viwanja vingi havijapata hati na kupatikana kwa nyumba nyingi zimemalizika kujengwa kabla ya kupata hati, jambo ambalo linakuwa kinyume na taratibu. Kutokana na taratizu za kujenga, mara nyingi unakuta mtu yupo tayari kutaka kujenga lakini anakosa *permit* ya kuanza kujenga kutokana na ucheleweshwaji huo wa kupata kibali cha kuanza kujenga. Ni muhimu Serikali ijitahidi kuhakikisha, maafisa husika wanajitahidi kuharakisha *process* hii.

Maeneo ya wazi kwa ajili ya mapumziko yenye mandhari nzuri, maeneo ya michezo na maeneo ya michezo kwa watoto wadogo, yalitengwa tangu zamani katika Jiji la Dar es Salaam na miji mingine. Kwa masikitiko makubwa, maeneo hayo yamechukuliwa na kugawiwa kwa wananchi kujenga nyumba. Mfano mkubwa ni wa Dodoma, *Master Plan* imeingiliwa sana. Barabara ya kuelekea *Area D*, nyumba

zimejengwa kandokando ya barabara, maeneo ya karibu na *Airport*. Aidha, naiomba Serikali ihakikishe eneo la Chimwaga, ambapo Chuo Kikuu cha Dodoma kitajengwa, eneo la barabara wa Watumwa litunzwe. Hii ni muhimu sana, hatutaki kupotosha au kupoteza historia ya nchi yetu ya Tanzania na pia ni lazima kuheshimu *Master Plans* zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya kuanza kuchangia hoja hii, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuteua Makada wazuri kuiongoza Wizara hii. Uteuzi wa Mheshimiwa John P. Magufuli kuwa Waziri na Mheshimiwa Rita L. Mlaki kuwa Naibu wake, wakisaidiwa na Katibu Mkuu mahiri sana, Bibi Salome Sijaona, umeipa hadhi nzuri Wizara hii. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nzuri aliyoanza nayo Mheshimiwa Waziri na timu yake ni nzuri sana na ningependa kutumia nafasi hii kutoa ushauri ufuatao kwa ajili ya utekelezaji wa uhakika kwa maendeleo ya Sekta hii:-

Kwanza, uamuzi uliotolewa na Serikali kuwa vifaa vya ujenzi wa nyumba Mjini Dodoma kama njia muafaka ya kuendeleza mji huu, basi vifaa vyote viuzwe bila kodi. Hivi uamuzi kama huu uliishia wapi? Ulisaidia sana kazi ya kujenga nyumba.

Pili, ujenzi wa nyumba za kuishi watumishi mjini, kwa nini ujenzi wa maghorofa hautumiki ili kuwe na matumizi mazuri ya ardhi na kukwepa miji yetu isipanuke sana?

Tatu, kwa kuwa uwezo wa watu wengi mjini kuweza kujenga nyumba ni muda wa miaka mitatu, je, isingekuwa vizuri tukapanga maeneo ya kujengwa kwa muda maalumu ili kila mtu achague eneo ambalo masharti yake yawe wazi ikiwa ni pamoja na aina ya nyumba, gharama yake na muda wa kujenga; pia kuwepo maeneo kwa ajili ya watu wenye kipato kidogo, ambapo pia muda utapewa kuliko Sheria iwe ya aina moja?

Nne, kwa kuwa MKUTABITA ndiyo mkombozi mkubwa kwa watu wetu, je, usingefaa wakati wa kugawa viwanja pia Benki zihusishwe za kutoa mikopo kwa kuzingatia thamani ya mali alizonazo mwombaji ikiwa ni pamoja na kushauri kiasi cha mkopo kwa ujenzi wa nyumba mjini?

Tano, kuna haja ya kuongeza Hati Miliki za Ardhi na inasambaa vijijini ili kuwawezesha wananchi kuingia ubia na wawekezaji na kupatia mikopo. Hii ndiyo njia pekee ya kuwawezesha wananchi wawahi kujipatia ardhi ambayo ndiyo ufunguo wa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi ni nguzo kuu ya kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusu ardhi, hivyo ni muhimu yaongezwe na kupewa uwezo wa kushughulikia migogoro. Maana malimbikizo ya malalamiko yanazidi kuongezeka

badala ya kupunguzwa na hali ya baadaye itakuwa mbaya na hasa baada ya watu kujua thamani ya ardhi.

Sita, suala la rushwa kwa viwanja ni donda ndugu. Badala ya Wizara pekee kuachiwa mzigo wa kupambana na rushwa hiyo, Sheria itungwe ili Uongozi wa Halmashauri na Uongozi wa Mikoa (RCs), kupewa madaraka ya kuadhibu moja kwa moja wahusika na taarifa kupelewa kwa Wizara husika.

Nalisema hili kwa sababu mwaka 1996, nikiwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, nilimfukuza Afisa Ardhi (Mkoa), kwa tuhuma hizo za rushwa na jeuri katika utendaji wake wa kazi, lakini alirejeshwa na Wizara na kuwa mimi sikuwa na madaraka ya kufanya hivyo. Tuendeleo kuboresha Sheria zetu ili ziwadhibiti kwa dhati, wakorofi kama hao, tusimwachie Waziri peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo yaliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 ni budi ikaandaliwa *Programme of Action* kwa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu, ili kila mdau ahusishwe kwa kusimamia utekelezaji wake.

Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, alielekeze Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), lije lijenge Sumbawanga. Manispaa hii bado ni mpya na inanza kuvutia watu wengi kuja huku kwa shughuli za biashara na hasa baada ya kuona barabara ya lami itanza kujengwa, ofisi na nyumba za kuishi ni chache na wananchi wanahitaji nyumba kwa matumizi yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu walau katika ku-*wind up*, Mheshimiwa Waziri, ajaribu kugusia suala la wananchi wa Kijiji cha Itwimila A, Sogesca Kata ya Kiloleli, kuhusu ile kambi iliyokuwa kambi ya ujenzi ambayo Wizara ya ujenzi iliwapatia wananchi kwa ajili ya matumizi ya shule ya sekondari.

Mheshimiwa Rais Benjamin W. Mkapa, alifuta iliyokuwa hati ya umiliki iliyotolewa kwa *SK Investments Ltd*. Sasa wananchi wanaomba Wizara, isigawe ardhi hiyo, bali itumike sasa kwa mahitaji yao na si vinginevyo. Nitashukuru sana, japo kwa kauli ya Wizara kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ili wananchi wasikie na wajue haki yao inalindwa kwa mujibu wa Sheria Namba 4 na 5 ya 1999 ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaunga mkono hoja ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia hoja katika maeneo yafuatayo: Kitengo cha kutathmini mali za wananchi ambao wameathirika kwa kupitiwa aidha na

barabara, bomba la mafuta au nguzo za umeme. Kitengo hiki kimekuwa kikilalamikiwa mara kwa mara kuhusu utendaji wake. Hapo mwaka 2005, TANESCO walikwenda kupima njia ya umeme katika Vijiji vya Mkupuka, Kitembo na Kibiti. Mara baada ya kupima, waligundua kuwa, kulikuwa na vitu vingi vitakavyoathirika ikiwa ni pamoja na nyumba, mikorosho, miembe na mazao mengine. Wananchi wenye nyumba nao pia waliambiwa wasizitengeneze/kukarabati nyumba zao, kwani zitabomolewa ili kupitisha njia hiyo ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 2005 hadi sasa, wananchi hao hawajalipwa hata senti moja, kwa sababu watathmini (*valuers*), bado hawajafanya kazi zao. Ninaomba katika majumuisho yako, utoe taarifa kuhusu tatizo hilo. Sambamba na hili kuna wananchi wanane wa Kibiti, ambao walibomolewa nyumba zao na thamani ya nyumba ikawa ni ndogo. Aidha, wananchi hawa walilalamika bei hiyo ndogo na *valuers* walikuja kutathmini tena, lakini hadi sasa malipo yao ya pili bado hayajatolewa.

Utaratibu wa kutoa hati miliki una urasimu mkubwa, kwa mwananchi wa kawaida ni vigumu sana kuweza kupata. Ni vizuri basi urasimu huo upunguzwe ili kuhakikisha wananchi wengi wa vijijini, wanapata hati miliki ya nyumba na mashamba yao ili kuzitumia kupata mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, yaangaliwe sana yasivunje sheria. Taatibu za kuunda Mabaraza hayo zizingatiwe. Kisha, Mabaraza yajiepushe na hongo na hasa rushwa katika kusimamia haki kuhusu masuala ya ardhi. Pili, Serikali isimamie upimaji wa viwanja vya makazi. Hivi sasa, Mamlaka za Upimaji wa Viwanja vipya ni muhimu sana, lakini hawapewi pesa za kutosha kupima viwanja. Hali inayofanya wananchi wajenge watakavyo, kisha Serikali inawavunja. Serikali ielekeze nguvu zake kwenye kuelimisha watendaji wake na wananchi, kuhusu umuhimu wa mpangilio mzuri wa matumizi ya ardhi. Wananchi wanabughudhiwa pale wanapotakiwa kuvunja makazi au maeneo yao ya biashara waliyokwisha yaendeleza. Aidha, Serikali inaulizwa ilikuwa wapi wakati wananchi hao wakijenga/ wakiendeleza maeneo hayo?

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri mnayoifanya tangu mlipoteuliwa na Rais kushika nyadhifa hizo, nampongeza sana Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Naomba ufafanuzi wa haya yafuatayo: Kuhusu viwanja ambavyo havijaendelezwa kwa muda mrefu, ambavyo Wizara imeamua kuvichukua ili vigawiwe kwa watu wengine walio tayari kuviendeleza, nawapongeza kwa hilo. Nataka kujua baada ya kuvinyang'anya mtawapa Halmashauri wavigawe?

Nyumba za Serikali ambazo wameuziwa wananchi na wamemaliza kulipa madeni yao, lakini hawajapewa hati za kumiliki majengo/nyumba hizo. Je, ni lini mtawapa hati za kumiliki wale ambao tayari wameshamaliza kulipia nyumba hizo?

Maeneo ya viwanja vya michezo pale Jangwani Dar es Salaam, yalitengwa maalum kwa ajili ya michezo. Lakini inashangaza, maeneo hayo mmeyagawa kwa wenye malori, *godown*, karakana ya kampuni moja iliyojenga Barabara ya Morogoro miaka mingi iliyopita. Inawezekana hao ni wavamizi, Wizara ina mkakati gani wa makusudi, kuhakikisha eneo hilo la jangwani linabaki kuwa la michezo tu kama lilivyokusudiwa hapo awali.

Ondoeni urasimu ili wananchi walipe kodi ya viwanja bila usumbufu na wala kusimama foleni muda mrefu

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. FELIX N. KIJIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba ya Wizara hii katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo ambalo limekuwa ni kilio kwa wananchi ambalo linatokana na Maafisa Ardhi, kutoa kiwanja kimoja kwa watu zaidi ya mmoja. Kasoro hii inalalamikiwa nchi nzima, lakini ukilifuatilia sana na kujua undani wake utakuta ni kasoro inayotokana na kutokuwa na utunzaji mzuri wa kumbukumbu. Aidha, tabia ya kufanyia kazi mezani badala ya kwenda kwenye *field* nako kumekuwa kukichangia kwa kiasi kikubwa. Iko haja ya kuondoa hali hii inayolalamikiwa, kwa kuweka usimamizi mzuri wa kuhakikisha Maofisa Ardhi, wanajikita kufanya kazi kwa kufika kwenye *Site*, badala ya hali ilivyo sasa. Tofauti ya kufanya hivyo ni Maafisa Ardhi, kuhusishwa katika upokeaji wa rushwa hata kama siyo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimfuata Afisa Ardhi ili aende kukupimia ardhi, kunakuwa na utendaji usioridhisha kutokana na maafisa hao wenye dhamana, kutokuwa na usafiri. Sababu hiyo pia inaweza kuwa kichocheo kimojawapo kinachosababisha *double allocation* ya viwanja. Ninadhani ni vyema sasa Wizara ijikite katika kununua magari na wakati mwingine pikipiki ili kuondoa tatizo hilo sugu katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumishi wa Wizara hiyo, wapewe nafasi ya kujiendeleza kielimu kwa sababu maafisa wengi na hasa wa Mikoani na Wilayani, wanafanya kazi kwa uzoefu na siyo kitalaam. Ninashauri Wizara ilipatie kipaumbele hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makusudi kabisa ni sharti Wizara iwahamishe Maafisa wake kuanzia ngazi ya Wilaya, kwa sababu Maafisa hao wanakaa kwenye vituo muda mrefu na kujikuta wanasahau maadili ya kazi na kujiingiza katika vitendo vya rushwa. Naomba zoezi hilo lianzie Mkoa wa Kigoma na Wilaya zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuiunga hoja hotuba ya Bajeti ya Wizara kwa asilimia mia moja.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara, kwa kazi nzuri sana. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao ushauri ufuatao kwa Wizara na Serikali kwa ujumla: Kwanza naishauri Wizara iendeleze jitihada zake za kushughulikia migogoro ya ardhi. Mheshimiwa Rais, alifanya jambo zuri kuunda Tume kila Wilaya. Kwenye Wilaya zenye migogoro mingi ya ardhi kama Wilaya ya Muleba, Tume hii inastahili kupewa muda zaidi ili kila mgogoro usikilizwe na kutolewa mapendekezo kwa Mamlaka husika. Aidha, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba, yanastahili kuimarishwa na kufuatiliwa kwa karibu kwa sababu yanaundwa na Wajumbe wasio na ujuzi wa kutatua migogoro. Kwa hiyo, malalamiko ni mengi kama ilivyokuwa kwa Mahakama za Mwanzo kutokana na rushwa. Rufaa kwenda Wilayani ni gharama sana, kwa mfano, Muleba inabidi waende Bukoba Mjini.

Pili, naishauri Serikali hususan Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, atembelee Kijiji cha Kyamyorwa, Wilaya ya Muleba kuwasikiliza wananchi. Serikali ya Kijiji, ilinilalamikia nikiwa na uongozi wa Chama na Serikali ngazi ya Wilaya, kwa Migogoro wa Kijiji na Kampuni moja ijulikanayo kama *Itende Company*, unapotoshwa na Watendaji wa Serikali, jambo lililopelekea watu wawili kufa katika mapigano. Naishauri Serikali, isipuuze malalamiko ya wananchi, kwani maafa zaidi yanaweza kutokea. Mheshimiwa Waziri, lazima anihakikishie kwamba, atakwenda huko baada ya Mkutano huu wa Bunge. Wananchi wanaelekea kukosa imani na Serikali yao.

Tatu, naishauri Serikali katika kutekeleza sera nzuri ya kuanzisha mashamba makubwa makubwa ya watu binafsi, izingatie mahitaji ya wananchi wanyonge, waishio katika vijiji jirani. Migogoro itapungua iwapo mashamba makubwa yakianzishwa mbali sana na vijiji ili na wanavijiji waweze kupanua mashamba yao madogo. Aidha, kiwango cha ardhi anayopewa mtu mmoja au Kampuni moja kitazamwe upya. Kampuni moja kupewa maelfu ya ekari karibu na vijiji vyenye shida ya ardhi, kutatuletea matatizo makubwa siku za usoni.

Nne, naishauri Serikali itekeleze ushauri mzuri wa kuhimiza Mashirika kujenga maghorofa zaidi na kuwauzia wananchi kuliko kusambaza nyumba ndogo ndogo mijini, ambazo zinamaliza ardhi na kuongeza gharama kwa Serikali katika kutoa huduma katika makazi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii na Naibu wake, pamoja na wataalamu wake, kwa kuandaa bajeti hii na kuwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo matatizo mengi sana ya viwanja kuuzwa mara mbili (*double allocations*), kwa wananchi wengi. Hili ni kero kubwa sana, kwani mwananchi anachagua eneo ambalo angependa kuishi, anafuatilia na kupata kiwanja. Wakati anajikusanya apate nguvu ya kujenga, watumishi hao hao wa Ardhi Wilaya wanagawa tena viwanja hivyo kwa watu wengine.

Pale mwenyewe anapofuatilia, anaambiwa aongeze hela ili apewe mahali pengine. Hii ni aibu kwa Wizara hii na inaleta usumbufu mkubwa sana. Kwa wale waliochukuliwa viwanja na kujikuta wanapoteza hela na muda wa kufuatilia haki zao, kwa sababu ya tamaa za watumishi wa Ardhi. Naiomba Wizara iangalie suala hili kwa makini sana na kuondoa kero na usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu ubinafsishaji wa mashamba makubwa, yanayolimwa na wananchi maeneo mbalimbali yakiwepo ya Mbarali huko Mbeya na Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo vijana wengi sana na wananchi wengi, ambao kwa miaka mingi wanalima kwenye maeneo hayo na kuendesha maisha yao. Naomba Serikali aliambie Bunge hili, baada ya mashamba hayo kubinafsishwa, imeandaa mpango gani kwa vijana, akina mama na akina baba, waliokuwa wanategemea mashamba yao kuweza kuendesha maisha yao sasa na familia zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Serikali kukosa mipango mahiri ya kupima maeneo na kuweka mipango miji kabla ya wananchi kujenga makazi yao. Tabia ya Serikali kutulia kimya, huku wakiangalia wananchi wakijenga nyumba zao kwa nguvu zao ndogo kabisa na kwa miaka mingi, halafu baada ya muda fulani Serikali inatangaza kubomoa nyumba hizo. Je, wakati wote wananchi hao wanajenga nyumba hizo, Serikali ilikuwa wapi? Serikali kweli inajali nguvu za wananchi hawa? Hata kama wanafidiwa, ni kidogo sana, hawawezi kujenga nyumba kama zinazobomolewa. Hali hii inaongeza umaskini kwenye Taifa hili, badala ya kuondoa umaskini kwa wananchi wake. Naishauri Wizara, iandae mpango wa kupima maeneo ya makazi kwa mikoa yote kabla ya kujengwa kwa nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la watumishi wa Wizara hii ya Ardhi, kujichukulia viwanja vingi kwa kujipendelea kutokana na nafasi zao. Mtu mmoja anachukua viwanja mpaka kumi maeneo mbalimbali, matokeo yake anashindwa kuyiendeleza na pia anawanyima wananchi wengine haki, wenye nia na hitaji la lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia viwanja vingi eneo la *Mbezi Beach*, Dar es Salaam, ambavyo vina miaka mingi havijaendelezwa hadi Wizara inapokuja sasa, ni vya watumishi wenye ubinafsi na uchu wa kujilimbikizia wao tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Wizara ina rekodi za watu wote wenye viwanja, ni kwa nini wanatoa viwanja hadi kumi kwa mtu mmoja ili afanye biashara wakati Tanzania haki ya kumiliki ardhi ni ya kila Mtanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu inakataa kuuza ardhi kwa watu wasio wazawa wa nchi hii. Wawekezaji kutoka nje wanaweza kukodishiwa kwa muda fulani na sio kumilikishwa. Ardhi yetu ni kwa ajili yetu sisi na vizazi vijavyo. Naomba Waziri alieleze Bunge hili ni vigezo gani vilitumika kummilikisha Raia wa *South Africa*, eneo la zaidi ya hekta 500, kwa ajili ya kujenga hoteli na kuendesha shughuli za kitalii huko Serengeti – Mara (*Grumet Reserve*). Je, Sheria na Katiba ya Nchi yetu zimefuatwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo lingine la baadhi ya Halmashauri hapa nchini, kutangaza kuwa kuna eneo litapimwa na hivyo wananchi wanaohitaji viwanja wajiandikishe na kutoa hela. Watumishi na wananchi wanajiandikisha na muda mrefu unapotea bila viwanja hivyo kutolewa. Mfano ni Halmashauri ya Morogoro, ambapo wananchi wamelipia viwanja kwa muda wa miaka mitatu sasa na wamekuwa wakiambiwa wataoneshwa maeneo hayo bila mafanikio hadi sasa. Tunaomba Wizara, ifuatilie matatizo haya huko Wilayani ili kuondoa kero zinazowakera wananchi kwa muda mrefu na kuchafua Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata muda wa kuchangia.

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii, kutoa pongezi zangu za dhati, kwa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, iliyotayarishwa kwa utaalum wa aina yake. Nachukua pia fursa hii, kumpongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kazi yao kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, napenda kuelezea hali ya uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji inayoelekea kusababisha majanga makubwa Wilayani Mbozi, hususan kwa wakazi wa Jimbo la Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu mkubwa zaidi unatokana na ujenzi usiozingatia taratibu, kutokana na ugawaji holela wa viwanja kwenye vyanzo vya maji pale Ichenjezya Mjini Vwawa na *Mbozi Mission*, ambapo ni chanzo cha Mto Nkana. Mto huu wenye urefu wa zaidi ya kilometa 350, hutupita katika Kata zisizopungua sita Wilayani Mbozi na hivyo kuwa chanzo cha maji kwa wakazi wasiopungua 250,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ujenzi wa nyumba, vyoo vya shimo, kupanda migomba na mianzi, kulikofanywa kwa makusudi kwenye chanzo cha Mto huo pale Mjini Vwawa, hivi leo (baada ya kuwepo kule juzi), maji yamekauka ingawa miaka ya nyuma jambo hilo halikuwahi kutokea. Tarehe 03 Mei, 2006 nilipita pale na Wanahabari wa TvT na kupiga picha ya eneo hilo likiwa na chemchemi nzuri kabisa, lakini leo maji hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, janga la pili kutokana na tatizo hili ni milipuko ya mara kwa mara ya ugonjwa wa kipindupindu, inayotokea Jimboni Mbozi Magharibi

kutokana na wananchi hao kutumia maji yenye kinyesi kutoka kwenye vyoo vya nyumba zilizojengwa kwenye chanzo cha Mto Nkana pale Ichenjezya, Vwawa Mjini na *Mbozi Mission*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uharibifu wa mazingira kutokana na ujenzi holela hata kwenye vilima na vyanzo vya maji, liko pia Mji Mdogo wa Tunduma Jimboni Mbozi Magharibi. Hapa taratibu za ujenzi zinakiukwa kiasi cha kutisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya wananchi ni: -

(i) Ili kuokoa maisha ya watu wasiopungua 250,000 Wilayani Mbozi, hususan Jimboni Mbozi Magharibi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, iwaondoe watu waliojenga nyumba kwenye vyanzo vya Mto Nkana pale Ichenjezya Mjini Vwawa na pale *Mbozi Mission*.

(ii) Watumishi waliogawa maeneo hayo ya vyanzo vya maji kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, wachukuliwe hatua za kinidhamu.(

(iii) Wizara ibatilishe ujenzi wa nyumba kiholela Mjini Tunduma ili kuepusha janga la jangwa na mmomonyoko wa udongo, ambao unanyemelea mji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

MHE. JEREMIAH S. SUMARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya 2006/2007.

Kwa kuwa Tanzania hakuna Benki ya Nyumba; na kwa kuwa bila makazi bora maisha bora hayawezekani; na kwa kuwa makazi bora ni mahitaji ya msingi; na kwa kuwa Watanzania wengi hawana uwezo wa kujenga nyumba bora bila mkopo; na kwa kuwa Benki ya Biashara hazikopeshi kwa ajili ya kujenga nyumba za makazi (*they borrow short and lend short*); na kwa kuwa sio jambo la busara kutegemea Benki za Biashara kujiingiza kwenye Sekta hii (*Long Term Lending*); na kwa kuwa mtaji unaohitajika kuanzisha Benki ya Nyumba ni mkubwa na kwa hiyo, siyo rahisi kwa Sekta Binafsi kuanzisha Benki ya Nyumba (kwa kuwa pia ni uwekezaji *risky*); na kwa kuwa Ilani ya CCM ya 2005 – 2010 inatamka maisha bora kwa kila Mtanzania; je, kuna sababu gani za msingi za Serikali kutoanzisha tena Benki ya Nyumba chini ya utaratibu tofauti na *THB* ya 1972?

MHE. JUMA SAID OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia uzima na afya na kuweza kufika katika kikao cha leo cha Bunge. Namwomba Mwenyezi Mungu, atuzidishie uzima na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza wewe, pamoja na Mwenyekiti Mwenza, Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kwa kutoa taaluma mbalimbali kwa Wabunge. Pia, napenda kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Naibu

Waziri, pamoja na Watendaj wote wa Wizara hii, kwa hotuba yao iliyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna migogoro mingi kati ya wakulima na wafugaji. Ninaiomba Wizara, iandae utaratibu mzuri, utakaoleta maslahi baina ya wakulima na wafugaji. Wakulima wawe na maeneo yao kwa shughuli za kilimo na wafugaji watengewe maeneo mazuri kwa malisho ya mifugo yao ili kuepusha kuhamahama kwa wafugaji na mifugo yao hivyo kuweza kusababisha migogoro na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mipaka kati ya nchi yetu na baadhi ya nchi jirani, linahitaji kupatiwa ufumbuzi wa kudumu. Pia, migogoro ya mipaka ya ardhi kati ya Wilaya na Wilaya kwa baadhi ya Mikoa, ipatiwe ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ni rasilimali muhimu sana na urithi wa Watanzania wote, naiomba Wizara iandae mipango madhubuti itakayohakikisha matumizi bora ya ardhi. Hii ni pamoja na kujua maeneo ya mifugo, maeneo ya kilimo na maeneo ambayo yatatumika kwa ajili ya makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la makazi ni vyema yakatengwa maeneo kwa ajili ya michezo, barabara, sehemu za biashara ndogo ndogo na kadhalika. Hii itasaidia kuwafanya walengwa wawe na uhakika wa kufanya shughuli zao bila ya usumbufu wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa asilimia kubwa ya Watanzania ni wakulima, wakiwemo na wafugaji, mipango mizuri ya matumizi ya ardhi itasaidia kukikiza kilimo na kuendeleza mifugo na hivyo kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa John P. Magufuli, kwa ujasiri alionao katika utendaji kazi. Naamini Wizara hii imepata mchapakazi. nampongeza vile vile kwa kuwawezesha wananchi wake kupata barabara ya lami. Bila kufanya hivyo, namhakikishia kuwa, Chato isingepata lami milele. Nasi wana-Geita imetupa nguvu, kuidai Serikali kukamilisha kipande cha Usagara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara afanye yafuatayo: -

(i) Iweke wazi mpaka wa Ineta na Biharamulo. Kuna mgogoro mkubwa na wasiwasi miongoni mwa wananchi wa Katoro, ingawa mipaka inaeleweka kwa wanakijiji.

(ii) Naomba utaratibu wa kutoa hatimiliki urahisishwe. Utaratibu uliopo ni mgumu na unachochea rushwa.

(iii) Mkakati ufanywe kupunguza bei ya bati, kwani wananchi walio wengi huwa hawafaidiki na mikopo hasa wakulima wadogo vijijini. Serikali itoe *subsidy* kwa viwanda husika ili kuwawezesha wananchi kununua mabati kwa bei nafuu.

(iv) Kuwepo na uthamanisho wa ardhi. Sheria inaruhusu malipo yafanyike kwa mazao tu au nyumba, haiangalii kuwa mtu ametunza ardhi hiyo kwa muda mrefu. Huondolewa bila utaratibu au malipo. Ardhi ipewe thamani tena kubwa kwani ndiyo uhai wa jamii husika.

(v) Kutokana na matatizo ya madini, tunaomba vijiji vya Wilaya ya Geita na Chato, vipimwe na kutolewa hatimiliki mapema iwezekanavyo.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri anayoifanya, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Rita L. Mlaki. Aidha, nawapongeza kwa kuteuliwa kuwa manahodha wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Serikali kwa kuipatia Kilindi hadhi ya kuwa Wilaya, karibu miaka minne sasa. Ni kweli tumerithi Afisa Ardhi, Mipango Miji na *Surveyor* kutoka Handeni. Pamoja na matatizo mengi na kashfa nyingi alizonazo Afisa Ardhi, tunashukuru kuwa angalau tumekumbukwa kuwa tunahitaji watumishi.

Awali ya yote, naomba kama wapo Maafisa Ardhi, wenye sifa zinaendana na Awamu ya Nne, basi mtuangelie Kilindi. *Surveyor* muda mfupi tu baada ya kuhamishiwa Kilindi, ambako tunamhitaji sana, ameenda masomoni, mantiki haikueleweka kwetu. Kilindi baada ya kuwa Wilaya, kuna matatizo ya mipaka ya Kiwilaya. Suala hili limeletwa Wizarani muda mrefu na hivi sasa inasababisha kuwe na migoro. Ni lini Serikali itatutulia tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la matatizo ya mipaka ya vijiji nalo linazua utata mkubwa. Hakuna *program* yoyote ya kuweza kulifanya zoezi maalum katika Wilaya mpya ili kuondoa kero hiyo? Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 74, jedwali linaonesha kwa mwaka mzima 2005 – 2006 ni Mkoa mmoja tu wa Iringa uliopimiwa vijiji. Haiwezekani kuwa na mkakati wa makusudi kutatua tatizo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama mwakilishi wa Wanakilindi, kusahihisha usemi unaotamkwa sana kuwa Kilindi kuna ardhi ya bwelele, watu waende huko, ufutwe kabisa. Hali hii imeleta wageni wengi, ambao wengi wao wamechukua ardhi kwa eka Sh.10,000/= halafu kwa miaka hawajaonekana.

Tatizo hili limeleta kero, sasa inasababisha kumwaga damu kwani zile jamii zimepanuka, watoto na wajukuu wamekuwa na miji yao ardhi hakuna, Serikali inawezaje kuingilia kati ili kusaidia suala hili nyeti na hatari?

Kamati ya Ardhi katika kuangalia migogoro, imezidisha migogoro kwa kutaka kuondoa wafugaji au wakulima, ambao wamekuwepo kwa muda mrefu. Waende wapi? Sasa wameanza kuchomeana nyumba. Madiwani walikuwa hapa kutaka kumwona Mheshimiwa Waziri, nimewasihi wasubiri niulize. Naomba majibu ili nisisimame kwenye vifungu.

MHE. DORAH H. MUSHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa, pamoja na wengine wote walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali ndani ya Chama cha Mapinduzi Taifa. Aidha, nachukua nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, kwa hotuba nzuri waliyowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuchangia suala la Mererani. Tangu mwaka 2003, Rais wa Awamu ya Tatu aliruhusu Mererani, Wilaya ya Simanjiro kuwa Mji Mdogo. Nashindwa kuelewa, tokea muda huo mpaka leo, hakuna kinachoendelea. Naomba Wizara hii inieleze ni kwa nini agizo hilo halitekelezwi? Tunataka Mererani ipewe hadhi na iwe Mji kama Miji mingine ili tuweze kuharakisha maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watu kuhamishwa katika eneo la Kipawa, jirani na Uwanja wa Ndege, wananchi hawa wanalalamika sana kwamba, eneo hilo lilishapimwa na wananchi wanangojea kufidiwa ili waondoke kwenda kuhamia maeneo mengine. Je, ni kitu gani kimekwamisha au kama Serikali imeamua kuacha, basi wekeni wazi ili wananchi wasikae bila kujua la kufanya. Wengi wao wameshindwa kuendeleza viwanja vyao, wengine nyumba zao zilikuwa zimejengwa na kupauliwa kabisa. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba amemkwamisha mwananchi huyu? Naomba Wizara iweke wazi au iwaachie waendeleo na shughuli zao, kuliko ilivyo sasa hivi, waambiwe ni lini wanafidiwa. Naomba jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mheshimiwa John P. Magufuli, kwa kasi yake ya kuelewa na kushughulikia masuala ya ardhi. Tatizo ninaloliona ni uwezo wa wataalamu, walioko katika ngazi ya wilaya kuelewa na kutafsiri Sheria za Ardhi. Aidha, wananchi walio wengi nao hawazijui Sheria za Ardhi na hata taratibu za kupata hati miliki hawazijui. Nashauri kuwe na taratibu za kuwaelimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza MKURABITA, rasilimali waliyonayo wakulima ni ardhi. Je, kuna utaratibu wa ki-mradi wa kuanza zoezi la kupima mashamba na kuwawakilisha kimila wakulima? Ili kuharakisha zoezi hilo, nashauri Wizara ambazo zinahusika moja kwa moja na upimaji wa mashamba, zishirikiane na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kupunguza gharama na kuharakisha

zoezi la upimaji. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Idara ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi, inapima mashamba (*Topographical Surveys*) katika miradi yote ya umwagiliaji. Kwa nini tusiweke utaratibu wa kushirikiana?

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara na Mashirika yote, yaliyo chini ya Wizara hii. Hata hivyo, napenda kutoa mapendekezo yafuatayo kuhusiana na Wizara hii:-

Wizara ifikirie upya sera ya vijiji ili badala ya kuendelea kuvigawa na kuvipima kutokana na kuongezeka kwa wanavijiji, ibuni utaratibu wa kuviunganisha vijiji kabla ya kuvipima na kubuni muundo mpya wa kiutawala, kwa vile hali ilivyo mahali pengine vijiji vitaendelea kuungana kama mnyororo. Mtindo wa sasa wa kuendelea kugawa vijiji na kuvipima rasmi, hautatui tatizo hili. Kuna haya ya kutazama suala hili. Mahali pengi vijiji vya katikati, Rubanwa katikati hukosa ardhi wakati vijiji vya nje vina ardhi ya kutosha.

Wizara ifikirie upya msimamo wake wa kuwanyang'anya viwanja wale walioshindwa kujenga majengo mijini na kuviuza kwa tenda. Kitendo hiki kinawaondoa Watanzania maskani na kuwafanya mamilionea au matajiri wapate viwanja na kuishi mijini. Kwa vile sharti la kujenga nyumba kwa kipindi cha miaka mitatu, linakwama kutokana na kukosekana kwa benki ya nyumba (mikopo) nchini, Wizara itendelea na mtindo huu milele. Naogopa wanyonge wataumia zaidi badala ya kusaidiwa. Kwa nini wasisaidiwe, watakwenda wapi? Ushauri wangu zijengwe nyumba za ghorofa na kuwagawia sehemu ya nyumba.

Wizara itazame upya msimamo wa kuwanyang'anya wanyonge, viwanja walivyopewa kisheria. Badala yake ishirikiane na Wizara nyingine, kuunda Benki ya Mikopo ya Nyumba nchini, vinginevyo tunaandaa miji ya matajiri.

Shirika la Nyumba litakiwe na liwezeshe kujenga nyumba za bei nafuu na za bei kubwa ili kuwawezesha wanyonge kupata nyumba. Vipi wenye viwanja wasishirikishwe na *NHC* ili kuwekeana utaratibu mzuri wa kufaidika na viwanja vyao. Kama ni lazima, basi utaratibu mpya wa kugawa viwanja ubuniwe ili waombaji wathibitishwe uwezo wa kujenga katika kiwanja *within three years* na wahusika wathibitishwe uwezo wa mwombaji.

Katika miji mingi, wajenzi wa nyumba ni watu wenye kipato kidogo, ambao hujenga nyumba kwa kudunduliza na hivyo kuchukua muda mrefu kujenga nyumba. Tanzania ni nchi ya ajabu, kwa sababu watu wanajenga nyumba bila mikopo. Tusilinganishe nchi yetu na nchi za Ulaya, mazingira ni tofauti.

Wizara ishirikiane na Halmashauri za Wilaya au Miji ili kujenga miji ya mfano, kwa ubora wa mpangilio wa majengo, huduma na kadhalika, badala ya mtindo wa sasa wa wapimaji kufuata ujenzi holela (*squatters*), kama ujenzi ulivyo katika maeneo ya Kariakoo, Manzese na Mwanjelwa - Mbeya.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii ya Wizara hasa hutokana na Mheshimiwa John P. Magufuli, alivyo mahili kwa kila anapoenda kwenye Wizara na kuimudu utafikiri alizaliwa nayo. Pia Naibu Waziri na watendaji wake wote wa Wizara hii, kwa kuleta mageuzi makubwa katika utendaji kazi hasa ikizingatiwa Wizara hii ilikuwa ina sifa mbaya sana. Lakini leo hii mambo yameshaanza kurekebisha hivyo, nina imani yote tutakayoshauri yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba, sisi tunadhibiti kwenye maeneo ya madini ufugaji, uvuvi na kilimo, tuna matatizo sana ya umilikaji wa ardhi, kwa kuzingatia kuwa wananchi wetu hawajui sheria hivyo, kupelekea kutokutambua haki zao za msingi hasa katika umilikaji wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Geita, kumekuwa na matatizo makubwa kama ya fidia ambayo ilitolewa kidogo baada ya wahusika kutambua kuwa wamepunjwa, migogoro inaendelea hadi hivi sasa. Kwa kigezo hiki, naomba Vijiji vya Geita vipimwe na kupewa hati miliki ambayo itakuwa kinga kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii isaidie kutoa michoro ya ujenzi wa nyumba vijijini, yenye bei nafuu, pamoja na kuwawezesha wananchi kwa kuwauzia vifaa vya ujenzi kwa bei nafuu, kama inashindikana basi Serikali ipange bei moja kwa vifaa vyote vya ujenzi Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna waliojenga kwenye milima hasa mkoani Mwanza, nashauri wananchi hao wapelekewe miundombinu ya kutosha ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira. Kama itashindikana, Serikali iwatafutie eneo na kuwajengea nyumba na miundombinu ya uhakika badala ya kutoa fidia ambayo mwananchi akipewa hawezi kujenga nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kulikuwa na bomoa bomoa na watu wengi sana waliathirika kwa kutokujua sheria, naomba wananchi hao angalau wapewe kifuta machozi, hasa wale waliobomolewa katika barabara la Kilwa na ujenzi wa barabara haujaanza hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msisistizo, namwomba Mheshimiwa Waziri, airekebishe Wizara hii kama alivyofanya kwenye Wizara ya Ujenzi na kwa kuanzia tu wapime vijiji vyote vya Geita, Bukombe, Sengerama na Chato, ili kutimiza masharti ya kuwa mkoa, kama Serikali ilivyojibu swali langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri pamoja na matatizo mbalimbali yanayowakabili.

Nchi nyingi duniani, hutumia utaratibu wa *Mortgage Lending* ili kuwawezesha wananchi na makampuni kujinunulia nyumba za kuishi na za biashara kwa njia ya mikopo. Mikopo ya aina hii, inaweza kutolewa na vyombo vya fedha (mablenki), vilivyopo na hasa vile vyenye mitaji mikubwa kama vile *NBC, Stanchart, Barclays, CRDB* na kadhalika, ili mradi Serikali itengeneze mazingira rafiki kwa mikopo ya aina hii, hususan kwa kufanya marekebisho katika sheria zetu ili kurahisisha taratibu za mablenki kukamata na kuuza (*foreclose*), mali zilizowekwa kama dhamana kwa mikopo. Aidha, ni vizuri ieleweke kuwa, Benki ya *ABSA*, ambayo ni mbiu mkubwa katika benki yetu ya *NBC*, inatoa mikopo mingi ya ujenzi wa nyumba za gharama mbalimbali huko Afrika ya Kusini. Nashauri Serikali ifanye mazungumzo ya karibu na benki hii, ili kubaini maeneo/sheria zinazohitaji kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa vibali vya ujenzi unachukua muda mrefu sana tena kwa usumbufu. Hali hii inasababisha ucheleweshaji wa kuanza ujenzi wa viwanja husika na hivyo kutumia vibaya muda wa miezi 36 ya kuendeleza viwanja. erikali itatue tatizo hili haraka.

Taratibu za utoaji na uandikishaji wa hati za viwanja mbali na vile vya miradi maalum ya upimaji viwanja, huchukua muda mrefu sana tena kwa usumbufu mkubwa. Nashauri Wizara ifanye marekebisho yatakayosaidia upatikanaji wa hati za viwanja vyote haraka iwezekanavyo, kama ilivyo katika viwanja vya miradi maalum ya upimaji. Tatizo hili linaathiri pia uandikishaji wa hati za wanaouziana nyumba/viwanja vilivyo endeleva au nyumba na kadhalika, zinazowekwa dhamana katika vyombo vya fedha, kwa ajili ya mikopo. Hii ni miongoni mwa kero zinazoathiri utoaji wa mikopo ya nyumba.

Kuna haja ya kuanzisha vitengo maalum kwa shughuli hii ili kuharakisha uandikishaji wa *Mortgages*, pamoja na *Transfer Deeds from one owner to another*.

Uvamizi wa Viwanja vya Matumizi Maalum kama vile mashule, viwanja vya michezo, Serikali isikubali kuachia wale wanaobadili matumizi ya viwanja bila kuzingatia taratibu. Aidha, wanaofanya hivyo waadhibiwe vikali ili waachane na tabia hii mbaya. Siyo jambo rahisi kwa wananchi kuendeleza viwanja vyao katika kipindi cha miezi 36, ukizingatia matatizo niliyoyaeleza hapo juu; bila mikopo na ucheleweshaji wa *building permits*. Kwa hiyo, kuwanyang'anya wananchi viwanja vyao ni kuwaingiza katika Lindi la umaskini mkubwa, nashauri zoezi hili lisimamishwe na Serikali iwajengee wananchi mazingira ya kuweza kujenga katika viwanja vyao na siyo kuwanyang'anya. Kama Serikali itaendelea na utekelezaji wa azimio lake ni dhahiri kwamba, itaendeleza ujenzi wa matabaka ya walionacho na wasiokuwa nacho.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote Wizarani, kwa kuandaa hotuba nzuri, yenye mwelekeo mzuri. Hata hivyo, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali kwa kuanzisha Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (*NHBRA*). Hata hivyo, naomba kujua yafuatayo: Ni tafiti ngapi zimeshafanyika hadi sasa tangu Wakala huo uanzishwe na tafiti hizo zimewanufaisha wananchi kwa kiasi gani katika kuwajengea nyumba bora?

Ni Mikoa au Wilaya ngapi zimefaidika hadi sasa na uanzishwaji wa Wakala huo na wakala una mpango gani katika kuhakikisha kwamba, huduma hiyo inawafikia wananchi wengi zaidi hasa wa vijijini?

Je, tafiti na ushauri uliotolewa na wakala kuhusu bei za vifaa vya ujenzi, umewasaidiaje au umeongeza kasi ya ujenzi wa nyumba bora kwa kiwnago gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyumba za Mbweni, zilizopo Jijini Dar es Salaam, kwa kiasi kikubwa zimejengwa bila kuzingatia *original map*, matokeo yake kumeanza kujitokeza migogoro ya viwanja hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nimeuziwa nyumba Na. 58 *block 330* huko Mbweni na nyumba hiyo ina tatizo la *plot*, kwa maana kwamba, ilijengwa bila kuzingatia ramani ya awali, pamoja na nyumba nyingine. Hali hii imesababisha baadhi ya wakazi wasiokuwa na subira, kuanza kufanya ukorofi katika mipaka ya viwanja vya nyumba hizo. Nimejitahidi sana kuwasiliana na Mkurugenzi Mkuu wa *Tanzania Building Agency (TBA)*, ili kurekebisha hali hiyo, amejitahidi sana kuzuia. *TBA* wanasema kwamba baada ya kugundua tatizo hilo waliwasiliana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili wakalipime eneo hilo jipya. *TBA* wamesema wameshailipa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kazi hiyo. Ninachoomba Wizara hii iliharakishe upimaji wa viwanja hivyo haraka inavyowezekana ili kuepusha wakazi wanaoishi kwenye nyumba hizo wasigombane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linalonikera ni hili la wakala huu wa majengo (*TBA*), kuendela kuwa chini ya Wizara ya Miundombinu. Hii inashangaza sana kwa sababu *TBA* wanashughulika na majengo hasa ya makazi na tuna Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; kwa nini iwe chini ya Wizara ya Miundombinu? Mimi napenda nishauri kati ya Wizara hizo mbili basi ni vizuri *TBA* iwekwe chini ya Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi alivyoanza kuisafisha Wizara hii. Tunashukuru kwamba, baada ya Wizara kubaini kwamba, baadhi ya maafisa wake wanamiliki viwanja vingi, imeamua kuwanyang'anya, hili linatia moyo sana. Hata hivyo, kuwanyang'anya tu hakutoshi, mimi nashauri kwamba, pia wachukuliwe hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi. Hili litakuwa fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuendelea kupima vijiji na kuvipa hati miliki, hatua hii itavirekebisha vijiji na wananchi wanaoishi katika maeneo hayo kuweza kutumia hati hizo kupata mikopo. Nashauri Wizara, iongeze kasi ya upimaji ili wananchi wengi zaidi wafaidike na zoezi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SIGFRID S. NG'ITU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali naomba niunge mkono hoja kwa asilimia zote mia moja, ni nzuri sana.

Namwomba Mheshimiwa Waziri, yeye mwenyewe, msaidizi wake au hata Wakurugenzi wote, waje kule kwetu kuona hali halisi, kwa vile sisi ni Wilaya mpya. Nimeona kwenye jedwali ndani ya kitabu chako cha bajeti kuwa, Ruangwa ilikopa Sh. 2,130,000/= kwa ajili ya *PDRF*, hazijarudishwa hadi sasa. Nadhani tabia hii itasababisha tuonekane wabaya machoni penu. Je, nikienda kuwabana Halmashauri kule kwetu nitakuwa nimekosea? Bila shaka tunakosa mengi kwa kutokulipa deni hili.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, huyo ndio alikuwa msemaji wetu wa mwisho, kwa hoja ya Wizara hii. Kabla sijamwita Mheshimiwa Naibu Waziri, nawatambulisha wageni 30 kutoka Matawi ya Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Kati wa *NBC*, ambao wako kwenye *public gallery*, karibuni sana. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ikiwa ni bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne.

Nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuchaguliwa na Watanzania walio wengi, kuliongoza taifa letu, Awamu hii ya Nne. Pia nampongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, kwa kujaliwa kushika nyadhifa za juu za nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi, kuwa katika Bunge hili kwa kipindi cha miaka mitano. Kipekee nachukua nafasi hii, kumshukuru Rais kwa kunitua katika Serikali yake ya Awamu ya Nne na wananchi wa jimbo langu la Kawe, kwa kunichagua kuwa Mbunge wao kwa kipindi kingine cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mwisho na sio kwa umuhimu, napenda nimshukuru mume wangu mpendwa, Ndugu Theofras Elifuraha Mlaki na watoto wangu, Nambua, Mcharo na Lawrence, kwa msaada na *support* kubwa wanayonipa, kuniwezesha kufanya kazi yangu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nakwenda kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Muda niliopewa sio mrefu sana, lakini nitajitahidi kuchagua hoja muhimu, ambazo ningependa kuzijibu kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza na Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mbunge wa Ilala, ambaye ameongelea kuwa *National Housing* wanawanyanyasa wapangaji na kuwatoa bila ya wao kusikilizwa na kwamba sio anawatetea kwa sababu

hawajalipa kodi. Napenda tufafanue hili, Shirika linaendesha shughuli zake kwa misingi ya sheria, zinazotawala masuala ya upangishaji wa nyumba na sheria inayotumika kwa sasa ni Sheria Na. 11 ya mwaka 2005.

Chini ya Sheria hii, mpangaji anapovunja kanununi za upangaji kwa mfano, kutolipa kodi ya pango, mwenye nyumba ana haki ya kumtoa kwenye nyumba. Utaratibu unaofuata ni pamoja na kumpa *notice* mpangaji ya mwezi na baada ya kipindi hicho kupita, basi mwenye nyumba hupeleka taarifa kwa dalali wa mahakama ili wantoe kwenye nyumba. Dalali huyo ndio mwenye wajibu wa kumtoa mpangaji kwenye nyumba.

Huu ndio utaratibu wa sheria na tumeona hata Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na sisi kwamba, deni lilikuwa kubwa sana la *National Housing*, shilingi bilioni kumi na moja na milioni saba na laki saba. Hilo ni deni kubwa sana, ambalo lingeweza kutusaidia kujenga nyumba za kuuza na kupangisha kwa manufaa ya Watanzania walio wengi. Baada ya Mheshimiwa Waziri, kutoa ile *notice*, tumeweza kukusanya shilingi bilioni tatu na zaidi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, akubali kutuunga mkono kwa manufaa ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende suala lingine, ambalo amechangia Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, ameongelea kuwa kuna nyumba ziliwahi kuuzwa na hizo nyumba ziliuzwa ili kulipunguzia mzigo Shirika la Nyumba na sasa ametoa wazo kwamba, nyumba zilizoko Upanga, wale wapangaji kwa sababu pia matengenezo ni duni, wangeuziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu kupitia Shirika la Nyumba, iliuzwa nyumba walizokuwa wanakaa wapangaji ndogo ndogo zipatazo 5,000 katika miji mbalimbali nchini.

Kweli lengo lilikuwa ni kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, kupunguza mzigo wa uendeshaji kwa kuwa kodi ilikuwa ndogo, ikilinganishwa na gharama za matengenezo.

Lakini kwa zile nyumba ambazo nyingi, zilitaifishwa na Serikali mwaka 1971, Wizara yangu haina mpango wa kuziuzwa, kwa sababu ndicho chanzo kikuu cha mapato cha shirika na ndizo zinazotoa mtaji wa ujenzi wa nyumba mpya na kuliendeleza shirika ambalo kwa sasa linajiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matengenezo duni, ni kweli shauri ya kodi ndogo, ndio sababu matengenezo yanakuwa duni. Hata hivyo, Shirika limebuni mpango wa kuzikarabati nyumba zake kwa kiwango kikubwa, ndani ya miaka tano, kuanzia mwaka huu na fedha zitakazopatikana zitajenga nyumba nyingine na vilevile itabidi tuongeze kodi kwa kufuatana na bei ya soko angalau kwa asilimia 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa wazingatie ukurasa wa 81 wa kitabu chetu cha hotuba kuna jedwali ambalo linaonyesha kwamba tumekarabati nyumba 1,481 zilifanyiwa matengenezo katika miji mbalimbali kwa gharama ya shilingi bilioni 3, 733.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwenda kwenye suala lingine la Mbunge mwenzangu wa Dar es Saalam Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, ambaye vile vile ameona kwamba nyumba za chini zimeuzwa wapangaji wa maghorofa nao wanaomba kuuziwa. Mheshimiwa anaongelea nyumba ambazo ziko pale Keko, Ubungo yale *ma-flat* pamoja na Ilala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufafanua tena zaidi kwamba Shirika linajiendesha kibiashara, shirika liliuza nyumba ambazo zilionekana zinaleta hasara kwa shirika ambazo ni ndogo ndogo lakini hizi kubwa ambazo ni kama hayo maghorofa haya tunapata mapato ya kuridhisha na gharama za matengenezo ya hizi nyumba pia ni ndogo hivyo halikusudii kabisa na ninasikitika kumwambia kuziuzwa hizi nyumba za maghorofa kama alivyoomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja nyingine ambayo ameiongelea Mheshimiwa Ruth Msafiri. Kweli anasikitika na amesema kwamba Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yaangaliwe sana yasivunje Sheria na taratibu za kuunda Mabaraza hayo izingatiwe na Mabaraza yajiepushe na hongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Ruth Msafiri, kwa sababu katika vijiji kuna migogoro mingi sana ya ardhi, binafsi nimetembelea vijiji kadhaa na nimeshuhudia migogoro mingi na Wizara yangu inajitahidi kuunda Mabaraza mengi iwezekanavyo na nikiwa kama msimamizi wa Mabaraza hayo ninaahidi kuyafuatilia kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara imeweka muundo, sifa na kanuni za Wajumbe wa Baraza hilo, Sheria pia imeweka utaratibu wa kutaka Wajumbe wa Baraza hilo na kuwa kila mjumbe wa Baraza atateuliwa na Halmashauri ya Kijiji na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji ina maana palepale kwa wananchi wenyewe ili kuhakikisha kuwa hao watu wanaochaguliwa siyo wala rushwa katika kusimamia masuala ya ardhi na haswa ya watu ambao wana matatizo katika vijiji husika. Kwa hiyo, tunawashauri wanavijiji wawachague wajumbe ambao wana sifa nzuri ili waweze kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niongelee suala la ucheleweshaji wa hati. Hili suala kusema kweli limewakera wengi na kumekuwepo na ucheleweshaji wa hati kutokana na sababu kadhaa ambazo Serikali sasa iko tayari kuzisahihisha na kushirikiana na Wizara zinazohusika kutengeneza hati kwa haraka.

Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, amesema kwamba tunachelewa sana kutengeneza hizi hati. Hizi zinacheleweshwa kwa sababu kuu tatu, kwanza hati hizi zinatengenezwa katika Halmashauri za Miji, hizi Halmashauri kule kuna wataalam ambao wanaitwa Maafisa Ardhi Wateule.

Sasa kutokana na kutokuwepo wataalam wenye sifa za kuandaa hizi hati wa kutosha kunakuwepo na ucheleweshaji, vile vile kuna vifaa ambavyo vinatumika kama ambavyo mmeona kwenye hati kuna kikaratasi ambacho kinakaa ndani kinachoonyesha *plot* iko wapi hii inatengenezwa kwa vifaa maalum ambayo hii karatasi inaitwa *Deed Plan*. Hii vile vile vifaa vyake vya kutengeneza vinakuwa vinaadimika na mwishowe hata wanapotengeneza Halmashauri wanachelewesha kuleta kwa Kamishna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pamoja na kushirikiana na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) tutashirikiana ili kuangalia ku-*fast track* zoezi la kutengeneza hati kwa sababu tumegundua kwamba na wananchi mmesema kwamba zitasaidia sana katika kupata mikopo na kupunguza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuongelea suala lingine ambalo ameliongelea Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, kuhusiana na kushughulikia mipaka ya nchi yetu. Ni kweli ni muhimu kushughulikia mipaka ya nchi yetu na kuna wengine wameuliza sana kuhusu Ziwa Nyasa, ningependa kusema kwamba Wizara yetu imefanyia kazi maelezo ya Mheshimiwa Rais kwa kuzialika nchi za Msumbiji na Comoro kurejea mazungumzo ya mpaka katika Bahati ya Hindi.

Kuhusu mpaka katika Ziwa Nyasa natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wavute subira, Waheshimiwa Marais wastaafu Rais Benjamin Mkapa na Rais Bakili Muluzi, walikwishakaa kukubaliana kwamba mpaka utapita wapi na sasa hivi viongozi waliochukua Serikali kwa awamu hii wanasimamia hilo na tumeshaanza mazungumzo na nchi ya Malawi kuhakikisha kwamba mipaka hiyo inazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema kuhusu hoja aliyoisema Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, kuhusiana na nyumba za *National Housing*. Ameeleza kabisa kuhusiana na nyumba ya Mheshimiwa Marehemu Masanywa ambayo ilikuwa kiwanja namba 444 Mtaa wa Mahando. Ni kweli bado utafishwaji wa nyumba, mwaka 1971 Serikali ilipokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wamiliki wa nyumba zilizotaifishwa, Serikali ilitoa uzito wa jambo hilo ikilazimika kuunda Kamati ya Huruma na *Appeals Tribunal* ambazo zilikasimiwa kupokea na kuyachambua malalamiko ya namna hii. Kamati hizo zilikuwa na muda maalum ulioisha mwaka 1980 kwa kushughulikia hizi hoja na watu wote ambao walikuwa na hoja walirejeshewa nyumba au sehemu ya nyumba zao kwa masharti maalum. Mlalamikaji katika kipindi hicho alikuwa na haki ya Kisheria kuwasilisha hoja yake ili apatiwe uamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na malalamiko yaliyoletwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Pili alisisitiza kwamba umilikaji wa nyumba hii ya Mahando uendelee kuwa chini ya Serikali na kumbukumbu za barua tunazo. Wizara yangu haijapata maelezo yoyote juu ya utekelezaji wa ahadi aliyopewa mke wa Marehemu, Bi Erica Maswanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barua inayoonyesha kwamba iliandikwa na Katibu Mkuu lakini ilikuja tu kopi katika Wizara yetu kusema kwamba apewe *flat* ya vyumba vitatu. Tatalifuatilia hilo na tungemwomba Mheshimi wa Aziza Sleyum Ally,

aje kwa karibu tuweze kulitazama hilo suala na kuongea na yeye tuone tutalisuluhisha namna gani.

Kuhusu nyumba ambazo Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, alizodai kwamba zinakaliwa na watu ambao wanalipa kodi kwa watu binafsi badala ya Shirika la Nyumba, Wizara yangu haina taarifa wala vielelezo vinavyohusu madai yake. Hata hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge aniletee taarifa alizonazo juu ya jambo hili ili niweze kulishughulikia mara moja na kutoa maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nyumba iliyopo Mtaa wa Longido Kiwanja Namba 405 Dar es Salaam haimilikiwi na Shirika la Nyumba, mlalamikaji alijibiwa hivyo na Shirika kwa barua yenye kumbukumbu ambazo namba zake tunazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kushukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kuanza kuchangia hoja nyingi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, lakini kabla sijamaliza tu yote haya nitakayoyachangia nataka nianze kwa kusema neno kubwa kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango mbalimbali ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamechangia katika suala linalohusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kusema kupitia hotuba ya Waziri Mkuu na hotuba nyingine zilizowasilishwa hapa wako Waheshimiwa Wabunge 34, waliochangia kwa maandishi leo wako Waheshimiwa Wabunge 65, waliochangia kwa kusema wako 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa ruhusa yako sitawataja hawa ambao walichangia kwenye hotuba zilizopita kwa sababu hata majibu yao tumekwisha yatayarisha na kesho watayapata wote hawa 34. Lakini niwataje hawa ambao wamechangia kwa maandishi leo na wale waliochangia kwa kusema leo.

Waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Lawrence Masha, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Christopher Chiza, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Brigedia Jen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Vita Kawawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Mheshimiwa

Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Michael Laizer na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa James Lembeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Mwinchoum Msoni, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga na Mheshimiwa Zaynab Vulu. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Profesa Feetham Banyikwa, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Andrew Chenge na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni nao naomba niwataje kama ifuatavyo, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq na Mheshimiwa Rita Mlaki Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana wote ambao wamechangia katika hoja mbalimbali zilizotolewa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakavyoona ni Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wamezungumzia kuhusu suala la ardhi na hii inadhahirisha wazi kabisa kwamba suala la ardhi ni muhimu katika maendeleo ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kama ambavyo unajua ina ukubwa wa kilometa za mraba 945,000 na tangu tupate Uhuru wananchi wamekuwa wakiongezeka siku hadi siku. Kwa mfano katika miaka ya 1967 idadi ya watu katika nchi nzima ilikuwa karibu milioni 12 lakini tumeona katika suala la makazi watu waliyokuwa wakiishi katika maeneo ya mijini ilikuwa ni 5.7% na kwa sasa hivi ambapo tuna jumla ya wakazi milioni 35 asilimia ya watu wanaoishi katika maeneo ya Mijini ni 25% kwa hiyo 75% ni ya wale wanaoishi katika sehemu za vijijini. *(Makofi)*

Lakini tumeona pia katika matatizo haya katika asilimia zote za hawa watu wanaoishi katika maeneo ya mijini ni 75% wanaishi katika maeneo ambayo hayajapangwa yaani *unplanned areas*. Kwa Tanzania ukiangalia katika matokeo Shirika la *UN Habitat Tanzania* tuko kwenye hatua mbaya zaidi ya watu ambao wanaishi kwenye maeneo ambayo hayajasajiliwa na *unplanned areas*, kwa hiyo tuna jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba matatizo haya yanaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ulivyoona na kama walivyochangia Waheshimiwa Wabunge wengi wameelezea kuhusu migogoro mingi ambayo imekuwa ikijitokeza katika masuala ya ardhi. Migogoro hii imekuwa ikiongezeka kwa sababu sasa wananchi wameshatambua ardhi ni mali, migogoro imekuwa ikijitokeza mingi baada ya ardhi kupewa thamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi tu cha mwaka uliopita ni zaidi ya migogoro ambayo ilifikishwa kwenye Mahakama za Ardhi za Wilaya ilikuwa zaidi ya 4035 katika kipindi cha mwaka mmoja na hii ni migogoro iliyofikishwa kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya. Bado hatujataja migogoro iliyofikishwa kwenye Mabaraza ya Kata, Vijiji, katika Mahakama Kuu za Ardhi, kwa hiyo, kimsingi suala la ardhi lina migogoro mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu tumejiweka tayari katika kutatua matatizo mengi, kwa hiyo, michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wote napenda kusema kwa wazi kabisa kwamba tumeipokea na tutaifanyia kazi kwa sababu hii ni changamoto kwetu katika kuhakikisha kuwa suala la Ardhi linatafutwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona katika kazi za upimaji kwa mfano katika Mikoa zaidi ya viwanja 21,710 na mashamba zaidi ya 1,631 na vijiji 232 vilipimwa na kupatiwa maamuzi mbalimbali. Utaona pia katika jedwali letu ambalo tumelitoa kuanzia jedwali namba moja hadi 17 tumeelezea kazi mbalimbali ambazo zimefanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika kipindi cha mwaka mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakavyoona na kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza tatizo kubwa ni bajeti. Wizara ya Ardhi bajeti yake ni shilingi bilioni 18 ambazo tunaziomba kwa sasa, lakini ukilinganisha na matatizo ambayo yapo ni kweli kabisa nakubaliana na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba pana umuhimu wa kutenga fedha nyingi ili kuweza kutatua matatizo haya, kwenda kutatua migogoro Mabaraza ya Ardhi, kwenda kupima nchi nzima Vijiji na kadhalika haya yote yanahitaji *resources*. Kwa hiyo, ni kweli nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wamezungumza kwamba kuna umuhimu wa kuangalia namna ya kuwekeza zaidi katika masuala ya fedha ili Sekta hii ya Ardhi iweze kuleta mchango mkubwa katika masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka jana zaidi vijiji 119 vilipimwa na vilivyopimwa vilihusu katika Mkoa mmoja tu. Katika bajeti ya mwaka huu tumepanga kupima vijiji 3,104 na katika upimaji huo tumezingatia sana katika mikoa

mingine ambayo ilikuwa haijapimwa hata kijiji kimoja. Mkoa wa Lindi vijiji vyake vilikuwa havijapimwa, Mkoa wa Rukwa vijiji vyake vilikuwa havijapimwa, Mkoa wa Tanga vijiji vyake vilikuwa havijapimwa, Mkoa wa Kigoma *percentage* kubwa vijiji vyake vilikuwa havijapimwa na kadhalika. Kwa hiyo tumeamua katika bajeti ya mwaka huu kuhakikisha kwamba Vijiji mbalimbali ni lazima vipimwe ili wananchi waweze kufaidi hali halisi ya uchumi na maendeleo ya sehemu zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumbukumbu za Bunge hili kwa mfano katika Mkoa wa Arusha ulikuwa na Vijini 304 lakini palikuwa na vijiji vilivyokuwa vimepimwa 270 na vijiji ambavyo vilikuwa havijapimwa ni 34 ambavyo viko katika Wilaya ya Ngorongoro. Katika bajeti ya mwaka huu tunavipima vijiji vyote 34 vilivyopo katika Wilaya ya Ngorongoro.

Katika Mkoa wa Dodoma, vijiji ambavyo vilikuwa vimeshapimwa ni 464 na ina jumla ya vijini 464 lakini hata hivyo tutaangalia kama patakuwa na vijiji vingine ambavyo vitaweza kufanyiwa marekebicho, kwa hiyo, wao wana bahati nzuri kwamba vijiji vyao vimepimwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkoa wa Iringa una jumla ya vijiji 702, lakini vijiji ambavyo vilikuwa havijapimwa ni 563 na mwaka jana vilipimwa vijiji 119 kwa hiyo katika Bajeti ya mwaka huu napo tumepanga fedha kwa ajili ya kupima vijiji vilivyopo katika mkoa wa Iringa.

Katika mkoa wa Kagera vijiji viko zaidi ya 660 na karibu vyote vimepimwa isipokuwa vijiji 20 kwa hiyo, katika bajeti ya mwaka huu mkoa wa Kagera vijiji vitakavyopimwa ni vijiji 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma una vijiji 232 na karibu *percentage* kubwa ya vijiji vya Kigoma ni vijiji vichache tu vilivyokuwa havijapimwa kwa hiyo, vile vitakavyokuwa vimebaki kutokupimwa mwaka huu tunavipima vyote. Katika Mkoa wa Kilimanjaro viko vijiji 438 na vyote vimepimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Lindi kuna jumla ya vijiji 429 vilivyopimwa ni 30 tu kwa hiyo katika bajeti ya mwaka huu tutapima vijiji vilivyobaki 391. Katika Mkoa wa Manyara vijiji vilivyopo ni 312 ambavyo vimepimwa ni 307 kwa hiyo katika bajeti ya mwaka huu tutapima vijiji 5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara vijiji vilivyopo ni 438, vilivyopimwa ni 423 kwa hiyo, mwaka huu tutapima vijiji 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mbeya una vijiji 770 na ambavyo vilikuwa vimeshapimwa ni 222 ambavyo havijapimwa ni 548 kwa hiyo katika bajeti ya mwaka huu hivyo ambavyo havijapimwa vyote tutavipima katika mkoa huu wa Mbeya.

Mkoa wa Morogoro vijiji ambavyo vipo kwa ujumla ni 584, ambavyo vimeshapimwa ni 346 kwa hiyo ambavyo havijapimwa napo katika bajeti ya mwaka huu tutavipima.

Mkoa wa Mwanza vijiji ambavyo vipo kwa mkoa mzima ni 616 na vyote vimepimwa lakini hata hivyo tumepanga vijiji kama vitano vitamipimwa ambavyo vitaongezeka.

Mkoa wa Mtwara una vijiji 578, ambavyo vimepimwa ni 324, vilivyobaki ni 254 kwa hiyo katika mwaka huu kuna vijiji ambavyo tutavipima katika mkoa huu wa Mtwara. *(Makofi)*

Katika mkoa wa Pwani kwa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kuna vijiji 424 na vijiji vyote havijapimwa hata kimoja kwa hiyo, katika mwaka huu tutavipima vyote vijiji vilivyopo katika Mkoa wa Pwani. Mkoa wa Rukwa kuna vijiji 351 na *percentage* kubwa vilikuwa havijapimwa navyo tunavipima katika mwaka huu. *(Makofi)*

Mkoa wa Ruvuma una vijiji 432 na vyote vimeshapimwa, Mkoa wa Shinyanga una vijiji 861, vijiji 557 vimeshapimwa na vilivyobaki na hasa hasa katika Wilaya ya Bukombe tutavipima katika bajeti ya mwaka huu. Mkoa wa Singida wana vijiji 548, vijiji vilivyopimwa ni 149 katika bajeti ya mwaka huu tutaendelea kuvipima vile vilevyobaki na Mkoa wa Tabora wana vijiji 485, vijiji vilivyopimwa ni 474 mwaka huu tutawapimia vijiji vilivyobaki ambavyo ni 11. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tanga una vijiji 728 karibu vyote havijapimwa isipokuwa vichache katika bajeti ya mwaka huu tumeamua kuvipima vijiji vyote vilivyopo katika Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nitoe hii taarifa kwa sababu katika hotuba yangu ya mwanzo nimeeleza ni idadi kiasi gani za vijiji vitakavyopimwa na ili kuweza kuwaletea maendeleo ya kweli wanakijiji na ili kuweza kuzuia matatizo mengi mbalimbali tumeamua kuvipima vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze tu baadhi ya maneno ya jumla kabla sijaanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa hapa ni kuhusu suala la miradi ya viwanja 20,000. Wizara yangu imeamua kuanzisha mpango wa kupima viwanja ili kuondoa kero ya kuwa na viwanja na kuondoa kero za wananchi katika masuala ya viwanja. Mradi huu ulianza kwa gharama ya shilingi bilioni 8.9 kwa Dar es Salaam lakini hadi sasa hivi kwa Dar es Salaam tumeshapima zaidi ya viwanja 31,000 na tunaendelea kupima katika Mkoa wa Mwanza viwanja 9500, Mkoa wa Morogoro viwanja 4000, Mbeya viwanja 5000 na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tungependa kutoa wito kwa Halmashauri zote za Wilaya katika nchi hii. Katika makusanyo ambayo huwa wanayapata waweze kuweka mipango yao ya kuweza kupima viwanja ambavyo wanaweza wakavitumia katika kuendeleza maeneo yao na kupunguza tatizo la viwanja. Lakini pia ningependa nitoe wito kwa zile Wilaya ambazo zilipewa mkopo kwa ajili ya kupima viwanja, Wilaya hizi zirudishe hizo pesa zilizopewa ili Wilaya nyingine nazo ziweze kukopeshwa kama

Revolving Fund. Wilaya hizi ambazo hazijarudisha fedha ni pamoja na Mwanga, Hai, Monduli, Babati, Kondoa, Maswa, Tarime, Bukoba, CDA Dodoma, Iringa, Mufindi, Mbarali, Njombe, Songea, Tunduru, Masasi, Newala, Luangwa, Liwale na Bagamoyo. Hizi Wilaya bado hazijarudisha fedha zilikopeshwa kwa ajili ya kupima viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nazipongeza Wilaya za Nkasi, Mpanda, Sumbawanga, Jiji la Mbeya, Ileje, Mtwara, Kibaha, Hanang, Kigoma Vijijini na Jiji la Tanga kwani wao wamemaliza kurudisha fedha ambazo walipewa kwa ajili ya mkopo. Mheshimiwa Andrew John Chenge, ananiuliza Biharamulo, lakini napenda kumfahamisha kuwa Biharamulo haikupata mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza hili kwa sababu mahitaji ya viwanja katika nchi yetu ni kubwa sana ni zaidi ya viwanja 500,000 vinahitajika katika miji inayokua. Ili kupambana na suala la makazi holela, ili kupambana na suala la kupata watu wanaoishi katika 75% kwenye maeneo ambayo ni *unplanned* ni vizuri sasa jukumu kubwa likawekwa pamoja na Wizara kushughulikia lakini Halmashauri zetu nazo zikabuni mipango mbalimbali ya kuweza kuhakikisha kwamba maeneo yao yanapimwa.

Suala lingine ambalo limezungumziwa ni kuhusu suala la Kurasini. Sheria ya utoaji wa ardhi yaani *Land Acquisition Act No. 47* ya mwaka 1967 na Sheria ya Mipango Miji yaani *The Town and Country Planning Ordinance Cap 37(8)* ya mwaka 1956 na Sheria ya Utwaaji Ardhi yaani *Land Acquisition Act No. 47* ya mwaka 1967 kwa mujibu wa vifungu 34 na Sheria Namba 47 ya mwaka 1967 Waziri anayehusika na ardhi ana mamlaka ya kutangaza eneo lolote la mji au pembazoni kuwa ni eneo la uendelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la uendelezaji la eneo la Kurasini suala hili lilitangazwa kwa mujibu wa kifungu namba 34 cha Sheria Namba 47 ya mwaka 1967 ya Utwaaji wa Ardhi yaani *Land Acquisition Act No. 47* ya mwaka 1967. Eneo la Kurasini lilitangazwa na Mheshimiwa Rais mwaka 1994 kwa kupitia tangazo la Serikali Namba 202 la mwaka 1994, hili suala ni kwa ajili ya kuendelezwa na bahati nzuri tumekwisha toa taarifa nyingi za kutosha kuhusu uendelezaji wa eneo haya ili liweze kuendana na ukuaji na upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika suala hili la kuendeleza eneo la Kurasini tumekuwa tukishirikiana na uongozi wa Mkoa, uongozi wa Wilaya na tumefanya matukio mbalimbali ikiwa ni pamoja na miradi kuitambulisha kwa viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam ilikuwa tarehe 11 Julai, 2006, Mradi kuutambulisha kwa viongozi wa Wilaya na Manispaa ilikuwa 12 Julai, 2006, Mradi kuutambulisha kwa viongozi wa Kata za Kurasini, Mtoni na Mitaa ya Kata hiyo ambayo ndipo eneo la mradi ilifanyika tarehe 14 Julai, 2006 na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuthibitisha kwenye Bunge lako ni kwamba wale wote watakaoathirika na mradi huo lazima patakuwepo na *compensation* na *compensation* hiyo nzuri na hili ndiyo lengo kubwa la kuendeleza eneo la Kurasini. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanaohusika na maeneo hayo wasiwe na wasiwasi waweze kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha kwamba haki zinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumziwa ni katika suala la Mabaraza ya Ardhi na Mabaraza mbalimbali. Kwa mujibu wa Sheria Namba 2 ya mwaka 2002 kuna Mabaraza yanayoshughulikia ardhi ambayo yapo aina nne, kuna Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, kuna Mabaraza ya Ardhi ya Kata haya yapo chini ya TAMISEMI. Ningependa kutoa wito kwenye Serikali za Vijiji ambazo hazijaunda Mabaraza haya basi zifanye hivyo katika kuhakikisha kwamba Mabaraza haya yapo hapo kwa mujibu wa Sheria katika kupunguza matatizo ya wananchi. Lakini pia kuna Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya ambayo kama nilivyoeleza yapo 23 katika mikoa yetu mbalimbali lakini katika bajeti ya mwaka huu tumepanga kuongeza mengine saba ili tuweze kushughulikia kero mbalimbali zinazohusu wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako baadhi ya Wabunge wamezungumzia kuhusu suala la kubadilisha matumizi ya ardhi. Ni kweli wapo baadhi ya Wabunge wamezungumzia kuhusu suala la kubadilisha matumizi ya ardhi, ni kweli kuna maombi ambayo yameletwa Wizarani watu wakiomba kubadilisha matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi haya yote tunayafanyia kazi katika Wizara na tunayafanyia hivyo kwa sababu pamekuwa na udanganyifu mwingine mkubwa sana unaoletwa pale, unakuta unaletwa mabadiliko ya ardhi kumbe ile ardhi ni *open space*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mtu anaomba kule mabadiliko ya ardhi kwenye makazi kumbe anataka kujenga *Petrol Station*. Kwa hiyo, tumeamua maombi yote tuyafanyie kazi ikiwa ni pamoja kutuma Maofisa wa Wizara katika maeneo yale. Ili tutakapokuja kumshauri Mheshimiwa Rais katika kutoa mabadiliko yale yawe kweli yamezingatia haki na sheria tulizoziweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona katika Miji yetu kwa mfano, kwa sasa hivi *Petrol Station* zinajengwa nyingi sana, lakini kwa mujibu wa sheria inasema Kituo kimoja cha mafuta hadi Kituo kingine kinatakiwa kiwe kwenye umbali wa kilometa mbili au kilometa tatu. Lakini ni tofauti kabisa katika hali halisi katika Miji yetu unakuta mita moja, mita mbili kuna *Petrol Station* na hili ni tatizo kubwa. Kwa sababu tunatengeneza mabomu ya baadaye katika Miji yetu. Kwa hiyo, Wizara imeamua isitoe mabadiliko ya matumizi ya ardhi mpaka pale itakapojiridhisha na kuona kwamba mabadiliko hayo yamezingatia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo limezungumzwa sana linalohusu viwanja ambavyo havijaendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iko pale kwa kuzingatia sheria na kwa bahati nzuri katika mwaka 1995 palianzishwa Sera ya Ardhi na ilifanyiwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa muda huu ningependa nimpongeza sana Mheshimiwa aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wakati huo

Mheshimiwa Edward Lowassa, ambaye kwa sasa hivi ni Waziri Mkuu kwa jinsi alivyoisimamia hii Sera. Ni nchi chache duniani zenye Sera ya Ardhi, Tanzania ni mojawapo yenye Sera za Ardhi . Lakini katika mwaka 2000 palianzishwa Sera ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Gideon Cheyo, kwa kusimamia hii Sera ya Makazi ambayo ndiyo sasa inatoa mwelekeo mkubwa na kwa sasa Mheshimiwa Gideon Cheyo ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi na ambaye ndiyo mojawapo wa watu wanaotoa ushauri katika Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza haya kwa sababu tuna jukumu kubwa la kutetea na kulinda sheria zetu. Katika sheria hizo ndipo pale palipowezesha kuanzishwa Sheria namba nne ya Ardhi mwaka 1999, pakaanzishwa Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba tano ya mwaka 1999, ikaanzishwa Sheria namba mbili ya mwaka 2002 na kwa sasa katika kikao cha Bunge cha mwezi Oktoba, 2006 tutaleta Sheria nyingine inayohusu makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la makazi linahitaji kuchukuliwa kwa nguvu kubwa na hii ni kwa sababu ardhi tuliyokuwa nayo bado ni ile ile, lakini watu wamekuwa wakiongezeka wakati ardhi haiongezeki, na ndiyo maana ardhi ni lazima izingatiwe kwa kuwa na matumizi makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, katika suala la Tegeta, viwanja tunavyovizungumzia vya Tegeta, Mbezi na Boko, viwanja vile vilitolewa kwenye miaka ya 1980, tulichofanya mwaka huu tumepiga picha katika maeneo yale kwa ndege ili tuangalie ni maeneo gani yamekwishaendelezwa. Baada ya matokeo ya zile picha tumekuta kuna viwanja vingi sana havijaendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo orodha hapa ya viwanja ambavyo ni zaidi ya 1,088 ambavyo havijaendelezwa, ni mapori. Ninaposema havijaendelezwa maana yake hata nyumba ya nyuma haijajengwa, hata *fence* haijajengwa, hata choo hakijajengwa. Kwa hiyo, ni eneo ambalo ni poro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia viwanja hivi vimetolewa mwaka 1980 na katika hati walizopewa ilikuwa katika miezi 36 waviendeleze hivyo viwanja. Miezi 36 ikapita, wakaongezewa miezi 36 mingine hawakuviendeleza hata kwa kupeleka tofali tu, wakaongezewa miezi 32 mingine, kwa sababu ukijumlisha kuanzia mwaka 1980 mpaka leo mwaka 2006 ni zaidi ya miaka ishirini na kitu. Viwanja hivi matatizo yake sasa hivi imetokea nini, pametokea matapeli ndiyo vimeleteleza mambo ya *double allocation*. Kiwanja kimoja kinakuwa na watu watano na imeleta vurugu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niwathibitishie kwamba viwanja hivi si vya watu wadogo. Katika orodha niliyonayo na watu ambao wameandikiwa hati ya kuyang'anywa mmojawapo ni Naibu Waziri wangu. Nataka nieleze ukweli kwa sababu

msema kweli ni mpenzi wa Mungu. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba wananchi wengi wa maeneo ya Dar es Salaam ambao kwa asilimia 75 wanaishi kwenye makazi holela yasiyopimwa wakati kuna viwanja zaidi ya 1,000 na kitu watu waliopewa tangu mwaka 1980 hajajenga hata choo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 1980 ikapita miaka kumi, ikaja mwaka 1990, ikaja mwaka 2000, ikaja mwaka 2006 havijaendelezwa chochote, lakini tumekuta viwanja vingine ni vya matapeli. Anaandika pale jina la mtu wakati yule mtu hana hata hiyo habari kwamba hicho ni kiwanja chake. Kuna majina ya watu wengi tu wameandikishwa hivyo viwanja, lakini ni utapeli uliokuwa unafanywa ndani ya Halmashauri zetu pamoja na Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilifikiri mimi hili tungesifiwa sisi Wizara kwamba tumeanza kuchukua hatua. Wale watu hatujawanyang'anya, tulichofanya tumewaandikia *notice* na *notice* ile ni siku 90 kwamba katika orodha yetu jina hili linaonekana ni kiwanja chako, tunaomba utujibu kama ni chako ama kama sio chako na baadaye hatua zinafuata. Lakini katika hiyo ambayo tumewapa siku 90 waweze kujibu, yapo matatizo mengi ya msingi. Wapo wengine walifungwa, sasa kama alifungwa angeweza kujenga nyumba wakati amefungwa kule, ataeleza kwamba nilifungwa katika Mahakama fulani.

Kwa hiyo, naomba niongezewe siku zingine za kujenga, tutasikiliza. Vipo viwanja vingine vina migogoro vimekuwa na kesi Mahakamani na maamuzi yale hajamalizika, pale tutasema hapa palikuwa na kesi, tunasubiri. Huo ndiyo utaratibu wa sheria na Utawala Bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni chimbuko la matatizo mengi. Kwa mfano, kiwanja ambacho kimezungumzwa cha Mheshimiwa Rita Mlaki, amekuja akaniambia yeye hana kiwanja katika sehemu hiyo. Kwa hiyo, kuna watu waliandika wakasema ni kiwanja chake. Sasa utapeli wa namna hiyo inawezekana umefanyika hata kwa Mheshimiwa Gideon Cheyo au kwa nani? Sasa kwa nini msitupe nafasi ya kuchambua haya ili kusudi tuweze kutatua matatizo vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nilizungumze hili kwa sababu limezungumzwa kwa uchungu mkubwa. Lakini ninachotaka kueleza hili hatulifanyi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pekee yake, tunalifanya kwa ushirikiano mkubwa na Halmashauri husika. Kwa mfano, tarehe 21 Julai, 2006 tulifanya kikao na watu wa Manispaa katika Wilaya zote za Jiji la Dar es Salaam na walihusika wakiwemo Ma-DC na kadhalika na kadhalika. Tunajaribu kuchambua na kuangalia tatizo liko wapi ili kusudi masuala ya utapeli katika ardhi yaishe. Tunataka siku moja mtu anapotafuta ardhi anabonyeza kwenye *computer* anataka ardhi hii anapewa na hicho ndicho tunachokitaka kukifanya katika nchi nzima. Zoezi hili ni lazima tulizingatie kwa sababu tuko hapa kwa ajili ya kutekeleza sheria, na sheria ina kikomo chake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nashangaa wale watakaoniambia kwamba tuache hivi, tuache hivi, wakati mimi nimeapa kulinda sheria, Naibu Waziri wangu ameapa kulinda sheria, Waheshimiwa Wabunge tumeapa kulinda sheria na migogoro ya ardhi ni mingi.

Tuko watu milioni 35, kwa hiyo, aidha, huyo mtu ana mgogoro na mke wangu ndani ya nyumba anayoishi au ana mgogoro na nyumba ya jirani, ana mgogoro na shamba alilionalo au ana migogoro ya mpaka.

Kwa hiyo, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi sijawahi kuona Wizara ya namna hii kila siku ni migogoro tu, migogoro tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya kwanza nimefika ofisini nimekumbana na barua zaidi ya 100 zote ni za migogoro na watu wamejaa pale wanasubiri kutatuliwa migogoro. Kwa hiyo, mimi ningeeomba Waheshimiwa Wabunge mtuhurumie, lakini mtupe nguvu katika kutatua hii migogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameshaunda Tume katika Wilaya zote za kuchambua migogoro. Mimi na Naibu Waziri na Wizara tumeshawaandikia Wakuu wa Wilaya wote wawe Wenyevitikuchambua migogoro, bado kuna Mahakama za Ardhi za Kata, za Vijiji, za Wilaya na kwenye *High Court*, yote ni migogoro ya ardhi na Mheshimiwa Gideon Cheyo ana *experience* ya migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa migogoro hii yote msipotupa nafasi ya kufanya kazi ambayo ni ya kujituma na kumtegemea Mungu zaidi tutashindwa kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika migogoro hii kuna matapeli wengi. Viwanja hivi huwezi ukasema ni kiwanja cha nani, kwa sababu mtu anapokuwa na viwanja 20 anabadilisha majina, atajiita jina hili, atajiita jina hili na anaweza akataja hata jina la Mheshimiwa Mbunge. Sasa tunachofanya sisi ni kuchambua kwa kuandikia zile *address* walizozitumia katika hati zao za kuomba viwanja. Tunawaandikia na kuwapa *notice* ya siku 90 aeleze kama ni kiwanja chake, kwa nini hajakiendeleza hicho kiwanja, ndicho tunachofanya na baadaye maelezo yasiporidhisha, tutapeleka kwa mujibu wa Sheria kwa Mheshimiwa Rais afute hati, ili kusudi tuwape watu wengine na tunaowapa sio matajiri.

Kwa hiyo, kama kuna Waheshimiwa Wabunge wana watu watahitaji viwanja hivyo, waandike orodha wanilettee hapa kwamba wangependa katika Wilaya zao hawa watu wapewe viwanja. Tusizuiwe kutekeleza Sheria. Bunge lituruhusu kutekeleza Sheria ili kusudi migogoro ya ardhi tuipunguze jamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro hii ipo mingine ni ya miaka arobaini na kitu kabla hata mimi sijazaliwa, nimekuta migogoro hii ipo kwenye Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeliomba Bunge migogoro ya ardhi ni mingi. Tupewe nafasi tuishughulikie. Wale matapeli wa kuuza viwanja ambao wao wamekaa *standby* kwa ajili ya kuuza viwanja vya Mbezi kwa shilingi milioni 200 wakose

hiyo nafasi. Viwanja viwe vinatolewa kwa hatua ambayo tumeanza kuichukua kwenye viwanja 20,000. Watu wanaomba viwanja wanapata na kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamenionba hapa viwanja wameishapata. Hata Waandishi wa Habari wameomba viwanja wamepata. Huu ndiyo ukweli tunataka twende na kasi hiyo na ndicho anachotaka Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini matatizo mengi ya ardhi hayawezi yakabebeshwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pekee yake, kuna Maofisa Ardhi ambao mnakaa nao huko kwenye Wilaya zenu ni matatizo na ninaongea hivi kusudi na wao wanisikie huko katika Wilaya zao wamekuwa ni kero sasa, kwa sababu ni kero sisi sote tuna jukumu la kushirikiana kuwatambua hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningewaomba Waheshimiwa Wabunge, najua mnaishi na Maofisa Ardhi huko ambao wengine ni matatizo sana. Nileteeni majina yao na matatizo yao ili kusudi tushirikiane na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tuwashughulikie hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuja Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alisema ikiwezekana tufukuze hata watumishi 1,000 na mimi kufukuza watumishi wala siogopi. Nilipokuwa Waziri wa Ujenzi wakati huo tulifukuza Wakandarasi 1700, tulifukuza Ma-engineer 221, tulifukuza ma-architect zaidi 75, pamoja na watu wengine hawapendi kufukuza. Lakini kuna umuhimu wa kufanya hivyo kama tunataka kujenga nidhamu ya utendaji kazi katika nchi yetu. Tusipofanya hivyo kila siku kilio kitaendelea katika nchi yetu. Watu watadhulumiwa, migogoro itaendelea na kila siku itakuwa ni migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wafugaji na wakulima na ndiyo maana tumeamua sasa hivi tupime hivi vijiji. Kwa sababu vijiji vingi vilivyokuwa havina wafugaji na nini ndiyo vyenye migogoro. Tukishapima mambo yataenda vizuri. Lakini kuna hatua nzuri ambazo zimechukuliwa. Katika bajeti ya mwaka huu zimetengwa shilingi bilioni mbili, za kuangalia maeneo mazuri watakayohamishiwa wafugaji. Maelezo yametolewa vizuri na viongozi wetu na juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu ameunda Tume ya Naibu Mawaziri watano wameenda mpaka kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningepomba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mwanzo ni mgumu mtupe nafasi Serikali hii iweze kutimiza malengo yake katika kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala limezungumzwa la *National Housing*. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri amelifafanua vizuri. *National Housing* ni Shirika lililoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba mbili ya mwaka 1990 ipo sheria na wala sio *Tanzania Building Agency* ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 30 ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *National Housing* inajiendesha yenyewe kibiashara, haipati ruzuku hata senti tano kutoka Serikalini. *National Housing* katika kipindi cha kuanzia tangu mwaka jana ilikuwa inadai zaidi ya bilioni 11 ambapo wapangaji wake waliokuwa wanakaa kwenye nyumba walikuwa wamekataa kulipa, wapo waliokuwa wamekataa kulipa kwa zaidi ya miaka kumi, wakitupeleka Mahakamani wale wa Moshi. Kodi ya pango ya *National Housing* ni kidogo ukilinganisha na *market value*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Shirika linalojiendesha kibiashara, Shirika tulilolianzisha kwa mujibu wa Sheria za Bunge, hii sheria namba mbili ya mwaka 1990 limekuwa likijitahidi kufanya kazi kubwa na ndiyo maana mwaka jana palibadilishwa sheria ya wapangaji badala ya mpangaji kuwa mfalme, mpangaji naye anajua namna ya kulipa.

Ile sheria namba 11 ya mwaka 2005 ikafanyiwa *amendment* na ile sheria inasema mtu usipolipa anatafutwa dalali, wanashika hata mali zao wanakutoa nje, baada ya kupewa *notice* ya siku 30. Hiyo ndiyo sheria tuliyopitisha katika Bunge hili. Kama tunaona haifai tui-*amend*. Lakini hiyo ndiyo sheria inayosaidia *National Housing* kufanyakazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitisha hiyo sheria, *National Housing* sasa hivi ilikuwa ikusanye shilingi bilioni 10 mwaka huu, lakini imekusanya bilioni 19 na inaendelea kukusanya na ndiyo maana imepanga kujenga nyumba nyingine 338 katika nchi nzima. Ni kwa sababu ya hiyo kazi inayofanywa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *National Housing* imeanza sasa kuingia ubia inataka kubadilisha Miji yetu. Kwa Dar es Salaam zaidi ya majengo kumi yanajengwa yenye ghorofa kumi, kumi. Tumeamua waingie ubia kujenga majengo na majengo mengine *actually* yatafunguliwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 15 Agosti, 2006. Jengo moja litakuwa la ghorofa kumi, lingine litakuwa la ghorofa 12 ni kwa sababu ya kazi nzuri zinazofanywa na *National Housing*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tutajenga majengo mengine zaidi 27 ambayo yatagharimu zaidi bilioni 37 katika njia hii ya uwekezaji na ubia. Lakini *National Housing* imeamua pia kujenga nyumba ambazo zitakuwa zinatumiwa kuwauzia watu. *National Housing* sasa hivi iko kwenye majadiliano na Shirika moja la Marekani la *OPIC* ambalo linataka kujenga zaidi ya nyumba 10,000 hapa na ni kwa sababu wameiona *National Housing* ni mahali pazuri pa kuwekeza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge pamoja na matatizo madogo madogo yanayojitokeza ya hatua mbalimbali ambazo zinawagusa wengine ndugu zetu tuziache sheria zifanye kazi ili Miji yetu isiwe sasa ikawa na makazi holela ya asilimia 75 bali iwe na makazi ya kudumu na mazuri yanayopendeza yenye nyumba za ghorofa nzuri nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yaliyozungumzwa ni mengi sana ili kusudi nisimalize muda. Naomba nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe ambaye amezungumza kwa niaba ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, ameipongeza Wizara na ametoa ufafanuzi mwingi ambao tunatakiwa kuufanyia kazi na kuufuata sisi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme naipongeza sana Kamati ya Kilimo na Ardhi, wameifanya kazi nzuri sana. Ushauri wao wote naupenda sana na huyu aliyeniletea maji ninamshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Kamati ya Kilimo na Ardhi ni mzuri sana na mimi nataka kumthibitishia Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe na Kamati yote kwamba ushauri wao tutauzingatia na tutakapokutana katika bajeti nyingine tutatoa maendeleo ya jinsi ushauri utakavyokuwa umetusaidia hapa. Kwa hiyo, nawashukuru sana, wamezungumza mambo mengi, lakini kutokana na hali halisi ya muda siwezi nikayazungumza mengi. Lakini ushauri wao nimeupokea kwa asilimia mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Cheyo ambaye ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani amezungumza mambo mengi, ametoa takwimu nyingi na amesema anapongeza kwa kupata fedha kibao katika Wilaya yake katika sherehe nafikiri ya Nanenane. Lakini kwa jinsi mimi nilivyokuwa ninajua katika taarifa ambayo nimepewa na Mheshimiwa Andrew Chenge na mimi ninawapongeza sana wananchi wa Bariadi kwa kumchagua Mheshimiwa Andrew Chenge kuwa Mbunge wao. Mheshimiwa Andrew Chenge amefanya kazi nzuri sana. Kwa sababu katika masuala ya ardhi ni utekelezaji wa Sera za CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi kila mahali ninapotafuta utekelezaji wa Sera za CCM ninamtafuta Mheshimiwa Andrew Chenge ambaye pia ni Mwanasheria ambaye anazifahamu vizuri Sera za CCM. Lakini pia ninampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, pamoja na kwamba hayuko hapa, katika kipindi chake aliweza kutetea sana na kuiwezesha Wilaya ya Bariadi kupimiwa viwanja vijiji 140 na hii ni katika kutekeleza Sera za CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Cheyo amezungumzia kwamba ukitaka hata eka 20,000 unazipata, huo sio utaratibu. Ardhi kwa sasa hivi ina thamani kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika matatizo tunayoyapata sasa hivi katika ardhi ni kwamba kuna mikataba ya *forgery* ya kuwarubuni wanavijiji na Wenyeviti wa Vijiji na zinaletwa hati Wizarani kwa ajili ya kusainiwa. Ni juzi tu kwa mfano, palikuwa na ardhi ilikuwa inaombwa zaidi ya eka 500 katika Wilaya ya Bukoba Vijijini. Nilipompigia simu Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera akasema hiyo ardhi katika Wilaya ya Bukoba Vijijini itatoka wapi? Lakini ukiangalia *document* zote zipo, hati ya kusainiwa na Mwenyekiti wa Kijiji na kadhalika. Kwa hiyo, katika hili suala tusipoangalia, suala hili la kumilikisha ardhi ekari 20,000 zinatolewa, ekari 100,000 zitatolewa, tutakuwa na migogoro iliyozikumba nchi nyingine ikiwemo Zimbabwe. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ni lazima tuzingatie Sheria ya Ardhi Namba nne ya mwaka 1999, Sheria ya Ardhi Namba tano ya mwaka 1999, lakini ni lazima pia tuzingatie kwamba Sheria hairuhusu kummilikisha mtu ambaye si raia wa Tanzania na hii ndiyo Sera ya Ardhi ya mwaka 1995. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine Mheshimiwa John Cheyo ninampongeza kwa sababu alikuwa anarudia rudia yale ambayo yako kwenye Sera ya Ardhi ya mwaka 1995 na ya mwaka 2000 na huo ndiyo wajibu wa kukumbushana. Sikuweza kuyaandika haya yote na kwa hiyo, na yeye amepata nafasi akayaandika yale ambayo ningeweza nikayaandika, nampongeza Mheshimiwa John Cheyo na hasa kwa sababu haya yamefafanuliwa vizuri katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Cheyo, amezungumzia kuhusu nyumba zilizouzwa za Serikali. Nisingependa sana kutoa ufafanuzi wa hili kwa sababu nyumba za Serikali zilizouzwa, ziliuzwa katika Wizara ambayo si Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na wakati zikiuzwa zilizingatia wazi Sheria Namba 30 ya mwaka 1997, ilipitishwa kwenye Bajeti ya mwaka 2002. Mheshimiwa John Cheyo anafahamu, ilipitishwa kwenye Bajeti ya mwaka 2003/2004, ilipitishwa kwenye Bajeti mwaka 2004/2005, ilipitishwa kwenye bajeti ya 2005/2006 na sasa imepitishwa kwenye Wizara ya Miundombinu kwenye bajeti ya 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Cheyo hakusema huko ananisubiri tu mimi niko kwenye Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ndiyo aanze kuzungumza. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inahusika na nyumba za *National Housing* sio nyumba za Serikali. Lakini Mheshimiwa John Cheyo alitakiwa pia azungumzie kwenye hotuba yake nzuri na ndefu yenye *data* za kuchanganya kwamba Serikali kupitia hiyo Sheria Namba 30 ya mwaka 1997 Serikali imekwishajenga nyumba zaidi 1,500 na mojawapo ni hizi nyumba anazozipita akitoka Dar es Salaam ambazo ziko Dodoma na ambazo zaidi ya nyumba 150 zitatumika kama Nyumba za Chuo Kikuu cha hapa Dodoma. Hayo Mheshimiwa John Cheyo hakuyasema anapita pale kwenye barabara kila siku anaangalia mkono wa kushoto hakulielezea Bunge. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemwomba Mheshimiwa John Cheyo, a-*concentrate* na yale yanayohusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, yale mengine asubiri bajeti itakayokuja atazungumza hayo anayotaka kuyazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa ujumla Mheshimiwa John Cheyo, nampongeza yale mengine yote aliyozungumza kwa sababu amezungumza yaliyo kwenye Sera ya Ardhi ya mwaka 1995, kwenye Sera ya Makazi ya mwaka 2000 na Sheria mbalimbali zinazohusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, nampongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally amezungumza mengi, ametoa mfano wa *document* ambazo ametupa hapa, ninamshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally kwa sababu ametupa *information* ambazo zitatusaidia kufanya kazi, tutazifanyia kazi. Lakini kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri tulipofanya uchunguzi wa haraka haraka hasa katika nyumba ambayo ameitaja nyumba namba 405, tumekuta hii nyumba ilikuwa ya ndugu Hamid Amiri katika mwaka wa 1999 na alikuwa amemilikishwa kwa miaka ya 1966, hii nyumba baadaye ilienda kwa ndugu Balitazari Njileti kwenye miaka ya 1974, baadaye hiyo nyumba ikaenda kwa *State Motors Corporation* kwenye mwaka 1978 na *State Motors Corporation* walishaiuza hiyo nyumba kwa Zainabu Yussuf Ali na Hussein Ali tarehe 10 Agosti, 2005. Kwa hiyo siwezi nikatoa ufumbuzi wa tatizo hili ambalo katika *document* tulizofuata Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi zinaelezea hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama kuna tatizo na inawezekana likawa ni tatizo la kisheria ningependa nimshauri dada yangu Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, kwamba awashauri wahusika waende Mahakamani. Kuna Mahakama za Ardhi ya Vijiji, kuna Mahakama za Kata, kuna Mahakama za Wilaya, kuna Mahakama Kuu, ili suala hili likatafutiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally napenda nimshauri kwa wale wapangaji ambao wamenunua nyumba za *National Housing*, Tabora na bado hawajapata hati, hili lazima nilitolee maamuzi. Kwa sababu wanaotoa hati ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, *National Housing* iko katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, sasa itakuwa ni ajabu nyumba zilizokuwa ni za *National Housing* zilizouzwa kwa wananchi, halafu zikashindwa kutolewa hati kwenye Wizara hii hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally na Waheshimiwa Wabunge, natoa amri sasa kwa sababu mimi ndiyo msimamizi wa Wizara hii, ziandaliwe hati za nyumba zote walizonunua wananchi *National Housing* ambao wamemaliza kulipa na hasa zile ambazo hazina migogoro ya Kimahakama. Wataalam wangu ambao bahati nzuri wananisikia hapa mkashughulikie hilo katika kipindi cha mwezi mmoja. Nina uhakika baada ya kusema hili Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, atanisamehe asitoe shilingi twende tukafanye kazi. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, amezungumza mambo mengi na ushauri mwingi, nampongeza sana Mheshimiwa Ponsiano Nyami na ninampongeza kwa Wilaya yake kwa kulipa lile deni ambalo Wilaya nyingi zimeshindwa kulipa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ponsiano Nyami pia amesema ardhi ni uhai, viumbe vyote wanategemea ardhi. Ugawaji wa ardhi ni vyema ukazingatia maeneo ya watu pia wanaokaa pale, Wizara hii ilikuwa imeoza, wananchi wengi wananiunga mkono. Maneno yale yalinifurahisha sana, ukiungwa mkono na mtu ambaye ni Mfipa, unakuwa na matumaini makubwa. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ponsiano Nyami ninamshukuru sana. Nataka kumhakikishia kwamba tutafanya kazi ndani ya kutuunga mkono katika hili. Lakini ninachotaka kusema ushauri wake mkubwa ameutoa. Wafipa ni watani wangu, kwa hiyo wanafahamu kule Rukwa kwamba wanazungumza na ndugu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingi wa Mheshimiwa Ponsiano Nyami ulikuwa mzuri sana, tumeuzingatia. Lakini kuhusu suala la mipaka ya Wilaya, baada ya Bunge hili kumaliza shughuli zake, tutawaandikia barua Wakuu wa Mikoa wote na Wakuu wa Wilaya wote kuhusu *Government Notice* ambazo zinaonyesha mipaka yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba hili na nakala tutampa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais ili kusudi Wakuu wa Wilaya wanapohama kwenda Wilaya nyingine anayekuja kukabidhiwa basi hii iwe moja ya *document* ya kukabidhi katika makabidhiano yao. Wakuu wa Wilaya wazipitie hizi *Government Notice* ambazo zimepitishwa ambazo ni za siku nyingi kustadi maeneo ya Wilaya zao na mipaka yao ili pasiendele kuwepo na migogoro kati ya Wilaya na Wilaya, kati ya Kijiji na Kijiji. Kwa hiyo, hili tutalifanya na tumekwishaanza kuziandaa ili kusudi migogoro hii ya ardhi katika Wilaya na Wilaya zianze kupungua na kama sio kuondoka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametoa pia ushauri kuhusu hatimiliki. Ametoa pia watumishi wanaohusika na ardhi ndiyo wabaya lakini ameniambia pia nyoka mwenye sumu yuko kwangu. Ukitaka kuua kichwa, kichwa kiko kwangu pale Wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakushukuru ndugu yangu Mheshimiwa Ponsiano Nyami, tutaendelea kufuatilia vichwa vilivyopo Wizara ya Ardhi, tutatumia viongozi na mamlaka yaliyopo kuvigonga vile vichwa ili Wizara ya Ardhi pawe mahali patakatifu. Ni mambo mengi yamezungumzwa lakini kwa ujumla tu niseme Mheshimiwa Ponsiano Nyami, ninakushukuru sana kwa michango yako mizuri uliyoitoa.

Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, amezungumzia juu ya rasilimali ya ardhi amezungumzia yanayotokea Mbarali ni changamoto kwa sasa watu wanaoelewa, amezungumzia viwanja 20,000 amezungumzia mashamba ya Magereza kwamba kwa nini yasiendelezwe. Kwa nini tusichukue sheria ambazo tunazitumia kwa viwanja ambavyo haviendelezwi. Nataka kukuthibitishia Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, sheria ni msumeno tutaanza kuzingatia yale yote yanayohusu sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, amezungumzia kuhusu viwanja nimeshalifafanua vizuri na ningemwomba ndugu yangu Mtemvu tuachie tufanye kazi na bahati nzuri nilikuja Temeke hata wakati wa kampeni na watu walifurahia sana, bado ninakumbuka. Kwa hiyo, tuache tufanye kazi kwa kuzingatia sheria na wananchi wa Temeke watafaidika na hili. Kama kuna tatizo la viwanja basi wewe tueleze ni wananchi wangapi wa Temeke wanahitaji viwanja katika maeneo ya Temeke na sisi tutawapa *consideration* ya kwanza kabla ya wengine.

Mheshimiwa Damas Nakei, naye amezungumzia kuhusu migogoro mingi katika maeneo yake na kuna migogoro katika shamba la sehemu ya Babati. Ninachotaka tu kusema haya yote tumeyazingatia na tutafuata ushauri lakini tutaona ni namna gani tutaweza kuyatatua. *Engineer Stella Manyanya*, amezungumzia kuhusu maeneo kwa mfano yatengwe kwa ajili ya miundo misingi kama kujenga *transformer* na kadhalika. Hili tumekuwa tukilizingatia sana katika mradi wetu tunaajenga wa viwanja 20,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, amezungumzia ahadi ya Mheshimiwa Rais katika kupanga mji wa Kibaha. Nataka kumthibitishia Mheshimiwa Gama kwamba ahadi ya Rais ni ahadi ya Rais sisi ni lazima tuitekeleze. Kwa hiyo, mji wako ni lazima upangwe katika mpango wa kisasa. Lakini katika tatizo la eneo la Mailimoja kwamba wapo kwenye *Road Reserve*. Sheria ya *Road Reserve* ambayo ni Sheria Na. 167 ya mwaka 1967 ambayo ilikuwa *gazetted* mwezi Mei, 1967 lakini ambayo sheria hii imeanza kutumika tangu mwaka 1938 inaelezea wazi kuhusu maeneo ya *Road Reserve* ukianzia Dar es Salaam. Kutoka Dar es Salaam mpaka jengo lile la *TANESCO* ni mita 75 yaani futi 75 kila upande. Baada ya pale karibu kilometa 10 ni mita 300 kila upande, baada ya hapo mpaka kwenye daraja la Kibaha ni mita 400 kila upande. Baada ya daraja la Kibaha kuelekea mpaka Ruvu zinapungua zinakuwa futi 75. Kwenye daraja la Ruvu zinaongezeka zinakuwa futi 300. Baada ya hapo na nchi nyingine zote ni futi 75 kila upande hii ndiyo sheria ya *Road Reserve*. (*Makofi*)

Sasa mimi nilifikiri hili suala unaweza ukalipeleka vizuri kwa wenzetu wa Miundombinu wakajua ni namna gani mnaweza mkalijadili na kulitatua na mkaleta ushauri kama kuna kubadilisha sheria kwamba wananchi wa Kibaha barabara iwe mita mbili sisi hatuna tatizo, kama watasema sisi wanaongeza kusudi walipwe *compensation* sisi hakuna tatizo. Kwa sababu kitu kikubwa tunataka tulinde sheria za nchi hii ili nchi yetu ijengwe katika mazingira ya kisasa. Lakini kwa ujumla mji wa Kibaha tumeshautangaza katika mabadiliko ya kisasa na mimi nina uhakika mji wa Kibaha utakuwa wa kisasa kama unavyotaka wewe Mheshimiwa Dr. Zainab Gama na tutaendelea kushirikiana na wewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, amezungumzia kuhusu Wilaya mpya ya Mvomero, Wizara ya Ardhi kasi haipo kwa nini haijatoa *approve* kwa viwanja vilivyopimwa mwaka 2000 na kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Saddiq kama kuna viwanja ambavyo vimeshapimwa zimeshapitishwa kwenye Halmashauri yako na makubaliano ya Halmashauri yapo mimi niletee hiyo orodha tushughulikie pale Wizarani badala ya kutoa shilingi ukachelewesha na maendeleo ya sehemu nyingine. Lakini pia umesema Wilaya ya Mvomero ina wafanyakazi wa ardhi watatu tu. Hilo sio kazi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Wanaotakiwa kuajiri wafanyakazi wa Idara ya Ardhi kule Wilayani ni Halmashauri zenu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kaeni, pangeni bajeti mnataka Maofisa Ardhi wangapi ninyi aajirini sisi huku ruhusa. Lakini muajiri wale wenye *profession* watakaofanya kazi inayotakiwa. Watumishi wa Idara ya Ardhi walioko Wilayani wako chini ya TAMISEMI hawako chini

ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ndiyo maana siku nyingi nilikuwa nikipiga kelele wahamishiwe hata miezi sita tu Wizara ya Ardhi baada ya miezi sita tuwarudishe TAMISEMI wakakipate watarudi wachache ambao watakuwa wameshaji-*inform* vizuri. Lakini bahati nzuri hili tunalifanyia kazi na mwenzangu wa TAMISEMI na Mheshimiwa Waziri Mkuu tunalishughulikia ni namna gani nidhamu tunaweza kuwa tunachukua *direct* kwa hao wahusika ili kujenga nidhamu katika watumishi wa ardhi katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ritta Mlaki, amenisaidia kujibu hoja mbalimbali na mimi nampongeza sana. Kwa kweli tunashirikiana naye vizuri sana ni mpole hana matatizo tunafanya kazi kwa kushirikiana. Lakini pia nawapongeza sana Katibu Mkuu wangu Mama Salome Sijaona, anafanya kazi nzuri sana na ninawapongeza Makamishna, Kamishna wa Ardhi, Wakurugenzi wangu wote mnapoona migogoro hii na kazi zinazofanywa hiyo ni changamoto kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tutakubaliana kwamba majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa kweli yaliandaliwa. Kwa niaba yenu nimpongeze sana. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Kifungu 1001 – *Administration and General*... ..3,848,128,700/=

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, *vote 48, sub vote 1001*, kifungu kidogo 250100, Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo sana na Mshahara wa Waziri lakini nimeshika kifungu kwa sababu katika mchango wangu nilioutoa kwa maandishi nilielezea katika Wilaya yetu ya Namtumbo kuna vijiji ambavyo vinapakana na Mbuga ya Wanyama ambao wananchi katika vijiji hivyo wanalima mashamba yao ambayo yapo karibu na mbuga hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kipindi cha karibuni kuna baadhi ya Makampuni ya Uwindaji yalipewa vibali vya kuwinda vitalu na Makampuni hayo mipaka yake wameweka mpaka katika mashamba ya vijiji. (*Makofi*)

Hivyo nilikuwa naomba ufafanuzi kwa sababu niliomba Wizara iwasiliane na Wizara ya Maliasili na Utalii ili waweze kutuma Maofisa wao kuja kuona ni jinsi gani ya kuweza kuweka mipaka hiyo vizuri na kuviachia vijiji hivyo ardhi ya kutosha kwa kilimo

ambacho ndicho kinachowaletea tija na ili kukidhi mahitaji yao ya ardhi ya baadaye Serikali izingatie kwa kuwa familia za vijiji hivyo zinaongezeka kwani tunazaliana sana. Naomba ufafanuzi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Vita Kawawa swali lako halihusiani moja kwa moja na Wizara ya Ardhi labda tumsikie Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye ndiye anahusika na suala hilo. *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Kawawa kwamba tutatuma maofisa kama tulivyokubaliana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Na kwa kuwa vitalu hivi ni vipya naamni kabisa suala hilo litashughulikiwa. *(Makofi)*

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 48*, programu namba 10, *sub vote 1001* kifungu kidogo 250100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi pamoja na mambo mengine niligusia dhana nzima ya *mortgage financing*. Nchi yetu inarudi nyuma hasa katika kuendeleza ujenzi wa miji yetu kwa sababu hatuna *mortgage financing facility*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Mortgage financing facility* si lazima ianzishwe *institution* mpya kwa ajili hiyo. Ni suala tu la kufanya marekebisho katika sheria zetu za Ardhi na hasa jinsi ya kushughulikia mambo yanayohusiana na *registration* ya *mortgage* na jinsi gani kama *mortgager* amefanya makosa ya kutokulipa. Benki au *institution* iliyotoa ile *mortgage* inaweza ikashika *property* inayohusika na kujirudishia fedha zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amekuwa kimya kabisa juu ya suala hili. Naomba ufafanuzi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo kwa Mheshimiwa Siraju Kaboyonga kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilieleza kwamba waliochangia kwa maandishi ni watu 67. Nimezungumza hapa mpaka nimegongewa kengele ya mwisho. Kwa hiyo tatizo ni muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimeeleza wale wote waliochangia kwa maandishi tutawajibu, wale waliochangia kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango majibu tayari tumeshayatayarisha yapo hapa na kesho asubuhi watayapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia leo tutakaa na wataalamu wangu kila Mbunge aliyechangia kwa maandishi tutamjibu. Nilichoweza kujibu leo ni wale waliochangia kwa kuzungumza hapa nao sikumaliza vizuri.

Suala la *mortgage financing* lipo na linafanyiwa kazi na Serikali yetu. Nimesema kwamba Shirika la Nyumba sasa hivi National *Housing Corporation* linazungumza na Shirika moja la *OPIC* kutoka Marekani kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zaidi ya 10,000 katika nchi hii. Kitakachofanyika pale ni *mortgage financing*. Serikali kwa sasa hivi inashirikiana na Wizara ya Fedha na kuna *paper* waraka ambao umeshaandikwa unafanyiwa kazi. Katika kurekebisha baadhi ya sheria zetu kuwapa watu haki ya wale ambao wanakuja ku-*invest* hapa kwa mfano *foreclosure* na kadhalika. Hili nalo linafanyiwa kazi. (*Makofi*)

Lakini pia nimezungumzia pamekuwa na mabadiliko ya Sheria Na. 11 ya mwaka 2005 inayoruhusu mtu ambaye halipi kodi anaweza akatolewa kwenye nyumba. Ile ni sheria na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali. Kuna Sheria ya Ardhi, kuna Sera ya Ardhi ya mwaka 1995, kuna Sheria ya Makazi, lakini ninachotaka kukueleza ni kwamba suala la *mortgage financing* na hasa baada ya *Tanzania Housing Bank* kuondolewa linafanyiwa kazi na Serikali na watahusika watu ambao ni *Private Partners* ni *PPP* ndiyo itakayoendelezwa katika masuala ya ujenzi wa nyumba.

Kwa hiyo, nataka kukuthibitishia kwamba hili linafanyiwa kazi na Serikali katika kuhakikisha watu waanze kuwa wanapata mikopo katika kujenga nyumba za makazi katika nchi hii. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Simwoni Mheshimiwa Waziri Muhammed Seif Khatib, nilitaka atupe Kiswahili cha *mortgage finance*.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo au kuuliza swali, voti 48, programu ya 10, *sub vote* 1001, kifungu kidogo cha 250100, Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina matatizo ya Mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Ninachotaka ni ufafanuzi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dodoma una Wilaya sita na vijiji 465. Lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amelieleza Bunge lako Tukufu kwamba katika Mkoa wa Dodoma vijiji 50 ndivyo vitakavyopimwa. Sasa la kwanza napenda nielezwe vigezo vilivyotumika kupata vijiji 50? Halafu la pili, hivi vijiji vyote ambavyo vimepimwa katika Mkoa wa Dodoma hati pamoja na ramani ni lini vitaandaliwa? Ahsante.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa ndugu yangu Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kama ifuatavyo. Naye ametoa hoja yake kwa

maandishi na ni katika hizo hoja ambazo tungeweza kuzijibu kwa maandishi na tukampa *details* zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuamua kwamba katika Mkoa wa Dodoma tumepima hivyo vijiji vichache ni kwa sababu Mkoa wa Dodoma umeshapimiwa vijiji 464. Katika bajeti ya mwaka huu Mkoa wa Dodoma pia utahusika katika kupigwa picha za anga. Sasa mimi nilifikiri katika hii *resources* ndogo inayopatikana katika nchi hii basi ni vizuri na wengine ambao hawajawahi kuona hata kijiji kimoja kilichopimwa nao watafaidika kidogo. Kwa mfano, Mkoa wa Rukwa hakuna hata kijiji kimoja kilichopimwa pamoja na kwamba tunawasifu wao wakulima wazuri. Sasa wakulima hawa tutawaendelezaje kama vijiji vyao hatutawapimia. Tanga wana vijiji zaidi ya 700 na havijapimwa. Lakini katika nchi nzima kuna vijiji 14,000 na vijiji ambavyo vimeshapimwa ni 6,500 vikiwemo vijiji 464 katika Mkoa na vikiwemo hata vya Mpwapwa anakotoka Mheshimiwa George Lubeleje.

Sasa ningemwomba Mheshimiwa George Lubeleje, awaachie na wengine mwaka huu sio kila kitu ni wewe tu, kila mwaka. Tumepata bajeti ndogo basi tuitumie na kwingine. Kigoma wana vijiji 332 Kigoma hapajapimwa hata kijiji kimoja. Kwa hiyo, malalamiko mengine ni lazima tuyazingatie hapa katika kutekeleza na kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Kwa hiyo Mheshimiwa George Lubeleje na ndugu zangu wa Mpwapwa na Wagogo wote wavumilie katika hilo. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa George Lubeleje amekuelewa na sisi wa Kongwa pia tumekuelewa. (*Kicheko*)

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *Vote 48* Programu 10, kifungu kidogo 1001 kifungu kidogo zaidi 250100 napenda kupata ufafanuzi. Wanarikumbusha nitaje Mshahara wa Waziri. Mheshimiwa John Magufuli ni jirani yangu, hata kusimama, nilisimama kwa aibu kweli. Sikupenda kusimama kwa sababu amezungumza vizuri na alikuwa amejiandaa, nampongeza sana. Lakini kwenye hili kwa sababu nimetumwa na wapiga kura naye atanisamehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia nimepongeza hatua ya Mheshimiwa Rais ya kuunda Tume kila Wilaya ambazo zimefanya kazi nzuri sana kutatua migogoro mingine ambayo ilishakuwa sugu ikawa inasuluhishwa kwa muda mfupi. Halafu nikaomba kwamba kupitia kwako unaweza ukamfikishia Mheshimiwa Rais maombi awaongeze muda waendeleo kutatua migogoro hii kwa sababu muda umepita kazi yao nzuri, migogoro ni mingi hasa Wilaya ya Muleba hawajafanya kazi sawa sawa. Wenye migogoro wanasema hawajasikilizwa au kuligusia. Najua sio wewe unayepaswa kuongeza muda ni Mheshimiwa Rais, lakini hata kusema utalipeleka, hilo la kwanza.

La pili, nikazungumza kwamba Mabaraza ya Ardhi hasa kwenye sehemu zenye migogoro mingi kama Wilaya ya Muleba kwa sababu ya ufinyu wa maeneo mimi

kwenye jimbo langu ardhi ya kuwapatia vijana sina. Hilo halikuhusu, nitakuja kuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atutafutie eneo mimi nitatafuta mabasi twende mbali. Wilaya ya Muleba hakuna, Biharamulo hakuna, Geita hakuna, wao wanakuja kwetu kwa sababu ni nchi moja. Sasa nikasema hivi haya Mabaraza mtayafanya namna gani hasa haya ya kwetu huko Muleba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi nikasema hili tatizo la Kyamiyorwa watu wameshakufa wawili, watu wanapigana na mwekezaji nikasema Sera ya Serikali kugawa ardhi karibu na vijiji mtaitafakari na kuirekebisha kwa sababu nchi yetu ni kubwa hii, wawekezaji wapeleke mbali na vijiji kupima vijiji haitoshi. Unapima kijiji, unawaonyesha mpaka mnaishia hapa wanapakana na mtu binafsi migogoro haitakwisha. Pima wasogeze wawekezaji mbali nikasema hilo ni suala la kisera, haukusema. Lakini sasa nikasema ndiyo ukinjibu kwamba utakuja Kyamiyorwa ukasikiliza hawa watu wanaopigana kila siku wanauana na yenyewe itaniridhisha sawa sawa. Naomba ufafanuzi wewe ni jirani yangu Chato na Muleba Kusini sisi ni majirani kilometa kama saba sasa watu wanauana kwangu taja na Kyamiyorwa unakuja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba majibu.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Wilson Masilingi. Kwanza ningemwomba asishike huo Mshahara wa Waziri kwa sababu akiushika nitashindwa hata kupata nauli za kwenda Kyamiyorwa kusikiliza tatizo lake. Kwa hiyo, aniachie huo mshahara na apitishe hii bajeti. (*Makofi*)

Lakini suala la mgogoro wa Kyamiyorwa Wizara yangu inalifahamu, wahusika wameshaandika na wameshalalamika Wizarani kwangu na suala hili pia limeshafikishwa mpaka kwenye Ofisi ya Rais na Mheshimiwa Rais ameshatupa maelekezo ya kufanya. Suala hili pia mimi nimeshatuma Tume iliyoongozwa na Kamishna wa Ardhi kwenda kule kusikiliza matatizo ya Kyamiyorwa ambapo kuna mtu alikufa na wengine wakaumia kwa kupigwa risasi kwa sababu ya tatizo hilo hilo la ardhi.

Sasa ripoti ya Tume yangu nimeipata hivi karibuni tu bado nilikuwa najiandaa kwa ajili ya bajeti sijaipitia yote. Lakini pia nilisikia kwamba palikuwa na kesi kwenye Mabaraza ya Ardhi ya huko. Sasa sijui uamuzi ulitolewa kuhusu tatizo hili lakini ninachotaka kukuthibitishia Mheshimiwa Wilson Masilingi tutalifuatilia hili suala na kwamba unaomba lile Baraza lililoundwa na Mheshimiwa Rais liongezwe muda.

Mimi kwa kweli huo ni mzigo mzito kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu amekusikia nina uhakika anaweza akamnong'oneza Mheshimiwa Rais na watapanga na Mheshimiwa Rais ana vyombo vingi vya kuweza kujua kama panahitaji kuongezwa muda au lile Baraza lililoundwa kule Muleba ni wazembe tu wachukuliwe hatua na kadhalika. Kwa sababu kuna mambo mengine mengi inawezekana Baraza lililopo wale wahusika hawajui kutekeleza wajibu wao, kwa hiyo hawawezi waka-*affect* kuongezwa muda wakati Mabaraza mengine labda yameshamaliza kazi likawa tatizo liko Muleba tu.

Sasa ile ni Tume ya Rais siwezi nikamsemea na vyombo vipo ushauri utaupata vizuri. Lakini kuhusu matatizo ya Mabaraza ya Ardhi. Mabaraza ya Ardhi kwanza ni Mabaraza mapya, yako 23 tu katika nchi nzima. Ni vizuri tukawapa nafasi. Lakini ni kweli pia baadhi ya Mabaraza ya Ardhi yameanza kulalamikiwa hata kwa kupata rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Mwenyekiti wa Mabaraza ya Ardhi yuko hapa Mkurugenzi anayehusika awajulishe yale Mabaraza ambayo tumeshayaunda 23 wasijihusishe na rushwa. Nilisikia kwenye vyombo vya habari nafikiri Babati kwamba kuna mmoja ameshikwa na hela ya rushwa. Sasa tutayapitia upya Mabaraza haya. Kwa sababu Mabaraza haya mwenye Mamlaka ya kuyaunda ni Waziri nitapitia na niangalie CV zao wale ambao tutaona hawafai tutawatoa ili kusudi wasiwe chanzo cha migogoro katika Mabaraza ambayo tumeyaunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa nitoe wito pia kwamba Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na ya Kata ambayo yako chini ya TAMISEMI Serikali na Halmashauri zetu za Wilaya zifanye juu chini kuyaunda yale Mabaraza ili kupunguza migogoro ambayo mingine haitakiwi hata kwenda kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, suala la kwenda huko tutakaa mimi, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wangu baada ya kusoma ile ripoti na tutakuwa tunawasiliana na Mkuu wa Mkoa na bahati nzuri Mkuu wa Mkoa ni mchapakazi sana na DC na kadhalika na wewe tuone ni namna gani tunaweza tuka-solve hili tatizo la Kyamiyorwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Wilson Masilingi, jirani yangu naomba usinitolee mshahara wangu kwa sababu nitashindwa kutunza watoto wangu na wewe nina uhakika hutafurahi. *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa John Cheyo, sikujibu wewe naona unaamka hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na maelezo mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa John Magufuli kuhusu Mabaraza yale aliyounda Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jana vile vile au juzi katika maswali ya nyongeza nadhani Mbunge wa Pangani alieleza vile vile kwamba kuna tatizo na alikuwa anaomba utaratibu wa kuwezesha Baraza lile kuendelea na muda wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema hatuwezi kufanya uamuzi wa pamoja kwa sababu hatujui ni nini hasa kimetokea lakini tutayatazama *case by case* ili tuone ni nini na tuweze kumshauri Rais aweze kuongezea muda. *(Makofi)*

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *programu 10, sub vote 1101*, kifungu kidogo 250100. Mshahara wa mdogo wangu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kuna haja kufuatana na alivyokuwa anasema Mheshimiwa Waziri kufuata sheria na mojawapo ya sheria mama ni Katiba ya

Tanzania ambayo inatambua kuwepo kwa Kambi ya Upinzani na mchango wa Kambi ya Upinzani unajulikana na Rais mara nyingi ameweza kutambua pamoja na Waziri Mkuu. Maneno ambayo ameyasema Mheshimiwa Waziri yameonyesha chuki yake ya Kambi ya Upinzani. Lakini aliye tu, Kambi hii itaendelea kudumu. *(Makofi)*

Kwa kuwa mimi ni mtu mzima siwezi kukaa nikabishana naye na najijua uwezo wangu na watu wangu, wapigakura wangu uwezo wangu wanaujua na mambo ambayo tumewafanyia, kwa hiyo, sitabishana naye. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nataka kujikita kwa jambo moja ambalo nilikuwa nimelizungumza wakati nachangia, nalo ni kuhusu viwanja vya Dar es Salaam kama viwanja 300 kule *Mbezi Beach* na kwingine. Kwanza mimi kama mtu mzima namezea mengine yote ya kunidharau, lakini namsifu Waziri kwa kujibu vizuri leo si kama wakati anajibu kwa waandishi wa habari. Leo Waziri amewahakikishia wale watapata haki kufuatana na sheria. Hili kwangu limeniridhisha na natumaini wananchi wote walio na viwanja kule *Mbezi Beach* watapewa nafasi. Lakini ninachotaka kuuliza hapa, kama katika hizo nafasi na katika zama za sasa ambapo Serikali imeweza kuuza nyumba za Serikali, imeweza kuuza mashamba kwa nini hawa watu wasipewe nafasi ya kuweza kuuza vipande vya ardhi zao na fedha hizo wakazitumia kujenga nyumba kuliko kunyang'anywa kwa nguvu ya sheria. Ningependa ufafanuzi kwa hilo. *(Makofi)*

La pili Waziri amezungumza sana kupima vijiji, lakini ina maana gani kupima vijiji kama mwanakijiji mmoja mmoja hapimiwi ardhi yake na akapewa hati yake. Kwa sababu kupimiwa kijiji halafu na kijiji unakipa hati kusema kweli na wale wote mnaochangamkia kupimiwa vijiji mjue sheria hii ina maana unamny'ang'anya ardhi mwananchi. Hili ndilo jambo ambalo mnatakiwa kuwaeleza wananchi. Kwa hiyo, msichangamkie sana kupimiwa hati itatolewa kwa Baraza au kwa Halmashauri ya kijiji na wenyeji wote wale watakuwa na *subsidiary right of occupancy* ya kimila ambayo itawapatia matatizo sana katika kupata mikopo.

Kwa hiyo, ningependa hilo lisemwe na wananchi wahakikishiwe wazi kuwa sambamba na kupimiwa vijiji pia wananchi watapimiwa ardhi mmoja mmoja. *(Makofi)*

La mwisho nilipokuwa nazungumza juu ya nyumba zilizouzwa sikushangaa Waziri alivyozungumza na alivyojibu kwa sababu na yeye amenunua nyumba ya Serikali kwa bei ya chee. Kwa hiyo, nisingeshangaa alivyojibu hilo swali. Lakini hapa mimi ninataka kuuliza.....

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu, mengine nitauliza baadaye.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo kwa kifupi ya kaka yangu Mheshimiwa John Cheyo. *(Makofi)*

Kwanza nataka kumthibitishia Mheshimiwa John Cheyo kwamba mimi naheshimu Katiba ya nchi na natambua kuwepo kwa Kambi ya Upinzani na yeye ni

Waziri Kivuli na mimi Waziri Kamili na hata nilipokuwa nikijibu nilijibu nikijua huyu ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani tena bahati nzuri ni kaka yangu. *(Makofi/Kicheko)*

Katika suala la viwanja vya Dar es Salaam anasema leo amejibu vizuri ananipongeza kuliko siku nilipokuwa nikijibu na waandishi wa habari. Kwanza yeye si mwandishi wa habari na hakuwepo, kwa hiyo, hawezi akajua nilivyowajibu waandishi wa habari. Waandishi wa habari nilitoa maelezo mazuri na ndivyo walivyoandika. *(Makofi)*

Sasa leo wewe unasema sikuwajibu vizuri waandishi wa habari wakati nilipokuwa nikizungumza na waandishi wa habari hukuwepo na wewe si mwandishi wa habari. Kwa hiyo, majibu ya Serikali yamekuwa ni hivi hivi kama nilivyojibu leo, ni mazuri na yataendelea kuwa mazuri. Kwa hiyo, kama ameyapongeza majibu haya ni mazuri basi atoe nafasi Mheshimiwa John Cheyo, tutekeleze haya majibu mazuri kwa kufuata Sheria na kuzingatia Sheria zetu za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa John Cheyo, amezungumza wahusika hao ambao wataweza kunyang'anywa viwanja wapewe nafasi hicho ndicho tulichofanya tumewaandikia *notice* ya siku 90. Siku 90 ni miezi mitatu wajieleze kwamba mimi nilikuwa na kiwanja, lakini wakati wa kukiendeleza nilikwenda kwenye kampeni na nimeshinda, basi tutamsikiliza. Kama alikuwa kwenye kampeni ameshinda au mimi nilikuwa nimefungwa au kesi yangu ilikuwa mahakamani ama shauri langu liko Manispaa, tutamsikiliza. Wale watakaoshindwa kutoa maelezo katika hizo siku 90, tunafuta. Huu ndiyo mwelekeo wa sheria. Wamekaa na viwanja hivi tangu mwaka 1980. Leo ni mwaka 2006 zaidi ya miaka 25 mtu hajaendeleza popote, picha za anga ninazo hapa. Hakuna chochote ni pori na matapeli hata waliofukuzwa Wizara ya Ardhi kwa sababu wanavifahamu hivyo viwanja ndiyo wanafanyakazi ya utapeli kwa wananchi.

Mheshimiwa mwenyekiti, kuna *block* moja lina viwanja 740 havijaendelezwa. Sasa tunazungumzia kuhusu watu wengine wanakosa mahali pa kujenga wanajenga kwenye *unplanned area*. Kama Dar es Salaam zaidi ya asilimia 75 wakati wapo waliopewa miaka zaidi ya 20 hawajaviendeleza huu si utawala bora na hii si sera ya CCM. Tusubiri sera za wenzetu watakao shinda wawaachie watu wasiviendeleze viwanja hata kwa miaka 50 lakini si CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *notice* zile zinawatosha wajibu wenye matatizo, tutawasikiliza na tutazingatia, wenye kesi mahakamani tutawasikiliza, wenye migogoro ya ardhi tutawasikiliza ili kusudi tujenge utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupima vijiji kuna maana gani kama watu hawapimiwi viwanja? Sasa sifahamu kama Mheshimiwa John Cheyo amesoma vizuri ukurasa wa 70 jedwali namba sita. Ninaomba nimfafanulie, kazi za upimaji zilizoidhinishwa na kuletwa kutoka mikoa mbalimbali. Viwanja vilivyoletwa Wizara ya Ardhi kutoka Mikoa mbalimbali ni 21,710 vilipimwa na mashamba zaidi ya 631, vijiji 232. Kwa hiyo, katika kazi za kupima zipo zinazofanywa na watalaam wa Halmashauri

za Wilaya katika Wilaya mbalimbali na huwa zinaletwa Wizarani kuidhinishwa. Lakini zipo pia ambazo zinafanywa *direct* na Wizara ya Ardhi katika kupima vijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashagaa sana kuona mtu badala ya kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kuanza kupima vijiji vyake ili wananchi wale wapate hati, waweze kujua matumizi bora ya ardhi, wapi watalima, wapi watafuga na wapi watafanya shughuli nyingine, anasema kuna maana gani kupima vijiji? Sasa sifahamu lakini katika sera ya CCM inasisitiza hili, upimaji wa vijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi namshukuru kaka yangu Mheshimiwa John Cheyo, kwa michango yake mizuri aliyoitoa. Lakini ningemwomba kwenye hili asiendele kutoa shilingi atuache tuendelee kutekeleza yale ambayo tunatakiwa kuyatekeleza ikiwemo na kupima viwanja na vijiji katika Wilaya ya Bariadi na kama yako matatizo mengine ya kimsingi ambayo angependa kuyaeleza sisi tuko tayari kumsaidia hata baada ya kipindi cha maswali haya. (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri kwa majibu yake na vitu viwili ambavyo ninataka maelezo zaidi. Pia niliuliza wale watu ambao viwanja vyao mnataka kuchukua nimefurahi kwamba mtawapa *notice* hapo hakuna tatizo. Nataka kujua kwa kuwa sasa dhana ya mwaka 1980 ilikuwa ni matumizi tu na dhana ya sasa ya mwaka 2006, ardhi ni mali. Ni kwa nini hawa watu wasipewe nafasi kama wakitaka kuuza baadhi ya viwanja vyao aidha nusu kama vile Serikali inavyouza mashamba? Hilo moja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa John Cheyo, samahani kabla hujaendelea ni ufafanuzi tu kusudi twende wote kwamba mtu amepewa kiwanja anawezaje kuuza sehemu ya kiwanja ambacho ni *entity* moja ili tuelewane wote?

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu katika dhana nzima ya MKURABITA ni pamoja na kurasimisha mali uliyonayo na nimesema kiwanja ni mali. Kwa nini mtu asirasimishiwe hicho kiwanja chake akakigawanya kama anataka na *sub division* inawezekana akauza? Hilo moja.

La pili, sitaki kuonekana kutokueleweka. Mimi sipingi vijiji kupimwa, ni vizuri vijiji vikapimwa na kupima maana yake kuweka *beacons* kwamba kijiji hiki kinaishia hapa na kijiji kile kinaishia pale. Lakini ugomvi ulioko katika nchi yetu si kati ya vijiji na vijiji, ugomvi ulioko ni kati ya wanavijiji, ndiyo maana nasema kwa nini kazia isiwe si kupima viwanja ni kupima ardhi ya kila mwanakijiji hili ndilo ninalotaka kuelewa huu mpango wa bilioni mbili utaenda sambamba na kupima kijiji pamoja na ardhi ya wanakijiji mmoja mmoja ili wapate hati. Kwa hiyo, naomba msipotoshe Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sifahamu kwa nini kaka yangu Mheshimiwa John Cheyo, hataki kuelewa. Hili Bunge lingekuwa la wasukuma tu, ningeanza kumueleza kisukuma. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza si utaratibu, mtu amepewa kiwanja cha ukubwa fulani akigawe halafu auze sehemu nyingine. Kwa sababu suala la kugawa ardhi ni la sheria namba nne ya mwaka 1999 na sheria namba tano ya mwaka 1999, ndiyo inasimamia masuala ya kugawa ardhi. Sasa Mheshimiwa John Cheyo anataka atuongeze kwenye migogoro mingi zaidi, kwa sababu kwa sasa hivi tuna *double allocation* anataka tumpe huyo mtu aleyepewa sijui mwenye *double allocation* naye aongeze. Kama zilikuwa *double allocation* mbili azidishe mara mbili ziwe nne. Kwa hiyo, tutakuwa watu wa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemwomba Mheshimiwa John Cheyo, anielewe na aielewe Serikali tunachofanya hapa ni kupunguza migogoro kama si kuondoa kabisa migogoro ya ardhi. Kuna *forgeries*, kuna utapeli, kuna kila uchafu kwenye masuala ya ardhi na ndiyo maana tumeona tutumie sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu waliobambikizwa viwanja kwamba ni vyao wakati si vyao na ndiyo maana tumewaandikia *notice* watu wote 1,000 ili kusudi wale ambao watahinda kujibu katika siku 90 tutajua hivi viwanja ni vya *forgery*. Tunataka tulifanye hili zoezi katika nchi nzima na mimi nilifikiri Mheshimiwa John Cheyo angetuelewa hili kama kuna matatizo Mheshimiwa John Cheyo atatueleza kwamba hapa kuna tatizo au hata kama kuna mtu wake mmoja ambaye anataka kukigawa kile kuna taratibu za kugawa viwanja kwa sababu kila maeneo huwa yanapangwa kulingana na sheria namba 378 ya mwaka 1956 ya *Town Planning* kama kuna mahali panatakiwa kujengwa vijiji pamejengwa hoteli au shule huwezi ukajenga *night club*. Sasa leo huyu anataka kugawa aki *divide* tu mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli hili haliwezekani kwa mujibu wa sheria. Lakini suala la kusema kwamba wapewe muda, wamepewa *notice* ya miezi mitatu inawatosha kujibu na tutachambua tutashirikiana na Kamati za Manispaa na tumeshaanza kuifanya hii kazi tunataka tuwe *fair* na wale watakaoshindwa ku-*defend* tutawafutia na si kwa Tegeta tu au Mbezi hata Bariadi ambao wameshindwa kuviendeleza tangu mwaka 1980. Sheria lazima ichukue nafasi yake. Kwa hiyo, Mheshimiwa John Cheyo tuelewe tunatekeleza sheria, ni kazi ngumu na masuala ya nyumba yana ugumu mkubwa na wewe kaka yangu Mheshimiwa John Cheyo una-*experience* kubwa ya matatizo ya nyumba. Sitaki kueleza yaliyokupata siku za nyuma. Sasa Mheshimiwa John Cheyo tuache tutekeleze sheria. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu viwanja na mashamba katika jedwali namba tatu, usajili wa vyeti na ardhi ya kijiji kati ya miliki na kadhalika wameeleza zilizotolewa. Kwa mfano katika usajili wa vijiji ambavyo vilitolewa hati za vijiji. Lakini mashamba pia yanaendelea kupimwa. *Plots* za watu zinapimwa kwa kushirikiana na Halmashauri na watendaji walioko katika Halmashauri zetu za Wilaya. Hili ndilo lengo katika kutatua matatizo. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, awali naomba nichukue nafasi hii kumpongeza kaka yangu kwa kazi nzuri aliyoifanya na ninaimani kuwa wananchi wa Tabora na maeneo mengine yote

wamefurahia sana majibu yake na mwongozo wake aliyoutoa. Kwa hiyo, sina budi ya kusema kwamba naunga mkono hoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 48*, programu 10, *sub vote 1001*, *item 250100*, Mshahara wa Waziri, sina maana ya kuushika lakini nataka maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majibu ambayo ameyatamka Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani labda anasahau kuwa pia alishawahi kutamka yale ambayo aliyotamka na alichotamka ni kinyume na yale ambayo alitamka kipindi cha maswali na majibu.

Kwa hiyo, nimemshangaa sana leo alivyotamka kuhusu suala la nyumba ambazo zilitaifishwa na Mwalimu na laiti kama kungekuwa kuna uwezo wa kushika kifungu cha Naibu Waziri cha mshahara leo mimi ningekishika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya kwamba amesema kuwa nyumba zile ambazo zilitaifishwa hazirudishwi kwa sababu muda ule umeshapita. Lakini siku ambayo alijibu swali hapa Bungeni tarehe 22 Juni, 2006 alisema kuwa kuna watu katika wale ambao nyumba zao zilichukuliwa wengine waliondoka hapa nchini moja kwa moja na wengine walilipwa fidia hata miaka ya karibuni kuna watu waliolipwa fidia. Hili alilitamka ndani ya Bunge na *Hansard* ninayo. (Makofi)

Sasa nimeshangaa leo aliposema kuwa toka miaka kumi ya mwanzo waliyoweka utaratibu wa kuweza kurudishiwa nyumba kwa kuwa hawakuweza kuomba hawajarudishiwa na hawatarudishiwa. Sasa wakati anajibu haya nadhani labda alikuwa hajaelewa au alikuwa ana matatizo gani. Kwa hiyo, ninaomba anijibu je, majibu yao hapa Bungeni wakati wanajibu maswali yale wanayojibu ndiyo halali au haya wanayojibu wakati wa bajeti? (Makofi)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, kwa kukubali kutuunga mkono baada ya kutoa maelezo mengi yanayohusu masuala ambayo aliyazungumza.

Mimi naomba nitoe ushauri kwa Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, kwamba suala la nyumba zilizotaifishwa ni suala ambalo linahitaji *information* nyingi. Lakini palitolewa kipindi maalum mpaka kwenye miaka nafikiri 1980 kwamba wale waliokuwa na *appeal* zao wazipeleke kwenye Ofisi ya Rais. (Makofi)

Sasa kwa sababu sina taarifa nyingine za zaidi zinazohusu ufafanuzi huu na kwa vile swali tulilolijibu hapa Bungeni, siwezi kukumbuka swali lilikuwa linauliza nini, mimi namwomba dada yangu Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, kwamba hili suala lake ambalo anataka tulitolee ufafanuzi hata aniandikie barua akielezea na kuweka hizo *attachments* na nini kinatakiwa kishugulikiwe, kama hicho kinachoshughulikiwa kita-*involve* Wizara yetu tu tutashughulikia. Lakini hata kama kita-*involve* pia Wizara zingine tutatafuta ufafanuzi ili kusudi tuweze kumjibu vizuri Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, asitoe mshahara wangu kwa sababu tunauhitaji kwa ajili ya kufanya kazi hizi ngumu ambazo tumepewa na Serikali. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Labda nikumbushe tu kwamba Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, alileta *file* ambalo tulilipeleka na lina *documents* nyingi kwa sababu ya muda labda hamkuweza kupitia lakini mojawapo ni barua ya Mheshimiwa Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi, inayoagiza mambo fulani fulani kwa hiyo, pamoja na kusema kwamba alete *documents* lakini kumbe mna nyingine ambazo mnazo za kufanyia kazi. (*Makofi*)

MHE. MGANA I. MSANDAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *Vote 48, program 10, sub vote 1001, item 250100*, mshahara wa Waziri. Nimeshika mshahara wa Waziri kwa sababu kipengele cha kushughulikia mipaka ya Mikoa hakipo na vile vile kipengele 270120 inayohusu upimaji wa vijiji kitaifa hata kwenye *volume* tu hakipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechangia kuhusu mpaka wa Mkoa, Mkoa wa Manyara, Arusha, Singida na Shinyanga. Miaka mingi nimekuwa nasema huu mpaka upitiwe upya ili wananchi waelezwe mpaka halisi unapita wapi. Kila mwaka nimekuwa naambiwa hakuna hela. Lakini namshukuru Mheshimiwa Waziri leo amesema kwamba Wakuu wa Wilaya walikuwa hawafanyikazi zao vizuri ndiyo maana wanataka waanze kukabidhiana *Government Notice* mara wanapohamishwa. Sasa nataka majibu huu mpaka utapitiwa lini? Kipindi cha nyuma walikuwa wanasema hela hakuna na wana kitengo kabisa kinachoshughulikia tatizo la mipaka ya Mikoa na Kitaifa. Sasa naomba hilo Waziri anijibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, Waziri amekiri mwenyewe hapa kwamba kuna maafisa wazuri kule Wilayani na wabovu wapo. Sasa mimi nimechangia nikawaambia Maafisa Ardhi wa Wilaya wameingilia kijiji cha Kinankamba wakahamisha *beacons* na kukikata katikati kijiji cha Kinankamba nataka uniambie watalishughulikia kwa haraka wa namna gani naomba majibu ya kuridhisha.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu na kutoa ufafanuzi kwa rafiki yangu Mheshimiwa Mgana Msindai. Unajua katika watu waliokuwa wanategemewa watasimamisha mshahara wangu hata siku moja sikutegemea Mheshimiwa Mgana Msindai kwamba angeweza kuusimamisha. Kwa sababu nilipokuwa Wizara ya Ujenzi, kila siku alikuwa anasema anaunga mkono na barabara zake zote ni nzuri lakini leo amenigeuka. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mgana Msindai kwamba suala la mipaka kati ya Mkoa na Mkoa, kati ya Wilaya na Wilaya na kati ya nchi yetu na nchi jirani, linasimamiwa vizuri na Wizara yangu na ndiyo maana katika majibu nilipokuwa nikitoa maelezo hapa kuna *Government Notice* ambazo zimetolewa za kila Mkoa na kila Wilaya. Lakini viongozi walioko kule Mkoani na Wilayani hawataki kuzifuata. Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanatakiwa wawe na *Government Notice* za maeneo yao na ndiyo maana katika jibu la msingi nimeeleza

tumeshanza kuandaa *Government Notice* za Wilaya zote katika nchi tutawapelekea Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na Mheshimiwa Mgana Msindai nitakupa nakala ya Mkoa wako ili kusudi uzipitie. Maeneo yale yako kwenye *Government Notice* kwamba mpaka upo hapa basi ndiyo mwisho na wasikae wanagombania mipaka kwanza wote tuko Tanzania. Kwa hiyo, suala la mipaka ni kutoa *Government Notice* kwa viongozi wote ili waweze kufuatilia. (*Makofi*)

Kuhusu upimaji wa vijiji amesema hakuna kifungu hapa, kipo kifungu na bado hatujakifikia na kimetengewa shilingi bilioni mbili. Lakini pia katika kitabu kingine zimetengwa shilingi milioni 720. Kwa hiyo, tusingesema kwamba tunapima vijiji 3104 wakati hakuna fedha. Kwa hiyo, fedha zipo hata katika Mkoa wa Singida viko vijiji vitakavyopimwa. Kuhusu maofisa Ardhi wa Wilaya ambao wamekigawa kijiji chao huko, sasa Maofisa Ardhi wa Wilaya wameajiriwa na Halmashauri ya Wilaya yeye ni Mjumbe kama Diwani sasa wakae na Mkurugenzi wake, wale waliofanya dhambi kule wawafukuze, wapeleke ripoti kwa Mheshimiwa Mizengo Pinda, mambo yanakwisha na mimi sina tatizo nitasema safi kabisa.

Mheshimiwa mwenyekiti, sasa mchukue hizi sheria mazitumie kwa sababu wale kama wamefanya dhambi na sheria zipo na Ofisa wake mkubwa ni Mkurugenzi wa Halmashauri si wafanye hicho basi, washughulikie na sisi Wabunge tuwaseme na mimi nakupongeza kwa sababu umesema kwa sababu inawezekana huyo Ofisa Ardhi alikupa kura lakini bado unamsema, wewe ni mwanaume kabisa safi endelea hivyo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kuna *addendum* ya *sub vote 2002*, kuna kifungu kidogo 310700, kinachuhusiana na masuala haya ya upimaji wa vijiji kilichotengewa shilingi bilioni mbili hakionekani kwenye kitabu hiki nafikiri ndiyo maana Mheshimiwa Mgana Msindai, aliuliza. Tunaendelea, Mheshimiwa Stella Manyanya.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana, *vote 48, programme 10, sub vote 1001, item 250100*, mshahara wa Waziri. Sitauchukua lakini naomba kwa kuwa nilimwuliza kuhusu masuala ya kiwanja cha *TIRDO* ambayo ni Taasisi nyeti inayoshughulikia wajasiriamali wengi na MKUKUTA utafanikiwa tu endapo Taasisi hii itafanya kazi zake vizuri. Kuna wafadhili ambao wanataka ku-*support* Taasisi hii lakini wanashindwa kwa kuwa hati haziko pale. Nilitegemea katika majibu yake Mheshimiwa Waziri angalau angegusia kwa sababu Taasisi hii ni kubwa na nyeti lakini sijamsikia kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri angalau anipe muda kama alivyoweza kutoa katika maeneo mengine kwamba wale ambao walihusika na upimaji wa kiwanja kile kwa sababu mafaili yote yalikuwa yanashughulikiwa kwa wakati mmoja iweje *file* moja linapewa hati jingine linanyimwa, hilo la kwanza

La pili, wale watu waliokuwa wanaenda kupima kule ni wataalam wanafahamu fika kulikuwa na *infrastructures* za Taasisi ile na wakaamua kupimia ndani bila kujadili masuala ya *compensation* na mambo mengine. Kwa hiyo, haya si masuala ya kuwaachia hawa ambao wanahusika na hivi viwanja viwili kwa sababu tatizo hilo limesababishwa

na Ardhi kutoka kuzingatia taratibu zinazostahili. Naomba anifahamishe angalau atatumia muda gani katika kufuatilia suala hili ili na mimi niweze kuwa na imani kwamba analishughulikia. *(Makofi)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, Mheshimiwa *Eng. Stella Manyanya*, alichangia kwa maandishi. Lakini kama nilivyosema, waliochangia kwa maandishi, ni Waheshimiwa Wabunge zaidi ya 67. Muda niliokuwa nimepewa ni kidogo, nisingeweza kujibu.

Mheshimiwa mwenyekiti, lakini hata hivyo, suala la Mheshimiwa *Eng. Stella Manyanya*, nilifikiri ni vizuri nilifuatilie vizuri, kwa sababu katika Wilaya ambazo zinaongoza katika migogoro, ni pamoja na Wilaya ya Kinondoni na kwa Dar es salaam, Manispaa nyingi zina migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sifahamu undani wake wa hili tatizo la *TIRDO* na ndio maana ninamwomba sana Mheshimiwa *Eng. Stella Manyanya*, kwa vile ameshalizingumza hapa, liko kwenye *Hansard* na *document* yake tunayo. Atuachie tuifanyie kazi na wataalam wanasikia na wao nina hakika hawatafurahi kuona mshahara wangu umekataliwa wakati mishahara yao ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia Mheshimiwa *Eng. Stella Manyanya*, hili suala tulifuatilie. Utupe muda na sisi tutakujibu ni namna gani tutalishughulikia. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, bado dakika sita tuingine kwenye ule utaratibu wa mafungu ya ujumla.

MHE. SULEIMAN AHMED SADDIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. *Vote 48, Programme 10, Subvote 1001*, Kifungu kidogo cha 250100 Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na baada ya maelezo yake yote ya jumla, mimi nasema naunga mkono hoja. Lakini naomba kidogo nimpe ushauri wangu kuhusu suala la Wilaya ya Mvomero.

Kwa kuwa Wataalam wote wako hapa, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Ardhi na kwa kuwa kutoka Dodoma kuelekea Dar es Salaam lazima upite Morogoro na kwa kuwa wiwanja vile vimepimwa kwa mamilioni ya fedha na vimechukua muda mrefu, wananchi wamelipa na hawajagawiwa: Naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelekezo kwa wataalam wake wapitie Morogoro Ofisi ya Ardhi Mkoa, wajue tatizo ni nini ili watoe maelekezo, wananchi wale wapewe wiwanja. Mvomero tuna nia ya kujenga mji wa kisasa na Wilaya mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelekezo, masuala mengine, mimi na yeye tutaandikiana kama alivyoshauri.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, kwa kutuunga mkono. *(Makofi)*

Lakini nataka nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq kwamba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ilituma wataalam Mvomero kwenda kuisaidia Halmashauri ya Mvomero namna ya kupima vile viwanja. Tilituma wataalam kutoka Wizarani. Sasa viwanja vikishamalizwa kupima, linabaki sasa ni jukumu la Halmashauri yenyewe kupanga. Sasa kwa sababu Halmashauri ya Mvomero na Wilaya ya Mvomero ni mpya, ninaweza nikaelewa tatizo liko wapi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, akubaliane na ushauri wangu kwamba kwa vile Wilaya ya Mvomero ni mpya, inawezekana yako matatizo ya msingi. Sasa tutakaa na wenzangu Wizarani tuone ni namna gani tunaweza tukafanya na kutoa ushauri, kwa sababu viwanja vimeshapimwa na tilituma wataalam kutoka Wizarani kwenda kusaidiana na wataalam wa kule. Sasa inawezekana kuna matatizo ya msingi.

Sasa tutakaa na wenzangu Wizarani tuone ni namna gani tunaweza tukafanya na kutoa ushauri, kwa sababu viwanja vimeshapimwa na tilituma wataalam kutoka Wizarani kwenda kusaidiana na wataalam wa kule. Sasa inawezekana kuna matatizo tu mengine ya utendaji au ya *coordination* au ya mipango kwa kutokujua kwa sababu ni Wilaya mpya. Nitamshauri Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, tuone ni namna gani tunaweza tukafanya hata kama ni kutuma tena wataalam wangu kwenda huko.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* 1,350,114,300/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* 336,113,400/=

MHE. OMAR S. KWAANGW’: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 48, Subvote 1003, Policy and Planning. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la ufafanuzi. Kwanza, sikusudii kuzungumza ya Babati kwa sababu Mheshimiwa Waziri anajua na yako kwenye meza yake na nimempa faili. Lakini nataka tu ufafanuzi juu ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri, wakati Mheshimiwa anajibu hoja za Wabunge kuhusu watendaji wabovu wa Wizara wa Ardhi ambao wako chini ya Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba kama hawa watendaji wa ardhi wangukuwa chini ya Wizara yake, basi angekuwa na nafasi ya kuwachukulia hatua wale wabovu na akasema kama angepewa miezi sita, wangerudi wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu ni suala la Sera na Mipango, naomba Serikali itoe ufafanuzi, tatizo liko kwa nani! Kama dawa ya hao watumishi wa Ardhi ipo kweli kwa Mheshimiwa John Magufuli, tatizo liko wapi? Liko Serikalini au lipo kwa Wabunge kushindwa kutunga sheria ili hao warudi kule! Tunaomba kwa sababu hapa kuna mambo mazito na ardhi ndiyo inagusa wananchi nchi nzima. Kila mwananchi, hii ndio rasilimali ya wananchi. Kama kuna watumishi wa Serikali ambao wanaharibu rasilimali hii na tunajua dawa yake inaweza kupatikana kwa maelezo ya Waziri, hebu tunaomba maelezo ya Serikali. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, una kama dakika moja na nusu hivi! *(Makofi)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu kwa haraka na kutoa maelezo kwa Mheshimiwa Omar Kwaangw’.

Suala la Maofisa Ardhi wenye matatizo katika Halmashauri za Wilaya na kadhalika liko ndani ya uwezo wa Serikali. Serikali inafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa sana na kwa bahati nzuri katika hili tumeshalifanyia mazungumzo mengi na Mheshimiwa Mizengo Pinda pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ujumla. Patakuwa na mikataba itakayokuwa inawekwa, itakayowadhibiti vizuri watendaji wale kule. Lakini ilinibidi nizungumze hivyo kwamba kama pangukuwa na uwezo, kusema uwezo, unaweza kusema ningekuwa na mabawa, sasa mabawa huna!

Nilisema pangukuwa na uwezo siku ile nilipokuwa nasema hee, na wakarudishwa, ndivyo nilisema kwamba wangerudi wachache. Lakini nina uhakika kwa sasa hivi kama alivyofanya Mheshimiwa Mgana Msindai na yeye Mheshimiwa Omar Kwaangw’, atafanya hivyo na Waheshimiwa Wabunge wengine watafanya hivyo. Watawataja wale watendaji walio wabovu. Tutashirikiana na Mheshimiwa Mizengo Pinda, tutachukua hatua katika kuwashughulikia mahali walipo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tutakubalina kwamba muda uliobaki, umeishaingia katika utaratibu wa Kanuni ambayo tutapitisha mafungu kwa ujumla.

Kifungu 1004 - *Management Information System*298,261,100/=
Kifungu 2001 - *Land Development* 1,340,990,900/=
Kifungu 2002 - *Surveys and Mapping* 1,554,602,400/=
Kifungu 2003 - *Customary Land Tribunal* 0/=
Kifungu 3001 - *Human Settlements Development* 5,963,455,300/=
Kifungu 3003 - *Housing Appeal Tribunal* 1,517,022,900/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Kifungu 1001 - *Administration and General* 169,000,000/=
Kifungu 1004 - *Management Information System* 0/=
Kifungu 2001 - *Land Development* 176,994,000/=
Kifungu 2002 - *Surveys and Mapping* 1,720,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

T A A R I F A

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima imepitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007, Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makisio ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!
(Makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)

*(Saa 01.44 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,
Tarehe 11 Agosti, 2006 saa tatu asubuhi)*